Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Arobaini – Tarehe 28 Julai, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na**:-**

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA NA BIASHARA):**

Taarifa ya Kamati ya Viwanda na Biashara kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka 2008/2009 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO):-**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Randama za Makadirio ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

## MASWALI NA MAJIBU

**Na. 289**

**Mabaraza ya Ardhi ya Kata**

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU** aliuliza**:-**

Kwa kuwa, Serikali imeanzisha Mabaraza ya Ardhi ya Kata katika Jimbo la Magu:-

(a) Je, ni zipi stahili za Wajumbe wa Mabaraza hayo na wanasimamiwa na chombo gani?

(b) Je, ni lini Wajumbe hao watapatiwa semina?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Festus Bulugu Limbu, Mbunge wa Magu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi ya Kata ni chombo ambacho kimeundwa kwa mujibu wa Sheria Mabaraza ya Kata sura ya 206 toleo la mwaka 2002. Pamoja na majukumu yake ya kawaida Mabaraza ya Kata yana madaraka ya kupokea na kusikiliza rufaa za migogoro ya ardhi kutoka katika Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji ambavyo vimo katika Kata husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, stahili za Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi ya Kata katika Jimbo la Magu ni kama ilivyo katika Wilaya zingine nchini. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999, na kama ilivyofafanuliwa na mwongozo wa sheria za Mahakama ya Ardhi wa mwaka 2005, posho za Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi ya Kata zitalipwa kwa viwango vya sheria ya fedha ya Serikali za mitaa ya mwaka 1982. Chanzo cha fedha za posho zitakazotokana na vyanzo vya mapato vya mabaraza ya Kata kama vile faini gharama za kesi na mchango wa Halmashauri na wadau wengine. mabaraza haya yanasimamiwa na Halmashauri za Wilaya husika. Mpaka tulipokuwa tunaingia katika kikao hiki Wajumbe wa Baraza hili katika Wilaya ya Magu walikuwa wamepewa shilingi elfu kumi na nne ambayo ilikuwa ni *flat rate*

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi ya Kata katika Wilaya ya Magu yalipewa semina juu ya uendeshaji wa mabaraza haya katika mwaka wa fedha 2007/2008. Semina hizo ziliendeshwa na wawezeshaji kutoka katika ngazi ya Wilaya na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Wawezeshaji hawa walikuwa wa fani za ardhi, sheria na rasilimali watu. Baada ya mafunzo mabaraza haya yalipewa vitendea kazi vya msingi kama vile majalada au mafaili na karatasi. Kwa kuwa

muda wa kazi wa Wajumbe wa mabaraza haya ni miaka mitatu, Halmashauri ya Wilaya ya Magu itaendelea kutoa elimu na vitendea kazi vya msingi kwa Mabaraza haya ili kuongeza ufanisi katika utendaji .

(c)Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu swali Na. 68 la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Namtumbo kwenye Mkutano wa Nane wa Bunge lako Tukufu, napenda kuzihimiza Halmashauri zote nchini kuhakikisha uanzishwaji wa mabaraza hayo kwa kila Kata na Kijiji unafanyika.

Vilevile ziandae mipango maalum ya kuwaelimisha na kuwawezesha watendaji wa mabaraza hayo katika kutekeleza majukumu yao. Hii ni pamoja na utoaji wa elimu kwa umma juu ya utumiaji wa mabaraza hayo.*(Makofi)*

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti namshukuru sana Waziri kwa majibu mazuri, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri haoni kwamba kuruhusu Mabaraza haya kujilipa kutokana na faini itabidi waongeze sana faini ili wapate pesa za kujilipa, haoni kwamba hiyo ni hatari?

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, toka mwaka 1974 ambapo vilianzishwa vijiji vya ujamaa mashamba yaligawiwa upya na baadhi ya watu wakawa wamehama, sasa hivi wanaanza kurudi kudai maeneo yaliyokuwa ya kwao wakati tayari yalishagawiwa na Serikali za vijiji kwa wananchi wapya, huo ni mgogoro mkubwa. Mheshimiwa Waziri anatoa kauli gani kuhusu hali hiyo?(*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unaporuhusu watu walete vitu na pesa zinazopatikana katika kesi ile ndizo zitakazotumika kulipa mabaraza, mimi sidhani kama hili linawezekana kwa sababu katika haya mabaraza kipo kiwango cha mwisho kinachotamkwa pale kwamba ni shilingi elfu kumi. Kwa hiyo hata kama watataka wawatoze sana ili ziongezeke kule wakapate ishirini hakuna, utaratibu huu mwisho wake ni shilingi elfu kumi hawawezi kufanya kinyume cha hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusu mgogoro wa ardhi kwamba ardhi ilishagawanywa halafu baadaye tena inachukuliwa inapelekwa kwenye kesi, Mabaraza haya yanaanzia kwenye vijiji yanakwenda kwenye Kata na yanapotoka kwenye Kata yanakwenda kwenye Wilaya na moja kwa moja kesi zile zinakwenda Mahakama Kuu. Huu anaosema kwamba unakuwa ni mgogoro mkubwa maana yake ni kwamba kama kuna mtu yeyote anayetaka kulalamika atakwenda katika hatua hiyo kulingana na ukubwa wa mgogoro unaozungumzwa hapo.

Na. 290

**Kuboresha Kituo cha Afya cha Nanjirinji –Kilwa**

**MHE. HASNAIN G. DEWJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kituo cha Afya kilichopo Nanjirinji Wilayani Kilwa kimeanza kutoa huduma lakini mpaka sasa hakina dawa, wataalam na gari la wagonjwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukiboresha kituo hicho ili kiweze kutoa huduma kwa ufanisi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha Nanjirinji kilichojengwa kwa masaada wa *TASAF* na nguvu za wananchi kilikamilika mwishoni mwa mwaka 2008. Kituo hicho kinahudumia wananchi wapatao 35,000 na kinapokea rufaa kutoka kwenye zahanati za Nakiu, Likawage na Nainokwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Watumishi; Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kama ilivyo katika maeneo mengi hapa nchini ina upungufu wa Watumishi. Kama alivyoeleza jana Mheshimiwa Waziri wa Afya, wastani wa upungufu wa watumishi wa Afya Kitaifa ni asilimia 62. Idara ya Afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ina watumishi 24 tu wakati mahitaji halisi ya Idara ni watumishi 689 kwa mujibu wa Ikama. Kituo cha Afya cha Nanjirinji kina watumishi saba ambao ni Mganga (*Clinical Officer*) mmoja, Muuguzi Mkunga mmoja na wahudumu wa Afya watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya madawa katika Halmashauri ni nzuri, vituo vya Afya na zahanati kwa kupitia mpango mpya wa kuagiza madawa yanayohitajika *(Integrated Logistic System –ILS)* huagiza MSD na kupata mgao kila robo mwaka. Kituo kilipata mgao wake kama kawaida mwezi Disemba 2008 na mara ya mwisho ilikuwa mwezi Aprili 2009. Mgao unaofuata wa Julai unategemewa wakati wowote. Sasa hivi uagizwaji umeshafanywa na Mfamasia wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa inao mpango wa kuboresha huduma katika kituo hicho. Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imewasilisha maombi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kuongezewa watumishi wenye sifa kwa mujibu wa Ikama.

Katika kuboresha huduma kwenye kituo hicho, Halmashauri itahamishwa wahudumu wa afya wawili kutoka Hospitali ya Wilaya kupelekwa Kituo cha Afya Nanjirinji mwezi Agosti, 2009. Vilevile, Halmashauri ina mpango wa kuongeza nyumba za watumishi kutoka nne zilizopo hadi sita katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 ili kuongeza motisha kwa watumishi wanaopangwa kufanya kazi hapo. *(Makofi)*

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mawili mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza;

(a) Kwa kuwa, Nanjirinji ni porini na maeneo mengi ya vijiji vya jirani ni mbali na katika swali langu la msingi niliulizia gari la wagonjwa, naona Waziri amesahau kunijibu kuhusu umuhimu wa kuwa na magari ya wagonjwa.

(b)Kwa kuwa, Lindi hakuna chuo cha kufundisha Manesi na Wakunga, Je, Serikali ina mpango gani kwa Mkoa wa Lindi kuwa na Chuo cha kufundishia Manesi na Wakunga

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema Mheshimiwa Dewji ni sahihi kwa sababu rekodi zetu hapa zinaonesha katika eneo lao kituo cha afya cha Njinjo kina *ambulance*, kituo cha afya Masoko kina *ambulance*, kituo cha afya cha Pande kina *ambulance* lakini kituo cha afya cha Nanjirinji hakina *ambulance*, kwa hiyo anachosema ni kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo kilomita anazozisema ni nyingi nimezitafuta zinaonesha kwamba kutoka Masoko Kivinje ni kilomita 190 ambako ndiko kuna hospitali ya Wilaya. Vile vile ipo karibu na hospitali ya Ruango wanakwenda kilomita 70. Kwa hiyo ni kweli anachosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna zoezi linalofanyika la *ambulance* nitamshauri Waziri Mkuu na Waziri wa Nchi ili tuone uwezekano wa kupatiwa *ambulance* kwa sababu kwa kweli wana tatizo hawa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Ahsante sana, namwona Waziri wa Afya anataka kujibu swali la pili.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kujibu swali la pili la Mheshimiwa Gulamabas Dewji, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tulipojibu swali la Mheshimiwa Balozi Mshangama, alikuwa ameomba ikiwezekana tuanzishe shule ya waganga pale Lushoto na

jibu tulilotoa ni kwamba, Mkakati wa kuongeza idadi ya wafanyakazi ni wa kitaifa. Hivi vyuo vyote tulivyonavyo hapa nchini ni kwa ajili ya Taifa zima, kwa hiyo tunachofanya katika mpango ya MMAM ni kuviimarisha na hapo baadaye tukiona kwamba kutakuwa na haja ya kujenga vingine tutafanya hivyo, lakini hivi tulivyo navyo wahitimu wanapelekwa kila mahali na kama alivyosema Naibu Waziri sasa hivi ni kwamba kituo alichokuwa anakizungumzia kina wafanyakazi ambao walisoma mahali pengine wala siyo katika Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba mpitishe bajeti yetu ili tujaribu kuongeza idadi ya watu na kufuatana na mahitaji yao tutawapeleka wengine katika Wilaya ya Lindi.

Na. 291

**Kupeleka mawasiliano ya simu za mipakani na maeneo ya kibiashara**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa suala la mawasiliano ya simu ni kitu cha msingi sana hasa kwwenye maeneo ya mipakani na maeneo yenye shughuli nyingi za kibiashara kama vile eneo la Kata ya Muhukuru mpakani mwa Tanzania na Msumbiji; eneo la Ifinga ambako kuna pori la akiba maeneo ya Mgazini kwenye eneo la mnada na soko kubwa la mahindi:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya mara kwa mara ya kupeleka mawasiliano ya simu kwenye maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano Sayansi na Teknolojia, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama Mbunge wa Peramiho napenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge juu ya umuhimu wa mawasiliano katika maeneo ya mipakani mwa nchi yetu yenye shughuli nyingi za kibiashara. mawasiliano ya simu ni muhimu sana, hii ni pamoja na umuhimu wake kwa ulinzi na usalama wa nchi yetu; ndiyo maana Serikali kupitia makampuni ya simu mbalimbali nchini imefanya juhudi kubwa ya kuboresha simu baina ya nchi yetu na nchi za jirani. Mfano Tanzania na Kenya eneo la Namanga na Holili, Mombasa na Tanga maeneo ya Horohoro, baina ya Tanzania na Uganda katika maeneo ya Bunazi pamoja na maeneo mengine ya mipakani ambayo hayakutajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lakini pia kampuni zetu za mawasiliano ya simu za mikononi zimewezesha kutumia mtandao mmoja kwenda katika nchi jirani, Mfano *Vodacom* ambao hushirikiana na Safaricom, *Zain* ambayo hutumika kwa nchi jirani za Kenya, Uganda, jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), na nchi zingine ambazo hazikutajwa ambapo mtandao wa Zain unatumika. Hata hivyo pamoja na juhudi hizo nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa katika eneo aliloainisha mawasiliano hayajaboreka kama tulivyotarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa anapenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama Mbunge wa Peramiho kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *Zain* ilishafanya tafiti za masoko katika eneo la Ifinga na maeneo mengine ili kuweza kufikisha mawasiliano, lakini tafiti hazijatosheleza kwa ujenzi wa mnara katika maeneo hayo kwa mwaka huu wa 2009. Kampuni ya *Zain* itaendelea na tafiti za masoko katika maeneo hayo mwaka 2010 na matokeo ya tafiti hizo yatapelekea ujenzi wa mnara katika maeneo hayo kabla ya mwezi Disemba 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza ahadi hiyo, Kampuni ya *VODACOM* imeshananza upembuzi ili kubaini hatua gani za kuchukua ili kuboresha mawasiliano katika Kata ya Muhukuru na maeneo ya Mgazini. Wataalam watafika maeneo hayo mapema mwezi Agosti, 2009. Baada ya ripoti hiyo ya wataalam ni matumaini ya kampuni kuwa shughuli zinazofuata baada ya ripoti ya kitaalam zitafanyika kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) ipo kwenye mikakati ya kusambaza na kuboresha huduma ya simu za mikononi kwa kutumia teknolojia ya "*Code Division Multiple Access (CDMA*)" katika maeneo mbalimbali nchini. Huduma hii ya mawasiliano iliyoanzishwa mwaka 2007 tayari inapatikana katika Miji Mikuu ya Mikoa na baadhi ya Miji ya Wilaya. Hata hivyo *TCCL* haijafanikiwa kufikisha huduma hii katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge kwenye Jimbo la Peramiho. Hata hivyo *TTCL* kwa sasa inafanya ujenzi wa mtandao wa intaneti (*broad band*) na upanuzi wa huduma za simu za mezani katika Mji wa Peramiho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *TIGO* imeliweka eneo la Muhukuru katika mipango yake endelevu ili kufanya utafiti wa awali kwa ajili ya kuweka mnara wa mawasiliano .

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muhula wake wa kwanza wa upanuzi wa mawasiliano Kampuni ya Simu ya ZANTEL itakuwa na mnara wa mawasiliano Peramiho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Peramiho kuwa nitafanya kila lililo katika uwezo wangu kuyashawishi makampuni ya simu za Mkononi kuona umuhimu wa kujenga minara katika maeneo ya Muhukuru,

Mgazini pamoja na Ifinga ili kuwaondolea kero wananchi wa Peramiho, kama ambavyo nimekuwa nikishirikiana na Waheshimiwa Wabunge katika maeneo mbalimbali yenye kero za mawasiliano, zinazofanana na zile za jimbo la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niulize maswali mawili ya nyongeza:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kabisa kwamba umuhimu wa ulinzi na usalama katika mipaka yetu ni jambo la msingi, na kwa kuwa mpaka wetu wa Tanzania na Msumbiji katika miaka ya nyuma umekuwa ndiyo kimbilio la mipenyo ya wageni kuingia kupitia eneo hilo, na kwa kuwa, wenzetu wa Msumbiji wana mtandao wa simu ambao kama sikosei unaitwa *Cemtel*,

Namwomba Mheshimiwa Waziri wakati tukisubiri upembuzi huo, kwa nini basi kampuni yetu ya *Celtel* isifanye ubia na kampuni ile ya Msumbiji kama inavyofanya katika maeneo mengine ambayo ameyataja na kukiri kwamba huduma hiyo inafanyika kwa utaratibu huo.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Dokta Maua Daftari ni Mtendaji kazi mzuri, msikivu na anasaidia sana kutatua kero za mawasiliano katika nchi yetu hii ya Tanzania, na sisi kama Wabunge tunakiri hilo na tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu na tunampongeza.

Je, yupo tayari kuja kuyatembelea maeneo hayo niliyoyasema angalau kupata mawazo zaidi ya kuboresha sayansi na teknolojia katika maeneo hayo niliyoyasema, hususani katika eneo la simu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Mhagama kwa kufuatilia shughuli zake za mawasiliano katika Jimbo lake.

Pili nataka nikubaliane naye kwamba kwa upande wa Msumbiji kuna kampuni ya *Cemtel* ambayo inafanana kabisa na kampuni ya *Zain*.

Ninachoweza kukifanya mimi ni kuwasikiliza wenzangu wa *Zain* wanasemaje kama kweli wanaweza wakafanya ubia au wanaweza kwa namna moja au nyingine kuwa na mawasiliano kwa kupitia *Cemtel* yanaweza kufika katika maeneo anayozungumza Mheshimiwa Mbunge. Lakini ajue tu kwamba hizi ni nchi mbili tofauti na kila mmoja itakuwa ina mipangilio yake ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi niko tayari kumtembelea katika maeneo yake ya Peramiho, na wale wengine ambao niliwaahidi kwenda katika maeneo yake ndiyo ninafanya mpangilio huo na Mheshimiwa Jenista unikubalie kwamba, hivi karibuni nilipata nafasi ya kumwita *CEO* wa *TIGO* ofisini kwangu kuzungumzia tu umuhimu wa simu mipakani na nimepanga *matrix* kwa ajili ya mawasiliano ya simu mipakani na maeneo mengine ili watakapopanga *plan* zao wa-*take into consideration* maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wote wanayalalamikia ambayo hayajafikiwa.(*Makofi*)

Na. 292

**Madai ya wakulima wa Chai na Wafanyakazi wa eneo la Balangai Tea Estate**

**MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, ni muda mrefu sana tangu mwaka 1998 wakulima wadogo wa chai na wafanyakazi wa eneo la Balangai wanadai malipo ya majani ya chai waliyowauzia wamiliki wa Balangai *Tea Estate* na pia malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi:-

(a) Je, ni nani hasa wamiliki wa Balangai *Tea Estate?*

(b) Je, ni lini watawalipa wanyonge hao madai yao wanayodai kwa zaidi ya miaka kumi sasa?

(c) Je, kitu gani wanachofanyiwa wanyonge wa Balangai, siyo aina moja ya ufisadi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba nitoe maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bangalai *Tea Estate* inajumuisha shamba la Bangalai lenye ukubwa wa hekta 212 na shamba la Dindira lenye ukubwa wa hekta 443 ikiwa ni mali zilizokuwa zikimilikiwa na *RALLI ESTATES* na kuendeshwa chini ya M/S George Williamson (T) *Ltd*. kama wakala. Mwaka 1995 mashamba haya yaliuzwa kwa kampuni ya *THL Investments* na kuendeshwa chini ya uenyekiti wa Bwana B.E Shamji.

Baada ya miaka 10 ya uendeshaji, kampuni hii ilikumbwa na matatizo ya ukosefu wa fedha na hivyo kuwalazimu kutafuta mwekezaji mwenye uwezo wa kifedha hali

iliyopelekea kuingia Mkataba wa Makubaliano (*Memorandum of Understanding –MOU*) na kampuni ya Mohamed *Enterprises* (T) *Ltd*. Mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya mafupi naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo Mbunge wa Bumbuli lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mmiliki halali wa Balangai *Tea Estate Ltd* ni THL *investment Ltd* chini ya Bwana B.E. Shamji.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikifuatilia kwa karibu sana madai ya wakulima na wafanyakazi hawa. Ucheleweshaji wa madai ya wakulima na wafanyakazi umetokana na kufunguliwa kwa kesi Na. 53 iliyofunguliwa mwaka 2007 mahakama ya Ardhi baina ya kampuni ya *THL Investment Ltd.* na Mohamed *Enterprises (T) Ltd*. Kutokana na kufunguliwa kwa kesi hiyo hatma ya madai ya wakulima na wafanyakazi hao itategemea maamuzi ya mahakama kwenye kesi hiyo.

(c)Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ucheleweshwaji wa haki za wakulima na wafanyakazi hawa umeendelea kuwepo kutokana na kesi iliyoko mahakamani. Hivyo baada ya kesi hiyo mahakamani kumalizika tatizo la madai haya litaweza kushughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi mara moja.

**MHE. WILLIAM H.SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo mawili, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri napenda kumwuuliza Waziri kwamba katika tathmini ya Serikali haoni kwamba hii ni jeuri na uonevu kwa sababu madai hayo ni ya mwaka 1998 na kesi imefunguliwa mwaka 2008; hii si jeuri tu kwa sababu hawa ni wanyonge na kwa hiyo wanaonewa?

Kwa kuwa, kwa muda wa miaka zaidi ya kumi sasa, wamekaa na fedha za wakulima milioni kumi kwa miaka kumi na miwili. Je, si halali kwamba wakati wanapolipa Serikali iwalazimishe kulipa na riba ya kibenki?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO,CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba madai haya yamekaa muda mrefu sana kuanzia mwaka 1998 lakini mwaka 2007 ndiyo kesi ikafunguliwa, kwa vile kesi hii iko mahakamani kwa sasa kwa kweli hatuwezi kuzungumza lolote mpaka hukumu itolewe.*(Makofi)*

Swali lake la pili la kuhusu kulipa riba nadhani baada ya kwamba kesi imekwisha Mahakamani watu watakaa na kuangalia ni vipi mkulima huyu na wafanyakazi hawa wanaweza kulipwa kitu ambacho kinaridhisha kwa sababu kusema kweli fedha hiyo, kama wangekuwa wameshapewa sasa hivi wangekuwa wameshaifanyia kazi kwa kiasi kikubwa.

Mwisho, napenda kumpongeza Mheshimiwa William Shellukindo kwa kazi kubwa anayoifanya kusema kweli ya kutetea wafanyakazi na wakulima wa chai na siyo shamba tu hili lakini pia na mashamba mengine ya chai nzima. Hongera sana Mheshimiwa Shellukindo. (*Makofi*)

Na. 293

**Mfumo Maalum wa Kuwezesha Jamii za Wafugaji na Wakulima – Manyara**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Kwa kuwa jamii za wafugaji Mkoani Manyara hazikopesheki kwa kutumia mifumo ya sasa ya kutumia *SACCOS* na vyombo vingine vya fedha kutokana na hali zao duni za maisha na kwa kuwa mfumo wa sasa wa uhamasishaji jamii kwa njia ya luninga (*television*), radio na magazeti haujawafikia na hivyo awamu zote za uwezeshaji wananchi hazijafahamika vizuri kwa jamii hizo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani kuhusu kuwasaidia walengwa hao?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa kuna haja ya kubuni mfumo tofauti wa kuziwezesha jamii hizo kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge Viti Maalum Manyara, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua matatizo yanayozikabili jamii zinazoishi maisha ya kuhama hama kama vile wafugaji. Serikali inaendelea kuwapalekea elimu, kuwashauri na kuwahimiza kuwa na makazi ya kudumu kwa kuwa inakuwa vigumu kutekeleza mipango ya maendeleo katika hali na staili za maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jukumu na nia ya Serikali yetu ya kuinua viwango vya elimu kwa wananchi wote, hasa wa maeneo ya vijijini uzoefu umeonyesha ni vigumu kuwahudumia vizuri wananchi wanaoishi maisha ya kuhamahama.

Hivyo Serikali inandelea kusisitiza umuhimu wa jamii hizi kuanza kuendesha shughuli zao za ufugaji kwenye makazi ya kudumu ili kuweza kuendesha ufugaji ulio bora na wa kisasa. Pia itakuwa rahisi kwa Serikali kutoa huduma zinge za kijamii kama,

afya, maji na hata kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu ya kuendeleza na kuboresha maisha yao.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaamini kwamba njia kuu ya kusaidia jamii ya wafugaji ni kuwapa elimu itakavyowawezesha kutambua umuhimu wa kubadili utamaduni wa kuhamahama na kuanzisha makazi ya kuduma. Tutakapokuwa tumefaulu katika azma hii, mikakati mipya stahiki itabuniwa ambayo itaongeza kasi na kiasi cha uwezeshaji wa jamii hizi kiuchumi.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala zima la kuwawezesha wananchi kiuchumi haikufanywa kwa kuzingatia kufanya utafiti wa kubaini mahitaji ya lazima ama *immediate needs* za wananchi na jamii mbalimbali hususan wananchi kama Wahdazabe na Wabarbar walioko Mkoani Manyara na kwa kuwa msingi wa maendeleo siyo tu kuwapa watu fedha ama kuwawezesha kuwapa mikopo bali hata kuwawezesha kuwajengea nyumba bora, kuwawezesha kuwa na afya bora na kuwapa elimu.

(a) Je, Serikali sasa kwa awamu inayofuata ya uwezeshaji wananchi kiumi itakuwa tayari kuangalia mahitaji ya lazima ama yale ya wakati huo kuzingatia kwamba wananchi wanafurahia uwezeshwaji pale ambapo wanawezeshwa kwa mahitaji ya wakati huo?

(b)Kwa kuwa wafugaji walioko Mkoa Manyara wana idadi kubwa ya Mifugo na kwa hiyo, wana fedha nyingi lakini bado hali yao ni duni na bado hawakopesheki kwa maana ya kwamba hawajawa na uwezo ama uelewa wa kutumia fedha hizo za mifugo wanayohoji vizuri. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kuwapa wafugaji soko la uhakika na kuwawezesha kuwapa pembejeo za mifugo kama madawa na mabwawa na majosho ni uhamasisha tosha wa kuwawezesha wananchi hawa kiuchumi. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusu utafiti ni kweli nakiri kwamba mpanga huo anaozungumzia Mheshimiwa Mbunge wa kuwawezesha wananchi kiuchumi haukufanyiwa utafiti mahususi kwa ajili ya mpango ule isipokuwa Serikali ilikuwa inafahamu na inafahamu mahitaji ya wananchi wake kiuchumi. Ninakubaliana naye kwamba kwa sababu jamii zetu nchini ni tofauti kuna haja ya kufanya utafiti anaozungumzia ili kubaini mahitaji halisi ya wakati tutakaokuwa tunatekeleza ile mipango maana yake kuwawezesha wananchi kiuchumi ni sehemu tu moja ya mpango mpana zaidi wa kuboresha maisha ya wananchi kwa ujumla.

Swali lake la pili, ninakubaliana naye kwamba ni kweli inawezekana kwamba mahitaji ya wananchi ambao wako kwenye maeneo ya ufugaji siyo lazima ni fedha maana ni dhahiri kwamba kwa mifugo yao wana pesa nyingi na ndiyo sababu hata dhana ile ya thamani kwa wafugaji hawa inaweza kuwa tofauti na sisi. Kwa hiyo, vyama vya akiba na Mikopo vikashindwa kuanzishwa na kuboreka. Kwa hiyo, nakubaliana naye.

Lakini la msingi hapa ni kwanza ni elimu, pili ni kuwashauri na kuwaomba waone kwamba kuna haja sasa ya kubadilisha wanavyotazama maisha ya kuhama hama.

Lakini vile vile tukumbuke kwamba hapa tunaweza kuwa tunakabiliana vile vile na tatizo la mila, desturi na tamaduni za jamii ya wafugaji.

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa fedha pekee ambazo wafugaji wafugaji wanaweza wakapata mkopo ni hizi fedha za JK lakini fedha hizi zimekuwa za siasa, za upendeleo na baadhi ya majimbo hawajapata hizo fedha mpaka leo. Wabunge wengine wanahukumiwa kwa ajili ya hizi fedha kwa sababu tulikwenda kusema kwamba hizi fedha zipo na Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza leo kutuambia Wabunge wanaotoka katika maeneo ambayo hayajapata hizi fedha kwamba msisubiri hizo fedha kwa sababu hazipo ili tuweze kwenda kuwaambia wananchi kwamba msiwe na matumaini tena na hizo fedha kwa Majimbo yote pamoja na Jimbo la Longido ambao hawakupata hizo fedha? Naomba jibu. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Michael Lekule Laizer swali lake zuri na lakini kali kama ifuatavyo:-

Kwanza sikubaliani naye sana kwamba kuna uhusiano wowote katika mpango huu wa kuwasaidia wananchi kiuchumi siyo mpango wa kisiasa. Lakini la pili sikubaliana naye kwamba kuna upandeleo wowote.

Maana yake kama tunavyokumbuka bilioni 21 hizi zilipotolewa ilitamkwa rasmi na Serikali kwamba kila Mkoa katika Mikoa yetu 21 ingepata shilingi bilioni 1 za kuanzia na Zanzibar kule Mikoa yao mitano kila moja ungepata milioni 100 isipokuwa Mkoa wa Magharibi ambao ungepata milioni 200.

Jambo hilo limetendeka. Lakini la pili nikiri kwamba mpango huu ulipoanza mwanzo kuna Wilaya ambazo hazikufikiwa. Lakini sababu ya msingi ilikuwa kwamba vyombo vyetu vya fedha vikuu *NMB* na *CRDB* havikuwa na matawi kwenye zile Wilaya na ndiyo sababu Serikali ikaamua kwamba itapeleka fedha zingine kupitia vyombo vingine vya fedha na kama tutakumbuka ziliteuliwa taasisi14 za fedha ambazo zimefanyakazi nzuri sana. Kwa bahati mbaya Mheshimiwa Mbunge anakotoka Longido bado mpaka sasa hivi nakiri hawajafikiwa na mpango huu.

Lakini sababu ya msingi ni kwamba pale shilingi 100 zilipotolewa kwenye taasisi ya fedha ambayo ingepeleka fedha hizi kwa ajili kwa mikopo kwa wananchi wa Longido taasisi ile baadaye ilirudi nyuma na haikuendelea na mpango ule.

Lakini Serikali bado imeendelea kujitahidi kutafuta taasisi nyingine ya fedha ambayo itakuwa tayari kuwapelekea wananchi wa Longido mikopo hii chini ya mpango huu na sasa tumepata shirika la *Pride* na shirika la *Pride* limetengewa shilingi 250

milioni kwa ajili ya Longido na kilichosalia sasa ni kukamilisha mikataba kati ya Serikali na shirika hili ili mpango huo uendelezwe kwenye Wilaya ya Longido. (*Makofi*)

Na. 294

**Makato Kwenye Malipo ya Pensheni**

**MHE. MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Kwa kuwa wastaafu hulipwa pensheni zao kupitia Benki ya *NMB* na kwamba hukatwa gharama za benki kwenye malipo hayo:-

Je, Serikali haioni kwamba kipato hicho ni kidogo na kukipunguza ni sawa na kuwanyanyasa wahusika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa siyo *NMB* pekee ambayo hutumika kwa hotuba huduma za kuwalipa wastaafu pensheni zao, ziko pia benki nyingine zinazotumika kutegemea na ukaribu pamoja na mstaafu mwenyewe kuwa na akaunti katika benki nyingine mbali na *NMB.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa pensheni wanayolipwa wastaafu kupitia akaunti zao za benki hukatwa gharama za huduma za kibenki. Hali hiyo inatokana kwamba benki kukata gharama kunapunguza kipato cha wastaafu.

Hata hivyo, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, benki hutoza gharama pale inapotoa huduma kwa mtu yoyote ikiwa ni eneo moja la mapato ya benki. Njia pekee ya kuwasaidia wastaafu ni kuongeza kiwango cha pensheni kila baada ya muda. Kwa kuwa huu ni wajibu wa Serikali, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itakuwa ikiongeza kiwango cha pensheni kila baada ya muda, kutegemeana na hali ya mapato ya Serikali yatakavyokuwa.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge, asaidiane na Serikali na ninaamini ana uwezo huo katika kuwaelimisha wastaafu juu ya matumizi ya benki, kwani ni njia salama na huchukua muda mfupi mstaafu kuweza kupata pensheni yake.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuishukuru Serikali kwa kweli kuweza kulijali kundi hili la wastaafu kwa sasa hivi na hasa hasa kulingana na jibu la Naibu Waziri jinsi gani alivyoweza kulijibu swali langu vizuri.

Kwa kuwa Serikali inakiri wazi kwamba kila wakati Serikali itakapokuwa inaongeza kipato chake basi na wastaafu watakuwa wanafikiria kuongezwa kipato chao. Je, Serikali haioni sasa hivi ni wakati muafaka wa kuanza safari ya kuwafikiria wastaafu hawa nao wakawaweka katika kiwango cha kima cha chini cha kipata cha nchi hii? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kuinua hali ya wastaafu ili iweze kwenda sambamba na maisha yalivyo kwa wakati ule.

Lakini kama nilivyosema kwamba kila mapato ya Serikali yatakapoongezeka Serikali nayo itaongeza kipato cha wastaafu na hiyo nia na lengo ambalo Mheshimiwa Mama Hewa anawaombea wastaafu tutafikia wakati muafaka Serikali nayo itafikia hapo. (*Makofi*)

Na. 295

**Kokoto Imara za Ujenzi wa Barabara**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa barabara imara unategemea pia uimara wa Kokoto zinazotumika kuchanganya lami.

(a) Je, ni maeneo gani katika nchi yetu yanayotoa kokoto zilizo imara na bora kwa ujenzi wa barabara?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa maeneo ya Kiwira Wilayani Rungwe yanatoa kokoto imara?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu wa Wizara yangu katika kazi za usanifu wa ujenzi wa barabara unaonyesha kwamba karibu maeneo mengi hapa nchini yana miamba inayofaa kwa ajili ya kutoa kokoto zilizo imara na bora kwa ujenzi wa barabara. Hii ni

kuondoa ukanda wa Pwani ambao una miamba ya chokaa. Kwa sehemu kubwa kokoto zitokanazo na miamba ya chokaa kwenye ukanda huo zina uimara na ubora ulio chini ya viwango vinavyohitajika kwa ujenzi wa barabara. Tatizo la ukosefu wa kokoto kwa kazi za ujenzi wa barabara kwenye baadhi ya Mikoa linatokana na kutokuwepo kwa makandarasi wanaojishughulisha na upasuaji wa miamba kwa ajili ya kokoto kwenye Mikoa hiyo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafahamu maeneo ya Kiwira Wilayani Rungwe kuwa ni moja ya maeneo yanayotoa kokoto bora na imara. Na ndio maana Serikali iliweza kuendesha mtambo wa kusaga kokoto kwenye eneo hilo tangu mwaka 1984 na kuanzia mwaka 2007/2008 Serikali iliamua kuendesha mtambo huo na mingine na aina yake kwa kutumia makandarasi.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika majibu ya msingi Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba ukanda wa Pwani una miamba aina ya chokaa ambayo inatoa kokoto ambazo ni hafifu. Je, anaweza akalieleza Bunge lako ni kwa nini basi mashine ya kusaga kokoto iliyokuwa Kiwira iliamua kuhamishiwa maeneo ya Pwani bila kuutarifu uongozi wa Mkoa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (k.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtambo huu wa kusaga kokoto uliokuwa Kiwira ulikodishwa kwa kampuni ya *Nambo* investment tokea mwaka 2007 kwa mkataba baina *Nambo* na *TEMESA*. Kwa sababu walikubaliana wenyewe hatuoni kwamba kulikuwa ni lazima tuuambie Mkoa kwa sababu ni ukodishaji ambao tulikubaliana kimsingi kwamba zile *non core asserts* ambazo hazitumiki zinaweza kukodishwa kwa mtu yeyote.

Ndiyo maana si mtambo huu tu, iko na mitambo mingine ambayo ilikuwa inamilikiwa *TRC* nayo pia ilikodishwa na hakukuwa kwamba kuna ulazima Mkoa uarifikiwe. Hivi sasa mtambo unafanyakazi Pwani, vizuri. Lakini ulikuwa uko katika matengenezo kwa muda mrefu umeanza mwaka 2008 matengenezo alikuwa anafanya mwenyewe ambaye amepewa ule mtambo. Kweli mtambo uligharimu hela nyingi sana mpaka kufika kuanza kufanya shughuli hizi za kusaga kokoto kule Pwani. (*Makofi*)

Na. 296

**Hali Mbaya ya Kiuchumi ya Shirika la Reli – TAZARA**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa mamlaka ya Reli ya Uhuru *TAZARA* inakubaliwa na hali mbaya kiuchumi kiasi cha kushindwa kutimiza wajibu wake sawasawa ikiwa ni pamoja na kutokulipa mafao kwa wastaafu, wanaoacha kazi na wanaofariki:-

(a) Je, hadi sasa ni watumishi wangapi waliostaafu, walioacha kazi na waliofariki dunia ambao bado hawajalipwa haki zao?

(b) Je, Watumishi hao kwa ujumla wao wanadai kiasi gani cha fedha na ni hatua gani za dharura zinachukuliwa kulipa fedha hizo?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani za dharura za kuinusuru *TAZARA*?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU):** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wengi wa *TAZARA* waliajiriwa katika kipindi kimoja wakati mamlaka ilipoanzishwa mwaka 1975.

Hivi sasa *TAZARA* inakabiliwa na tatizo la wimbi la wafanyakazi wengi wanaostaafu kwa wakati mmoja. Idadi ya watumishi waliostaafu *TAZARA* kwa upande wa Tanzania ni 1,077 waliokufa ni 623 na walioacha kazi ni 7 ambao hawajalipwa haki zao.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na idadi ya wastaafu iliyotajwa hapo juu, mamlaka inadaiwa kiasi cha *USD* milioni 20.7 kwa wafanyakazi waliokwishastaafu na *USD 30.9* kwa wafanyakazi ambao bado wako kazini. Kwa ujumla *TAZARA* inadaiwa USD milioni 51.6 kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi na wastaafu wote. Hata hivyo wadhibiti na wahakiki wakuu wa fedha za Serikali wa nchi za Tanzania na Zambia wameombwa kuhakiki madeni yote ya *TAZARA* ikiwa ni pamoja na pensheni za wafanyakazi ili kubaini kiasi halisi ambacho *TAZARA* inadaiwa na wafanyakazi na wastaafu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za dharura zilizochukuliwa awali ilikuwa ni pamoja na kuuza rasilimali za mamlaka ya *TAZARA* na kulipa madai hayo ya wafanyakazi. Hata hivyo kutokana na ukubwa wa deni ambalo *TAZARA* inadaiwa na wafanyakazi, hatua hiyo ya dharura haikuweza kutatua tatizo a kulipa deni lote.

Kwa hiyo, Serikali za Tanzania na Zambia zimeishauri *TAZARA* itafute fedha hizo kutoka taasisi za kifedha wakati Serikali mbili hizi za fedha za kuwekeza kwenye mtaji wa kampuni ili mamlaka ipate uwezo wa kujiendesha kwa faida na hatimaye kwa kutumia mapato yake iweze kulipa madeni hayo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania, Serikali imekuwa ikiweka fedha za miradi ya maendeleo katika bajeti ya Serikali kila mwaka kusaidia *TAZARA* ingawa fedha hizo ni ndogo kutokana na ufinyu wa bajeti. Pamoja na mchango

huo Serikali za Zambia na Tanzania kila baada ya miaka miwili zimekuwa zikiingia makubaliano na mikataba ya mikopo nafuu ya kiufundi na Serikali ya China ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia sana uendeshaji wa mamlaka hii.

Katika mwaka huu wa fedha 2009/2010 mkataba wa 14 unatarajiwa kuwekwa saini na Mawaziri wa Uchukuzi wa Zambia na Tanzania na kwa upande wa China Waziri atakayetuliwa na nchi hiyo. Aidha, Serikali za Tanzania na Zambia zinatafuta njia bora ya kuongeza mtaji kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kuendesha shughuli za *TAZARA*. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 23 (2) kinasema hivi "kila mtu anayefanya anastahili kupata malipo ya haki". Wafanyakazi hawa waliostaafu, walioachakazi na waliofariki wote walifanyakazi kwa mujibu wa Katiba na walistahili kwa kweli wapate malipo. Wafanyakazi hawa wamestaafu wengi kuanzia mwaka 2005 na wengine wamefariki tangu mwaka 2005 hawajalipwa haki zao.

(a) Je, kutokuwalipa haki zao kwa muda mrefu wakati walitumikia nchi yao vizuri sana si kuwanyima haki yao na uhuru wa kuishi Serikali inasema nini katika hilo?

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali/*TAZARA* imekuwa inasaini *protocols* hizi tangu miaka 1990 lakini hadi leo bado *TAZARA* ina hali mbaya. Tunaambiwa kwamba Serikali za nchi hizi mbili zitasaidia *protocol* ya 14 mwaka huu. Serikali inawahakikishia wafanyakazi wa *TAZARA* na Watanzania kwamba baada ya kusaini *protocol* ya 14 hali ya *TAZARA* na Wafanyakazi itaimarika na kuwa nzuri?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na yeye kuwa kifungu cha Katiba ambacho Mheshimiwa Mbunge amekisoma kwamba kila mtu ana haki ya kulipwa kutokana na shughuli anazozifanya.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kuanzia mwaka 2004/2007 wafanyakazi 1422 wa *TAZARA* wamelipwa na wamelipwa kutokana na kuuaza mali zilizokuwepo hii ni kwamba Serikali haijakaa kimya kwamba haikuwalipa wafanyakazi, imewalipa. Lakini kwa sababu ni wengi na wote waliajiriwa kwa pamoja na huenda wakastaafu kwa pamoja ilikuwa ni vigumu kuwalipa wote kwa pamoja.

Juhudi zinaendelea. Kuanzia 2008 Aprili, mpaka Juni, 2009 TAZARA iliendelea kulipa wastaafu bila hata kuuza hizo *asserts* zake walizokuwa nazo. Mwaka huu 2009/2010 tunategemea *TAZARA* itawalipa wastaafu wake bilioni 1.8 kwamba hizi ni juhudi za Serikali inazofanya katika kuona inasawazisha matatizo ya wafanyakazi wake. lakini wastaafu si wa *TAZARA* tu wako wengi hivi sasa hawajalipwa ni kutokana na ufinyu wa bajeti na mapato Seriklai ni machache, lakini jitida zinafanyika na zitaendelea kufanyika kuona wastaafu wote wanalipwa haki zao.

Mheshimiwa Spika, pili *protocols* kweli tunaingia na China na hivi sasa tunaingia *protocol* ya 14. Lakini *protocol* za 14 zinatusaidia tu lakini siyo ambayo ndiyo mwisho itatusaidia sisi kuona *TAZARA* inafufuka. Siku zote tunatakiwa tuweke *management*

inayoshughulika vizuri ili shughuli hizi ziweze kufanyika vizuri ndiyo maana huko nyuma mashirika mengi tuliyokuwa nayo yalikufa ni kwa sababu nafikiri *management* tulizoziweka hazikuwa udhibiti vizuri.

Hivi sasa *TAZARA* inajitahidi sana na imeingia mikataba na wateja wake wakubwa wanalipa *upfront* kwa ajili ya kutengeneza mabehewa hawakukaa tu kusubiri kwamba Serikali iwape ruzuku waweze kuendesha. Juhudi zinafanywa na sekta ya miundombinu *infrastructure development sector* kunawekwa fedha kwa ajili ya kusaidia *TAZARA*.

Ni mategemeo yangu kwamba baada ya kufanya utafiti wa kuona ni kiasi gani kinadaiwa Serikali hizi mbili kwa sababu hii *TAZARA* ni ya nchi mbili zitakaa na kubuni mbinu namna gani wataweza kumaliza tatizo hili la *TAZARA* na namna gani wanaweza kuifufua *TAZARA* kwa kutumia sekta binafsi. (*Makofi*)

Na. 297

**Upatikanaji wa Umeme Wilayani Karagwe**

**MHE. GOSBERT G. BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais alipotembelea Wilaya ya Karagwe mwaka 2008 aliwahakikishia wananchi juu ya upatikanaji wa umeme vijijini hususani sehemu za Bugene, Bisheshe, Nyakayanja, Ihanda, Rwabwere, Kamagambo, Nyakagoyagoye hadi Nyakaiga na sehemu za Kayanga, Ndama, Rukak, Nyabwegira, Kikilo, Ruyanga hadi Rwambaizi na kwa kuwa katika bajeti ya mwaka 2008/2009 Serikali imeahidi kutekeleza ahadi hiyo kabla ya mwaka 2010.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** ajibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Rais mwezi Januari, 2008 akiwa Jimboni Karagwe aliwahakikishia wananchi juu ya upatikanaji wa umeme vijijini hususan vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge katika swali lake. Napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa ahadi hiyo ilianza kutekelezwa tangu mwezi Aprili, 2008 kwa kuanza kutekeleza miradi ya kupeleka umeme katika vijiji vya Kayanga, Ndama (Rwambaizi), Ruhita, Nyabwigira na Kakilo.

Tayari nguzo za umeme zimeshakwenda kwenye vijiji hivyo. Gharama za utekelezaji wa miradi hiyo, ambayo inategemewa kukamilisha mwakani, 2010, ni shilingi 142,013,673.82 chini ya ufadhili wa *TANESCO*. Vijiji vya Busheshe, Nyaishozi na Ihembe vitapatiwa umeme chini ya ufadhili wa wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) kwa gharama ya shilingi 200,000,000. Sasa hivi taratibu za kuvipatia umeme vijijii hivyo iko katika hatua ya zabuni kama tulivyosema jana hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine yaliyotajwa ya Bisheshe, Nyakayanga, Nyaishozi hadi Ihembe yameombewa fedha kutoka wakala wa Nishati Vijiji ili usambazaji wa umeme uweze kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa Nishati kwa wakazi wa maeneo haya, Serikali ya Uganda ili kuhakikisha kuwa umeme unapatikana kutoka nchi hiyo ya jirani kutokea chanzo cha umeme wa Kikagati. Taratibu za msingi za kujenga miundombinu ya kusambaza umeme miji ya Murongo na Mtukula zinaendelea kwa ajili ya kupokea umeme kutoka Uganda. Taratibu hizi zinahusisha Wizara, *TANESCO, REA* na *EWURA*. Kwa nguvu hiyo namuomba Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja tuendelee kushirikiana na Wizara yangu ili kukamilisha kazi iliyobaki ya kusafirisha umeme huo kwenda kwenye vijiji tulivyotaja hapo juu. Kama tulivyosema wakati tukihitimisha maelezo ya makadirio na matumizi ya Wizara jana kazi hizi zitatekelezwa na *TANESCO* kwa ufadhili wa *REA* kadri fedha itakavyopatikana. Aidha, kwa sasa *TANESCO* inatafuta mkandarasi wa ujenzi wa njia hizo za umeme.

**MHE. GOSBERT G. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana na hasa kuwahakikishia wananchi wa Karagwe kwamba umeme unakwenda kupitia Nyaishozi hadi Ihembe. Lakini katika majibu yake sikusikia umeme wa vijiji vya Ihanda, Kamagambo, Nyakagoyagoye pamoja na Nyakaiga ambavyo nimeuliza katika swali la msingi. Ila hapa katika majibu yake amesema kwamba utakwenda kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

(a) Je, Serikali hizo fedha zitakuwa zinapatikana pengine kabla ya mwaka 2010?

(b) Wananchi wa Vijiji vya Bisheshe, Nyaishozi pamoja na Ihemba wamefarijika sana kupata taarifa hizi. Nilitaka nimuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, je, anaweza kuwatangazia wananchi wa vijiji hivyo waanze kufanya wiring na kununua vifaa vya umeme kwa maandalizi ya kupokea umeme huo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa kwamba usambazaji wa umeme utafanyika kwa awamu kwa kuanzia vijiji vya Ihanda, Rwabere, Kamagambo na Nyakagoyagoye hadi Nyakaiga kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

Sasa tunachosisitiza ni kwamba fedha hizi tunatarajia zitoke wakala wa Nishati Vijijini na wakala wa Nishati Vijijini kwa awali tunapeleka katika maeneo hayo milioni 200,000,000.

Lakini kwa sababu ya mfumo ambao tunajitengenezea wa kukusanya fedha za ziada kwa ajili ya wakala wa Nishati Vijijini, mimi ninamuomba Mheshimiwa Blandes tuendelee kushirikiana kwa sababu ni mradi ambao tayari umeshapata hata michoro ya awali kwa hiyo, ni mradi ambao unatekelezeka. (*Makofi*)

Hii ya pili huu umeme wa kwenda Nyaishozi Busheshe, Ihemba tayari milioni 200,000,000 zimekwenda. Mheshimiwa Blandes nakuomba nipe nafasi nikutane na *REA* na *TANESCO* ili nijue kama kwa milioni 200,000,000 hizi ni maeneo gani yale ambayo tayari watu waanze kufunga bulb na kwa pamoja tutakwenda kuwasha umeme huo wa Nyaishozi. (*Makofi*)

Swali lake la pili la kuhusu kulipa riba nadhani baada ya kwamba kesi imekwisha Mahakamani watu watakaa na kuangalia ni vipi mkulima huyu na wafanyakazi hawa wanaweza kulipwa kitu ambacho kinaridhisha kwa sababu kusema kweli fedha hiyo, kama wangekuwa wameshapewa sasa hivi wangekuwa wameshaifanyia kazi kwa kiasi kikubwa.

Mwisho, napenda kumpongeza Mheshimiwa William Shellukindo kwa kazi kubwa anayoifanya kusema kweli ya kutetea wafanyakazi na wakulima wa chai na siyo shamba tu hili lakini pia na mashamba mengine ya chai nzima. Hongera sana Mheshimiwa Shellukindo. (*Makofi*)

Na. 293

**Mfumo Maalum wa Kuwezesha Jamii za Wafugaji na Wakulima – Manyara**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Kwa kuwa jamii za wafugaji Mkoani Manyara hazikopesheki kwa kutumia mifumo ya sasa ya kutumia *SACCOS* na vyombo vingine vya fedha kutokana na hali zao duni za maisha na kwa kuwa mfumo wa sasa wa uhamasishaji jamii kwa njia ya luninga (*television*), radio na magazeti haujawafikia na hivyo awamu zote za uwezeshaji wananchi hazijafahamika vizuri kwa jamii hizo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani kuhusu kuwasaidia walengwa hao?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa kuna haja ya kubuni mfumo tofauti wa kuziwezesha jamii hizo kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge Viti Maalum Manyara, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua matatizo yanayozikabili jamii zinazoishi maisha ya kuhama hama kama vile wafugaji. Serikali inaendelea kuwapalekea elimu, kuwashauri na kuwahimiza kuwa na makazi ya kudumu kwa kuwa inakuwa vigumu kutekeleza mipango ya maendeleo katika hali na staili za maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jukumu na nia ya Serikali yetu ya kuinua viwango vya elimu kwa wananchi wote, hasa wa maeneo ya vijijini uzoefu umeonyesha ni vigumu kuwahudumia vizuri wananchi wanaoishi maisha ya kuhamahama.

Hivyo Serikali inandelea kusisitiza umuhimu wa jamii hizi kuanza kuendesha shughuli zao za ufugaji kwenye makazi ya kudumu ili kuweza kuendesha ufugaji ulio bora na wa kisasa. Pia itakuwa rahisi kwa Serikali kutoa huduma zinge za kijamii kama, afya, maji na hata kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu ya kuendeleza na kuboresha maisha yao.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaamini kwamba njia kuu ya kusaidia jamii ya wafugaji ni kuwapa elimu itakavyowawezesha kutambua umuhimu wa kubadili utamaduni wa kuhamahama na kuanzisha makazi ya kuduma. Tutakapokuwa tumefaulu katika azma hii, mikakati mipya stahiki itabuniwa ambayo itaongeza kasi na kiasi cha uwezeshaji wa jamii hizi kiuchumi.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala zima la kuwawezesha wananchi kiuchumi haikufanywa kwa kuzingatia kufanya utafiti wa kubaini mahitaji ya lazima ama *immediate needs* za wananchi na jamii mbalimbali hususan wananchi kama Wahdazabe na Wabarbar walioko Mkoani Manyara na kwa kuwa msingi wa maendeleo siyo tu kuwapa watu fedha ama kuwawezesha kuwapa mikopo bali hata kuwawezesha kuwajengea nyumba bora, kuwawezesha kuwa na afya bora na kuwapa elimu.

(a) Je, Serikali sasa kwa awamu inayofuata ya uwezeshaji wananchi kiumi itakuwa tayari kuangalia mahitaji ya lazima ama yale ya wakati huo kuzingatia kwamba wananchi wanafurahia uwezeshwaji pale ambapo wanawezeshwa kwa mahitaji ya wakati huo?

(b)Kwa kuwa wafugaji walioko Mkoa Manyara wana idadi kubwa ya Mifugo na kwa hiyo, wana fedha nyingi lakini bado hali yao ni duni na bado hawakopesheki kwa maana ya kwamba hawajawa na uwezo ama uelewa wa kutumia fedha hizo za mifugo wanayohoji vizuri. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kuwapa wafugaji soko la uhakika na kuwawezesha kuwapa pembejeo za mifugo kama madawa na mabwawa na majosho ni uhamasisha tosha wa kuwawezesha wananchi hawa kiuchumi. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusu utafiti ni kweli nakiri kwamba mpanga huo anaozungumzia Mheshimiwa Mbunge wa kuwawezesha wananchi kiuchumi haukufanyiwa utafiti mahususi kwa ajili ya mpango ule isipokuwa Serikali ilikuwa inafahamu na inafahamu mahitaji ya wananchi wake kiuchumi. Ninakubaliana naye kwamba kwa sababu jamii zetu nchini ni tofauti kuna haja ya kufanya utafiti anaozungumzia ili kubaini mahitaji halisi ya wakati tutakaokuwa tunatekeleza ile mipango maana yake kuwawezesha wananchi kiuchumi ni sehemu tu moja ya mpango mpana zaidi wa kuboresha maisha ya wananchi kwa ujumla.

Swali lake la pili, ninakubaliana naye kwamba ni kweli inawezekana kwamba mahitaji ya wananchi ambao wako kwenye maeneo ya ufugaji siyo lazima ni fedha maana ni dhahiri kwamba kwa mifugo yao wana pesa nyingi na ndiyo sababu hata dhana ile ya thamani kwa wafugaji hawa inaweza kuwa tofauti na sisi. Kwa hiyo, vyama vya akiba na Mikopo vikashindwa kuanzishwa na kuboreka. Kwa hiyo, nakubaliana naye. Lakini la msingi hapa ni kwanza ni elimu, pili ni kuwashauri na kuwaomba waone kwamba kuna haja sasa ya kubadilisha wanavyotazama maisha ya kuhama hama.

Lakini vile vile tukumbuke kwamba hapa tunaweza kuwa tunakabiliana vile vile na tatizo la mila, desturi na tamaduni za jamii ya wafugaji.

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa fedha pekee ambazo wafugaji wafugaji wanaweza wakapata mkopo ni hizi fedha za JK lakini fedha hizi zimekuwa za siasa, za upendeleo na baadhi ya majimbo hawajapata hizo fedha mpaka leo. Wabunge wengine wanahukumiwa kwa ajili ya hizi fedha kwa sababu tulikwenda kusema kwamba hizi fedha zipo na Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza leo kutuambia Wabunge wanaotoka katika maeneo ambayo hayajapata hizi fedha kwamba msisubiri hizo fedha kwa sababu hazipo ili tuweze kwenda kuwaambia wananchi kwamba msiwe na matumaini tena na hizo fedha kwa Majimbo yote pamoja na Jimbo la Longido ambao hawakupata hizo fedha? Naomba jibu. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Michael Lekule Laizer swali lake zuri na lakini kali kama ifuatavyo:-

Kwanza sikubaliani naye sana kwamba kuna uhusiano wowote katika mpango huu wa kuwasaidia wananchi kiuchumi siyo mpango wa kisiasa. Lakini la pili sikubaliana naye kwamba kuna upandeleo wowote.

Maana yake kama tunavyokumbuka bilioni 21 hizi zilipotolewa ilitamkwa rasmi na Serikali kwamba kila Mkoa katika Mikoa yetu 21 ingepata shilingi bilioni 1 za kuanzia na Zanzibar kule Mikoa yao mitano kila moja ungepata milioni 100 isipokuwa Mkoa wa Magharibi ambao ungepata milioni 200.

Jambo hilo limetendeka. Lakini la pili nikiri kwamba mpango huu ulipoanza mwanzo kuna Wilaya ambazo hazikufikiwa. Lakini sababu ya msingi ilikuwa kwamba vyombo vyetu vya fedha vikuu *NMB* na *CRDB* havikuwa na matawi kwenye zile Wilaya na ndiyo sababu Serikali ikaamua kwamba itapeleka fedha zingine kupitia vyombo vingine vya fedha na kama tutakumbuka ziliteuliwa taasisi14 za fedha ambazo zimefanyakazi nzuri sana. Kwa bahati mbaya Mheshimiwa Mbunge anakotoka Longido bado mpaka sasa hivi nakiri hawajafikiwa na mpango huu.

Lakini sababu ya msingi ni kwamba pale shilingi 100 zilipotolewa kwenye taasisi ya fedha ambayo ingepeleka fedha hizi kwa ajili kwa mikopo kwa wananchi wa Longido taasisi ile baadaye ilirudi nyuma na haikuendelea na mpango ule.

Lakini Serikali bado imeendelea kujitahidi kutafuta taasisi nyingine ya fedha ambayo itakuwa tayari kuwapelekea wananchi wa Longido mikopo hii chini ya mpango huu na sasa tumepata shirika la *Pride* na shirika la *Pride* limetengewa shilingi 250 milioni kwa ajili ya Longido na kilichosalia sasa ni kukamilisha mikataba kati ya Serikali na shirika hili ili mpango huo uendelezwe kwenye Wilaya ya Longido. (*Makofi*)

Na. 294

**Makato Kwenye Malipo ya Pensheni**

**MHE. MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Kwa kuwa wastaafu hulipwa pensheni zao kupitia Benki ya *NMB* na kwamba hukatwa gharama za benki kwenye malipo hayo:-

Je, Serikali haioni kwamba kipato hicho ni kidogo na kukipunguza ni sawa na kuwanyanyasa wahusika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa siyo *NMB* pekee ambayo hutumika kwa hotuba huduma za kuwalipa wastaafu

pensheni zao, ziko pia benki nyingine zinazotumika kutegemea na ukaribu pamoja na mstaafu mwenyewe kuwa na akaunti katika benki nyingine mbali na *NMB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa pensheni wanayolipwa wastaafu kupitia akaunti zao za benki hukatwa gharama za huduma za kibenki. Hali hiyo inatokana kwamba benki kukata gharama kunapunguza kipato cha wastaafu.

Hata hivyo, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, benki hutoza gharama pale inapotoa huduma kwa mtu yoyote ikiwa ni eneo moja la mapato ya benki. Njia pekee ya kuwasaidia wastaafu ni kuongeza kiwango cha pensheni kila baada ya muda. Kwa kuwa huu ni wajibu wa Serikali, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itakuwa ikiongeza kiwango cha pensheni kila baada ya muda, kutegemeana na hali ya mapato ya Serikali yatakavyokuwa.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge, asaidiane na Serikali na ninaamini ana uwezo huo katika kuwaelimisha wastaafu juu ya matumizi ya benki, kwani ni njia salama na huchukua muda mfupi mstaafu kuweza kupata pensheni yake.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuishukuru Serikali kwa kweli kuweza kulijali kundi hili la wastaafu kwa sasa hivi na hasa hasa kulingana na jibu la Naibu Waziri jinsi gani alivyoweza kulijibu swali langu vizuri.

Kwa kuwa Serikali inakiri wazi kwamba kila wakati Serikali itakapokuwa inaongeza kipato chake basi na wastaafu watakuwa wanafikiria kuongezwa kipato chao. Je, Serikali haioni sasa hivi ni wakati muafaka wa kuanza safari ya kuwafikiria wastaafu hawa nao wakawaweka katika kiwango cha kima cha chini cha kipata cha nchi hii? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kuinua hali ya wastaafu ili iweze kwenda sambamba na maisha yalivyo kwa wakati ule.

Lakini kama nilivyosema kwamba kila mapato ya Serikali yatakapoongezeka Serikali nayo itaongeza kipato cha wastaafu na hiyo nia na lengo ambalo Mheshimiwa Mama Hewa anawaombea wastaafu tutafikia wakati muafaka Serikali nayo itafikia hapo. (*Makofi*)

Na. 295

### Kokoto Imara za Ujenzi wa Barabara

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa barabara imara unategemea pia uimara wa Kokoto zinazotumika kuchanganya lami.

(a) Je, ni maeneo gani katika nchi yetu yanayotoa kokoto zilizo imara na bora kwa ujenzi wa barabara?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa maeneo ya Kiwira Wilayani Rungwe yanatoa kokoto imara?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu wa Wizara yangu katika kazi za usanifu wa ujenzi wa barabara unaonyesha kwamba karibu maeneo mengi hapa nchini yana miamba inayofaa kwa ajili ya kutoa kokoto zilizo imara na bora kwa ujenzi wa barabara. Hii ni kuondoa ukanda wa Pwani ambao una miamba ya chokaa. Kwa sehemu kubwa kokoto zitokanazo na miamba ya chokaa kwenye ukanda huo zina uimara na ubora ulio chini ya viwango vinavyohitajika kwa ujenzi wa barabara. Tatizo la ukosefu wa kokoto kwa kazi za ujenzi wa barabara kwenye baadhi ya Mikoa linatokana na kutokuwepo kwa makandarasi wanaojishughulisha na upasuaji wa miamba kwa ajili ya kokoto kwenye Mikoa hiyo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafahamu maeneo ya Kiwira Wilayani Rungwe kuwa ni moja ya maeneo yanayotoa kokoto bora na imara. Na ndio maana Serikali iliweza kuendesha mtambo wa kusaga kokoto kwenye eneo hilo tangu mwaka 1984 na kuanzia mwaka 2007/2008 Serikali iliamua kuendesha mtambo huo na mingine na aina yake kwa kutumia makandarasi.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika majibu ya msingi Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba ukanda wa Pwani una miamba aina ya chokaa ambayo inatoa kokoto ambazo ni hafifu. Je, anaweza akalieleza Bunge lako ni kwa nini basi mashine ya kusaga kokoto iliyokuwa Kiwira iliamua kuhamishiwa maeneo ya Pwani bila kuutarifu uongozi wa Mkoa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (k.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtambo huu wa kusaga kokoto uliokuwa Kiwira ulikodishwa kwa kampuni ya *Nambo* investment tokea

mwaka 2007 kwa mkataba baina *Nambo* na *TEMESA*. Kwa sababu walikubaliana wenyewe hatuoni kwamba kulikuwa ni lazima tuuambie Mkoa kwa sababu ni ukodishaji ambao tulikubaliana kimsingi kwamba zile *non core asserts* ambazo hazitumiki zinaweza kukodishwa kwa mtu yeyote.

Ndiyo maana si mtambo huu tu, iko na mitambo mingine ambayo ilikuwa inamilikiwa *TRC* nayo pia ilikodishwa na hakukuwa kwamba kuna ulazima Mkoa uarifikiwe. Hivi sasa mtambo unafanyakazi Pwani, vizuri. Lakini ulikuwa uko katika matengenezo kwa muda mrefu umeanza mwaka 2008 matengenezo alikuwa anafanya mwenyewe ambaye amepewa ule mtambo. Kweli mtambo uligharimu hela nyingi sana mpaka kufika kuanza kufanya shughuli hizi za kusaga kokoto kule Pwani. (*Makofi*)

Na. 296

**Hali Mbaya ya Kiuchumi ya Shirika la Reli – TAZARA**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa mamlaka ya Reli ya Uhuru *TAZARA* inakubaliwa na hali mbaya kiuchumi kiasi cha kushindwa kutimiza wajibu wake sawasawa ikiwa ni pamoja na kutokulipa mafao kwa wastaafu, wanaoacha kazi na wanaofariki:-

(a) Je, hadi sasa ni watumishi wangapi waliostaafu, walioacha kazi na waliofariki dunia ambao bado hawajalipwa haki zao?

(b) Je, Watumishi hao kwa ujumla wao wanadai kiasi gani cha fedha na ni hatua gani za dharura zinachukuliwa kulipa fedha hizo?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani za dharura za kuinusuru *TAZARA*?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU):** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wengi wa *TAZARA* waliajiriwa katika kipindi kimoja wakati mamlaka ilipoanzishwa mwaka 1975.

Hivi sasa *TAZARA* inakabiliwa na tatizo la wimbi la wafanyakazi wengi wanaostaafu kwa wakati mmoja. Idadi ya watumishi waliostaafu *TAZARA* kwa upande wa Tanzania ni 1,077 waliokufa ni 623 na walioacha kazi ni 7 ambao hawajalipwa haki zao.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na idadi ya wastaafu iliyotajwa hapo juu, mamlaka inadaiwa kiasi cha *USD* milioni 20.7 kwa wafanyakazi waliokwishastaafu na *USD 30.9* kwa wafanyakazi ambao bado wako kazini. Kwa ujumla *TAZARA* inadaiwa USD milioni 51.6 kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi na wastaafu wote. Hata hivyo wadhibiti na wahakiki wakuu wa fedha za Serikali wa nchi za Tanzania na Zambia wameombwa kuhakiki madeni yote ya *TAZARA* ikiwa ni pamoja na pensheni za wafanyakazi ili kubaini kiasi halisi ambacho *TAZARA* inadaiwa na wafanyakazi na wastaafu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za dharura zilizochukuliwa awali ilikuwa ni pamoja na kuuza rasilimali za mamlaka ya *TAZARA* na kulipa madai hayo ya wafanyakazi. Hata hivyo kutokana na ukubwa wa deni ambalo *TAZARA* inadaiwa na wafanyakazi, hatua hiyo ya dharura haikuweza kutatua tatizo a kulipa deni lote.

Kwa hiyo, Serikali za Tanzania na Zambia zimeishauri *TAZARA* itafute fedha hizo kutoka taasisi za kifedha wakati Serikali mbili hizi za fedha za kuwekeza kwenye mtaji wa kampuni ili mamlaka ipate uwezo wa kujiendesha kwa faida na hatimaye kwa kutumia mapato yake iweze kulipa madeni hayo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania, Serikali imekuwa ikiweka fedha za miradi ya maendeleo katika bajeti ya Serikali kila mwaka kusaidia *TAZARA* ingawa fedha hizo ni ndogo kutokana na ufinyu wa bajeti. Pamoja na mchango huo Serikali za Zambia na Tanzania kila baada ya miaka miwili zimekuwa zikiingia makubaliano na mikataba ya mikopo nafuu ya kiufundi na Serikali ya China ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia sana uendeshaji wa mamlaka hii.

Katika mwaka huu wa fedha 2009/2010 mkataba wa 14 unatarajiwa kuwekwa saini na Mawaziri wa Uchukuzi wa Zambia na Tanzania na kwa upande wa China Waziri atakayetuliwa na nchi hiyo. Aidha, Serikali za Tanzania na Zambia zinatafuta njia bora ya kuongeza mtaji kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kuendesha shughuli za *TAZARA*. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 23 (2) kinasema hivi "kila mtu anayefanya anastahili kupata malipo ya haki". Wafanyakazi hawa waliostaafu, walioachakazi na waliofariki wote walifanyakazi kwa mujibu wa Katiba na walistahili kwa kweli wapate malipo. Wafanyakazi hawa wamestaafu wengi kuanzia mwaka 2005 na wengine wamefariki tangu mwaka 2005 hawajalipwa haki zao.

(a) Je, kutokuwalipa haki zao kwa muda mrefu wakati walitumikia nchi yao vizuri sana si kuwanyima haki yao na uhuru wa kuishi Serikali inasema nini katika hilo?

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali/*TAZARA* imekuwa inasaini *protocols* hizi tangu miaka 1990 lakini hadi leo bado *TAZARA* ina hali mbaya. Tunaambiwa kwamba Serikali za nchi hizi mbili zitasaidia *protocol* ya 14 mwaka huu. Serikali inawahakikishia wafanyakazi wa *TAZARA* na Watanzania kwamba baada ya kusaini *protocol* ya 14 hali ya *TAZARA* na Wafanyakazi itaimarika na kuwa nzuri?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na yeye kuwa kifungu cha Katiba ambacho Mheshimiwa Mbunge amekisoma kwamba kila mtu ana haki ya kulipwa kutokana na shughuli anazozifanya.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kuanzia mwaka 2004/2007 wafanyakazi 1422 wa *TAZARA* wamelipwa na wamelipwa kutokana na kuuaza mali zilizokuwepo hii ni kwamba Serikali haijakaa kimya kwamba haikuwalipa wafanyakazi, imewalipa. Lakini kwa sababu ni wengi na wote waliajiriwa kwa pamoja na huenda wakastaafu kwa pamoja ilikuwa ni vigumu kuwalipa wote kwa pamoja.

Juhudi zinaendelea. Kuanzia 2008 Aprili, mpaka Juni, 2009 TAZARA iliendelea kulipa wastaafu bila hata kuuza hizo *asserts* zake walizokuwa nazo. Mwaka huu 2009/2010 tunategemea *TAZARA* itawalipa wastaafu wake bilioni 1.8 kwamba hizi ni juhudi za Serikali inazofanya katika kuona inasawazisha matatizo ya wafanyakazi wake. lakini wastaafu si wa *TAZARA* tu wako wengi hivi sasa hawajalipwa ni kutokana na ufinyu wa bajeti na mapato Seriklai ni machache, lakini jitida zinafanyika na zitaendelea kufanyika kuona wastaafu wote wanalipwa haki zao.

Mheshimiwa Spika, pili *protocols* kweli tunaingia na China na hivi sasa tunaingia *protocol* ya 14. Lakini *protocol* za 14 zinatusaidia tu lakini siyo ambayo ndiyo mwisho itatusaidia sisi kuona *TAZARA* inafufuka. Siku zote tunatakiwa tuweke *management* inayoshughulika vizuri ili shughuli hizi ziweze kufanyika vizuri ndiyo maana huko nyuma mashirika mengi tuliyokuwa nayo yalikufa ni kwa sababu nafikiri *management* tulizoziweka hazikuwa udhibiti vizuri.

Hivi sasa *TAZARA* inajitahidi sana na imeingia mikataba na wateja wake wakubwa wanalipa *upfront* kwa ajili ya kutengeneza mabehewa hawakukaa tu kusubiri kwamba Serikali iwape ruzuku waweze kuendesha. Juhudi zinafanywa na sekta ya miundombinu *infrastructure development sector* kunawekwa fedha kwa ajili ya kusaidia *TAZARA*.

Ni mategemeo yangu kwamba baada ya kufanya utafiti wa kuona ni kiasi gani kinadaiwa Serikali hizi mbili kwa sababu hii *TAZARA* ni ya nchi mbili zitakaa na kubuni mbinu namna gani wataweza kumaliza tatizo hili la *TAZARA* na namna gani wanaweza kuifufua *TAZARA* kwa kutumia sekta binafsi. (*Makofi*)

Na. 297

**Upatikanaji wa Umeme Wilayani Karagwe**

**MHE. GOSBERT G. BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais alipotembelea Wilaya ya Karagwe mwaka 2008 aliwahakikishia wananchi juu ya upatikanaji wa umeme vijijini hususani sehemu za Bugene, Bisheshe, Nyakayanja, Ihanda, Rwabwere, Kamagambo, Nyakagoyagoye hadi Nyakaiga na sehemu za Kayanga, Ndama, Rukak, Nyabwegira, Kikilo, Ruyanga hadi Rwambaizi na kwa kuwa katika bajeti ya mwaka 2008/2009 Serikali imeahidi kutekeleza ahadi hiyo kabla ya mwaka 2010.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** ajibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Rais mwezi Januari, 2008 akiwa Jimboni Karagwe aliwahakikishia wananchi juu ya upatikanaji wa umeme vijijini hususan vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge katika swali lake. Napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa ahadi hiyo ilianza kutekelezwa tangu mwezi Aprili, 2008 kwa kuanza kutekeleza miradi ya kupeleka umeme katika vijiji vya Kayanga, Ndama (Rwambaizi), Ruhita, Nyabwigira na Kakilo.

Tayari nguzo za umeme zimeshakwenda kwenye vijiji hivyo. Gharama za utekelezaji wa miradi hiyo, ambayo inategemewa kukamilisha mwakani, 2010, ni shilingi 142,013,673.82 chini ya ufadhili wa *TANESCO*. Vijiji vya Busheshe, Nyaishozi na Ihembe vitapatiwa umeme chini ya ufadhili wa wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) kwa gharama ya shilingi 200,000,000. Sasa hivi taratibu za kuvipatia umeme vijijii hivyo iko katika hatua ya zabuni kama tulivyosema jana hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine yaliyotajwa ya Bisheshe, Nyakayanga, Nyaishozi hadi Ihembe yameombewa fedha kutoka wakala wa Nishati Vijiji ili usambazaji wa umeme uweze kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa Nishati kwa wakazi wa maeneo haya, Serikali ya Uganda ili kuhakikisha kuwa umeme unapatikana kutoka nchi hiyo ya jirani kutokea chanzo cha umeme wa Kikagati. Taratibu za msingi za kujenga miundombinu ya kusambaza umeme miji ya Murongo na Mtukula zinaendelea kwa ajili ya kupokea umeme kutoka Uganda. Taratibu hizi zinahusisha Wizara, *TANESCO*, *REA* na *EWURA*. Kwa nguvu hiyo namuomba Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja tuendelee kushirikiana na Wizara yangu ili kukamilisha kazi iliyobaki ya kusafirisha umeme huo kwenda kwenye vijiji tulivyotaja hapo juu. Kama tulivyosema wakati tukihitimisha maelezo ya makadirio na matumizi ya Wizara jana kazi hizi zitatekelezwa na *TANESCO* kwa ufadhili wa *REA* kadri fedha itakavyopatikana. Aidha, kwa sasa *TANESCO* inatafuta mkandarasi wa ujenzi wa njia hizo za umeme.

**MHE. GOSBERT G. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana na hasa kuwahakikishia wananchi wa Karagwe kwamba umeme unakwenda kupitia Nyaishozi hadi Ihembe. Lakini katika majibu yake sikusikia umeme wa vijiji vya Ihanda, Kamagambo, Nyakagoyagoye pamoja na Nyakaiga ambavyo nimeuliza katika swali la msingi. Ila hapa katika majibu yake amesema kwamba utakwenda kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

(a) Je, Serikali hizo fedha zitakuwa zinapatikana pengine kabla ya mwaka 2010?

(b) Wananchi wa Vijiji vya Bisheshe, Nyaishozi pamoja na Ihemba wamefarijika sana kupata taarifa hizi. Nilitaka nimuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, je, anaweza kuwatangazia wananchi wa vijiji hivyo waanze kufanya wiring na kununua vifaa vya umeme kwa maandalizi ya kupokea umeme huo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa kwamba usambazaji wa umeme utafanyika kwa awamu kwa kuanzia vijiji vya Ihanda, Rwabere, Kamagambo na Nyakagoyagoye hadi Nyakaiga kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

Sasa tunachosisitiza ni kwamba fedha hizi tunatarajia zitoke wakala wa Nishati Vijijini na wakala wa Nishati Vijijini kwa awali tunapeleka katika maeneo hayo milioni 200,000,000.

Lakini kwa sababu ya mfumo ambao tunajitengenezea wa kukusanya fedha za ziada kwa ajili ya wakala wa Nishati Vijijini, mimi ninamuomba Mheshimiwa Blandes tuendelee kushirikiana kwa sababu ni mradi ambao tayari umeshapata hata michoro ya awali kwa hiyo, ni mradi ambao unatekelezeka. (*Makofi*)

Hii ya pili huu umeme wa kwenda Nyaishozi Busheshe, Ihemba tayari milioni 200,000,000 zimekwenda. Mheshimiwa Blandes nakuomba nipe nafasi nikutane na *REA* na *TANESCO* ili nijue kama kwa milioni 200,000,000 hizi ni maeneo gani yale ambayo tayari watu waanze kufunga bulb na kwa pamoja tutakwenda kuwasha umeme huo wa Nyaishozi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Maswali ya leo yote yameulizwa na Wabunge wa CCM kwa jinsi hiyo angalau nitoe swali moja la nyongeza kwa Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na pia umegundua hilo, matatizo ya umeme ya vijiji vya Wilaya ya Karagwe hayana tofauti sana na vijiji vya Wilaya ya Kigoma na hasa hasa maeneo ya ukanda wa ziwa na hivi sasa

baadhi ya Mashirika ya Umma kama Mamlaka ya Bandari na *NSSF* wameanza kwa nguvu sana kuwekeza katika baadhi ya maeneo ya Kigoma Kaskazini.

Waziri atakubaliana na ombi la wakazi wa vijiji vya Kigali, Mtanga, Mwamgongo mpaka Kagunga kuhakikisha kwamba *TANESCO* wanafanya upembuzi kuangalia uwezekano wa kupeleka umeme katika vijiji hivyo vilivyoko mpakani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikubaliane nae moja, nikatae moja. Moja ni kwamba matatizo ya Karagwe na Kigoma sasa hivi Karagwe *at least* umeme unatoka Kigoma kwa hiyo unafika, tatizo ni usambazaji. Lakini tatizo la Kigoma ni kubwa zaidi kwa sababu hata Kigoma yenyewe uzalishaji wa umeme ni tatizo.

Kwa hiyo nakubaliana nae kwamba, kwanza tukamilishe tatizo la uzalishaji wa umeme wa Kigoma na aidha pia nakubaliana nae kwamba *TPA*, *NSSF* kwa mazingira ya kiuchumi ya Kigoma mashirika mengi yanakwenda lakini sasa tatizo hili la umeme tumelisema jana, tunaendelea kulisisitiza na nakubaliana na wewe kwamba kuseema ukweli umeme ukifika unatakiwa usambazwa mpaka Kasulu kwa Mhehsimiwa Daniel Nsanzugwanko na maeneo mengine.

Kwa sababu maeneo yote haya ni maeneo kusema kweli kwamba *potentially* ni maeneo ambayo yana uwezekano wa uzalishaji mkubwa wa umeme, kwa hiyo nakubaliana na wewe kwamba tutakapomaliza tatizo la uzalishaji, tuhakikishe kwamba umeme huwo unasambazwa mpaka Magongo, Kagunga na mpaka maeneo ya Kasulu.

Na. 298

**Matumizi ya Gesi Asili Nchini**

**MHE. RUTH BLASIO MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, moja ya sababu zinazosaidia upunguzaji wa matumizi ya mkaa na kupunguza ukataji wa miti ni pamoja na wananchi kutumia gesi asili ambayo inazalishwa hapa nchini:-

(a) Je, ni kwa kiasi gani Serikali inahimiza matumizi ya gesi asili kwa gharama nafuu?

(b) Je, kuna kampeni yoyote inayoendeshwa ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI Alijibu**:- Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Nchini *(TPDC)* kwa kushirikiana na mwekezaji kutoka nje, kampuni ya *Pan African Energy* Tanzania, imeanzisha mradi wa majaribio (*pilot project*) ya matumizi ya gesi asili kwenye magari, taasisi mahospitali,mahoteli na majumbani.

Mradi umeanza kutekelezwa ambapo ujenzi mtambo wa kusindika gesi Ubungo umekamilika na kuzinduliwa mwezi huu tarehe 14 julai, 2009. Ujenzi wa kituo cha kujazia gesi iliyoshindiliwa cha Ubingo-Dar es Salaam umekamilika na ujenzi wa kituo cha kujazia gesi Mikocheni- Dar es Salaam unaendelea. Uunganishaji wa gesi asili kwenye Hoteli ya Jiji la Dar es Salaam upo kwenye hatua ya majadiliano ya mikataba ya kuuziana gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhimiza matumizi ya gesi asili, Serikali haijaweka kodi za *excise duty* kama ilivyo kwenye bidhaa za mafuta ya petroli. Kodi pekee katika bidhaa hii ni *VAT*.Aidha, Serikali inaagalia uwezekano wa kutotoza kodi ya excise duty kwa kipindi cha miaka mitano hadi kumi ili kutoa fursa kwa soko la gesi asili kukua, na kutotoza ushuru wa forodha (*import duty)* kwa vifaa vya magari yatakayotumia gesi asili (*conversion kits*) pamoja na majiko ya kupikia yanayotumia gesi asili. Hatua zote nilizozitaja zinalenga kuhimiza matumizi na kuifanya gesi asili kuwa ya gharama nafuu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Juni 2006 Serikali iliondoa kodi ya *excise* na *VAT* kwenye gesi ya kupikia *Liquidified Petroleum Gas (LPG)* na *VAT* na ushuru wa forodha kwenye mitungi ya gesi ili kuvutia watumiaji wengi zaidi wa gesi kwa nia ya kuongeza kasi ya matumizi ya biogesi na *SNV* ya Uhollanzi inaandaa mpango mpya wa uenezaji teknolojia husika.

Kwa upande wa biotaka Shirika la Kilimajaro *Industrial Development Trust* huzalisha vitofali vya puba za mbao mambavyo hutumika kama kuni kwenye baadhi ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia ina mkakati wa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kwa kuhamasisha uzaklishaji na usambazaji majiko bora ya mkaa, matanuti bora ya utengenezaji mkaa *( improved charcoal kilns*). majoko bora ya kuni, biotaka (*biowaste*) pamoja na vitofali vyake na kuhakiki ubaora wa nishati mbadala ya vitofali vya makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majiko bora yanaendelea kuzalishwa na kusambazwa na wadau hususan Asasi zisizokuwa za Kiserikali, Kampuni binafsi na Wajarisiamali wadogo wadogo. Aidha, asasi isiyo ya Kiserikali ya *TATEDO* kwa kushirikiana na Idara ya Misitu na Nyuki wanaendelea kuhamasisha utumiajai matanuri bora ya utengenezaji mkaa katika Mkoa wa Pwani. Matokeo chanya ya juhudi hii yanatarajiwa kuendelezwa katika mikoa mingine.

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Ruth Msafiri.

**MHE. RUTH BLASIO MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kufuatilia majibu aliyoniletea kwa maandishi naona kama bado hajamaliza ndiyo maana nilikuwa nasubiri kwa hamu. Lakini napenda kuuliza maswali mawili madogo kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa kuboresha matumizi ya gesi asilia, mkaa wa mawe, *solar,* biotaka na vitu vinginevyo vitasaidia kupunguza matumizi ya mkaa na kuni kwa wananchi hasa waishio vijijini na kwa ujumla wale wenye kipato cha chini.

Sasa hapa mbona mimi sijaona mkakati wowote wa maksudi wa kufanya kampeni za vijijini ili wananchi waache kutumia kuni na mkaa ili kuweza kuokoa miti na misitu yetu inayoteketea? (*Makofi*)

(b) Naamini kwamba Serikali itakubaliana na mimi kwamba imechukua muda mrefu sana kuweza kuanza kutumia hii gesi ambayo tumeipata kwa miaka mingi na wakati walipoanza hapa kuanza kuijaribisha, umeianzisha kwenye mahoteli makuba makubwa na kuacha wale ambao tulidhani kwamba ndiyo wangekuwa wafaidika wakubwa wa gesi hii.

Je, Serikali itakapokuwa sasa imetaka kupeleka gesi hii kwa wananchi, itaweka bei tofauti ya majiko na vifaa vinginevyo ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza kununua majiko hayo kwa bei ndogo kulinganisha na zile bei za Watanzania wote?

**MWENYEKITI**: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kuboresha matumizi ya gesi asilia na vyanzo vingine, nilichojibu kwenye majibu ya msingi ni kwamba tunaangalia matumizi bora ya vyanzo mbalimbali.

Kwa mfano niliposema hapa ni kwamba tunaangalia pia matumizi ya vitofali vya makaa ya mawe kwa sababu kwa bahati nzuri makaa ya mawe haya yako maeneo mengi ya kusini na ni rasilimali ambayo tunayo kwa wingi. Lakini makaa ya mawe pia yakitengenezwa vibaya yanasifika kwa mambo mawili.

Kwanza yanaweza hata kuunguza sufuria kwa hiyo kwa muda mrefu tangu mwaka 1985 kulikuwa na *Energy One Project* ya kuangalia matumizi mbadala ya nishati hizi mabalimbali, kwa hiyo napenda kumwanbia kwamba tuna Idara ya *Renewable Energy* chini ya *Assistant Commisioner* Mwihava, nakuomba Mheshimiwa Mbunge ufike pale ofisini kwangu twende pamoja na wao kwa pamoja watakupa mikakati mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti,mkakati moja ni huu wa kutumia mkaa wa mawe, mkakati mwingine ni kutumia kama tulivyosema pumba za mbao, kwa hiyo tutakuwa tunajielekeza kulingana na rasilimali inayopatikana kwenye maeneo hayo. kwa hiyo naomba nimuhakikishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mikakati inafanywa kwa bidii kabisa pale Wizarani na tunatarajia kwamba kwa maeneo husika kwa kadri ya unafu ya upatikanaji wa matumizi ya nishati hiyo ndivyo tutakavyo ielekeza kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili amesema matumizi ya gesi asilia haya yanakwenda mahotelini. Labda Mheshimiwa Ruth hukunisikia kidogo, nimesema hivi matumizi haya ya gesi asilia yanakwenda hotelini na baadhi ya maeneo ya Dar es Salaam kama *pilot project* lakini mradi wenyewe kwa awamu ya kwanza ni matumizi ya gesi asilia ya majumbani na kwenye taasisi ambazo yana lengo ya kuunganisha kaya zipatazo elfu 30 zilizopo Jijini Dar es Salaam na gharama yake kama tulivyosema jana ni kubwa kidogo, ni kama Dola za Kimarekani milioni 35. (*Makofi*)

Sasa katika hilo, pia tunatarajia tuunganishe taasisi kama Jeshi la Wananchi wa Tanzania Mgulani, Gereza la Keko na haya Mahoteli ni mahoteli makubwa makubwa kama *Movenpick* na nini ambayo yana-*consume* umeme mwingi. Kwa hiyo, tukiweza kupeleka *consumption* ya gesi badala ya umeme, umeme huu utatumika kwenda kwenye maeneo mengine. Kwa hiyo, hilo ndilo lengo, lakini tukimaliza na Dar es Salaam, tuna lengo ya kwenda kwenye miji mikubwa mingine.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda, nafikiri nikitazama tumeshapitiliza sana naomba wale wote ambao hamkupata nafasi, tusameheane kwa ajili ya hali ya muda. Maswali ni mengi kuliko muda ambao umetengwa, sasa ni kipindi cha utambulisho kwa wageni wetu naomba nichukue fursa hii kuwatambulisha wageni kama ifuatavyo.

Kwa sababu majina ni mengi nitajitahidi nitakapofika hatua fulani kwenda kwa makundi. Kwanza wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Dr.Mary Nagu ambao ni pamoja na mabalozi sina hakika kama balozi wote hawa wapo, *Ambassodors from the Embassy of the United States of America*, *Ambassodor from Sweeden, South Africa, India, Canada, Kenya, Swizerland, United Kingdom, China.*

Wageni wengine kutoka kwenye Mashirika ambayo yanaendana na Wizara hii ni pamoja na Mheshiiwa Pius Ngeze Mwenyekiti wa Bodi ya Kahawa. Ofisi ya Katibu ni vizuri mnapopata majina haya kuyafanyia *check up* kila siku asubuhi ili kujua haswa nani yupo Bungeni.

Alice Mwamaga, Rais wa *TCIA,* yule pale tunamwona. Ahsante sana karibu sana. Ndugu Akonai *CTI*, Kihuri Suma, Hussein Kamote baada ya hao tuna wageni 24 kutoka

Jimbo la Hanang wakiongozwa na Mathew Darema, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Wilaya ya Hanang, wote 24 msimame kwa wakati mmoja. Karibuni sana wageni wetu kutoka Hanang, karibuni Bungeni, karibuni sana. wageni 13. Vile vile wageni wa Mheshimiwa Waziri Viwanda, Biashara na Masoko kutoka Chama cha Mpira Wilayani Hanang, wanaongozwa na Afisa Utamaduni wa Wilaya Ndugu James Sulumo. Karibuni sana viongozi wa Chama cha Mpira na Bunge lina timu hapa kama mpo tayari tunaweza kupanga mechi, karibuni sana. Tuna wageni wa Mheshimiwa Magreth Sitta ambao ni viongozi waanzilishi wa Benki ya Wanawake popote pale mlipo simameni, wale pale. Mimi nilifikiri makofi ya akina mama yangekuwa mengi zaidi, maana Benki hii imepigiwa makelele sana hapa Bungeni na Wabunge wanawake. Tunawashukuruni sana, tunawapongezeni sana, karibuni sana. ((*Makofi*/*Kicheko*)

**WABUNGE FULANI**: Wataje.

**MWENYEKITI:** Wageni, sikuwa nimeleta orodha, kwa hiyo nimeletewa tu jina la kundi. Wageni wa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Cyril Chami ni viongozi 10 wa CCM kutoka Kata za Moshi vijijini, Kata ya Uru Kusini, Kata ya Uru kaskazini, Kata ya Uru mashariki, Kata ya Uru Shimbwe wa kiongozwa na Katibu wa Mbunge wa Moshi vijijini na Mheshimiwa Diwani Martin Malya kwa pamoja. Aah, wapo kwenye *Gallery* ya huku, ahsanteni sana na karibuni sana. Wageni 27 kutoka Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ambao ni Makatibu Wakuu na Maafisa wa Wizara inayojadiliwa wakiongozwa na Joyce Mapunjo, Katibu Mkuu na Dk. Shabani Mwijaka, Naibu Katibu Mkuu. Karibuni sana, karibuni sana viongozi mliofuatana na Mheshimiwa Waziri. Lakini pia kuna maafisa wengine 80 wa Wiara ya Viwanda, Biashara na Masoko ambao wako hapa leo, wageni wengine ni wageni wa Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya , Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ambao ni viongozi 21 wa Chama cha Mapinduzi na Serikali kutoka Jimbo la Urambo Magharibi wakiongozwa na Ndugu Hamisi Madili, Afisa Tarafa Kayuwa nao pia wako upande huu.(*Makofi*)

Wanaofuata ni wageni wa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. ooh, kumbe wapo hapa kwenye Gallery. Naomba niwatambulishe vizuri sasa wajumbe wa Bodi ya Benki ya Wanawake Tanzania nimepata orodha yao hapa. Mwenyekiti ni Ndugu Daniel Wilson Sumayani, karibu sana, Makamu Mwenyekiti Albina Chuwa, ahsante sana. Wajumbe ni Mama Hadija Simba, Victoria Makani, Macel Katemba, Timothy Mgonja, Husna Magembe na Ernest Chipata. Kwa mara nyingine karibuni sana hapa Bungeni.(*Makofi*)

Kwa hatua hii, naomba nitangaze taarifa ya kikao kwamba Waheshimiwa Wabunge Wanawake wa CCM kutakuwa na kikao leo tarehe 28 mwezi wa saba saa saba mchana, kikao hicho kitafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa nadhani itabidi msogee kwenda ukumbi mwingine kwa sababu kuna tangazo jingine litakalo tumia ukumbi huo huo wote mnakaribishwa, Wabunge wanawake wa CCM saa saba mchana.

Tangazo limeletwa na Mheshimiwa Lidiana Mgongo Katibu wa Wabunge Wanawake wa CCM. Wageni wa Ephraim Madeje, Dodoma Mjini ni pamoja na wananchama 18 tawi la magorofani Kata ya Kikuyu Kusini wanaongozwa na Theobalt Maini, Mwenyekiti wa Tawi ambao pia ni Waziri Mkuu Serikali ya wanafunzi Chuo cha Waandishi wa Habari *TSJ*, karibuni sana, karibuni Bungeni. Wageni wa Mheshimiwa Charles Keenja, ni mwenyekiti UWT Wilaya ya Kibaha ambaye pia ni Diwani, Ndugu Nuru Chaurembo Msumi, karibu sana, Ndugu Apolinary Lugebela, mwenyekiti wa CCM, Tawi la kimara Baruti, ndugu Juma Siri mjumbe katibu mkuu Kata ya Manzese, Ndugu Sultan Shomari, mwenyekiti CCM Kata ya Mezi, Ndugu Rehema Bashir mwenyekiti UWT Mburahati. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Athmani Janguo ni Bwana Halfani Janguo ni Bwana Halfani Mavala, mwenyekiti Jumuiya ya Wazazi Wilaya ya Kisarawe, yuko pale karibu sana, Maulid Mkumu, Mwenyekiti CCM Kata ya Kurui, Said Ali Majid, mwenyekiti jumuiya ya Wazazi Kata ya Marumbo, Ramadhani Mussa, mwenyekiti Jumuiya ya Wazazi Kata ya Vihingo na Said Halmasi Kikungwa Katibu CCM Kata ya Vihingo, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Mamuya ni Ndugu Salim Seif Mwenyekiti Umoja wa Vijana Kata ya Sokoni na ni mtumishi *Genearal Tyres*, karibu sana. Pia Alphonse Morris, mfanyakazi wa *General Tyres* karibu sana . Wageni wa Mheshimiwa Ruth Msafiri ni Nuru Msasa, mshauri wa mwalimu wa *Greendad* Muleba yuko kule karibu na Imani mtoto wa Mheshimiwa Ruth Msafiri ambaye anasoma *Nusery*. Yuko wapi Imani? Ebu mnyanyue kidogo, karibu sana Imani. ahsante sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini ni wanafunzi 30 toka shule ya msingi Juhudi, Kata ya Iganzo, katika Jiji la Mbeya na walimu 15 toka shule ya msingi Juhudi na shule ya msingi Ilinyi katika jiji la Mbeya. Karibuni sana walimu na wanafunzi kutoka Mbeya. Karibuni sana Bungeni Dodoma. Mgeni wa Mheshimiwa Josephine Gezabuke ni Ndugu Beatrice Balandaje, Katibu wa Vijana wa Mkoa wa Kigoma. Karibu sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Mbumbuli, ni wafanyakazi wa kiwanda cha *General Tyres* ambao bahati nzuri tumeshawatambulisha ambao pia walikuwa ni wageni wa Mheshimiwa Halima Mamuya, karibuni. Mgeni wa Mheshimwa Mohamed Abdallah ni Shabani Kizamba Mwenyekiti Umoja wa Vijana CCM Wilaya ya Pangani, karibu sana.

Wageni wa Mheshimiwa Mussa Zungu, Mbunge wa Ilala ni Asma Mussa, Eva Malenga, Sharif Mbulu na Yohana Mwila.Wageni wa Mheshimiwa Felista Bura ni ndugu Adiel Azaliwa kutoka Same Mashariki, yuko kule ahsante sana, Ndugu Gerald Bura, mtoto wake, Yusuph Bura na Bernard Pius watoto wa Abdiel.

Mgeni wa Mheshimiwa Mariam Mfaki ni Baraka Kange kutoka Dar es Salaam yule pale, pamoja na Mohamed Mfaki. Mgeni wa Mheshimiwa Willibrod Slaa ni Ndugu Halifa Masi, mtumishi wa Halmashauri ya Karatu, karibu sana.

Mgeni wa Mheshimiwa Hoogan Parmukh Singh ni Gurmet Sing Sohal ni binamu yake na mwana harakati wa Chama cha *Conservative* Uingereza pamoja na familia yake, wako pale karibuni sana Dodoma.

wageni wa Mheshimiwa Yonah Kevela na Mheshimiwa Daston Makweta ni madiwani 25 kutoka Halmashauri ya Wilay ya Njombe wakiomgozwa na mwenyekiti wao Valency Kabelege ni wa Majimbo ya MboziI kaskazini Mbozi magharibi, karibuni sana wageni wetu kutoka Njombe. Baada ya orodha hiyo, mnivumilie tuendele na matangazo ya vikao.

Mheshimiwa John Momose Cheyo anawaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali kwamba kutakuwa na Kikao leo tarehe 28 Julai, 2009 saa saba mchana katika Ukumbi 231, Mheshimiwa John Cheyo anawatangazia wajumbe wa *PAC* saa saba mchana leo Ukumbi Namba 231.

Mheshimiwa Mohamed Msanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anawaomba wajumbe wa Kamati yake ya Miundombinu kutakuwa na kikao leo saa saba mchana chumba 219. *(Makofi)*

Mheshimiwa George Malima Lubelege anawatangazia wajumbe wa Kamati yake ya Katiba, Sheria na Utawala kuwa kuna kikao leo tarehe 28 Julai, 2009. Leo saa saba na nusu mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa, na niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge ni muhimu sana kuhudhuria kikao hiki wajumbe wa Kamati nyingine cha Mheshimiwa Lubeleje kwa sababu pamoja na mambo mengine tutajadili, mswada wa *CDCF*. (*Makofi*)

Mheshiniwa Willium Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini anawaomba wajumbe wa Kamati yake leo saa nane mchana chumba 133 jengo la Utawala mkutane.Mheshimiwa Gosbert Blandes, Makamu Mwenyekiti Kamati ya Sheria Ndogo anaomba wajumbe wa kamati hiyo saa saba mchana katika ukumbi wa Mseka “B”.

Mheshimiwa Lugai anaomba wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwamba leo saa saba mchana Ukumbi 227 waudhurie bila kukosa. Mwisho niliwaruka kwa kuwataja wageni wa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kuwataja moja kwa moja naomba sasa niwataje, Bi Saumu Bendera, Mwenyekiti wa UWT, Mkoa wa Tanga, karibu sana. Bi. Frida Lituga UWT Mkoa, karibu, Bi. Mary Chatanda, Mjumbe wa Baraza la UWT Mkoa wa Tanga na Katibu wa CCM Mkoa wa Morogoro. Bi. Zubada Titu - mwenyekiti Wilaya ya Lushoto wa UWT, Zainab Mvaa - Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Pangani,

Bi. Zubeda Titu - Mwenyekiti wa Wilaya ya Lushoto UWT Zainabu Mvaa - Mwenyekiti Wilaya ya Pangani, Theresia Gawile -Mwenyekiti Wilaya Korogwe, Ndugu Margareth Ngereza - Mwenyekiti Korogwe Mji na Ndugu Hadija Mlugu - Mwenyekiti Mkinga. Naona aliyekosekana Mwenyekiti wa Kilindi tu, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya matangazo yote haya sasa tuendelee. Katibu! Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri, niwakumbushe Wenyeviti wa Kamati za Bunge tangazo ambalo alilitoa Mheshimiwa Spika akiwa hapa Mezani jana, kwamba Kamati ya Uongozi inataka kukutana leo Ukumbi wa Spika saa 7 mchana, nawakumbusha tu. Mheshimiwa Waziri, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2009/20010
### Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, namshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani aliyonayo kwangu kwa kunikabidhi madaraka ya kuongoza na kusimamia majukumu ya Wizara ya Viwanda yangu, na Wizara ambayo ni nyeti namshukuru sana. Aidha, namhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa nitaendelea kuyatekeleza majukumu aliyonikabidhi kwa moyo, uwezo na ujuzi wangu kwa ushirikiano na Baraza la Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge. Vile vile, namshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri aliyoitoa tarehe 10 Juni, 2009 kwa Taifa kupitia kwa Waheshimiwa Wabunge na

Wazee wa Dodoma. Hotuba hiyo ilifafanua juhudi za Serikali katika kukabiliana na athari zinazotokana na kuporomoka kwa uchumi duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuukubali na kuupitisha Mpango wa KILIMO KWANZA ambao unaweka mkazo kwenye kuongeza tija katika sekta ya kilimo, ili iwe nguzo ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Hii ni kwa vile nchi zilizoendelea zilianzia na mabadiliko ya kilimo cha kujikimu kwenda kwenye kilimo cha kisasa. Katika kuleta mageuzi haya, Wizara yangu ina mchango muhimu kwani tija katika kilimo inapatikana pale ambapo Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko zitahusishwa kikamilifu. Wizara yangu itahakikisha kuwa inashirikiana na wadau wengine katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa KILIMO KWANZA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuchukua fursa hii, kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mchango wake mkubwa katika kuhamasisha maendeleo endelevu katika sekta za Viwanda, Biashara na Masoko. Ushiriki wake katika shughuli mbalimbali za sekta unadhihirisha jinsi anavyothamini umuhimu wa sekta hii katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo aliyotoa kwa ajili ya kuendeleza sekta za Viwanda, Biashara na Masoko. Aidha, nakiri kwamba, hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu na majibu aliyoyatoa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge imetoa mwongozo ambao umenirahisishia kufanya mawasilisho na pia kuweka misingi itakayorahisisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Vile vile, nawashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano wao mzuri ambao umerahisisha utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wananchi na wadau mbalimbali, hususan asasi za sekta binafsi zikiwemo *TCCIA, CTI, TPSF, TNBC, ACT, VIBINDO, TWCC* na *LAT* kwa michango yao katika kuendeleza sekta za Viwanda, Biashara na Masoko ambazo Wizara yangu inasimamia.

Ninashukuru Taasisi za Sekta Binafsi kwa ushirikiano walioonesha na michango muhimu waliyotoa ikiwa ni pamoja na michango yao katika kuandaa hotuba hii. Naomba waendelee na ushirikiano huo ili tuweze kuendeleza sekta hizo ambazo ni muhimu katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ningependa kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Hanang kwa ushirikiano walionipa nami naendelea kuahidi kuwa nitajitahidi kuwawakilisha ili wafikie matarajio yao. Aidha, naishukuru familia yangu na hasa mume wangu mpendwa Prof. Joseph Nagu kwa upendo, ushirikiano na msaada wake pamoja na watoto wetu Tumaini, Neema, Deo na ndugu wengine wanaokaa nami ambao wamenipa utulivu na hivyo kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu inavyopaswa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka uliopita, Bunge lako Tukufu lilipata majonzi kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu ambao walishiriki kutoa michango iliyotuwezesha kujadili na kufikia maamuzi muhimu. Kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa pole kwa ndugu, jamaa za Waheshimiwa Wabunge wenzetu hao na Wabunge wote kutokana na misiba hiyo. Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliotutoka ni hayati Richard Said Nyaulawa, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini; hayati Faustine Kabuzi Rwilomba, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Busanda; na hayati Phares Kabuye, aliyekuwa Mbunge wa Biharamulo Magharibi. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi – Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia kuwapongeza Wabunge wapya waliochaguliwa katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Wabunge hao ni: Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini (CCM); Mheshimiwa Lolensia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Jimbo la Busanda (CCM); na Mheshimiwa Oscar Mukasa Rwegasira, Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi (CCM); na Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, Mbunge wa Jimbo la Tarime (CHADEMA) kwa kushinda chaguzi ndogo zilizofanyika katika kipindi hicho. Nitaendeleza ushirikiano wangu kwa Waheshimiwa Wabunge hawa wapya kama ninavyofanya kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote wa Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mbunge wa Jimbo la Makunduchi (CCM), akisaidiwa na Makamu wake Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Jimbo la Mkinga (CCM), ambao wamechambua kwa kina mapendekezo ya Bajeti ya Wizara hii na kutoa ushauri na mapendekezo muhimu yanayolenga katika kuboresha utendaji wa sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko. Mara zote mchango wa Kamati hiyo umekuwa na umuhimu wa pekee katika kuendeleza, kusimamia na kuboresha utendaji wa sekta hizi. Nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja na michango ya Kamati imezingatiwa katika hotuba ninayoiwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mashariki; na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Mbunge wa Jimbo la Kilosa; kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo wa ujumla katika masuala ya Mipango, Uchumi, Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika hotuba za Mawaziri waliotangulia. Maoni ya Wabunge hao yamesaidia kuboresha mipango ya Serikali katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru viongozi wenzangu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, nikianza na Naibu Waziri, Mhe. Dr. Cyril A. Chami (Mb), Katibu Mkuu Joyce K. G. Mapunjo, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Shaban Ramadhani Mwinjaka, Wakuu wa Idara na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara. Aidha,

nawashukuru wataalamu na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kujituma katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 na utekelezaji wake, kwa kutambua Dira na Dhima ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ambayo inaelekeza kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko yenye lengo la kuwapatia maisha bora Watanzania kwa kuongeza tija na kuinua uchumi, Wizara inatekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, ibara ya 36 mpaka 37 na 40 mpaka 41 zilizoweka msisitizo katika maeneo ya viwanda, biashara na masoko. Wizara imetekeleza maelekezo hayo kama ifuatavyo:-

Sekta ya Viwanda, Ukuaji wa Sekta ya Viwanda Kufikia Asilimia 15 Ifikapo 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa Sekta ya Viwanda umeongezeka kutoka asilimia 8.5 mwaka 2006 mpaka asilimia 9.9 mwaka 2008. Ukuaji huu ulikuwa na kasi ndogo kuliko ilivyotegemewa kutokana na uduni wa teknolojia zinazotumiwa na wazalishaji, uhaba na uhafifu wa miundombinu; gharama kubwa na kutokuwa na uhakika wa upatikanaji wa huduma za maji na umeme; pamoja na udhaifu wa uongozi na stadi za biashara. Aidha, kasi ndogo ya ukuaji wa sekta ilichangiwa pia na misukosuko ya masoko ya fedha na mitaji iliyotokea na kusababisha matatizo ya kiuchumi duniani mwaka 2008. Serikali itaendelea kuweka mazingira bora kuwezesha sekta binafsi itekeleze majukumu yake vyema ili kuongeza kasi ya ukuaji wa viwanda.

Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kuimarisha Sekta ya Ngozi na Viwanda vya Ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati Unganishi wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi nchini. Mkakati huo umelenga katika kujenga uwezo wa kusindika ngozi na kutengeneza bidhaa za ngozi ikiwa ni pamoja na kuchochea uwekezaji katika sekta hiyo ambapo kwa sasa sehemu kubwa ya ngozi ghafi zinauzwa nje ya nchi. Aidha, Wizara inaendelea na mchakato wa kufufua Chuo cha Taaluma ya Ngozi (*Tanzania Institute of Leather Technology-TILT*).

Pia, utoaji wa mafunzo ya usindikaji wa ngozi kwa njia ya asili (*Rural Tanning)* pamoja na utengenezaji wa bidhaa za ngozi umefanyika kwa mikoa 7 yenye mifugo mingi ambayo ni pamoja na Arusha, Manyara, Singida, Shinyanga, Mwanza, Mara na Tabora. Vile vile, vituo vya kutoa mafunzo na uzalishaji wa bidhaa za ngozi vya Dar es Salaam na Morogoro vimeendelea kujengewa uwezo ili viendelee kuzalisha na kutoa

huduma bora zaidi. Hivi sasa kuna wajasiriamali zaidi ya 200 wanaojishughulisha na usindikaji wa ngozi na baadhi yao wameanza utengenezaji wa bidhaa za ngozi.

Serikali Kuendeleza Jitihada za Kuwapata Wabia wa Kuwekeza katika Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma na Mradi wa Chuma wa Liganga Ndani ya Mfumo wa Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuwapata wabia wa kuwekeza katika miradi ya makaa ya mawe wa Mchuchuma na chuma wa Liganga, wawekezaji 48 wameonesha nia ya kuwekeza katika miradi hiyo na hatua za kupata wawekezaji bora kati yao zinaendelea. Aidha, Mwekezaji wa kutekeleza Mpango wa Kasi Mpya wa kuzalisha chuma ghafi (*sponge iron*) amepatikana na mchakato wa ubia kati ya *NDC* na mwekezaji unaendelea. *(*d)Kuendelea Kuhamasisha Uanzishwaji wa Maeneo ya Uzalishaji kwa Ajili ya Uuzaji Nje *(Export Processing Zone – EPZ) n*a Uwekezaji wa Viwanda Ndani ya Maeneo Hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhamasisha uanzishwaji wa Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (EPZ), Mamlaka yake (EPZA) imeendelea kuhamasisha wawekezaji wa kujenga viwanda na kuzalisha. Njia zinazotumika kuhamasisha wawekezaji ni pamoja na vipeperushi, majarida, mabango, vyombo vya habari, na ushiriki katika makongamano ya kibiashara ndani na nje ya nchi. Kutokana na juhudi za uhamasishaji huo, kuanzia mwaka 2006 hadi 2008, jumla ya viwanda 46 vimesajiliwa chini ya mpango wa *EPZ,* vikiwemo 18 vya kujenga miundombinu ya EPZ na 28 ni viwanda vya uzalishaji. Viwanda ambavyo vimeanza uzalishaji ni pamoja na: *Cami Apparel Ltd, Unnats Fruits Processing Ltd, Kibo Trade Textile Ltd, Nethealth Ltd.* na *Honey Care Tanzania Ltd*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mamlaka ya EPZ na kwa kushirikiana na uongozi wa Mikoa wamebainisha na kutenga maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya EPZ na SEZ yenye ukubwa wa hekta 2,000 kwa kila mkoa katika mikoa 14 ambayo ni Pwani, Tanga, Arusha, Manyara, Mwanza, Mara, Kagera, Kigoma, Mtwara, Ruvuma, Kilimanjaro, Morogoro, Mbeya na Lindi.

Kuanzisha Utaratibu wa Kutenga Maeneo Maalumu ya Kiuchumi *(Special Economic Zones - SEZs)*, kwa Ajili ya Uzalishaji Utakaolenga Masoko yote ya Ndani na Nje

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatekeleza pia mpango wa maeneo maalum ya kiuchumi yaani *Special Economic Zones (SEZs*). Tayari kuna eneo moja lililopo Mabibo, Dar es Salaam ambapo mpaka sasa ujenzi wa miundombinu ya eneo maalum la kiuchumi la *Benjamin William Mkapa Special Economic Zone (BWM – SEZ*) umekamilika kwa asilimia 97. Vile vile, ofisi za Mamlaka ya EPZ zimekwishahamia katika eneo hilo ili kuongeza ufanisi katika kuhudumia wawekezaji. Eneo hilo litakodishwa kwa wawekezaji kwa ajili ya kujenga viwanda vya kuzalisha kwa mauzo ya

nje na ndani. Aidha, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya EPZ inaendelea kusimamia utekelezaji wa zoezi la kuendeleza maeneo makubwa ya EPZ na SEZ yaliyobainishwa katika mikoa 14 nchini. Katika uendelezaji huo, tayari zoezi la upimaji na uthamini mali (*valuation*) limekamilika katika mikoa ya Mara, Ruvuma na Manyara ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 6.8 kinahitajika kwa ajili ya kulipa fidia. Upimaji na uthamini unaendelea katika mikoa ya Pwani, Morogoro, Arusha na Tanga.

Kuendelea na Utekelezaji wa Programu Inayolenga Katika Kuimarisha Usindikaji wa Mazao ya Kilimo, Mifugo na Chakula

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha usindikaji wa mazao, Wizara imehamasisha sekta binafsi kuwekeza katika usindikaji wa mazao ya kilimo ambapo wawekezaji 19 wameonesha nia na tayari wamepata kibali cha kuwekeza katika usindikaji wa mazao kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC). Mazao hayo ni pamoja na matunda, mboga mboga, ngozi, pamba, katani, mbegu za mafuta ya kupikia, viungo na nafaka. Aidha, katika kukabiliana na changamoto zinazokabili viwanda vya usindikaji, Wizara imekuwa na utaratibu wa kukutana na wadau kisekta kwa lengo la kubaini hatua za kuchukuliwa kisera na kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imejijengea utaratibu wa kukutana na sekta binafsi kujadili masuala ambayo yanahitaji ufumbuzi wa pamoja. Vile vile, sekta binafsi inashirikishwa katika michakato ya kuandaa sera, sheria, kanuni na mikakati ya kuendeleza Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko. Wizara itaendeleza utaratibu huu kwa kuwa umekuwa wa manufaa.

Hadi sasa, Wizara imefanya mikutano na wenye viwanda vya saruji, mafuta ya kula na sabuni, ngozi na bidhaa za ngozi, kusindika pamba na kutengeneza mavazi na mbolea ambapo baadhi ya changamoto zilizojitokeza zimepatiwa ufumbuzi na nyingine zinaendelea kushughulikiwa. Kwa mfano, viwanda binafsi vimewezeshwa kuongeza usindikaji wa pamba na kunusuru sekta ya pamba iliyoathiriwa na msukosuko wa uchumi duniani ambao ulisababisha kukosekana kwa soko kutokana na kuanguka kwa bei ya zao hili duniani.

Kubuni Mpango wa Kuandaa Mabingwa katika Fani Mbalimbali za Sayansi na Teknolojia ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanya tathmini ya uwezo wa Taasisi zetu kuandaa mabingwa katika fani za sayansi na teknolojia kwa ajili ya matumizi ya viwanda. Chuo cha Elimu ya Biashara pamoja na kujikita kwenye stadi ya biashara, kimeendelea kutoa wataalam wa fani ya vipimo na mizani. Ili kuendeleza taaluma na teknolojia ya ngozi, tathmini ya mahitaji ya kufufua na kuendeleza Chuo cha Taaluma ya ngozi kilichopo Mwanza (*Tanzania Institute of Leather Technology* - TILT) imefanyika. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa sayansi na teknolojia katika maendeleo ya nchi hususan viwanda, Wizara imetoa eneo lililokuwa la CAMARTEC, huko Tengeru Arusha ili litumike kuanzisha Taasisi ya Kimataifa ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Kampasi ya Arusha ili kuhakikisha kuwa nchi inapata wahitimu wenye elimu na

teknolojia ya kutosha zinazolenga kuchochea ukuaji wa uzalishaji nchini. Vile vile, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Vyuo Vikuu nchini vina mchango mkubwa katika kuandaa mabingwa wa sayansi na teknolojia za viwanda. Hali kadhalika, Taasisi za CAMARTEC, TIRDO na SIDO zinaendeleza teknolojia kwa kutumia mikakati ya viatamizi (*incubators*) ambapo miradi michanga hulelewa hadi hatua ya kuingia kwenye soko.

Kuvutia Uwekezaji katika Viwanda vya Kuongeza Thamani Mazao mbalimbali ya Kilimo, Mifugo, Madini, Uvuvi na Maliasili

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika azma ya kuvutia uwekezaji nchini, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya EPZ imeendelea kutoa vivutio vya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje wakiwemo wanaosindika mazao mbalimbali ya kilimo na mifugo. Wawekezaji hao ni pamoja na *SAAFI Limited* cha Rukwa kinachosindika nyama, *Salex Tannery* cha Arusha na *Himo Tannery* cha Kilimanjaro vinavyosindika ngozi na kutengeneza bidhaa za ngozi; *Unnat Fruits Processing* cha Morogoro kinachosindika matunda, *Bakhresa Food Processing Ltd* cha Dar es Salaam kinachosindika nafaka na matunda; na *Jambo Modern Textiles* cha Arusha kinachosokota nyuzi za pamba. Serikali itaendelea kuhamasisha uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuweka vivutio maalum kwenye sekta zinazolenga uongezaji thamani.

Kuendelea na Ubinafsishaji na Ukodishaji wa Viwanda na Mashirika ya Umma Yaliyobaki

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda ambavyo bado havijabinafsishwa chini ya Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko ni kiwanda cha *Morogoro Leather Goods, Songwe Water Company* na *General Tyre East Africa Limited (GTEA*). Zoezi la kubinafsisha kiwanda cha *Morogoro Leather Goods* linaendelea ambapo tayari mtaalamu wa uthamini mali ili kupata bei elekezi amepatikana. Juhudi za kumpata mwekezaji wa kufufua kiwanda cha *General Tyre (EA) Ltd.* zinaendelea.

Aidha, Serikali imehamishia umiliki wa mali zilizokuwa za kampuni za *Tanzania Sheet Glass, Nyanza Glassworks,* KMTC na TAMCO chini ya NDC. Kufuatia umiliki huo, *NDC* inaandaa mpango wa kufufua viwanda hivyo kwa kushirikiana na sekta binafsi. Kwa sasa, eneo la TAMCO limekodishwa kwa kampuni binafsi kwa ajili ya kuunganisha magari makubwa. Pia, mashamba ya mpira ya Kihuhwi (Muheza) na Kalunga (Kilombero) yamerudishwa chini ya NDC baada ya Serikali kusitisha ubinafsishaji wake.

Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo(a) SIDO na Sera yenyewe ya Viwanda Vidogo Itatazamwa Upya ili Kuhakikisha Inakidhi Lengo Kuu la Kujenga Msingi wa Uchumi wa Kisasa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamilisha Mfumo wa Uperembaji na Tathmini *(M&E)* ya utekelezaji wa Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo.

Uperembaji na tathmini ukikamilika itawezesha kufanya mapitio ya Sera husika. Aidha, uandaaji wa mfumo huo ulishirikisha wadau mbalimbali. Vilevile, Wizara imeanza zoezi la kupitia upya sheria na majukumu ya SIDO ili kuhakikisha yanakidhi mahitaji halisi ya uchumi wa kisasa.

Kuongeza Ushiriki wa Sekta Isiyo Rasmi na Sekta ya Viwanda Vidogo na vya Kati (SMEs) katika Uzalishaji wa Bidhaa

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha ushiriki wa sekta isiyo rasmi katika uzalishaji, Wizara imeendelea kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Wafanyabiashara Wananchi (*National Enterprenuership Development Fund (NEDF)* kwa lengo la kuwapatia mtaji wajasiriamali wadogo wakiwemo wa sekta isiyo rasmi. Ili kuimarisha uzalishaji, kiwango cha juu cha mkopo kimeongezwa kutoka shilingi 500,000 kwa mwombaji hadi kufikia shilingi 2,500,000 kwa miradi ya uzalishaji. Katika mwaka 2008/2009, mfuko uliongezewa shilingi milioni 500 na hivyo kuwezesha kutoa mikopo ya thamani ya shilingi bilioni 3.646 kwa wajasiriamali 5,670 ambayo ilisaidia kuanzisha ajira mpya kwa watu 13,300 ikilinganishwa na mwaka 2007/2008 ambapo mikopo 3,219 ya thamani ya shilingi bilioni 2.28 ilitolewa.

Kuongeza Uwezo wa SIDO katika Uwezeshaji wa Kitaalamu na Mitaji katika Sekta ya Viwanda Vidogo na vya Kati

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wa SIDO kwa njia ya mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi katika fani mbalimbali. Katika mwaka 2008/2009 watumishi 55 walipatiwa mafunzo. Aidha, kupitia programu ya Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI), SIDO imepatiwa magari saba ambayo yatatoa huduma katika mikoa sita inayohusika na utekelezaji wa mradi huu. Vile vile, katika uongezaji wa mitaji, Serikali imeendelea kuchangia mtaji wa NEDF na kufikia shilingi bilioni 3.7 kutoka shilingi milioni 500 mwaka 1994. (d)Kuendelea Kushirikiana na Asasi Mbalimbali Kuboresha Mazingira ya Uzalishaji Viwandani Ikiwa ni Pamoja na Miundombinu, Sera za Fedha na Kodi na Kutenga Maeneo Maalumu kwa Ajili ya Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

Mheshimiwa Spika, *SIDO* kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na sekta binafsi imetenga maeneo na kujenga mabanda mikoani kwa ajili ya viwanda vidogo na biashara ndogo. Hadi sasa mabanda ya Viwanda 34 na vibanda vya biashara 234 yamejengwa katika mikoa mbalimbali. Wizara inaendelea kutekeleza programu ya EPZ ambayo ina mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji wa kada zote wakiwemo wajasiriamali wadogo. Vile vile, Wizara imeshiriki katika majadiliano ya maboresho ya sera za kodi na marekebisho kwenye Sheria ya Kodi na Ushuru wa Forodha katika maeneo ya mafuta ya kula, nguo na mavazi, saruji na ngozi na bidhaa za ngozi. Sekta ya Biashara , Katika Sekta ya Biashara, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 ilibainisha maeneo yafuatayo ya utekelezaji.

Kuendelea Kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda (EAC, SADC) na wa Kimataifa *(WTO)* kwa Lengo la Kupanua Soko la Bidhaa Zetu na Kuvutia Wawekezaji

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa ikiwa ni pamoja na kushiriki katika utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha na majadiliano ya kuanzishwa kwa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Rasimu ya Itifaki ya Soko la Pamoja imeandaliwa. Baadhi ya maeneo yanayohusiana na ardhi, vitambulisho vya kusafiria na makazi ya kudumu hayajafikiwa muafaka na nchi wanachama. Itifaki ya Soko la Pamoja inategemewa kusainiwa na Wakuu wa Nchi mwezi Novemba, 2009 na kuanza kutekelezwa rasmi mwezi Januari, 2010. Vile vile, Tanzania imeendelea kutekeleza Itifaki ya Biashara ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Nchi wanachama wa SADC walizindua Eneo Huru la Biashara mwaka 2008 nchini Afrika Kusini. Mchakato wa majadiliano ya kuanzisha Umoja wa Forodha wa SADC yameanza ambapo Tanzania inashiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kupanua fursa za masoko ya bidhaa zetu na kupunguza migongano ya kisera, nchi wanachama wa *EAC, SADC* na *COMESA* zimekubaliana kwa pamoja kurazinisha sera zake za biashara kwa lengo la kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara la Kanda hizo tatu. Mchakato umeshaanza na hatua za awali ambazo zimeshakamilika ni pamoja na kuandaliwa kwa uelekeo *(roadmap)* na Hadidu za Rejea kwa ajili ya kuanzisha muundo utakaowezesha kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara na Makubaliano ya Mashirikiano (*Memorandum of Understanding* - MOU).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inaendelea kuongoza majadiliano ya Ubia wa Uchumi (EPA) kupitia kundi la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu ushirikiano wa kibiashara na Jumuiya ya Ulaya. Iwapo maeneo muhimu yanayohusu masuala ya ushirikiano wa uchumi na maendeleo yataafikiwa, inategemewa Mkataba kamili wa EPA utasainiwa. Changamoto ya majadiliano hayo ni kwa Jumuiya ya Ulaya kutambua matatizo yetu ya uzalishaji duni na kutujengea uwezo kwa kuongeza fungu la misaada ya kifedha na kiufundi. Lengo la EPA ni kuleta maendeleo kupitia biashara kwa nchi changa, hivyo, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinashikilia msimamo wao katika suala la kushirikiana katika kujenga uchumi na maendeleo hususan katika kupata misaada ya kifedha na kiufundi .

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya biashara ya kimataifa ya Duru ya Doha yanayosimamiwa na Shirika la Biashara la Dunia (WTO). Kuanzia Novemba 2008, Tanzania imechukua Uenyekiti wa Kundi la Nchi Maskini Zaidi Duniani *(Least Developed Countries)* katika majadiliano ya WTO. Majadiliano haya ya "Duru ya Maendeleo" yalianza mwaka 2001 na yamekuwa yakisuasua kutokana na kutofautiana kwa misimamo kati ya nchi zilizoendelea na nchi zinazoendelea. Tofauti hizo zinahusu ni kwa kiasi gani nchi zilizoendelea zifungue masoko yao ya mazao ya kilimo au uondoshwaji wa ruzuku kwa wakulima wa nchi zao. Serikali itaendelea kujenga mshikamano na nchi zinazoendelea ili kuhakikisha nchi zilizoendelea zinafungua masoko kwa bidhaa za nchi zetu.

Kutoa Elimu ya Kanuni na Taratibu za Masoko na Biashara na Nchi za Nje Hususan Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi

za Kusini mwa Afrika (SADC), na Nchi Nyingine Ambazo Zinatoa Upendeleo kwa Bidhaa Zinazozalishwa katika Nchi Zinazoendelea

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi na Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE) imeendelea kuelimisha wadau na umma kuhusu kanuni na taratibu za biashara na masoko zilizopo kwenye Jumuiya za Kikanda na Kimataifa kwa njia ya redio, luninga na magazeti na pale inapobidi semina na warsha zimetumika. Semina hizi zimeendeshwa katika kanda sita za Tanzania Bara, Tanzania Zanzibar na kwa Waheshimiwa Wabunge Dodoma. Washiriki wa semina hizo ni pamoja na, Waheshimiwa Madiwani, Watumishi wa Serikali, Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Asasi Zisizo za Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza juhudi za kukuza ufahamu wa kanuni na taratibu za biashara na masoko, Wizara imeendelea kuhamasisha wafanyabiashara kutumia fursa za masoko zinazotolewa na nchi za China, Japan, Marekani, Canada na India ikiwa ni pamoja na kuwezesha Wafanyabiashara kutembelea nchi hizo. Aidha, mauzo ya bidhaa na mazao ya Tanzania katika masoko hayo yameongezeka.

Kuhimiza Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(TEKNOHAMA)* katika Biashara

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kutambua umuhimu wa matumizi ya TEKNOHAMA katika biashara (*e-commerce*), Wizara imeanzisha kitengo cha kuratibu shughuli za TEKNOHAMA zinazohusu upashanaji wa taarifa mbalimbali za kibiashara na masoko. Aidha kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano cha Wizara ni kiunganishi kati ya Wizara, Taasisi na Wadau na kinarahisisha upatikanaji na upashanaji wa habari mbalimbali za kisekta kupitia TEKNOHAMA. Vile vile, Wizara na Taasisi zake zimeanzisha tovuti ambazo zimerahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali zikiwemo bei na fursa za masoko zilizopo ndani na nje ya nchi. Sanjari na juhudi hizo, Wizara inaandaa Mkakati wa TEKNOHAMA wa kisekta (*Sector ICT stratergy*) ambao utaharakisha utekelezaji wa biashara mtandao katika ngazi mbalimbali.

Sekta ya Masoko. Katika Sekta ya Masoko, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 ilibainisha maeneo yafuatayo ya utekelezaji.

Kuendeleza Programu Maalumu ya Uuzaji Bidhaa Nje *(Export Development Strategy (EDS)* na Kuanzisha Mfuko wa Mauzo yaNje *(EDF)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanikisha azma ya Serikali ya kukuza mauzo nje, Wizara, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imekamilisha na kuanza kutekeleza Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje wenye matokeo ya haraka (*Quick Wins*). Mkakati huo umeainisha sekta za kipaumbele ambazo zitahusu: mazao ya korosho, pamba, maua, matunda na mboga mboga, nyama, ngozi, vito vya thamani, dhahabu, maeneo yenye vivutio vya utalii na huduma za kuendeleza biashara ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanikisha utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Mauzo nje, Wizara imeandaa na kutekeleza Mpango Unganishi wa Biashara ya Tanzania *(TTIS)* ambapo Serikali imekubaliana na Washirika wa Maendeleo kuanzisha Mfuko wa Pamoja (*Basket Fund*) ili kutekeleza Mpango huu nchini. Utekelezaji wa Mpango huu utawezesha kukabiliana na changamoto za uzalishaji kwa ajili ya masoko ya nje hivyo kunufaika na fursa za masoko katika nchi mbali mbali zikiwemo za *EAC* na SADC katika mfumo wa biashara ya utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu jitihada za kutafuta masoko ya mazao na bidhaa katika nchi mbalimbali, Wizara kwa kushirikiana na Vituo vya Biashara vya London na Dubai, BET na SIDO iliwawezesha wafanyabiashara kushiriki katika maonesho ya kitaifa, kikanda na kimataifa na kuwezesha kupatikana kwa masoko ya maua, mboga mboga, matunda, asali na viungo katika nchi za Mashariki ya Kati na za Jumuiya ya Ulaya.

Kuimarisha na Kuendeleza Mfumo wa Ukusanyaji, Uchambuzi na Usambazaji wa Taarifa na Takwimu za Masoko ya Mazao kwa Walengwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ukusanyaji, utunzaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu za masoko ya mazao ya kilimo na mifugo umepanuliwa kutoka mazao 44 mwaka 2007/2008 hadi 62 katika Wilaya 93 mwaka 2008/2009. Taarifa za masoko ya mifugo zimepanuliwa hadi kufikia taarifa za minada 30 katika mikoa 17. Aidha, upatikanaji wa taarifa za mifugo zinajumuisha nchi za Afrika ya Mashariki na Kati. Taarifa hizo husambazwa kwa kutumia ujumbe mfupi wa maandishi (SMS) kupitia simu za mikononi; magazeti; redio; na mtandao wa kompyuta. Wizara pia imeendelea kusambaza taarifa za masoko kwa vipeperushi, majarida na machapisho kupitia maonesho ya biashara kitaifa na kimataifa.

Kuandaa Kitabu cha Orodha ya Wanunuzi na Wasindikaji wa Mazao (Agri-business Directory) na Kuisambaza kwa Wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliandaa kitabu cha Orodha ya Wanunuzi na Wasindikaji wa Mazao kwa mara ya kwanza mwaka 2005/2006. Aidha, Wizara inahuisha na kuboresha taarifa na orodha ya wanunuzi na wasindikaji wa mazao ya kilimo ya kitabu hicho ili kuwapatia wadau taarifa zinazoendana na wakati.

Kutoa Mafunzo ya Jinsi ya Kutumia Taarifa Mbalimbali za Masoko kwa Vikundi vya Wazalishaji, Wasindikaji na Wafanyabiashara wa Kati ili Waweze Kuzalisha na Kuuza kwa Kufuata Mahitaji ya Soko

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imekuwa ikitoa mafunzo kuhusu utumiaji wa taarifa za masoko kwa wadau ambao ni pamoja na: vikundi vya wazalishaji; wasindikaji; na wafanyabiashara wa kati kupitia luninga, redio, vipeperushi, magazeti, majarida na maonesho mbalimbali ili waweze kuzalisha na kuuza kwa kufuata mahitaji ya soko. Aidha, Wizara kwa kupitia Wakala wa Vipimo,

imeendelea kutoa elimu maalum ya matumizi ya vipimo sahihi katika biashara. Wadau wamefaidika na taarifa hizi kwa kuweza kuingia kwenye masoko wakiwa na uelewa wa bei inayofaa.

Kuwezesha Halmashauri za Miji na Wilaya Kuwa na Vitendea Kazi vya Kukusanya, Kuchambua na Kutunza Taarifa za Masoko Katika Maeneo Yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuzijengea uwezo Halmashauri za miji na wilaya kuwa na vitendea kazi vya kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za masoko, Wizara imewapatia vitendea kazi wakusanyaji wa taarifa za masoko ya mazao na mifugo walioko katika Halmashauri 93 za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji. Vifaa vinavyotolewa ni pamoja na mashine za hesabu, mizani, mavazi maalumu (viatu vya mvua, kofia na koti), simu za mikononi na vocha za muda wa maongezi. Jitihada hizi za makusudi zinatarajiwa kuongeza tija na ufanisi wa ukusanyaji, uhifadhi, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko katika ngazi mbalimbali. Aidha, taarifa hizi zitawezesha kuwepo kwa mfumo mpana na endelevu wa mawasiliano ambao utachochea ari ya sekta binafsi kushiriki katika kukusanya na kusambaza taarifa za masoko na hatimaye kuwezesha wadau kufanya maamuzi sahihi.

Kuandaa Mikakati ya Kuendeleza Soko la Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamilisha Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo na inaandaa Mkakati wa kutekeleza sera hiyo. Aidha, Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (*Tanzania Trade Development Authority – TAN-TRADE*), imetungwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu. Kanuni za utekelezaji wa sheria hiyo zinaandaliwa. Vile vile, kada ya Maafisa Biashara katika Mikoa na Halmashauri inahuishwa ili kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa biashara ya ndani na hivyo kuongeza mchango wake katika uchumi wa nchi.

Kuratibu na Kufanya Tathmini ya Ubora wa Miundombinu ya Masoko

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Leseni za Maghala imefanya tathmini ya miundombinu ya masoko kwa lengo la kuanzisha mfumo wa stakabadhi za maghala. Mfumo huu utawezesha kupunguza uharibifu wa mazao baada ya mavuno, kuongeza muda wa kuhifadhi *(shelf life)* kabla ya kuuzwa, kuimarisha ubora *(grading)* na kuwezesha wazalishaji kupata bei sahihi ya soko kwa wakati. Tathmini ilifanyika kuhusu maghala yanayoweza kutumika katika mfumo huo, vituo vya kukusanyia mazao, barabara za vijijini na miundombinu mingine muhimu kwa mazao ya korosho (Mtwara, Lindi, Tanga, Pwani na Ruvuma); pamba (Shinyanga, Mwanza na Mara); mbegu za mafuta (Singida) na mpunga (Morogoro na Kilimanjaro). Tathmini hiyo imetumika na kuwezesha kuanzishwa kwa mfumo wa Stakabadhi za Maghala katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Shinyanga, Morogoro na Kilimanjaro. Uanzishwaji wa mfumo katika mkoa wa Singida kwa zao la alizeti upo katika hatua za mwisho. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu imeendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao iliyowezesha ujenzi unaoendelea wa masoko ya mazao katika Halmashauri za Wilaya za Simanjiro, Korogwe, Kyela, Mufindi na Nkasi. Programu hii imekamilisha ujenzi wa masoko ya mazao katika Halmashauri 20.

Kuweka Mfumo Utakaowezesha Matumizi ya Maghala Kama Dhamana ya Kukopea

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa Stakabadhi za Maghala huwezesha mazao yaliyohifadhiwa ghalani kutumika kama dhamana na hivyo kuwawezesha wakulima kupata mikopo kutoka taasisi za fedha wakati wakisubiri bei nzuri ya mazao hayo. Mfumo huu umeonesha mafanikio katika mazao ya korosho, mpunga, kahawa na pamba kwa vikundi vya kibiashara; vya wakulima; Vyama vya Ushirika vya Msingi na hata mkulima mmoja mmoja. Kwa kutumia mfumo huu, wakopaji wameweza kurejesha mikopo yao kwa wakati na hivyo kuzipa imani asasi za fedha kuendelea kutoa mikopo. Kwa mfano, Mabenki ya NMB na CRDB yalitoa mikopo iliyowezesha ununuzi wa zao la korosho Mkoani Mtwara na Lindi ya tani 60,000 msimu wa 2008/2009.

Kufuatia mafanikio yaliyopatikana kwenye zao la korosho, Wizara inaendeleza utekelezaji wa mfumo huo kwa mazao ya pamba na mpunga, na inatarajia kuanzisha mfumo huo kwa mbegu za mafuta na nafaka nyingine.

Kuhimiza Matumizi ya Maghala kwa Kuhifadhia Mazao ya Wakulima kama Mkakati wa Kupunguza Upotevu wa Mazao Kabla na Baada ya Mavuno

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika aya zilizotangulia nimetoa maelezo ya kina kuhusu faida na matumizi ya mfumo wa stakabadhi za maghala. Nachukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuunga mkono jitihada za Wizara yangu katika kuhamasisha umma kuhusu faida za matumizi ya mfumo huo, ambao pamoja na faida zake, kuna wafanyabiashara wanaoupinga kwa sababu za ubinafsi wao.

Ushindani na Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa na Huduma. Katika kuendeleza ushindani na udhibiti wa ubora wa bidhaa na huduma, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 iliainisha maeneo yafuatayo ya utekelezaji:-

Kuweka Mikakati itakayoliwezesha Taifa Kuhimili Ushindani wa Biashara Kimataifa na Kuwa na Uwezo wa Kushiriki na Kufaidika na Mfumo wa Biashara ya Kimataifa katika Mazingira ya Utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhimili ushindani wa kibiashara, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imekuwa na mikakati ya kusimamia utekelezaji wa viwango vya ubora kama ifuatavyo: kutoa leseni kwa wazalishaji wanaotimiza masharti ya ubora wa bidhaa; kufanya ukaguzi wa viwanda nchini kwa nia ya kuvisaidia na kuvielekeza ili viweze kuzalisha bidhaa zenye ubora unaotakiwa; kufanya ukaguzi mipakani kwa bidhaa zinazoingia nchini na kuwezesha maabara katika nchi yetu kupata hadhi ya upimaji unaokubalika kimataifa. Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na TBS inakamilisha utaratibu wa kuanzisha Mfumo wa Upimaji wa Ubora wa Bidhaa kabla ya kusafirishwa kuja Tanzania *(Pre-shipment Verification of Conformity to Standards).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha ushindani wa kibiashara nchini, Tume ya Ushindani (FCC) ina mikakati ya kudhibiti bidhaa bandia kabla hazijamfikia

mlaji; kutoa elimu juu ya Sheria ya Ushindani kwa wadau; kuendesha kampeni za kuhamasisha walaji ili kuongeza uelewa wa masuala ya kisera na sheria za ushindani na pia juu ya haki na wajibu wa mlaji na kuunda Kamati za kanda za Kumtetea Mlaji. Aidha, Baraza la Ushindani (FCT) linapokea, linasikiliza na kuhukumu rufaa zitokanazo na kesi zinazohusu ushindani na udhibiti katika soko. Kuanzia kuundwa kwa FCT, jumla ya kesi saba na maombi 17 yalipokelewa ambapo kesi sita na maombi matatu yalisikilizwa. Kati ya kesi na maombi hayo, kesi tatu na maombi matatu yalitolewa uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha wafanyabiashara wanatumia vipimo sahihi ili kumlinda mlaji, Wakala wa Vipimo ina mikakati ya kudhibiti udanganyifu kwa kuweka stika maalum kwenye pampu za kuuzia mafuta; kuhakiki vipimo na kudhibiti matumizi ya vipimo batili kama *lumbesa*; kupiga marufuku matumizi ya mizani aina ya "*Steel Yard*" baada ya kubainika kuwa mizani hiyo ni rahisi kuchezewa (*tempered with*) na hivyo kuwaibia wakulima hasa wakati wa ununuzi wa pamba.

Kwa hivi sasa ambapo msimu wa ununuzi wa pamba umeshaanza, Wakala wa Vipimo kwa kushirikiana na Bodi ya Pamba wamekwishaanza kufanya ukaguzi katika maeneo ya ununuzi wa pamba ili kuhakikisha kuwa mizani inayotumika ni sahihi na wakulima hawaibiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusimamia haki za wabunifu na wasanii nchini, Chama cha Hakimiliki cha Tanzania (COSOTA) kina mikakati ya kuweka mawakala wa kukusanya mirabaha mikoani, kutatua migogoro kati ya wanachama, na kukamata na kuwashtaki wanaotumia kazi za wasanii bila idhini. Kuanzia mwaka 2006 hadi mwezi Juni 2009, COSOTA wamekusanya mirabaha ya shilingi 361,283,393.

Katika mwaka 2008/2009, kulikuwepo na kesi 14, kati ya hizo, 8 zimekamilika na 6 zinaendelea. Aidha, COSOTA ilipokea jumla ya migogoro 57 katika mwaka 2008/2009 na 23 kati ya hiyo imetatuliwa na iliyobakia inashughulikiwa. COSOTA imeendelea kukabiliana na uharamia wa hakimiliki (*copyright piracy*) katika mikoa ya Dar es Salaam, Ruvuma, Mtwara, Shinyanga, Tabora, Mwanza, Kilimanjaro na Arusha. Vile vile, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ina mikakati ya kuhakiki makampuni hai; kutumia TEKNOHAMA katika kusajili Makampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara, Hataza na Leseni za Viwanda.

Utafiti, Mafunzo na Maendeleo ya Teknolojia. Katika Utafiti, Mafunzo na Maendeleo ya Teknolojia, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 ilibainisha maeneo yafuatayo ya utekelezaji:

Serikali Kutafuta Wabia wa Kuendeleza Miundombinu ya Kiufundi Iliyopo Nchini Yenye Uwezo wa Kutengeneza Mashine na Mitambo (Machine Tools) na Kukuza Uwezo wa Kutengeneza Vipuri Mbalimbali

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) limeingia ubia na Kampuni ya *Serengeti Telecomm Group* (T) ili kuendeleza uzalishaji

katika Kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools Company (KMTC). Aidha, NDC kwa kushirikiana na TIRDO na TEMDO wanakamilisha upembuzi yakinifu na utafiti wa soko katika mwaka wa 2009/2010, ili kubainisha mahitaji ya vipuri na mashine ambazo zilikuwa zinazalishwa katika kiwanda cha KMTC hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za *SIDO, TIRDO, CAMARTEC* na TEMDO zimeendelea kutoa huduma za kiteknolojia katika sekta ya viwanda. Vituo vya Teknolojia *(Technology Development Centres)* vya SIDO vilivyoko katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Iringa, Kigoma na Lindi vimeendelea kutengeneza mashine na kuzisambaza nchini. Vile vile, utaratibu wa kulea wabunifu (*incubator program*) unatekelezwa na SIDO, *TEMDO, CAMARTEC, TIRDO* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Sekta ya Viwanda na Masoko na Changamoto zilizopo. Sekta ya Viwanda ina jukumu la kubadilisha Uchumi kuwa wa kisasa na unaojitegemea kwa kueneza matumizi ya Sayansi na Teknolojia za kisasa katika uzalishaji wa sekta nyingine hususan kilimo, mifugo, uvuvi, maliasili na madini. Vile vile, sekta hii ina mchango mkubwa katika kuboresha maisha ya wananchi ikiwa ni pamoja na kutoa nafasi za uhakika za ajira, kutoa mitambo na mashine zitakazo rahisisha kazi na hivyo kuongeza uzalishaji na thamani ya bidhaa. Aidha, matumizi ya sayansi na teknolojia yataongeza ufanisi na tija katika sekta hizo na hivyo kuwezesha bidhaa zinazozalishwa kuwa na ushindani katika soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwango cha ukuaji wa sekta ya viwanda kilifikia asilimia 9.9 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 8.7 mwaka 2007. Mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa uliongezeka hadi asilimia 9.4 ukilinganishwa na asilimia 9.2 mwaka 2007. Katika kipindi cha mwaka 2008, ajira katika sekta ya viwanda zilifikia 92,015 ikilinganishwa na ajira 91,112 mwaka 2007 (Jedwali Na.1). Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani hususan bidhaa za chakula na maziwa, kemikali, uchapishaji, na kuongezeka kwa bidhaa zinazouzwa nje.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji katika baadhi ya viwanda nchini, viwanda vya mbolea. Mbolea ni pembejeo muhimu katika kuboresha kilimo na kuongeza tija. Tanzania inayo malighafi nyingi ya kuzalisha mbolea za aina mbalimbali kutokana na kuwa na mwamba wa fosifati (*Phosphate rock*) na upatikanaji wa gesi asili (*natural gas*).

Malighafi hiyo itatuwezesha kuanzisha viwanda vya kutengeneza mbolea za aina zote kwa kilimo chetu hususan, *Phosphate, NPK, DAP* na *Urea* zitakazosaidia kuongeza tija kwenye kilimo, mauzo nje na kuongeza fursa za ajira kwa Watanzania.
Vile vile uzalishaji wa mbolea utakuwa kichocheo muhimu cha utekelezaji wa Mpango wa *KILIMO KWANZA* katika kuongeza tija na kuleta Mapinduzi ya Kijani na hatimaye kupunguza umaskini. Miaka iliyopita tulikuwa na kiwanda cha Mbolea cha Tanga ambacho kilikuwa kinapata malighafi yake kutoka Minjingu.

Baada ya kiwanda hicho kufungwa, kiwanda cha *Minjingu Fertilizer* kilianza uzalishaji wa mbolea za fosifati. Kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha tani 60,000 za

mbolea kwa mwaka na kimeongeza uzalishaji kutoka tani 6,500 mwaka 2005 na kufikia tani 40,000 mwaka 2008. Aidha, kiwanda kinatarajia kuzalisha mbolea ya aina ya NPK na kuongeza uwezo wa uzalishaji wa mbolea hadi kufikia tani 75,000 kwa mwaka. Kiwanda kimeajiri jumla ya wafanyakazi 441.

Taratibu za kuanzisha kiwanda cha Mbolea Mtwara kwa kutumia gesi asili zinaendelea. Makampuni kumi yameonesha nia ya kuwekeza katika kiwanda hiki. Aidha, makampuni manne yamewasilisha taarifa ya awali ya miradi yao itakayotumika kwa uchambuzi ili kumpata mwekezaji anayefaa. Makampuni hayo ni *Deepak Fertilizer and Petrochemical Ltd* na *TATA Chemicals and Petroleum Ltd* za India, *Polyserve Group Ltd* ya Misri, na *Helm Dungemittel GBMH* ya Ujerumani. Aidha, majadiliano kati ya Makampuni hayo na wazalishaji wa gesi yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya saruji, Tanzania ina malighafi zote muhimu za kuzalisha saruji katika sehemu nyingi ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika Mashariki hususan Kenya na Uganda. Malighafi hizo zitatuwezesha kuzalisha na hivyo kukidhi mahitaji ya soko la ndani na kuuza ziada nje. Tanzania kwa sasa inavyo viwanda vitatu ambavyo tayari vinazalisha saruji.

Viwanda hivyo ni *Tanzania Portland Cement Company Ltd (TPCC)*, *Tanga Cement Company Ltd*, na *Mbeya Cement Company Ltd*. Uwezo wa kuzalisha saruji wa viwanda hivi mwaka 2007 ulikuwa tani 1,770,000 kwa mwaka. Kutokana na ongezeko la mahitaji ya saruji katika miaka ya hivi karibuni, viwanda vya saruji vya TPCC Wazo na Tanga Cement viliwekeza katika kuongeza uwezo wa uzalishaji.

Kwa sasa, Kiwanda cha *TPCC* Wazo kimekamilisha upanuzi ambao umeongeza uwezo wa uzalishaji kufikia tani 1,400,000 za saruji kwa mwaka. Upanuzi huu umeongeza uwezo wa kuzalisha saruji nchini kufikia tani 2,470,000 kwa sasa. Uwezo huu unatarajiwa kufikia tani 2,970,000 itakapofikia mwishoni mwa mwaka 2009 ambapo kiwanda cha Tanga kitakamilisha upanuzi. Kiasi hiki cha uzalishaji kinatosha kukidhi mahitaji ya ndani ambayo yanakadiriwa kuwa tani 2,000,000 kwa mwaka.

Aidha ziada itakayopatikana itauzwa nje. Kwa hiyo tayari uzalishaji unaweza kukidhi matumizi ya saruji hapa nchini na kuwa na ziada kwa ajili ya kuuza nje. Aidha, sekta hii ya saruji sasa inatoa ajira ya moja kwa moja kwa wafanyakazi 1,700 na ajira nyingine nyingi zisizokuwa za moja kwa moja. Kuna Kampuni nyingine zimeonyesha nia ya kuwekeza katika eneo hilo. Kampuni hizo ni pamoja na *Athi River ya* Maweni Tanga, *Makonde Cement* ya Mtwara na *Tancem* ya Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwishoni mwa mwaka 2007, ulijitokeza upungufu wa saruji nchini uliosababisha bei ya saruji kupanda kufikia wastani wa shilingi 16,000 kwa Dar es Saam na shilingi 25,000 katika mikoa ya pembezoni kwa mfuko wa kilo 50. Upungufu huo ulitokana na ongezeko kubwa la mahitaji ndani na nje ya nchi ukilinganisha na uzalishaji. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali ilichukua hatua za makusudi kwa kuondoa ushuru wa ziada “*Suspended duty*” kwa saruji inayoagizwa kutoka nje na pia kusitisha uuzaji nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi zilizofanywa na Serikali na Viwanda katika kuhakikisha upatikanaji wa saruji, bado bei ya saruji haikushuka kwa kiwango kilicho stahili. Katika kukabiliana na hali hii, Wizara ilishirikiana na viwanda ili kuhakikisha bei za saruji inapungua kwa kiasi kinachostahili ili kumpunguzia mlaji makali ya bei. Kutokana na makubaliano yaliyofikiwa, viwanda vimechukua hatua za kufungua vituo vya usambazaji saruji katika mikoa mbali mbali nchini na kutoa punguzo kubwa zaidi la bei kwa wasambazaji wanaopeleka saruji kwenye mikoa ya pembezoni. Hivi sasa, bei ya saruji ya mfuko wa kilo 50 imeshuka kufikia wastani wa shilingi 12,000 kwa Dar es Salaam na shilingi 15,500 kwa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya nyuzi na nguo, kutokana na kuimarika kwa sekta ya viwanda vya nguo na uanzishwaji wa viwanda vipya, uzalishaji katika sekta hii umeongezeka kutoka mita za mraba milioni 99.1 mwaka 2005 na kufikia mita za mraba milioni 150 mwaka 2008, sawa na ongezeko la asilimia 34. Hata hivyo, sekta hii ya nguo inatumia asilimia 20-30 tu ya pamba inayolizalishwa hapa nchini, na kiasi kilichobaki huuzwa nje kikiwa ghafi. Kutokana na hali hiyo, mchango wake kwa uchumi wa taifa kwa njia ya ongezeko la thamani bado ni mdogo. Aidha, kutokana na msukosuko wa uchumi uliojitokeza duniani, ambao unaathiri uuzaji wa zao la pamba, napenda kuwahakikishia wazalishaji wa pamba kuwa Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Taasisi nyingine katika kutekeleza mikakati ya kuongeza matumizi ya pamba nchini ili kuwapatia wakulima wa pamba soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivi ni khanga, vitenge, *T-shirts*, vyandarua, mablanketi, *linen* na mashuka. Aidha, kiwanda cha *Tabotex* kinazalisha nyuzi na kiwanda cha Uzi Bora *Ltd.* kinazalisha nyuzi za kushonea. Wizara inachukua hatua za makusudi kuhamasisha wawekezaji kuanzisha uzalishaji wa aina nyingine za nguo na mavazi.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya ngozi, Tanzania ni nchi ya tatu Afrika kwa kuwa na mifugo mingi yenye uwezo wa kuzalisha ngozi zenye futi za mraba milioni 88.7 kwa mwaka. Mauzo nje ya nchi ya ngozi zilizosindikwa katika kiwango cha *wet blue*, *crust* na *finished leather kwa* mwaka 2007 yaliongezeka hadi kufikia Shilingi bilioni 16 kutoka Shilingi bilioni 1.6 mwaka 2005. Hili lilikuwa sawa na ongezeko mara kumi. Aidha, ongezeko hili limetokana na viwanda kuimarisha uwezo wa usindikaji na ushiriki wa wajasiriamali wadogo katika usindikaji na bei nzuri ya bidhaa hizo katika soko la nje. Pamoja na ongezeko hilo kwa mwaka 2007, bei ya ngozi zilizosindikwa pamoja na ngozi ghafi kwa mwaka 2008 zilishuka kwa kasi kutokana na mtikisiko wa uchumi na kifedha duniani. Wizara itaendelea kuwezesha na kuhamasisha uwekezaji zaidi ili tuweze kusindika ngozi zilizolundikana ili kuongeza muda wa kuhifadhi kabla ya kuuzwa *(shelf life)* na hivyo kupata bei nzuri kwa ngozi zilizosindikwa katika kipindi ambapo uchumi utakuwa umetengamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa sasa vipo viwanda vitano vya kusindika ngozi kwa kiwango cha kati - *semi-finished leather*. Viwanda hivi vina uwezo wa kusindika futi za mraba milioni 44.5 ambazo ni asilimia 50 ya ngozi yote inayozalishwa kwa mwaka. Viwanda hivi vimetoa ajira kwa wafanyakazi 440. Pia, wapo wajasiriamali wadogo 200

wanaojishughulisha na usindikaji wa ngozi kwa njia ya asili *Rural Tanning* na baadhi yao wanazalisha bidhaa za ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya chuma, Viwanda vya kuyeyusha chuma vimeongezeka kutoka viwanda vitano mwaka 2005 na kufikia viwanda 19 mwaka 2008. Ongezeko hilo limetokana na uboreshaji wa sera za uwekezaji, kukua kwa sekta ya ujenzi na udhibiti wa uuzaji chuma chakavu nje ya nchi. Kutokana na kuimarika kwa sekta hii, Tanzania hivi sasa inauza nondo nje wakati miaka mitatu iliyopita ilikuwa haiuzi nje. Aidha, Tanzania ina viwanda vitatu vya bati ambavyo vilizalisha tani 31,743 mwaka 2008, ikilinganishwa na tani 29,737 mwaka 2005 (Jedwali Na. 2).

Mheshimiwa Spika, sekta ya biashara, lengo la Sekta ya Biashara ni kuinua ufanisi na kuweka uhusiano mpana katika uzalishaji nchini, pamoja na kujenga uchumi anuai unaohimili ushindani katika masoko ya nje kama njia ya kuchochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa Sekta ya Biashara ya Ndani katika Pato la Taifa ulikua kwa asilimia 14.1 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 13.8 mwaka 2007. Katika mwaka 2008, ukuaji wa mchango wa Sekta ya Biashara ya Ndani katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 10 ikilinganishwa na asilimia 9.8 kwa mwaka 2007. Shughuli za kiuchumi zinazojumuishwa katika biashara ya ndani ni pamoja na uuzaji wa jumla, reja reja na matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008, thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi ilikuwa Dola za Marekani milioni 3,036.7 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 2,226.6 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 36.4. Ongezeko hilo lilichangiwa na ongezeko la mauzo ya bidhaa asilia na zisizo asilia. Mazao ya bidhaa za asilia yalichangia asilimia 13.8 na mauzo ya bidhaa zisizo asilia yalichangia asilimia 74.8 ya mauzo ya bidhaa nje. Aidha, asilimia 11.4 ni mauzo ya bidhaa nyingine zikiwemo mbogamboga, nta, ngozi, mbao na bidhaa za mbao. Thamani ya mauzo ya bidhaa asilia zikiwemo pamba, chai, tumbaku, korosho, kahawa, katani, na karafuu iliongezeka hadi Dola za Marekani milioni 418.4 mwaka 2008 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 319.7 mwaka 2007 ikiwa ni ongezeko la asilimia 30.9.

Ongezeko hili linatokana na kupanda kwa bei ya mazao hayo katika soko la kimataifa. Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia ilikuwa dola milioni 2,270.6 mwaka 2008, ikilinganishwa na dola milioni 1,704.5 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 28.8. Ongezeko hili limechangiwa na ongezeko la mauzo nje ya bidhaa zilizoongezewa thamani kama vile nyuzi za pamba na katani.

Thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani iliongezeka kwa asilimia 113.8 ambapo mwaka 2007 mauzo yalikuwa dola za Marekani milioni 309.8 na yalipanda kufikia dola milioni 662.3 katika mwaka 2008. Aidha, mapato yatokanayo na biashara ya huduma ikijumuisha utalii, usafirishaji na huduma nyingine yaliongezeka hadi dola milioni 2,168.9 mwaka 2008 kutoka dola milioni 1,875.7 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 15.6. Ongezeko hilo lilitokana na ongezeko la idadi ya watalii na bei za huduma katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo hali ya biashara ya nje ilibadilika

ghafla kuanzia mwishoni mwa mwaka 2008 kutokana na athari zilizotokana na mtikisiko wa uchumi duniani. (Jedwali Na. 4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na juhudi za makusudi za kukuza uhusiano wa biashara baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa ambapo juhudi hizo zimelenga kwenye kutafuta fursa za masoko yenye masharti nafuu, wawekezaji makini, na kuboresha mazingira ya kufanya biashara. Juhudi hizi zimeendelea kuleta mafanikio katika biashara ya bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeendelea kunufaika na fursa za masoko nafuu ya Jumuiya ya Ulaya na Uswisi, chini ya mpango wa Uza Kila-Kitu Isipokuwa Silaha (*Everything But Arms* - EBA). Kutokana na fursa hizo, mauzo ya bidhaa na mazao ya Tanzania kwenda Jumuiya ya Ulaya na Uswisi kwa mwaka 2008 yaliongezeka kufikia Dola za Marekani milioni 957.4 ikilinganishwa na mauzo ya Dola za Marekani milioni 759.3 kwa mwaka 2007. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 26.1. Kwa upande wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) ambayo sasa ni Eneo Huru la Biashara, mauzo ya Tanzania katika soko hilo yaliongezeka kufikia Dola za Marekani milioni 443.4 kwa mwaka 2008 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 301.1 kwa mwaka 2007, hili ni ongezeko la asilimia 47.3.

Kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo iko katika hatua ya Umoja wa Forodha, biashara miongoni mwa nchi wanachama iliongezeka kwa kasi kubwa. Mauzo ya Tanzania kwenda nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 172.8 mwaka 2007 hadi Dola za Marekani milioni 315.5 kwa mwaka 2008 sawa na ongezeko la asilimia 82.6. Ongezeko hili lilichangiwa na kukua kwa mauzo ya Tanzania kwenda Kenya kutoka Dola za Marekani milioni 101.1 mwaka 2007 hadi Dola za Marekani milioni 235.0 kwa mwaka 2008, sawa na ongezeko la asilimia 132.4. Thamani ya bidhaa zilizouzwa nchini Uganda iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 46.1 mwaka 2007 hadi Dola za Marekani milioni 53.8 kwa mwaka 2008.

Aidha, manunuzi ya bidhaa za Tanzania kutoka Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 106.5 mwaka 2007 hadi Dola za Marekani milioni 204.8 mwaka 2008, sawa na ongezeko la asilimia 92.3. Hivyo kwa ujumla kumekuwepo na urari chanya kati yetu na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2008 ambapo tumeuza bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 315.5 ikilinganishwa na manunuzi ya bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 204.8. Kwa miaka miwili mfululizo (2007 na 2008) Tanzania imekuwa na urari chanya wa biashara na Kenya. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wafanyabiashara wetu kwa kufikia hatua hii ambayo ni muhimu kwa uchumi na maendeleo yetu. Aidha, napenda kuwahakikishia kuwa Wizara yangu itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili wafanyabiashara wetu waendelee kuuza zaidi katika masoko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda nchi tunazofanya nazo biashara kwa wingi ambazo ni China, Japan, India, Hong Kong na

Umoja wa Falme za Kiarabu iliongezeka kufikia Dola za Marekani milioni 610.9 kwa mwaka 2008 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 378.2 kwa mwaka 2007. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 61.5. Aidha mauzo ya bidhaa kwenda Bara la Amerika yaliongezeka hadi Dola za Marekani milioni 64.2 kwa mwaka 2008 ikilinganishwa na Dola milioni 42.5 kwa mwaka 2007 ikiwa ni ongezeko la asilimia 51.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya manunuzi ya bidhaa kutoka nje iliongezeka hadi Dola za Marekani milioni 6,439.9 mwaka 2008 kutoka Dola za Marekani milioni 4,860.6 mwaka 2007 sawa na asilimia 32.5. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za kukuza mitaji kwa shughuli za kiuchumi katika uzalishaji viwandani, mawasiliano, uchukuzi, ujenzi na madini. Thamani ya uagizaji wa bidhaa za kati hasa ya petroli na bidhaa zake iliongezeka kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia hasa katika kipindi cha Januari hadi Oktoba, 2008. Manunuzi ya huduma yaliongezeka hadi dola milioni 1,598.0 kutoka dola milioni 1,415.4 mwaka 2007, sawa na asilimia 12.9.

Hata hivyo, uagizaji wa bidhaa za matumizi ya kawaida ulipungua, hususan uagizaji wa chakula ambao ulipungua kutoka dola milioni 315.4 mwaka 2007 hadi dola milioni 290.9 mwaka 2008 kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula nchini .

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Masoko, katika kuhakikisha kuwa biashara na mazao, bidhaa na huduma katika masoko ya ndani, kikanda na kimataifa inaendelea, Wizara inatekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na; kuendeleza usindikaji wa mazao ili kuyaongezea thamani; kutafuta mbinu za kuingia katika masoko mapya na yenye masharti nafuu; kuendeleza soko la ndani; kuendeleza miundombinu ya masoko kama vile maghala; barabara za vijijini na masoko na minada ya kuuzia mazao na mifugo; kuwezesha upatikanaji wa taarifa muhimu za masoko kwa wakati; kuweka mifumo ya kuwakinga wakulima dhidi ya mabadiliko ya bei na kujenga uwezo wa Sekta Binafsi kushiriki katika usindikaji na uuzaji wa mazao na bidhaa kwa kuzingatia mahitaji ya masoko ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, asilimia kubwa ya mazao ya asilia kama kahawa, pamba, korosho, tumbaku, ngozi na nyama huuzwa nje nchi bila kusindikwa. Kwa mfano, zaidi ya asilimia 70 ya korosho zote huuzwa nchini India zikiwa ghafi. Mwenendo wa bei ya mazao asilia katika soko la dunia kwa mazao ya kahawa, pamba, korosho, chai na tumbaku katika nusu ya kwanza ya mwaka 2008/2009 ulikuwa wa kuridhisha. Kwa mfano, bei ya kahawa ilipanda kwa asilimia 1.2, pamba kwa asilimia 17.6, korosho ghafi kwa asilimia 17.5, chai kavu kwa asilimia 18 na tumbaku kwa asilimia 31.2 ikilinganishwa na bei za mwaka 2007/2008. Hata hivyo, bei za mazao hayo zilianza kuporomoka baada ya kutokea msukosuko wa kiuchumi duniani. Kwa mfano, bei ya zao la pamba nyuzi ilishuka kutoka wastani wa Dola za Marekani 0.58 kwa ratili mwanzoni mwa mwezi Oktoba, 2008 hadi kufikia wastani wa Dola za Marekani 0.40 mwezi Novemba 2008, sawa na anguko la asilimia 45. Kushuka kwa bei ya mazao haya kulitokana na makampuni ya nje yaliyokuwa yakinunua mazao hayo kusitisha uagizaji kutokana na kukosa mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa mazao ya Tanzania hayakosi soko kutokana na kuyumba kwa uchumi wa dunia, Wizara imekutana na wadau wa ndani ili kuweka utaratibu wa kuimarisha soko la mazao hayo ndani ya nchi na kuweka mikakati ya kuyasindika mazao hayo ili kuyaongezea thamani na pia kuongeza muda wa kuyahifadhi (*shelf life*) kabla ya kuuzwa. Vile vile, viwanda vyetu vikiongeza usindikaji wa mazao, ajira zitaongezeka kwa wananchi. Hatua hiyo, iliweza kuokoa marobota 200,000 ya pamba yaliyokuwa yamekwama kuuzwa kutokana na bei ndogo. Hadi kufikia mwanzoni mwa mwezi Julai 2009, ni marobota 6,000 tu ya pamba nyuzi ya msimu wa 2008/2009 ambayo yalikuwa hayajauzwa ikilinganishwa na zaidi ya marobota 200,000 mwezi Desemba 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wastani wa bei ya mkulima kwa mazao asilia zilipanda au kushuka kutegemea mahitaji na upatikanaji wa mazao hayo katika soko la dunia. Mfano wastani wa bei ya mkulima kwa kilo ya korosho ilipanda kutoka Shilingi 610 kwa kilo mwaka 2007/2008, hadi Shilingi 675 mwaka 2008/2009, chai kutoka Shilingi 100 hadi Shilingi 115; na tumbaku ya mvuke kutoka Shilingi 1,170 mwaka 2007/2008 hadi Shilingi 1,500, mwaka 2008/2009. Ongezeko hilo ni la asilimia 10.6 kwa zao la korosho, asilimia 15 kwa zao la chai na asilimia 28 kwa zao la tumbaku. Aidha, wastani wa bei ya mkulima kwa zao la kahawa zilishuka kutoka shilingi 1,750 hadi Shilingi 1,550 katika kipindi hicho na bei ya zao la pamba ilishuka kutoka Shilingi 475 kwa kilo hadi Shilingi 450.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mazao ya chakula, kumekuwa na ongezeko kubwa la bei hasa kwa mazao ya mahindi, maharage na mchele. Wastani wa bei ya jumla ya mahindi ilipanda kutoka shilingi 18,047 kwa gunia la kilo 100 mwaka 2007 na kufikia shilingi 31,727 mwaka 2008 sawa na ongezeko la asilimia 75.8. Bei ya maharage kwa gunia lenye uzito wa kilo 100 ilipanda kutoka wastani wa shilingi 57,365 mwaka 2007 hadi shilingi 90,670 mwaka 2008 sawa na ongezeko la asilimia 58.1. Bei ya mchele iliongezeka kutoka shilingi 57,779 mwaka 2007 na kufikia shilingi 91,198 mwaka 2008 sawa na ongezeko la asilimia 57.8. Kupanda kwa bei za mazao ya chakula kulisababishwa na kuongezeka kwa matumizi mbadala ya mazao ya chakula, kupungua kwa ugavi (*supply*), kuongezeka kwa bei za pembejeo na ongezeko la gharama za uzalishaji na usafirishaji kutokana na kupanda kwa bei ya nishati ya mafuta.Changamoto, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005, Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko inakabiliwa na changamoto ambazo zinahitaji kuwekewa mikakati ya utekelezaji ili kuhakikisha kuwa malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa. Changamoto zinazoikabili Wizara yangu kwa ujumla ni pamoja na:

- Kuendeleza na kuiwezesha sekta binafsi ili itekeleze majukumu yake kama mhimili mkuu wa uchumi;
- Kuchukua hatua za makusudi za kuwalinda wazalishaji dhidi ya biashara isiyo halali hususan kutoka nje;
- Kuhakikisha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya uwekezaji na biashara;
- Kuendeleza na kuimarisha miundombinu ya uzalishaji, biashara na masoko;

- Kuhakikisha uzalishaji wa mazao na bidhaa unakidhi mahitaji ya ubora unaotoa ushindani katika soko la ndani na nje;

- Kuendeleza na kujenga uwezo wa wajasiriamali wa kuibua na kutumia fursa za uzalishaji, biashara na masoko;

- Kuendeleza na kuhamasisha uwekezaji kwenye viwanda vitakavyotumia malighafi za hapa nchini ili kuongeza ajira;

- Kujenga mazingira yatakayowezesha matumizi ya teknolojia bora na za kisasa;

- Kukabiliana na kuyumba kwa bei ya mazao na bidhaa katika masoko ya dunia;

- Kuwezesha upatikanaji wa taarifa za kisekta kwa wakati, sahihi na zinazojitosheleza; na

- Kuhamasisha mafunzo yatakayowezesha upatikanaji wa mabingwa na stadi mbalimbali katika uzalishaji na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji ya mpango wa Mwaka 2008/2009 na Malengo ya Mwaka 2010. Jukumu kuu la Wizara ni kuwezesha, kuratibu na kusimamia maendeleo ya Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko kwa kukuza ushiriki wa sekta binafsi kupitia sera, sheria, taratibu na mikakati iliyopangwa. Utekelezaji wa jukumu hili unazingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005; Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025; MKUKUTA; Malengo ya Maendeleo ya Milenia; Sera za Uchumi Jumla na Maagizo ya Viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekikti, Spika, sekta ya viwanda, katika mwaka 2008/2009 Wizara ililenga kutekeleza mambo muhimu yafuatayo: Mkakati Unganishi na Mpango Kamambe wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda nchini; kutekeleza Mkakati Unganishi wa Sekta ya Viwanda vya Ngozi Nchini; kushirikiana na Wabia katika Kuanzisha Viwanda Mama; kukamilisha Uandaaji wa Sheria ya Kusimamia Biashara ya Chuma Chakavu Tanzania; kuimarisha Taasisi za Utafiti na Teknolojia za Maendeleo ya Viwanda; na kufanya Tathmini ya Maendeleo ya Viwanda na kuendelea na zoezi la Kuperemba Viwanda Vilivyobinafsishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamilisha Rasimu ya kwanza ya Mkakati Unganishi na Mpango Kamambe wa Kuendeleza Viwanda nchini (*Intergrated Industrial Development Strategy and Master Plan-IIDS& MP*). Rasimu hiyo imewasilishwa kwa wadau mbalimbali ili kupata maoni na hatimaye kukamilisha mkakati huo kwa utekelezaji. Mkakati huu ni wa kutekeleza Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda, 1996 - 2020 (*Sustainable Industrial Development Policy - SIDP*). Nia ya Mkakati huo ni kuunganisha nguvu za wadau wengine na serikali katika kutekeleza sera hiyo kwa kuongeza uzalishaji wa bidhaa za viwandani na huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara katika kutekeleza Mkakati Unganishi wa Sekta ya Ngozi imeendesha mafunzo ya usindikaji wa ngozi kwa njia asili "*Rural Tanning*" ambayo yamefanyika kwa wajasiriamali 171 katika mikoa ya Arusha (15), Manyara (18),

Singida (20), Shinyanga (69), Mwanza (18), Mara (17) na Tabora (14). Vile vile, rasimu ya mwongozo wa mafunzo wa kufundishia utengenezaji wa bidhaa za ngozi imeandaliwa na itaanza kutumika kufundishia wajasiriamali wa bidhaa za ngozi mwaka 2009/2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya mahitaji ya kufufua na kuendeleza Chuo cha Taaluma ya Ngozi (*Tanzania Institute of Leather Technology - TILT*) imekamilika. Vile vile, uandaaji wa taarifa na takwimu *(baseline data)* sekta ya viwanda vya ngozi nchini umekamilika. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na kufufua na kuimarisha vituo vya mafunzo na uzalishaji vya Dar es Salaam na Morogoro; kununua vitendea kazi vikiwemo gari na kompyuta; na kuwezesha wadau wa sekta kushiriki katika maonesho ya bidhaa za ngozi nchini Ethiopia. Vile vile, mafunzo yalitolewa kwa watumishi wa Wizara na wadau wengine kuhusu sera na sheria ya mazingira ili kuwawezesha kusimamia na kutekeleza kikamilifu masuala ya mazingira katika uzalishaji viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uendelezaji wa viwanda mama, juhudi za kutekeleza miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga zinaendelea zikiwemo zile za ujenzi na uendelezaji wa miundombinu muhimu (*packaged projects)*. Wawekezaji wapatao 48 wameonesha nia ya kuwekeza katika miradi hii (Jedwali Na. 7). Kazi ya kubainisha mwekezaji mahiri wa kuwekeza katika mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma, mwendelezaji wa kufanya uchorongaji kwa mradi wa chuma cha Liganga na uendelezaji wa miundombinu inaendelea. Mwekezaji wa kutekeleza Mpango wa Kasi Mpya wa kuzalisha chuma ghafi (*sponge iron*) amepatikana na mazungumzo ya ubia kati ya NDC na mwekezaji yanaendelea. NDC ikishirikiana na *Geological Survey of Tanzania* (GST) imekamilisha kufanya utafiti wa awali wa kijiolojia (*Geophysical Mapping*) katika mradi wa Chuma cha Liganga ili kupata taarifa muhimu za kusaidia uelewa wa miamba (*ore body*) ilivyo na kubainisha wingi na aina ya madini pamoja na sehemu za kufanya uchorongaji. Utafiti huu umebainisha kuwepo kwa mashapo ya chuma zaidi ya tani bilioni 1.2 zilizokadiriwa awali. Vile vile, NDC imeingia ubia na kampuni ya *Pacific Corporation East Africa Limited* ya Australia kwa lengo la kufanya utafiti wa mradi wa Makaa ya Mawe katika eneo la Ngaka wilayani Mbinga. Taarifa za awali za utafiti huo zinaonesha kuwapo kwa tani milioni 179 za makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujiandaa na utekelezaji wa miradi hii, NDC kwa kushirikiana na Uongozi wa Wilaya ya Ludewa, wameandaa utaratibu wa kulipa fidia kwa wananchi watakaoathirika katika utekelezaji wa miradi hii. Utaratibu huu unajumuisha awamu nne tofauti ambazo ni:-

Kutoa elimu kwa wananchi walioko katika maeneo ya miradi; kutambua mipaka ya maeneo ya miradi; kuandaa matumizi bora ya ardhi; na kulipa fidia. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara kupitia *NDC* na kwa kushirikiana na Wataalamu wa Ardhi wa Wilaya ya Ludewa na wadau wengine wakiwemo wawakilishi kutoka vijiji vinavyohusika wamekamilisha majukumu ya kutoa elimu kwa wananchi ili kufahamu haki zao na kutambua mipaka katika eneo la Mchuchuma. Aidha, hatua zilizobakia zitafanyika baada ya kuwapata wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uliofanywa mwaka 2007 kuhusu mradi wa magadi (*soda-ash*) kupitia *NDC* ikishirikiana na kampuni ya TATA Chemicals ya India umebainisha kuwa kuna mita za ujazo milioni 217 za magadi kwenye Ziwa Natron. Kiasi hiki cha magadi kinaweza kudumu kwa miaka 46 ikiwa kiwango cha uzalishaji kitakuwa tani 500,000 kwa mwaka.

Pamoja na mradi huu kuwa manufaa makubwa kwenye fungamanisho la kisekta, utafiti wa kina unahitajika ili kuweka bayana athari za kimazingira na kiikolojia zinazoweza kujitokeza kutokana na utekelezaji wa mradi huu, ili ziweze kutafutiwa ufumbuzi kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi. Katika kuendeleza Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (SEZ), Mamlaka ya EPZ imekamilisha ujenzi wa miundombinu wa eneo la Benjamín William Mkapa, Mabibo Dar es Salaam kwa asilimia 97.

Mamlaka imeanza kuhamasisha wawekezaji wa kujenga viwanda katika eneo hilo. Wawekezaji 25 wamewasilisha maombi na kati ya hao, watano waliotimiza vigezo wamepewa leseni. Wawekezaji hawa watajenga viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, kutengeneza pembejeo na vifungashio vya bidhaa za kilimo na kutengeneza vifaa vya maabara za shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, jumla ya wawekezaji 18 wamepewa leseni za *EPZ*, ambapo wawekezaji saba ni wa ujenzi wa miundombinu ya viwanda (*EPZ Developers*) na wawekezaji 11 ni wa uzalishaji (*EPZ Operators*). Kuanzia mwaka 2006 hadi 2008 jumla ya viwanda 46 vimeshasajiliwa chini ya mpango wa EPZ; kati ya hivyo, 18 ni vya kujenga miundombinu ya EPZ na 28 ni viwanda vya uzalishaji. Viwanda hivi vimewekeza mtaji wa dola za Kimarekani 180 milioni; vimeweza kuuza nje bidhaa zenye thamani ya dola za Kimarekani 120 milioni na kuajiri wafanyakazi 7,500.

Kazi za kupima na kuthamini maeneo ya *EPZ* zimekamilika katika mikoa ya Mara, Ruvuma na Manyara ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 6.8 kinahitajika kulipia fidia. Upimaji na uthamini unaendelea katika mikoa ya Pwani, Morogoro, Arusha na Tanga. Aidha, upembuzi yakinifu (*Feasibility Study)* na utayarishaji wa matumizi ya ardhi *(land use plan)* unaendelea katika eneo la EPZ la Mbegani-Bagamoyo. Uendelezaji wa eneo la Mbegani utakuwa katika mfumo wa 'Satellite Town' na utahusisha ujenzi wa bandari ya kisasa na ujenzi wa uwanja wa ndege katika kijiji cha Zinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuboresha usimamizi na kupanua wigo wa wawekezaji katika maeneo maalumu, Wizara imekamilisha maandalizi ya Waraka wa kuunganisha mifumo ya EPZ na SEZ na kuanzisha mfumo wa Maeneo Maalumu ya Kukuza Uchumi (*Economic Development Zones* – EDZs). *(Makofi)*

Mfumo wa *EDZ* utawezesha wawekezaji wanaozalisha bidhaa kwa Mauzo ya nje *(EPZ)* na wale wa soko la ndani *(SEZ)* kuwekeza katika miundombinu ya pamoja hivyo

kuleta ufanisi katika usimamizi na kuongeza tija. Malengo ya uanzishaji wa *EDZ* ni pamoja na:-

(a) Kuwa na mfumo mmoja unganishi wa sekta mbalimbali utakaowaweka wawekezaji wa soko la ndani na nje katika miundombinu ya pamoja na hivyo kuongeza tija;

(b) Kuboresha utekelezaji na usimamizi kwa kuwa na chombo kimoja cha kusimamia maeneo maalumu;

(c) Kutoa fursa ya kuanza kutumika kwa mfumo wa SEZ;

(d) Kutumia fursa na uzoefu wa nchi za Asia hususan China, Vietnam, India na Malyasia katika kuandaa Maeneo ya Kukuza Uchumi (*Economic Development Areas*) ambayo hujumuisha miundombinu muhimu kama barabara, bandari, viwanja vya ndege, huduma na kijamii na makazi hivyo kuwavutia wawekezaji wengi katika sekta tofauti; na

(e) Kuweka msukumo katika utumiaji wa raslimali na fursa nzuri za uwekezaji zilizopo nchini ikiwa ni pamoja na malighafi zilizopo, fursa za masoko, pia amani na utulivu wa kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya EPZ kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imekamilisha maandalizi ya Mpango Mkakati wa utekelezaji wa EPZ kwa miaka mitano (*EPZ Strategic Plan*) ambao, pamoja na mambo mengine, umeweka utaratibu wa kuhamasisha uwekezaji katika maeneo ya *EPZ/SEZ* (*Promotional Strategy*); utaratibu wa kuhudumia wawekezaji (*Facilitation Strategy*) ikiwa ni pamoja na kuanzisha kituo cha kutoa huduma kwa wawekezaji *(One Stop Service Centre);* na mkakati wa kuendeleza miundombinu ya maeneo yaliyotengwa (*EPZ Infrastructure Development Strategy*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuma chakavu ni mojawapo ya malighafi katika viwanda vya chuma nchini. Chuma chakavu hurejelezwa na kutumika katika kuzalisha nondo, misumari na vyombo vya nyumbani. Hivyo, biashara ya chuma chakavu inachangia kutoa suluhisho la uchafuzi wa mazingira unaotokana na kuzagaa kwa chuma chakavu nchini.

Hata hivyo, biashara hiyo isipodhibitiwa kikamilifu, inatoa mwanya kwa wafanyabiashara wasio waaminifu kung’oa vyuma vya miundombinu na kuuza kama chuma chakavu. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za kutunga Sheria ya Kusimamia Biashara ya Chuma Chakavu Tanzania.

Aidha, Waraka wa mapendekezo kutunga Sheria ya Kusimamia Biashara ya Chuma Chakavu Tanzania upo katika hatua ya kupata maamuzi. Katika kipindi cha mpito, Serikali imepiga marufuku uuzaji nje wa chuma *(iron)* na chuma cha pua *(Steel),* shaba, *"Aluminium"* na shaba nyeupe *(Brass)* nje ya nchi kwa vile viwanda vyetu vina uwezo wa kuviyeyusha.

Aidha, kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya chuma chakavu na ukuaji wa sekta ya viwanda, Wizara yangu inaelekeza nguvu kwenye uzalishaji wa chuma ghafi *(sponge iron*) kupitia Mpango wa Kasi Mpya ili kukidhi mahitaji ya chuma nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Serikali imeendelea kuzijengea uwezo Taasisi zinazohudumia sekta ya viwanda kiteknolojia zikiwemo *SIDO, TIRDO, CAMARTEC* na *TEMDO* kwa kujenga maabara, kununua mitambo na vitendea kazi, kujenga miundombinu na kugharimia mafunzo ya watumishi ya muda mrefu na muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamilisha uperembaji na tathmini ya makampuni na viwanda vilivyobinafsishwa vilivyo chini ya Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko. Zoezi hili lilifanyika katika Kanda za Mashariki (Dar es Salaam na Pwani); Kaskazini, (Tanga, Kilimanjaro na Arusha); Nyanda za Kati na Juu Kusini (Morogoro, Iringa na Mbeya) na Kaskazini Magharibi (Mikoa ya Tabora, Mwanza na Mara). Taarifa ya awali kwenye Kanda ya Mashariki inaonesha kuna zaidi ya asilimia 50 ya makampuni na viwanda vilivyobinafsishwa nchi nzima. Aidha, utafiti huu umebainisha kuwa viwanda 28 na makampuni 7 ya biashara yaliyomo katika kanda ya mashariki yamefufuliwa.

Viwanda 16 kati ya hivyo vimewekeza zaidi ya kiwango kilichoahidiwa na viwanda 12 vimewekeza chini ya kiwango kilichoahidiwa kwenye Mikataba ya Mauzo. Makampuni 7 ya biashara yanaendelea kutumia rasilimali (assets) zilizokuwepo wakati wa kubinafsishwa. Vile vile, utafiti huo ulibainisha kuwa Makampuni ambayo yanatumia rasilimali za zamani ni yale yaliyobinafsishwa kwa utaratibu wa '*Management Employees Buy Out* (MEBO)', ambayo yanamilikiwa na wafanyakazi na menejimenti ambapo mikataba yao haikuwa na masharti ya uwekezaji. Uperembaji huo ulibainisha kuwa viwanda *BORA Shoes, Ubungo Farm Implements, Trailers and Lowloader Co. Ltd. (TRALLCO), Tanganyika Tegry Plastics, Light Source Maufactures, Ubungo Spinning Mill Ltd* na *LRT Motors Ltd.* vimebadilisha shughuli za awali kutokana na hali halisi ya mazingira katika soko.

Taarifa za awali katika kanda za Kaskazini; Nyanda za Kati; Juu Kusini; na Kaskazini Magharibi zimeonyesha kuwa kati ya makampuni 33 yaliyobinafsishwa, makampuni 20 yamefufuliwa na yanafanya kazi vizuri. Baadhi ya makampuni yaliyofufuliwa ni Kiwanda cha *Tanzania Pharmaceutical Industires, Mwatex, Tabotex, Morogoro Canvas Mill, Sabuni Industries* na *Mufindi Paper Mills.* Aidha, makampuni 11 bado hayajafufuliwa na mawili yapo katika hatua za kuyafufua. Katika jitihahada za

kuboresha upatikanaji wa takwimu sahihi za utendaji wa viwanda nchini, Wizara kwa kushirikiana na *UNIDO* imeandaa utaratibu wa kutumia mfumo wa kimataifa wa kutathmini maendeleo ya viwanda ambao utaanza kutumika mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Sekta ya Viwanda Vidogo kuondoa umaskini. Jukumu hili linafikiwa kwa kuweka mazingira bora ya kibiashara yatakayoiwezesha sekta kukua na papo hapo kuboresha huduma za kuendeleza wajasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo yaliyowekwa kwa mwaka 2008/2009 kwa Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ni pamoja na kukamilisha sensa ya viwanda vidogo na biashara ndogo; kuhamasisha uendelezaji wa ubunifu na usambazaji wa teknolojia muafaka; kuendeleza programu ya viatamizi; kutekeleza Programu ya Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini *(MUVI)* na kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya sensa ya viwanda vidogo na biashara ndogo yamekamilika. Ukusanyaji wa takwimu unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2010. Takwimu hizo zitawezesha kuandaa mipango ya kuendeleza sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara kwa kupitia *SIDO* imesambaza mashine 72 za teknolojia mbalimbali kwa wajasiriamali. Teknolojia hizo ni pamoja na za usindikaji na ufungashaji wa vyakula; utengenezaji wa majiko sanifu na nishati mbadala; utengenezaji wa matofali, chokaa, chaki na sabuni; ukamuaji wa mafuta ya kula kutokana na mbegu za mafuta; na usindikaji ngozi kwa kutumia njia za asili. Tekinolojia hizo zimesaidia kuimarisha na kuongeza ubora wa shughuli za kiuchumi na bidhaa za wajasiriamali. Vile vile, uhawilishaji wa utengenezaji wa mashine ya kupanda mbegu kwa jembe la kukokotwa na ng’ombe ulifanyika mkoani Shinyanga.

Aidha, *SIDO* imewawezesha wajasiriamali kutengeneza na kusambaza teknolojia 42. *SIDO* pia, ilitengeneza na kusambaza mashine ndogo 213 na vipuri vya aina mbalimbali 3,204. Zaidi ya hayo, Shirika hilo lilihamasisha matumizi ya teknolojia ya ubanguaji wa korosho, usindikaji wa mihogo na ukamuaji wa mafuta ya mawese katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara kupitia Taasisi ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo *(TEMDO)* imetengeneza na kuifanyia majaribio mitambo ya kutengeneza mkaa kutokana na vumbi la mkaa na mabaki ya mimea. Kadhalika, *TEMDO* imetengeneza na kujaribisha mtambo wa uzalishaji umeme kutokana na nguvu ya upepo. Mitambo hiyo kwa sasa ipo kwenye hatua ya kusambazwa kwa watengenezaji ili iweze kutengenezwa kwa wingi na kuwafikia watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kulea wabunifu unasaidia kuendeleza teknolojia mpya zinazoibuliwa na wavumbuzi. Utaratibu huu hapa nchini unatekelezwa na *SIDO*, *CAMARTEC*, *TIRDO*, *TEMDO* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa kushirikiana na Benki ya Dunia tunatarajia kuanzisha viatamizi vya mfano *(Incubators models)* vya *TEKNOHAMA* katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na vya uzalishaji wa bidhaa *TIRDO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini *(MUVI)* inatekelezwa katika mikoa sita ambayo ni Pwani; Tanga; Manyara; Mwanza; Iringa na Ruvuma. Programu hii huendeleza viwanda vidogo vijijini kwa njia ya kuendeleza mazao kwa kuzingatia dhana ya mlolongo wa thamani *(value chain)*. Katika mwaka 2008/09, yaliainishwa mazao yatakayopewa kipaumbele na pia ulifanyika ununuzi wa magari na vifaa vitakavyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, *SIDO* imetoa huduma za ushauri kwa wajasiriamali 21,922 katika maeneo ya uendelezaji wa biashara na shughuli za uzalishaji, mafunzo kwa wajasiriamali 11,203 katika maeneo ya ujasiriamali na ujuzi maalum ikiwa ni pamoja na mafunzo ya usindikaji ngozi katika mikoa ya Mara, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Singida, Manyara, Arusha, Kagera na Morogoro. Aidha, maonesho 13 ya bidhaa za wajasiriamali 2,152 yalifanyika ambapo bidhaa ziliuzwa zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.72. Vile vile, wajasiriamali 5,670 walipata mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.6 ambayo imetoa fursa za ajira mpya 13,300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Biashara. Katika mwaka 2008/2009, Wizara ilikuwa na malengo ya kukuza sekta ya biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine za jumuiya za kikanda na kimataifa hususan kwa: kuendeleza Uhusiano wa Kibiashara na Uwekezaji na Nchi za Asia, Mashariki ya Mbali na Nchi nyingine Duniani; kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kushiriki Kikamilifu Katika Mchakato wa Kuingia Katika Soko la Pamoja na kutekeleza Itifaki ya Biashara ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*; na kuendeleza Majadiliano ya Ubia wa Uchumi na Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(Economic Partnership Agreement – EPA).* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kutumia kikamilifu fursa mbali mbali za masoko ya bidhaa na huduma kama vile masoko yenye masharti nafuu ya India, China, Japan na Korea ya Kusini chini ya mpango wa uuzaji bila kiwango na ushuru (*duty free quota free*). Kutokana na juhudi hizo, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda nchi za China, Japan, India, Hong Kong na Umoja wa Falme za Kiarabu mwaka 2008 ilikuwa Dola za Marekani milioni 610.9 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 378.2 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 61.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishaeleza, Wizara yangu imeendelea kushiriki katika utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha na inashiriki kikamilifu katika majadiliano ya kuanzishwa kwa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ushirikiano huo umewezesha kukuza mauzo ya bidhaa za Tanzania kwa nchi

za Jumuiya ya Afrika Mashariki kutoka Dola za Marekani milioni 172.8 mwaka 2007 hadi Dola za Marekani milioni 315.5 mwaka 2008, sawa na ongezeko la asilimia 82.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kutekeleza Itifaki ya Biashara ya *SADC* na tarehe 17 Agosti, 2008 nchi wanachama wa *SADC* walizindua rasmi Eneo Huru la Biashara mjini Johannesburg. Majadiliano yameanza yenye lengo la kuelekea Umoja wa Forodha wa *SADC* (*SADC Customs Union*) kwa mujibu wa Kalenda ya shughuli za *SADC*. Thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 301.1 mwaka 2007 hadi Dola milioni 443.4 mwaka 2008, sawa na ongezeko la asilimia 47.3.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashauriano na wadau kuhusu Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi *(EPA)* katika ngazi ya kitaifa na kikanda yanaendelea kwa nia ya kupata misimamo ya nchi wanachama na kikanda. Majadiliano hayo yanayoendelea yalipangwa kukamilika ifikapo tarehe 31/7/2009. Hata, hivyo lengo hilo halitafikiwa kutokana na Jumuiya ya Ulaya kushinikiza kuingiza masuala ambayo ni ya hiari kama vile masuala mengine yahusuyo biashara (*trade related issues*) yaani sera ya ushindani, manunuzi ya serikali, hakimiliki na biashara, mazingira na maendeleo endelevu. Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ikiwemo Tanzania hawakubaliani na shinikizo hilo kwani maeneo hayo hayajafikiwa makubaliano chini ya mjadala na *WTO*.

Suala la msingi lililoifanya Tanzania kukubali kuingia kwenye majadiliano ya *EPA* ni pamoja na kuwa na mashirikiano ya kiuchumi na maendeleo ambayo yanalenga kupata misaada ya kifedha na kiufundi ili kukabiliana na changamoto za uzalishaji na usambazaji bidhaa. Eneo hilo lina mvutano mkubwa na hivyo kuashiria majadiliano kutokamilika kwa muda uliopangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Masoko. Katika mwaka 2008/2009, Wizara ililenga kutoa elimu kwa umma juu ya fursa za masoko na Matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala; ujenzi wa masoko ya kimataifa (*Integrated International Markets*) ya Mazao ya Kilimo; kuanzisha Mfumo Unganishi wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu ndani na nje ya nchi utakaounganisha wadau mbali mbali (*Global Intergarted Information System*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kukuza biashara ya ndani na nje, Serikali inakamilisha taratibu za kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(TAN-TRADE)* ambayo itaratibu na kusimamia maendeleo ya biashara ya ndani na nje ya nchi. Wizara inaandaa kanuni za kuanzisha Mamlaka hiyo baada ya sheria yake kupitishwa na Bunge. Pamoja na juhudi za kuanzisha Mamlaka hiyo, maendeleo ya biashara ya ndani yanapewa kipaumbele kwa kuwa zipo faida nyingi zitokanazo na soko la ndani ikiwa ni pamoja na kutoa fursa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kuuza na kuendeleza bidhaa zao, kuongeza ajira na kuendeleza teknolojia mbalimbali.

Aidha, soko la ndani ni chachu ya maendeleo ya biashara ya kimataifa. Kutokana na umuhimu wa soko la ndani, napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa Wizara na Taasisi zote za Serikali kununua bidhaa zinazozalishwa nchini kwa lengo la kulijengea

uwezo taifa kuzalisha bidhaa bora zitakazoshindana kimataifa. Ni wakati muafaka sasa Watanzania tukatekeleza wito wa “*NUNUA TANZANIA UJENGE TANZANIA*”. Wizara yangu itaandaa Waraka kwa Serikali ili suala hili liwe ni la mpango maalumu wa kukuza bidhaa zinazozalishwa nchini. Hatua hii itahamasisha makampuni ya ndani kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu imeendelea na juhudi za kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa kukamilisha taratibu za utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara. Wizara ilikamilisha kanuni za kutekeleza sheria hiyo. Utekelezaji wa sheria hii utafanywa kwa awamu, ambapo awamu ya kwanza itahusisha Halmashauri za Wilaya / Miji / Manispaa / Majiji zipatazo 24 ili kutoa fursa ya kuanisha mafanikio na maeneo yatakayohitaji maboresho. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu *TAMISEMI* inafanya tathmini ya kutambua uwezo wa Halmashauri zilizoteuliwa ili kuzijengea uwezo kwa ajili ya utekelezaji wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Bodi ya Leseni za Maghala na kwa kushirikiana na wadau wengine imekuwa ikiendesha mafunzo ya kuhamasisha jamii kutunza mazao katika maghala na hivyo kupunguza upotevu, kuongeza thamani ya mazao, kupata bei nzuri na kuwezesha upatikanaji wa mikopo. Elimu ya matumizi ya mfumo wa Stakabadhi za Maghala imetolewa katika mikoa mbalimbali ikiwa ni pamoja na Tanga, Pwani, Morogoro, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Singida, Shinyanga na Mwanza. Wizara itaendeleza juhudi za kukuza matumizi ya mfumo wa Stakabadhi za Maghala kwa kupanua wigo wa mazao na maeneo mengine; kuimarisha Bodi inayosimamia Mfumo huu kwa kuajiri watendaji wa kutosha na kuiwezesha Bodi hiyo kuwa na vitendea kazi vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaratibu maandalizi ya ujenzi wa masoko ya kimataifa katika maeneo ya Segera na Makambako kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya husika ili kuwezesha kupatikana kwa wawekezaji au wahisani watakaojenga masoko hayo. Ili kufanikisha ujenzi huo, hatua za awali ikiwa ni pamoja na upembuzi yakinifu umekamilika. Upimaji wa maeneo yatakapojengwa masoko hayo unaendelea. Ukubwa wa eneo la soko la Segera umeongezwa kutoka hekta 40 hadi hekta 500. Kamati za Usimamizi wa ujenzi wa masoko hayo zimeundwa zikihusisha wajumbe kutoka Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Halmashauri za Wilaya husika. Wizara inaendelea na taratibu za kukamilisha mpango kabambe wa ujenzi wa masoko hayo ili kuitisha mkutano wa wawekezaji.

Aidha, pamoja na uratibu wa ujenzi wa masoko hayo yatakayokuwa ya kimataifa, Wizara inaendelea na kuzishauri Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji kupanga na kuendeleza miundombinu ya masoko ili kukuza biashara katika maeneo yao. Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga imeanza mchakato wa ujenzi wa soko la Kimataifa la Kasesya. Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano katika kufanikisha ujenzi wa masoko hayo na mengine yatakayoanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kushiriki katika mchakato wa kujenga mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu za masoko utakaounganisha taarifa za kibiashara ndani na nje ya nchi. Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaandaa Mkakati wa Taarifa za Masoko ambao utawezesha kuandaliwa kwa mfumo mpana wa taarifa za kibiashara utakaounganisha wadau ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta Binafsi ina nafasi kubwa katika kubuni mikakati ya kuendeleza Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko. Kutokana na umuhimu wa Sekta Binafsi, Wizara imekuwa na vikao vya pamoja kwa lengo la kujadili na kupata ufumbuzi wa matatizo yanayokwamisha maendeleo ya viwanda, biashara na masoko na kutoa mapendekezo Serikalini. Wizara itaendeleza utaratibu huo, ikiwa ni pamoja na kutoa nafasi za kuungana nao kwenye misafara ya nje, kushawishi taasisi za fedha kutoa mikopo yenye masharti nafuu ili waweze kuongeza rasilimali zao na kuweza kuzalisha bidhaa na huduma kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushindani na Udhibiti wa Bidhaa na Huduma. Katika mwaka 2008/2009, Wizara ilikuwa na malengo ya kuratibu ushindani, sera, kanuni za biashara na kusimamia ubora wa bidhaa na huduma; kufanya majaribio ya kituo cha ufungashaji na kuwezesha maabara zake kuthibitishwa umahiri wa utendaji kazi zake' (*Laboratory Accreditation to ISO 17025*); na, kuthibitisha umahiri wa maabara za chakula, mazingira na kemia katika Taasisi ya *TIRDO* (*Accreditation of Food, Environment and Chemistry laboratories*), mafunzo, utafiti na maendeleo ya teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Ushindani *(FCC)* zimendelea na kusimamia ushindani kwa kudhibiti matumizi mabaya ya ukiritimba, uundaji magenge na muungano ambao unaathiri ushindani. Vile vile *FCC* imeendelea kutoa elimu na uhamasishaji kwa wadau jinsi ya kubainisha na kudhibiti bidhaa bandia. Tume imeendelea kufanya ukaguzi na udhibiti katika maeneo makuu ya kuingilia nchini ili kubaini bidhaa kama zinakidhi viwango vinavyotakiwa. *FCC* imeendelea kutoa elimu kwa mlaji juu ya madhara ya bidhaa bandia kwa usalama, afya, mazingira na uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Baraza la Ushindani *(FCT)* liliendelea kupokea, kusikiliza, kuhukumu na pitio za rufaa zitokanazo na ushindani na udhibiti wa soko. Jumla ya rufaa tano zilipokelewa na kati ya hizo kesi tatu zimeshasikilizwa na kutolewa uamuzi. Baraza pia limepokea maombi 13 ambayo yapo katika hatua mbalimbali za kusikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, maafisa wa *COSOTA* wamepata mafunzo juu ya masuala ya Hakimiliki ili kuongezea uwezo wa kitaalamu kwenye fani ya Hakimiliki.

*COSOTA*, pia imeendelea na zoezi la ukusanyaji wa mirabaha inayotokana na matumizi ya kazi za sanaa kibiashara kwa wamiliki wa hoteli, baa, migahawa, kumbi za disko na majumba ya starehe ili kukuza maslahi ya watunzi. Kuanzia mwezi Juni, 2008, *COSOTA* imekusanya jumla ya Shilingi milioni 89.7. Kati ya fedha hizo, jumla ya

Shilingi milioni 34.8 zimegawiwa kwa wasanii 956 wa fani ya muziki na maigizo nchini. Aidha, *COSOTA*, imetoa jumla ya leseni 305 kwa wasanii mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zoezi la ukusanyaji wa mirabaha linakabiliwa na tatizo la baadhi ya wafanyabiashara kutotoa ushirikiano kwenye kulipa mirabaha. Hivyo, kesi 30 zimefunguliwa dhidi ya wamiliki wa biashara zinazostahili kulipa mirabaha. *COSOTA* itaendelea kuwaelimisha wafanyabiashara ili wapate uelewa wa umuhimu wa kulipa mirabaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA)* katika kipindi cha 2008/2009, iliendelea kutekeleza majukumu yake ya usajili na kusimamia Sheria za Makampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara, Hataza na Leseni za Viwanda. Hadi kufikia Juni, 2009 makampuni 5,357 na majina ya biashara 11,708 yalisajiliwa ukilinganisha na makampuni 5,133 na majina ya biashara 9,946 yaliyosajiliwa mwaka 2007/2008. Alama za biashara na huduma 1,448 zilipokelewa na kati ya hizo alama 536 zilisajiliwa na Hataza 40 ziliidhinishwa hadi kufikia Juni, 2009. Mwaka 2007/2008 jumla ya alama za biashara na huduma 609 zilipokelewa na kati ya hizo 247 zilisajiliwa na Hataza 55 ziliidhinishwa. Leseni za viwanda 65 zilitolewa hadi kufikia Juni, 2009 ukilinganisha na Leseni za viwanda 80 zilizotolewa mwaka 2007/2008. Kutokana na kazi hizo BRELA ilikusanya ushuru wa stempu wa shilingi milioni 167.9 na kuwasilisha Serikalini ukilinganisha na shilingi milioni 166.7 mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2008/2009 maabara mbili za Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* ziliweza kupata vyeti vya Umahiri wa Utendaji wake wa kazi (*Laboratory Accreditation*) na kufanya jumla ya maabara nne za Shirika ambazo zina vyeti vya namna hiyo hadi sasa. Maabara hizo ni za Ugezi (*calibration*), Mikrobiolojia, Kemia na Kondomu. TBS iliendelea na jukumu la kuratibu shughuli za kuwezesha maabara katika nchi yetu kufikia viwango vya upimaji vya kimataifa (*Laboratory Accreditation*). (*Makofi*)

Kusudi la jukumu hili ni kuziwezesha maabara mbalimbali katika taasisi zetu za umma ikiwemo Shirika la Viwango Tanzania, kupima sampuli na kutoa taarifa ya upimaji (*Test reports*) zinazotambuliwa duniani kote. Wizara kupitia TBS imeanzisha kituo cha vifungashio ili kuchangia katika kuboresha ufungashaji wa bidhaa za Tanzania. Pia wajasiriamali 280 waliwezeshwa kushiriki katika mafunzo ya ufungashaji bora katika mikoa ya Lindi, Manyara, Ruvuma, Mara na Tabora. TBS itaendelea kushirikiana na taasisi nyingine katika kusimamia viwango na kumlinda mlaji na mtumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafunzo, Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia. Katika mwaka 2008/2009, *TIRDO* imetoa mafunzo kwa wajasiriamali 427 katika nyanja za kurejeleza taka za plastiki, kutengeneza chaki, usindikaji mafuta ya mawese, uyeyushaji wa chuma, uzalishaji wa uyoga na usindikaji wa vyakula. Mafunzo haya yalitolewa katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Kilimanjaro, Morogoro,

Pwani, Ruvuma na Kigoma na makampuni sita ya kanda ya Kaskazini yamefundishwa uboreshaji wa bidhaa za chuma (*Foundry Technology*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajasiriamali 105 katika mikoa ya Iringa, Morogoro, Arusha, Tanga, Pwani, Ruvuma, Mtwara na Dar es Salaam wamepata mafunzo ya usindikaji wa matunda na mboga. Wazalishaji na wasindikaji 3,574 walipatiwa mafunzo kuhusu mfumo wa ufuatiliaji (*Traceability*) kama njia ya kuhakikisha kuwa bidhaa zinazouzwa nje ya nchi zinatimiza masharti ya viwango vya ubora na usalama. Pia, viwanda 38 vilipatiwa ushauri wa kitaalamu juu ya utekelezaji wa mfumo wa ufuatiliaji. Kwa kushirikiana na sekta binafsi, shirika limeanza utaratibu wa kuanzisha mfumo wa utambulisho wa bidhaa za Tanzania kwa kuanzisha *Global Standard 1 (GS 1)* ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashine 15 za kutengeneza chaki na mashine 10 za kusindika muhogo zimesambazwa na matembe matano ya kukaushia tumbaku yalitengenezwa katika mkoa wa Ruvuma. *TIRDO* imefanya uchunguzi wa nishati ya upepo (*windmill*) na kufunga mashine inayotumia nishati hiyo yenye uwezo wa kusukuma lita 26,000 za maji kwa siku ambazo zinahudumia wakazi wapatao 5,000 katika wilaya ya Korogwe ambao wamefundishwa jinsi ya kuiendesha na kuifanyia matengenezo.

Aidha, kwa kushirikiana na sekta binafsi mkoani Morogoro, Shirika limeunda mashine ya kukamua na kuzalisha mafuta ya mawese yenye viwango vya ubora vinavyokubalika, pia kukuza tija. Shirika pia limebuni, kutengeneza na kusambaza makaushio yanayotumia nishati ya jua 14 ya matunda, mboga mboga na samaki. Wajasiriamali 33 wamepatiwa mafunzo ya kutumia na kutengeneza makaushio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha ubora wa bidhaa za viwanda vyetu zinakubalika kimataifa, *TIRDO* imeendelea na juhudi za kuhakikisha kuwa maabara zake zinatambulika kimataifa (*Accredited*) ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa na kutoa huduma bora viwandani. Maabara ya chakula na mikrobiolojia imefanyiwa uhakiki wa mwisho na imependekezwa itambulike kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu na Wananchi kwa ujumla kwamba *CAMARTEC* imehamia eneo jipya la Njiro kutoka eneo la Tengeru na Serikali imeendelea kuijengea uwezo taasisi hiyo. *CAMARTEC* imeendelea kutekeleza shughuli za utafiti, kueneza matumizi ya teknolojia sahihi na rahisi (*simple appropriate technology*) za kilimo na ufundi vijijini ikiwemo kuyajaribu matrekta na zana zake yaweze kuingia sokoni. Kupitia mkakati wake mpya Kituo kimeendelea kuimarisha wajasirimali kuchukua na kueneza teknolojia zilizokwisha kuthibitika zikiwemo teknolojia za majiko, mashine ndogo za kukamua mafuta, mikokoteni ya ng'ombe na punda. Pia, Kituo kimeendelea kujenga miundombinu na kuagiza mashine za karakana katika kujipanga upya. Programu nyingine zinazoendelea ni kujenga karakana ya

uzalishaji wa mlolongo *(flexible assembly line*), kuimarisha *TEKNOHAMA* na shughuli za majaribio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CAMARTEC* pia inaendeleza programu ya viatamizi ili kueneza teknolojia zilizokwisha thibitika. Aidha, Kituo kinaongoza mpango wa kitaifa wa kueneza mitambo midogo ya *biogas*.

Mpango unalenga katika kujenga mitambo 5,000 nchi nzima katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2008. Aidha, uhamasishaji wa wadau katika kutumia mitambo ya *biogas* kuzalisha umeme unaendelea kwa kuangalia mtambo wa mfano uliojengwa kwenye kisiwa cha Shoka huko Mwanza uliozinduliwa mwezi Aprili, 2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (*TEMDO*) katika mwaka 2008/2009 ilibuni mitambo ya kukamua na kusindika mafuta yatokanayo na michikichi (mawese na mise); kusindika matunda (nyanya, embe, nanasi); kukamua na kusindika asali na bidhaa za asali; na kusindika maziwa. Mitambo hiyo, itazalishwa na kusambazwa kibiashara na wajasiriamali ikiwa ni pamoja na *SIDO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TEMDO* imeendelea kufanya majaribio ya teknolojia ya kutengeneza mkaa unaotokana na vumbi la mkaa, vumbi la mbao pamoja na mkaa unaotokana na mabaki ya mimea kama vile *jatropha*. Mpaka sasa matokeo ni mazuri na lengo la mradi huu ni kupunguza matumizi ya kuni na mkaa unaotokana na kukata miti. Mitambo hiyo itasambazwa katika miji. Mtambo wa kuzalisha umeme utokanao na nguvu ya upepo umekamilika. Mtambo huu wenye uwezo wa kutoa Kilowati tatu (3) za umeme umetengenezwa kwa kushirikiana na mjasiriamali mmoja wa Arusha na utafungwa sehemu za *KIA* Wilayani Hai kwa majaribio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiatamizi cha Teknolojia na Biashara cha *TEMDO* kinawezesha wajasiriamali kupata ujuzi, nyenzo, teknolojia na mitandao saidizi katika kuanzisha na kukuza biashara zao. Mpaka sasa wateja hao wamepatiwa sehemu za kufanyia kazi, teknolojia (mashine na vifaa), usajili wa biashara, leseni za biashara pamoja na kuwezeshwa kushiriki maonesho mbalimbali ili kutangaza biashara zao. Mpaka sasa kiatamizi cha *TEMDO* kimeweza kutoa ajira kwa watu 150. Aidha, *TEMDO* imeendelea kutoa ushauri na mafunzo kwa viwanda vya saruji, sukari, bia, chai, kahawa, pamba, katani na vifaa vya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masuala Mtambuka, Kudhibiti Rushwa. Katika mwaka 2008/2009, Wizara iliendesha semina za namna ya kuzuia na kupambana na rushwa kwa watumishi wa Wizara na taasisi zake, kukusanya maoni ya wadau wa ndani na nje, kutekeleza mkataba wa huduma kwa wateja na kuunda timu ya kuboresha huduma kwa wateja wa nje na ndani. Vile vile, Kamati ya Kupambana na Rushwa (*Integrity Committee*) imehudhuria mafunzo ya miundo mbinu ya uadilifu.

Aidha, Wizara iliendelea na jukumu la kuelimisha umma kuhusu utendaji wa Wizara kwa kutumia vyombo vya habari. Kuhusu manunuzi, Wizara imekuwa ikifuatilia

mikataba yote ya manunuzi na kuhakikisha kuwa inatekelezwa kwa uwazi na bila upendeleo kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Janga la *UKIMWI*. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, wafanyakazi wamepatiwa mafunzo ya jinsi ya kujikinga na *UKIMWI* na kupimwa afya zao. Wizara iliwawezesha wafanyakazi kupata huduma ya kupima kwa hiari kwa kuleta watalaamu wa upimaji Wizarani. Waelimishaji rika 50 wamepatiwa mafunzo na Wizara itaendelea kuwahamasisha watumishi kupima afya zao mara kwa mara na kutoa huduma ya lishe, virutubisho (*food supplements*) na usafiri kwa watumishi wanaoishi na virusi vya *UKIMWI*. Wizara iliendelea kuhamasisha wadau wa viwanda, biashara na masoko kujali afya za wafanyakazi likiwemo suala la elimu ya *UKIMWI* mahala pa kazi. Vile vile, kwa kushirikiana na *TACAIDS* na wadau wengine, Wizara imehakikisha kinga zinapatikana mahali pa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mazingira. Katika mwaka 2008/2009, Wizara katika kutekeleza Programu ya Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi na Utunzaji wa Mazingira nchini, ilitoa mafunzo ya mazingira kwa wadau wa sekta za viwanda vya usindikaji ngozi na utengenezaji wa bidhaa za ngozi, nguo na mavazi, chuma na bidhaa za chuma pamoja na viwanda vya madawa na kemikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya Mwaka 2009/2010. Mpango na malengo ya utekelezaji kwa Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko katika mwaka 2009/2010, umezingatia changamoto zinazokabili sekta kwa ujumla. Pia utekelezaji wa mipango hiyo itazingatia miongozo mbalimbali ikiwemo mpango wa *KILIMO KWANZA* ambao unaweka kipaumbele kwenye kuboresha mfumo wa kilimo nchini. Wizara yangu itashiriki kikamilifu katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango kwa kufanya mambo yafuatayo:

(a) Kuongeza upatikanaji na usambazaji wa zana za kilimo na pembejeo hususan mbolea na madawa;

(b) Kuendeleza usindikaji ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, kupunguza upotevu baada ya kuvuna na kuongeza muda wa kuhifadhia mazao kabla ya kuuza (*shelf life)*;

(c) Kukuza uwezo wa kutumia fursa za masoko zilizopo za *AGOA*, *EBA*, China, Japan, Canada na India kwa kujenga uwezo wa kuzalisha bidhaa zenye ubora na wingi unaotakiwa;

(d) Kuendeleza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala kwenye mazao ya kilimo kama njia ya kukabiliana na mabadiliko ya bei ya mazao;

(e) Kuendeleza kilimo cha mkataba hususan mbegu za mafuta;

(f) Kuimarisha upatikanaji wa taarifa za masoko ya mazao na kuwaunganisha wakulima na masoko maalumu; na

(g) Kuendeleza miundombinu ya masoko ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda. Kwa kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara yangu imelenga kutekeleza yafuatayo katika Sekta ya Viwanda:-

- Kuendeleza zoezi la uwekezaji katika mradi wa makaa ya mawe ya Mchuchuma, Chuma cha Liganga na mradi wa magadi (*soda ash*) wa ziwa Natron; na tafiti za miradi mingine ikiwemo uanzishaji wa viwanda vya mbolea katika Kanda za Maendeleo.
- Kutekeleza Mkakati Unganishi na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda nchini.
- Kukamilisha uandaaji wa Sheria ya Kusimamia Biashara ya Chuma Chakavu Tanzania.
- Kufanya utafiti wa maendeleo ya viwanda.
- Kuandaa taarifa kuhusu fursa za uwekezaji katika miradi ya maendeleo ya viwanda.
- Kuendelea na Utekelezaji wa Mkakati Unganishi wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi.
- Kuimarisha taasisi za utafiti na maendeleo.
- Kuimarisha usindikaji wa mazao ya Kilimo na kuhamasisha uanzishaji wa Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje *(EPZ)*.
- Kukamilisha mchakato wa kuunganisha mipango ya *EPZ* na *SEZ* na utayarishaji wa Sheria ya Maeneo Maalum ya Kujenga Uchumi (*Economic Development Zones - EDZ Act*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, malengo ya Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ni pamoja na:-

- Kuendelea kutoa ushauri, mafunzo, mitaji, huduma za kiufundi kwa wajasiriamali wadogo.
- Kuzalisha na kusambaza teknolojia kwa watumiaji.
- Kuendeleza miundombinu ya viwanda vidogo na biashara ndogo.
- Kuendeleza programu ya viatamizi.
- Kukamilisha *Baseline Survey* ya viwanda vidogo na biashara ndogo.
- Kuifanyia mapitio Sheria iliyoanzisha *SIDO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Biashara. Katika mwaka 2009/2010, malengo ya Sekta ya Biashara ni pamoja na:

- Kuhamasisha matumizi ya fursa za masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.
- Kuendeleza juhudi za kukuza uhusiano wa kibiashara na nchi nyingine.
- Kuendelea kushiriki katika majadiliano ya kukamilisha uanzishwaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- Kuendelea kutekeleza Itifaki ya Biashara ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*).
- Kuendelea na majadiliano ya ubia wa kiuchumi kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Jumuiya ya nchi za Ulaya *(EU).*
- Kuendelea na majadiliano ya Duru ya Doha.

Katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Halmashauri ya Biashara ya Nje itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuimarisha Kituo cha Biashara Zanzibar.
- Kuanzisha vituo vitatu vya biashara vya kanda katika mikoa ya Mwanza, Mbeya na Arusha.
- Kuratibu ushiriki wa wajasiriamali wa Tanzania katika maonesho ya kimataifa ya ndani na nje ya nchi.
- Kufanya utafiti wa Masoko na bei ili kupanua wigo wa masoko kwa kubaini mahitaji ya masoko kwa bidhaa zetu.
- Kuandaa na Kuongoza Maonesho ya Kibiashara ndani na nje ya nchi.
- Kuanzisha programu ya kuwa na utambulisho wa kitaifa kwa bidhaa *(branding*).

Sekta ya Masoko. Katika mwaka 2009/2010, Sekta ya Masoko itaendelea kushughulikia upatikanaji wa masoko ya kikanda na kimataifa na kuimarisha mikakati ya kuimarisha soko la ndani. Ili kutimiza azma hii Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- Kukamilisha Mkakati wa Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo.
- Kutekeleza Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje; na Mpango Unganishi wa Biashara *(Tanzania Trade Integration Strategy - TTIS).*
- Kuendeleza biashara ya ndani.
- Kuendeleza mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara *(TAN-TRADE).*
- Kushirikiana na Sekta Binafsi katika kubuni na kutekeleza mikakati ya masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.
- Kuendeleza na kuboresha mfumo wa ukusanyaji, uhifadhi, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko.

- Kuendeleza miundombinu ya masoko.
- Kuendeleza utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani.
- Kushirikiana na sekta binafsi katika kutekeleza mpango wa *"KILIMO KWANZA"*.
- Kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa kutekeleza Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara (BARA).
- Kuwezesha uanzishwaji wa kilimo cha mkataba kwa mazao ya mbegu za mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushindani na Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa na Huduma. Shirika la Viwango Tanzania kwa mwaka 2009/2010 litaendelea kutayarisha viwango vya kitaifa; kutoa leseni za ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini na zinazoagizwa kutoka nje. Wizara kupitia, Shirika itaendelea kutoa mafunzo ya ufungashaji wa bidhaa kupitia Kituo cha Ufungashaji (*Packaging Technology Centre*) kwa wazalishaji na wafanyabiashara.

Vilevile, Kituo kitatoa huduma za kupima sampuli za vifungashio kwa lengo la kuhakiki ubora wa vifungashio (*packaging materials*) vinavyozalishwa hapa nchini na vile vinavyotoka nje ya nchi. Juhudi hizi zitachangia katika utekelezaji wa Mpango wa *KILIMO KWANZA*. Shirika litaendelea na juhudi za kuhakikisha kwamba maabara zote za mashirika zinapata vyeti vya umahiri wa utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa bidhaa zinazoingia nchini zina ubora unaokubalika, Shirika litaendelea kufungua vituo vya ukaguzi mipakani na kuanza utekelezaji wa mfumo wa ukaguzi wa ubora wa bidhaa kabla ya kuingizwa nchini *(Pre–shipment Verification of Conformity to Standards).* Utaratibu huu utaanza kutumika ifikapo mwezi Oktoba 2009. Shirika litaendeleza zoezi la kufanya ukaguzi wa viwanda vyote hapa nchini.

Aidha, TBS itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Udhibiti (*Regulatory Bodies*) kama vile *TFDA*, *EWURA* na *WMA* ili kuhakikisha kuwa biashara nchini inaendeshwa kwa misingi ya haki na kumlinda mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Ushindani katika mwaka 2009/2010 itaendelea kukuza na kulinda ushindani katika uchumi kwa kuendesha mafunzo kwa wadau, kufanya utafiti kuhusu ushindani katika soko na kushughulikia mashauri yanayohusu ushindani. Aidha, katika jukumu la kumlinda mlaji, Tume itaendeleza mapambano dhidi ya bidhaa bandia, pia itaendelea kutoa elimu kwa mlaji husussan, kuhusu haki na wajibu wa mlaji. Tume itaendelea pia kutoa huduma za Sekretarieti kwa Baraza la Taifa la Kumtetea Mlaji, hivyo kuendeleza jitihada za uanzishaji na uendelezaji wa Taasisi huru za Utetezi wa Mlaji. (*Makofi*)

Baraza la Ushindani *(FCT)* litaendelea kusikiliza mashauri ya rufaa kutoka Mamlaka za Uthibiti ikiwemo Tume ya Ushindani. Pia, Baraza litatoa elimu kwa umma kuhusu majukumu yake kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa 2009/2010, Wakala wa Vipimo utaendelea na jukumu la kuhakikisha kuwa vipimo sahihi vinatumika katika

biashara. Uhamasishaji zaidi wa kutambua faida za vipimo sahihi utaendelea kufanyika katika mikoa mbalimbali. Aidha, Wakala wa Vipimo utapanua maeneo ya kazi zake kwa kusimamia usahihi wa vipimo katika sekta za Afya, Usalama na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, *COSOTA* itafungua ofisi za kikanda mkoani Mwanza kwa kanda ya Ziwa, Mbeya kwa kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Dodoma kwa kanda ya Kati na Magharibi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafunzo, Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Chuo cha Elimu ya Biashara kwa kushirikiana na taasisi rafiki za nje na ndani ya nchi kitajikita katika kuanzisha mafunzo katika ngazi za cheti na stashahada katika eneo la ujasiriamali; kuimarisha na kupanua miundombinu ya kufundishia; kuimarisha mafunzo kwa walimu na kuboresha mitaala. Vile vile Chuo kinakamilisha taratibu za kuanza kutoa mafunzo ya ujasiriamali katika ngazi ya shahada. Aidha, katika ya Chuo kitaendeleza na kuimarisha kada ya kati ya wafanyakazi katika maeneo ya Uhasibu, Masoko, Ununuzi, Ugavi, Uongozi wa Biashara, Mafunzo ya Kompyuta, Mizani na Vipimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/2010, *TIRDO* itaendelea kufanya utafiti katika kuzalisha bidhaa kutokana na mabaki ya mazao ya kilimo; *food stabilizers*; ubora wa chumvi inayotokana na maji ya bahari; uyoga wenye sifa za tiba; kusambaza teknolojia za matumizi ya nishati ya jua na upepo; na usindikaji na uyeyushaji wa vyuma. Aidha, *TIRDO* itahakikisha maabara zake zinathibitishwa umahiri wa utendaji (*Accreditation*) ili zikubalike kimataifa; itashirikiana na sekta binafsi kusimamia uanzishwaji wa mfumo wa kimataifa wa utambuzi wa bidhaa (*Bar code*); na itasajili bidhaa za Tanzania katika mfumo wa kimataifa wa utambuzi (*Global Standard 1*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, *CAMARTEC* imepanga kutekeleza ujenzi wa karakana ya kuunda mashine (*Flexible Assembly Line)*; kuendelea na utengenezaji wa trekta ndogo 20; kuimarisha kitengo cha majaribio ya zana za kilimo na teknolojia za vijijini; na kuendeleza matumizi ya mashine za kupanda moja kwa moja kwenye kilimo hifadhi (*Direct seeders/drills*).

Vilevile, *CAMARTEC* itasambaza mitambo mikubwa ya *biogas* ya uzalishaji wa umeme na mitambo midogo ngazi ya kaya; kuimarisha Kitengo cha Uatamizi wa Teknolojia na Kitengo cha Kuegesha Teknolojia (*Technology Park*); na kuendelea na utengenezaji wa gari la gurudumu tatu kwa ajili ya usafirishaji katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, *TEMDO* imelenga kuendelea kubuni, kuendeleza na kusambaza mitambo ya kusindika mazao ya kilimo na mifugo, kusindika ngozi na bidhaa za ngozi, na nishati mbadala. Aidha, *TEMDO* itaendelea kutoa huduma ya kiatamizi cha teknolojia na biashara ili kuwezesha wajasiriamali 10 kuingia kwenye biashara rasmi kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masuala Mtambuka, Kudhibiti Rushwa. Katika kipindi cha 2009/2010, Wizara itaendelea kuelimisha na kubaini mianya ya rushwa hivyo kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Janga la *UKIMWI*. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya jinsi ya kujikinga na *UKIMWI* na kuhamasisha upimaji wa afya za wafanyakazi kwa hiari. Wizara itaendelea kuwawezesha wafanyakazi kupata huduma ya kupima, lishe, virutubisho *(food supplements)* na usafiri kwa watumishi wanaoishi na virusi vya *UKIMWI*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mazingira. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati inayohusu masuala ya utunzaji na usimamizi wa mazingira pamoja na Programu ya Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi na Utunzaji wa Mazingira kwa wadau wa Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko nchini.

Aidha, Wizara imejipanga kuendelea kufuatilia na kushughulikia uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za viwanda ikiwa ni pamoja na viwanda vya kusindika ngozi, nguo na chuma ambavyo vimekuwa vikilalamikiwa sana na wananchi kuwa shughuli zao zinachafua mazingira. (*Makofi*)

Maendeleo ya Rasilimali Watu. Wizara ina jumla ya Watumishi 203 ikilinganishwa na Ikama ya Watumishi 243, ambayo ni pungufu kwa watumishi 40. Kati ya watumishi hao 203, watumishi 14 ni waajiriwa wapya. Hata hivyo, wengi wa watumishi hao wanatarajia kustaafu hivi karibuni. Aidha, kuna pengo kubwa kati ya watumishi wa ngazi ya juu na chini. Hivyo, Wizara inachukua juhudi za makusudi kuhakikisha kuwa mpango wa kurithishana madaraka (*Succession Plan*) unazingatia changamoto hiyo.

. Kwa msingi huo, Wizara itaendelea kuajiri, kutoa mafunzo na kupandisha vyeo watumishi wake katika ngazi mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, jumla ya Watumishi 48 walipata mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika taasisi za elimu ndani na nje ya nchi. Aidha, watumishi 42 walipandishwa vyeo. Wizara kwa mwaka wa fedha 2009/2010 inatarajia kuajiri watumishi 20, na pia itatoa mafunzo na kujenga uwezo wa watumishi wake kulingana na mpango wa mafunzo.

Shukrani. Napenda kuzishukuru nchi rafiki ambazo kwa njia moja au nyingine zinawezesha Wizara yangu kufanya kazi kwa ufanisi. Nchi hizo ni pamoja na Austria, Canada, China, Denmark, Finland, Korea ya Kusini, Ireland, Norway, Uswisi, India, Japan, Marekani, Sweden, Uholanzi, Uingereza na Ujerumani. Na mwisho shukrani zangu za kipekee ni kwa Mashirika ya *UNIDO, ILO, IFAD, WTO, UNCTAD, UNDP, OPEC Fund, WIPO, ITC, CFC,* Benki ya Dunia *(WB),* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* ambazo zimetoa mchango mkubwa katika kufanikisha shughuli mbali mbali za Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko. Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2009/2010. Matumizi ya Kawaida. Wizara na taasisi zilizo chini yake inaomba kutengewa jumla ya Shilingi 26,498,512,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ili iweze kutekeleza majukumu niliyoelezea ya kuendeleza sekta za Viwanda, Biashara na Masoko kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Kati ya fedha hizo, shilingi 17,080,079,900 ni kwa matumizi ya mishahara na shilingi 9,418,432,100 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara na taasisi zake. Matumizi ya Maendeleo. Wizara inaomba jumla ya shilingi 29,206,157,000 kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo katika Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, ninaomba kutoa maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99 (7) Toleo la Mwaka 2007, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunilinda na kunipa uhai hadi kufikia siku ya leo ninapowasilisha maoni haya. Pili, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuwashukuru Wapiga Kura wangu wa Jimbo la Magomeni Zanzibar, kwa imani yao waliyonipa ya kuwa Mbunge wao. Na mimi ninawaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nia safi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokutana na Uongozi wa Wizara, Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko aliieleza Kamati kuhusu masuala yafuatayo:-

- Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.
- Mapato na Matumizi hadi Juni 2009.
- Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.
- Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nampongeza Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, (Mb) kwa Hotuba yake nzuri aliyoitoa hivi punde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati. Kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, Kamati yangu ilitoa Mapendekezo na Maagizo 13. Kamati

inaipongeza Serikali kwa kutekeleza baadhi ya Maagizo kwa ukamilifu. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutekeleza maagizo ambayo hayakutekelezwa kikamilifu au kutotekelezwa kabisa.

Kwa mfano, hatma ya Kiwanda cha Magurudumu cha Arusha, mpaka wakati huu haijafahamika, Miradi ya Chuma cha Liganga na Makaa ya Mawe Mchuchuma bado ni masuala tete. Hali kadhalika, jitihada za kuyaongezea nguvu za kifedha mashirika ya *NDC* na *SIDO* hazijaridhisha na suala zima la Wamachinga wageni kuendelea kufanya biashara ambazo zinaweza kusimamiwa na wananchi bado halijapatiwa ufumbuzi.

Makadirio ya Matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo. Katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, Wizara imetengewa Shilingi Bilioni Sita, Milioni Tisini, Laki Tano, Sabini na Nane Elfu (6,090,578,000/=) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na taasisi zake zimetengewa Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Nne na Saba, Laki Tisa, Thelathini na Nne Elfu (20,407,934,000/=). Hivyo, jumla ya Matumizi ya Kawaida ni Shilingi Bilioni Ishirini na Sita, Milioni Mia Nne Tisini na Nane, Laki Tano, Kumi na Mbili Elfu (26,498,512,000/=). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2009/010 Shilingi Bilioni Ishirini na Tisa, Milioni Mia Mbili na Sita, Laki Moja, Hamsini na Saba Elfu (29,206,157,000/=), zimetengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Tatu Thelathini na Nane, Laki Nne, Ishirini na Tatu Elfu (19,338,423,000/=), ni fedha za ndani na Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Nane Sitini na Saba, Laki Saba, Thelathini na Nne Elfu (9,867,734,000/=) ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati. Masuala ya Jumla. Wakati Kamati inajadili Taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ilipata fursa ya kuzungumzia Msukosuko wa Uchumi ambao unaendelea Duniani kote na jinsi unavyoathiri Sekta ya Viwanda na Biashara. Kamati yangu iliitahadharisha Wizara kuhusu umuhimu wa kuweka mikakati ya kujihami na kujinasua na janga hili kubwa na la kihistoria kama ambavyo baadaye lilifafanuliwa vizuri na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Fedha na Uchumi katika hotuba zao hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inapendekeza yafuatayo kuhusu janga hilo:-

·Kutokana na hali ya Uchumi Duniani kuyumba, Kikundi Kazi kinachoongozwa na Gavana wa Benki Kuu kitoe mapendekezo yake kwa wakati kuhusiana na Sekta ya Viwanda na Biashara na Serikali iyafanyie maamuzi mapendekezo hayo haraka iwezekanavyo. Itakuwa jambo zuri iwapo Serikali itakuwa ikitoa taarifa katika kila

mwanzo wa Mkutano wa Bunge kuelezea hali ya msukosuko dhidi ya Uchumi na Mwenendo wa Sekta ya Viwanda.

·Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na Serikali kwa ujumla isisite kuingilia kati na kufanya maamuzi ya haraka haraka kwa madhumuni ya kunusuru Viwanda muhimu (*Strategic),* kimoja kimoja au kisekta kwa uchumi wa nchi, hususan vile vinavyoendana na utekelezaji wa Sera ya Kilimo Kwanza na

·Jitihada zaidi zifanyike kutafuta misaada ya Kimataifa ili kunusuru uchumi wetu. Hii ikiwa ni pamoja na kufuatilia maamuzi ya Kundi la Nchi Tajiri Duniani, *(G8).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuingia kwenye Uchumi wa Soko, biashara ya ndani ilikuwa na mpangilio mzuri wa kusimamia shughuli hii. Soko la ndani lilikuwa ni msingi imara ulioendeleza Kilimo na Viwanda. Hivi sasa, soko la ndani limevurugika na hivyo, kwa kiwango kikubwa, kuathiri ukuaji wa Viwanda na Kilimo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefarijika kwa Serikali kutambua kasoro hiyo na kuleta Bungeni Muswada wa kuanzishwa kwa Mamlaka ya Biashara *(TANTRADE)* ambayo inatarajiwa kuondoa mapungufu hayo. Ni vema Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ikaharakisha ukamilishaji wa Kanuni ili *TANTRADE* ianze rasmi kazi zake katika Mwaka huu wa Fedha, ili biashara ya ndani ipate fursa ya kuchangia viwanda na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitika kwamba zaidi ya miaka miwili baada ya Sheria ya Biashara (*BUSINESS LICENCING AND REGISTRATION ACT)* kupitishwa na Bunge lako Tukufu bado utekelezaji wake haujaanza. Kutokufanya hivyo kunakwaza wawekezaji pamoja na kuongeza gharama za kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhusiano wa Sekta za Kilimo na Viwanda. Shughuli za Sekta za Kilimo na Viwanda zinategemeana sana katika kuibua uchumi wa nchi yetu. Dhamira ya Taifa ni kuwa na uchumi wa kati *(Semi-Industrialized Economy)* ifikapo Mwaka 2015 na msingi wake ni kuanza na viwanda vya kusindika mazao (*Agro-based Industries)*. Kwa mantiki hii, ni muhimu Sekta ya Kilimo ikaihusisha Sekta ya Viwanda na Biashara ili aina ya uzalishaji wa mazao ukalingana na mipango ya Sekta ya Viwanda. Kwa kufanya hivyo, nchi itaondokana na uuzaji wa bidhaa ambazo hazijasindikwa *(raw-commodities)* na kwa maana hiyo hiyo kuwa na uuzaji wa bidhaa nje zenye ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima sekta hizi mbili ziwe wanandoa kweli kweli. Haiwezekani tukawa na Kilimo juu kwanza na Viwanda vikawa uvunguni halafu tukategemea kupata maendeleo. Kushamiri kwa ndoa hii kunategemea sana kuwepo kwa uwiano wa sera, mikakati ya kifedha, na vipaumbele vinavyowiana kati ya Sekta hizi mbili, ikiwa tunadhamiria kilimo kupanuka na kuzalisha kwa ufanisi na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosisitiza umuhimu wa kuweko mahusiano ya karibu baina ya sekta hizi mbili, ni dhahiri mafaniko ya kauli mbiu ”Kilimo Kwanza” matarajio yake hayatafikiwa ikiwa viwanda vinavyoshabihiana navyo havipewi kipaumbele. Leo hii viwanda kama vile vya matrekta na zana zake, na vya pembejeo havipo.Kwa mtazamo huu, Sekta ya Viwanda inabidi ipewe nafasi yake ya kuongoza Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muundo na Majukumu ya Wizara na Taasisi zake. Kutokana na majukumu mazito na, umuhimu wa mashirika yaliyo chini ya Wizara na mahusiano na wadau muhimu kama *CTI, TCCIA, TPSF*, na kwa kuzingatia mahusiano baina ya Wizara hii na taasisi za Kikanda na za Kimataifa; mfano *EAC, SADC, AU, EU/ACP (EPA), WTO, UNIDO, UNCTAD, ITC, WIPO n.k.*, Kamati inaamini kuwa muundo na rasilimali zilizopo kwa Wizara hazikidhi majukumu haya mengi na mazito waliyokabidhiwa.

Hivyo, Kamati inapendekeza Serikali ifanye tathmini ya kitaalam ya muundo huo kwa lengo la kuboresha utendaji wake ili kuongeza ufanisi. Tathmini na mapendekezo hayo yazingatie mahitaji ya rasilimali watu, fedha, miundombinu, na mifumo, kulingana na mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Utafiti na Maendeleo. Kamati imebaini kuwepo kwa taasisi nyingi za Huduma, Utafiti na Maendeleo ya Viwanda ambazo majukumu yake yanaingiliana; kwa mfano *SIDO, CARMATEC, TIRDO na TEMDO*. Zote zinafanya utafiti, kutengeneza vifaa vidogo vidogo vinavyofanana na kuanzisha shughuli za viatamizi. Kamati inapendekeza shughuli zao zihuishwe na ikiwezekana ziunganishwe kwa lengo la kupunguza gharama na kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi Nyingine za Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Kamati ilipata fursa ya kutembelea baadhi ya taasisi zilizo chini ya Wizara na kupata taarifa, na ina maoni yafuatayo :-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)*. Kumekuwepo na sheria mbili zinazokinzana zinazosimamia shughuli za *NDC;* hivyo kuathiri uwekezaji hasa kwa wale wanaotoka nje. Kamati inashauri Serikali iharakishe kutunga Sheria mpya ya *NDC* itakayokidhi mazingira ya uwekezaji kwa wakati huu. Kutokana na mtaji wa *NDC* kuwa mdogo, kulingana na majukumu yake hivi sasa na baadae, ni dhahiri kwamba, ipo haja kwa Serikali kutunisha mtaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa ajili ya Mauzo ya Nje *(EPZA)*. Lengo la kuanzishwa kwa Mamlaka hii ni kukuza uzalishaji kwa ajili ya uuzaji nje wa bidhaa za Tanzania, hususan kwa kukuza viwanda, kukuza mauzo ya nje, kuongeza ajira, kukuza teknolojia, kuunganisha bidhaa zetu na masoko ya kimataifa, kuhamasisha usindikaji wa mazao na kuongeza mapato ya fedha za kigeni

ambayo yatachangia katika uchumi na kuondoa umaskini. Aidha, mpango wa *EPZA* unatoa fursa kubwa ya ajira kwa watu wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya jukumu la EPZA ni kuhudumia wawekezaji. Wawekezaji wangehitaji kukaribishwa na kuhudumiwa katika ofisi zenye hadhi na hivyo kuwa na imani na Mamlaka. Hivyo kwa kuwa Mamlaka hii haina ofisi zenye hadhi, hali hii inachangia kukosa wawekezaji kwa kukosa imani na Mamlaka. Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko iisaidie Mamlaka kupata ofisi yenye hadhi ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa miundombinu ni kigezo muhimu sana katika kuwekeza, Kamati inashauri Serikali kuweka miundombinu mapema, ikiwemo umeme, maji, reli na barabara katika maeneo ya uwekezaji kabla ya kukaribisha wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana wawekezaji wa ndani hawana mwamko mkubwa wa kuwekeza katika miradi hii. Kamati inashauri Serikali kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuwekeza na kuwahamasisha wawekezaji wa ndani ili nao waweze kunufaika na faida itokanayo na Mamlaka hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na malengo mazuri ya *EPZA* kwa ajili ya mauzo ya nje, Kamati imebaini kwamba utekelezaji wake unasuasua. Ikiwa eneo la Mabibo lililoko Dar es Salaam ambapo fursa zote zinapatikana kwa urahisi limechukua muda mrefu kukamilika.Hivyo itachukua muda gani kukamilika kwa maeneo kumi na mbili (12) yaliyokwisha tengwa?. Hali kadhalika, mpango wa Mini Tiger 2020 hatma yake ikoje?. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mkakati wa kuharakisha utekelezaji wa malengo iliyojiwekea. Baraza la Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani. Pamoja na uzuri wa Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani, Mfumo huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Kutofahamika kwa wadau wengi.
- Kutokuwa na mtandao mpana nchini.
- Kutokuwa na ofisi.
- Kutokuwa na watendaji, akiwemo Mtendaji Mkuu.
- Kuwepo kwa mwingiliano wa usimamizi kati ya Wizara tatu - *TAMISEMI*, Viwanda, Biashara na Masoko, na Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri shughuli za Baraza na Bodi zisimamiwe na Wizara yenye dhamana ya mazao, pamoja na kuiwezesha kutimiza wajibu wake kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Vipimo na Mizani *(WEIGHTS AND MEASURES AGENCY)*. Kamati imebaini changamoto zifuatazo katika Wakala wa Vipimo na Mizani:-

- Sheria ya Vipimo ya 1982 imepitwa na wakati.
- Wakala umegubikwa na matatizo ya ofisi na vitendea kazi,hasa magari.
- Upungufu mkubwa wa mizani kubwa na ndogo nchi nzima.
- Kuingizwa kwa mizani zisizokidhi viwango.
- Gharama kubwa za ushuru kwa mizani zinazoingia nchini kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kushughulikia hangamoto hizi haraka iwezekanavyo. Aidha, Serikali isimamie ubora wa mizani zote zinazoagizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Magurudumu *(GENERAL TYRE EA. LTD)*. Kiwanda hiki kina wafanyakazi 318 ambao baada ya kiwanda kufungwa wako nyumbani na Serikali inawajibika kuwalipa mishahara yao ya kiasi cha TSh. Milioni Mia Moja na Ishirini (120,000,000.00) kila mwezi bila kufanya kazi.

Aidha, kuna mashine 79 zenye uwezo wa kufanya kazi, ambazo zimesimama kutokana na kufungwa kwa kiwanda. Serikali ikiwa na hisa asilimia 76, ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba rasilimali kama hii haina tija, katika kuchangia Pato la Taifa na wakati huo huo ujuzi wa wafanyakazi ukitoweka. Kufungwa kwa Kiwanda kumekuwa chanzo cha wafanyakazi kujiona yatima – hawana Baba wala Mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kunusuru teknolojia, mitambo na watalaam waliopo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ufufuaji wa kiwanda kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usajili na Leseni *(BRELA). BRELA* inafanya kazi ya kukutana na wawekezaji wa aina mbalimbali na hivyo inastahili kuwa na ofisi nzuri yenye kuwavutia wawekezaji na kuwa na imani na Wakala huu.

Kwa hali ya kusikitisha Wakala huu muhimu hauna ofisi yenye hadhi na hivyo kuwakatisha tamaa na kuwakosesha imani wawekezaji na Wakala. Kamati inashauri Serikali kuona uwezekano wa kuanza kutenga fedha kidogo kidogo ili *BRELA* waweze kujenga ofisi nzuri na yenye hadhi inayolingana na ofisi za TIC. Hii ifanyike pia kwa taasisi nyingine ambazo hazina ofisi, au zenye ofisi zisizostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenendo na Changamoto za Viwanda. Mwenendo wa Viwanda hapa nchini hauridhishi kutokana na kukabiliwa na changamoto nyingi kama ifuatavyo:-

- Miundombinu duni kwa maana ya , maji yasiyotosheleza, kukosekana kwa umeme wa uhakika na usiotosheleza, kutokuwepo kwa maeneo yaliyopimwa mahususi kwa ajili ya viwanda, kutokuwepo kwa njia za kutosha za kusafirishia mali ghafi na bidhaa za viwandani.

- Urasimu hasi bandarini na kwingineko.

- Mfumo wa kodi unaoathiri viwanda vya ndani; mfano viwanda vya viberiti , nguo, saruji, magunia, maziwa na ngozi.

- Ugumu wa kupatikana mikopo na gharama kubwa ya riba.

- Ushindani usio wa haki wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi dhidi ya bidhaa za ndani mfano sukari, kahawa, maziwa, viberiti, chai na hasa bidhaa feki na zilizo chini ya viwango.
- Ukosefu wa vivutio kwa viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotokana na kilimo, uvuvi, ufugaji n.k.

- Kasumba ya wananchi kutothamini bidhaa zinazozalishwa nchini.

- Kutokuwepo kwa sera na mkakati wa upendeleo maalum kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini kwa mfano samani za maofisini, vifaa vya shule na maabara, nyaya za umeme na transforma.

- Kukamilisha Sera ya Masoko na kuharakisha ujenzi wa masoko ya Kimataifa ya matunda na bidhaa za mbogamboga ya Segera na Makambako, pamoja na kuimarisha masoko ya msingi (*primary markets).*

Mheshiwa Mwenyekiti, Kutokana na changamoto hizi bidhaa zetu zimeendelea kuwa ghali na hivyo kushindwa kuhimili ushindani. Ili kuzikabili changamoto hizo na kuendeleza sekta hii, kamati inapendekeza hatua zifuatazo zifanyike:-

- Kuongeza ushuru wa bidhaa zinazoingizwa katika soko la ndani na zinazoleta ushindani usiokuwa wa haki (Unfair competition), dhidi ya bidhaa za viwanda vichanga vya Tanzania, kulingana na Sheria za WTO, kama mafuta ya kupikia, nguo,magunia, mavazi, viatu, mikoba n.k.

- Kuvilinda viwanda vyetu na kuwahamasisha wananchi na taasisi zetu kuthamini bidhaa zinazozalishwa nchini.

- Kuweka mazingira wezeshi ya kupunguza gharama za uzalishaji.

- Kubuni mikakati mipya yenye nia ya kuendeleza na kuviwezesha viwanda vidogo na vya kati vya wajasiriamali wetu ikiwemo mafunzo, mitaji na masoko kulingana na mahitaji.

- Kuwepo na mkakati ambao utawavutia wawekezeji wa usindikaji wa mazao ya kilimo (*Agro based Industries*) na bidhaa zinazohitajika kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi. Kamati imebaini wakati umefika kuchukua hatua za makusudi kwa wananchi kumiliki viwanda na biashara kwa viwango vya juu zaidi kwa sababu Watanzania wengi sasa wana elimu ya kutosha isipokuwa hawana mitaji. Kamati inaona kwamba Mifuko ambayo imeanzishwa ni midogo mno; hivyo tunahitaji ubunifu zaidi kuanzisha mifuko inayokidhi mahitaji, mfano *Venture Capital Fund* na Benki Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefarijika na kazi nzuri inayofanywa na *SIDO* ya kuwawezesha wajasiriamali wadogo, wakiwemo wale wanaobuni miradi mipya kwa mpango wa viatamizi (incubators). Kutokana na uzoefu wao wa miaka zaidi ya thelathini na mtandao wao mpana na mkubwa kuwafikia wajasiriamali nchi nzima, Kamati inapendekeza *SIDO* iwe miongoni mwa taasisi zinazofaidika na Mfuko wa Mabilioni ya Mheshimiwa Rais, ikiwa ni pamoja na kufikiria kwa makini zaidi vyanzo vingine vya kukuza mtaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maonesho ya 33 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar-es-Salaam. Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea Maonyesho ya 33 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyoandaliwa na *BET*.

Kamati inaupongeza Uongozi wa *BET* kwa kazi nzuri ya kukidhi matarajio ya biashara ya kimataifa, kukuza biashara ya ndani pamoja na kuboresha mazingira ya Maonyesho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini tatizo la viwanda vyetu vya ndani kutokushiriki katika Maonyesho, na haielewi ni kwa nini havitaki kutumia fursa hii kujitangaza. Kamati inaishauri Serikali kuona sababu ya viwanda hivi kutokushiriki na kuweka mkakati wa kuhamasisha ushiriki wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kufikiria haja ya kutenga eneo maalum kwa ajili ya wauzaji wa bidhaa zinazotengenezwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uboreshaji uliofanyika katika eneo hili la Maonyesho, Kamati inashauri litengwe eneo litakalojengwa hotel kubwa na nzuri

itakayokidhi mahitaji ya wafanyabiashara wanaoshiriki kwenye Maonyesho na hasa wageni kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010. Kamati ilipitia na kujadili kwa kina Taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na hatimaye kupitia Makadirio ya Bajeti hiyo kifungu kwa kifungu. Kamati yangu imeridhika na Malengo, Mipango na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Ili Wizara iweze kutekeleza Majukumu yake iliyoyapanga, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu kujadili na kukubali kupitisha kiasi kilichoombwa cha Shilingi Bilioni Hamsini na Tano, Milioni Mia Saba na Nne, Laki Sita, Sitini na Tisa Elfu (55,704,669,000/=). Kati ya Fedha hizo Shilingi Bilioni Arobaini na Tano, Milioni Mia Nane Thelathini na Sita, Laki Tisa Thelathini na Tano Elfu (45,836,935,000/=) zikiwa za ndani na Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Nane Sitini na Saba, Laki Saba, Thelathini na Nne Elfu (9,867,734,000/=) ni za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho. Kabla ya kuhitimisha taarifa yangu,kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne S. Makinda, (Mb), pamoja na Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama (Mb), Mheshimiwa Job Ndugai (Mb), na Mheshimiwa Zuberi A. Maulid (Mb) kwa kuendesha Vikao vya Bunge kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumshukuru Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Dkt. Mary. M. Nagu (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Cyril A. Chami (Mb), Katibu Mkuu Bibi Joyce Mapunjo, pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na taasisi zake kwa ushirikiano waliotoa wakati wa kuchambua na kujadili Taarifa ya Bajeti ya Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara kwa ushirikiano wao katika kuijadili Taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na hatimaye kutoa maoni haya. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: Mheshimiwa Abdisalaam I. Khatibu, Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbarouk K. Mwandoro, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Muhammad A. Chomboh, Mheshimiwa Abdallah S. Sumry, Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby, Mheshimiwa Ame P. Ame, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Haji J. Sereweji, Mheshimiwa Harith B. Mwapachu, Mheshimiwa Joseph J. Mungai, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o. (*Makofi*)

Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mheshimiwa Parmukh S. Hoogan, Mheshimiwa Rostam A. Aziz, Mheshimiwa Vuai A. Khamis na Mheshimiwa Yono S. Kevela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashilillah kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi ya kuichambua na kujadili Taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa wakati.

Aidha, niwashukuru Makatibu wetu Ndugu Angelina Langisi Sanga na Ndugu Abdallah Hancha kwa kazi nzuri ya kuihudumia Kamati ikiwa ni pamoja na kuandaa maoni haya ya Kamati. Mwisho kabisa nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi).*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chomboh. Kabla hatujaendelea naomba nitambue uwepo wa Madiwani wa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, wanaoongozwa na Makamu wa Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo. Naomba popote walipo wasimame. Nadhani wametoka kidogo, lakini tupo nao na tunawakaribisha sana. (*Makofi*)

Baada ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, tutaanza uchangiaji kama kawaida na kwa madhumuni ya kuwafanya watakaopata nafasi hiyo wajiandae, ningeomba niwataje wale ambao hawajachangia kabisa toka *session* hii ianze ambao watapata fursa ya kwanza. Nao ni Mheshimiwa Abdisalam Issa Khatib, atafuatiwa na Mheshimiwa *Captain* John Komba, na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. Halafu tutaendelea na tutaendelea kujulishana. *(Makofi).*

Kwa hatua hiyo, ninaomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Mheshimiwa Lucy Owenya. *(Makofi).*

**MHE. LUCY F. OWENYA – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba upokee shukrani zetu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya bajeti ya mwaka wa fedha 2009/2010 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99(7), Toleo la 2007. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa namna ya kipekee kabisa kuwashukuru wananchi na wote wenye mapenzi mema na Chama Cha Demokrasia na Maendeleo *(CHADEMA)*, kwa kuendelea kutuunga mkono katika mapambano dhidi ya kumkomboa mtanzania katika kugombania raslimali za nchi yao ili waweze kufaidika nazo. Aidha nina ahidi kuwa nitaendelea kukitumikia na kukitetea Chama Changu Cha Demokrasia na Maendeleo *(CHADEMA)* kadri Mwenyezi Mungu atakavyoniweka hapa Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawajibika kwa moyo wa dhati kuwashukuru viongozi wangu wakuu Mhe. Hamad Rashid Mohamed, (MB) Mbunge wa Wawi na Mhe. Dr Wilboard Slaa (Mb) Mbunge wa Karatu, kwa imani kubwa waliyo nayo juu yangu na kuniteua kuwa msemaji wa Wizara hii. Aidha napenda kumshukuru Naibu wangu Mh.Khadija Alqasim (Mb) kwa ushirikiano alionipa katika kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda kuishukuru familia yangu hasa mwanangu Yohane na mume wangu mpenzi Dr. Fidelis Owenya kwa kuendelea kusaidiana nami katika shughuli za siasa na uvumilivu walio nao kwangu wakati nikiwa mbali nao nikilitumikia Taifa. Mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa naomba kumshukuru Mhe Waziri Marry Nagu, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa na kuleta hotuba yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uzalishaji wa Viwanda na Pato la Taifa. Kabla ya kuanza kutoa yale tunayodhani kuwa ni mapungufu tunaomba kuuliza, ni lini Wizara itakuwa na majengo yake inayo yamiliki badala ya kulipa kodi kila mwaka? Kwani mwaka huu wa fedha kodi ni shilingi 720,000,000/= Hii ni hasara kwa Serikali kulipia kiasi kikubwa kama hiki, tukizingatia Wizara hii tayari bajeti yake haitoshelezi katika taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 sekta ya viwanda ilichangia asilimia 9.2 kwa pato la Taifa. Mwaka 2008 sekta ya viwanda ilichangia asilimia 9.4. Ni dhahiri kwamba sekta ya viwanda bado haitoi mchango stahiki katika pato la Taifa. Ukuaji wa Viwanda bado hauridhishi kwa kiasi fulani ukizingatia mali ghafi nyingi za viwandani zinapatikana hapa hapa nchini.

Pamoja na utandawazi kuwa moja ya sababu ya kuchangia ukuaji wa viwanda lakini bado Serikali inatakiwa kuwasaidia wazalishaji ili waweze kupunguza gharama za uzalishaji haswa katika maswala ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 ilibuniwa kwa kuzingatia maendeleo makubwa ya uchumi ya nchi za Kusini Mashariki ya Asia kama vile Malaysia na hususan ukuaji wa sekta ya viwanda, uuzaji wa bidhaa za viwanda nchi za nje na ongezeko kubwa la ajira katika sekta rasmi lililosaidia kupunguza umaskini kwa kasi kubwa. Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 ni kuhakikisha kuwa ifikapo 2025, Tanzania itakuwa na uchumi unaotegemea sekta nyingi na ulioendelea kwa kuwa na wastani wa viwanda vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mchango wa sekta ya viwanda bado ni mdogo sana. Viwanda vilichangia asilimia 9.4 ya pato la taifa mwaka 2008 ukilinganisha na asilimia 8.5 mwaka 2000, jaribu kuangalia tofauti ya miaka na tofauti ya mchango wa sekta kwenye pato la Taifa.

Katika Nchi za Kusini Mashariki ya Asia ambazo kwa kipindi fulani uchumi wao ulikuwa kama wa kwetu, sekta ya viwanda inachangia asilimia 25-30 ya pato la taifa. Katika miaka 4 iliyopita uuzaji wa bidhaa za viwanda umeongezeka kwa kasi kubwa lakini kwa kiasi kidogo *(volume)* kutokana na uzalishaji kuwa mdogo. Mwaka 2008 thamani ya bidhaa za viwanda zilizouzwa nje (dola milioni 662.3) zilizidi bidhaa asilia (dola milioni 418.4). Katika nchi yenye nguvu kazi ya zaidi ya watu milioni 20, wananchi walioajiriwa katika sekta rasmi ya viwanda mwaka 2008 ni 92015 tu. Lengo muhimu la kubadilisha mfumo wa uchumi kwa kuongeza ajira viwandani halijafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,  Uwekezaji wa Ndani. Katika hotuba zangu zilizopita niliuliza Serikali kuhusu mchakato mzima wa ufufuaji/uimarishaji wa viwanda vilivyobinafsishwa. Tunamtaka Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko alieleze Bunge lako Tukufu hatua ambazo Serikali imeshachukua mpaka sasa katika mpango wa kufufua Viwanda vya *General Tyre* cha mjini Arusha, Kilimanjaro Machine Tools, Kiwanda cha kutengeneza magunia, kiwanda cha ngozi cha Mjini Moshi, na kiwanda cha Tanganyika Packers cha Dar Es Salaam, na vinginevyo vingi vilivyokufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kuweza kuleta mapinduzi au mageuzi ya kweli ya viwanda *(industrial revolution)* lazima mageuzi haya yaendane na mapinduzi ya kilimo *(green revolution)*. Kambi ya Upinzani inaitaka serikali kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji na kutoa kipaumbele katika viwanda vya nguo  *(textile industries)* na usindikaji wa vyakula *(agro processing industries)*. Matunda ya mchakato huu yanaweza kuonekana zaidi ikiwa Serikali itaweka pia mazingira mazuri ya masoko hasa katika kuimarisha na kufufua vyama vya ushirika na kuweka msukumo zaidi wa soko kwa kutumia stakabadhi za maghala kama njia ya kuwalinda wakulima wadogo kwa nchi nzima na kwa mazao yote makubwa yanayozalishwa na wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kauli mbiu ya ‘Kilimo Kwanza’ kauli hii haiwezi kuendelea ukizingatia bado miundombinu yetu ni hafifu kama vile reli ambayo ndio njia pekee ya bei nafuu ya kusafirisha mizigo inayopelekwa mikoa ya mbali na eneo la uzalishaji. Hii ni pamoja na kukarabati barabara  hususani  za vijijini ambazo nyingi hazipitiki wakati wa mvua ili kuwawezesha wakulima kusafirisha mizigo yao kutoka vijijini kwenda kwenye soko kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umuhimu wa Kulinda Viwanda Vya Ndani ya Nchi. Tanzania ni nchi yenye uchumi mchanga ambao unategemea zaidi kilimo cha wakulima wadogo ili kuweza kujitosheleza kwa mazao ya chakula na mazao ya biashara.  Moja ya mazao yanayotegemewa kwa biashara ni pamba, kahawa, katani, tumbaku na  kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika historia ya maendeleo ya binadamu, inajulikana kuwa uchumi unaweza kukuzwa kwa haraka zaidi kama uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda unapewa kipaumbele kwani viwanda ni kama injini ya maendeleo.

Vile vile inajulikana kuwa nchi nyingi zilizoendelea kiviwanda zimeanza zaidi na viwanda vya nguo ndivyo vikachochea uanzishwaji wa viwanda vingine vikubwa. Viwanda vya nguo vinatoa ajira nyingi kwa watu kulinganisha na viwanda vingine. Tanzania kama nchi inayozalisha pamba kwa wingi, ina kila haki na wajibu wa kuanzisha, kuendesha na kuvilinda viwanda vya nguo hasa za pamba ili kuweza kujihakikishia ajira, upatikanaji wa mavazi mazuri kwa watu wake, majirani zake na dunia kwa ujumla.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania, toka enzi za awamu ya kwanza, iliona umuhimu wa kuanzisha viwanda vya nguo karibu sehemu zote za nchi.  Hadi mwaka

1990, kulikuwa na viwanda vya umma na vya binafsi zaidi ya 22 ambavyo vilikuwa vinaajiri watu zaidi ya 15,000 na kuzalisha nguo zaidi ya mita milioni 100 za mraba kwa mwaka.

Hata hivyo, uwezo huo wa uzalishaji ulikuwa hauwezi kutumia zaidi ya asilimia 20 ya pamba iliyokuwa ikilimwa Tanzania kwa wakati huo kutokana na teknolojia iliyokuwepo.

Hivi sasa, inakisiwa kuwa viwanda vya nguo vinavyofanya kazi hapa nchini havizidi 15 ingawa uzalishaji unaweza kuwa zaidi ya mita za mraba milioni 100 kwa mwaka kutokana na teknolojia ya uzalishaji ilivyo kwa sasa, kwa kuajiri watu si zaidi ya 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi zinatuonyesha wazi kuwa katika sekta hii ya nguo bado kuna fursa kubwa ya kuendeleza viwanda na kilimo cha Pamba lakini pia kuna udanganyifu mkubwa sana unaofanywa na waliomo kwenye sekta nzima ya nguo, jambo linalosababisha Taifa kupata hasara kupitia kadhia nzima ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madhara ya Udanganyifu wa Bei ya Manunuzi. madhara ya udanganyifu huu wa bei ya kununulia nguo ghafi yako wazi kwa uchumi wa nchi.

Kwanza kabisa Serikali inakosa mapato ambayo ingeweza kupata kama ushuru. Kwa mfano, kama mfanyabiashara ameingiza nguo container 1 lenye mita 90,000 sawa na kilo 12,960 na akalipia ushuru wa 25% kwa bei ya US$ 0.20 kwa mita, atalipa kiasi cha US$ 4.500 sawa na TSh.5,850,000/-.  Kama angelipa ushuru kwa bei ya chini kabisa ya US$ 0.58 kwa mita, angelipa kiasi cha US$ 13,050 sawa na TSH.16,965,000/-.

Kwa maana nyingine, kwa kudanganya bei ya kununulia kwa kiasi hicho mfanyabiashara anakuwa ameiibia Serikali ushuru wa TSh.11,115,000/-, kwa container 1, sawa na asilimia 66 ya ushuru wa halali.  Wizi huu haujajumuisha wizi wa kodi zingine ambazo zingeweza kuambatana na manunuzi haya, kama VAT, kodi ya mapato nk.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pengine ingefaa kusema hapa kuwa kuna njia nyingine tena wanayotumia baadhi ya wafanya biashara wasio waaminifu ili kukwepa ushuru na kodi na kusababisha ushindani haramu wa kibiashara.

Njia hii ni kudanganya kuwa ndani ya *Container* linaloingizwa nchini toka nje kuna nguo ghafi *(Grey cloth)* kwa ajili ya kuja kutengeneza Kitenge au Khanga wakati sehemu kubwa ya mzigo huo ni nguo zilizokwishatengenezwa tayari kwa kuuzwa kwa mtumiaji. Kwa kufanya hivyo, wafanya biashara kama hawa wanakwepa ushuru wa kodi kwa kiasi kikubwa na wanaweza vile vile kuanzisha ushindani haramu wa kibiashara na kuua viwanda na biashara za ndani ya nchi.

Kuna nyakati jozi moja ya Kitenge kilichopitishwa kwa njia kama hizo huuzwa Dar es Salaam kwa bei ya TSh.3000/- wakati Kitenge kama hicho hicho lakini kilichopatikana kihalali kinauzwa TSh.4000/-. Inasemekana bandari zinazopitisha sana bidhaa kwa njia za udanganyifu ni za Zanzibar na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo: Ili kunusuru uchumi wa nchi ikiwa ni pamoja na viwanda na ajira za wananchi, hatua zifuatazo zinapendekezwa zichukuliwe haraka:-

(1) Taasisi husika zitupie macho utendaji wa wakala kama *COTECNA* ili waweze kutenda haki katika ukaguzi wa bidhaa zote zinazoingizwa nchini toka nje ya nchi.

(2) Ukaguzi wa bidhaa zinapoingia nchini uimarishwe katika bandari zote kama vile inavyofanyika Dar es Salaam ili kubaini wafanya biashara wasio waaminifu.

Badala ya kutegemea invoice value kutoza ushuru na kodi kwenye bidhaa za nguo, utumike mtindo wa "*Minimum Dutiable Value*". Ili kuondoa mianya inayoweza kutumika vibaya kuendelea kudanganya, ushuru na kodi za nguo zingetozwa kwa uzito kama vile pamba. Ni rahisi kupima uzito kuliko kupima mita za urefu au za mraba au (*density*) ya nguo.

Inapendekezwa *Minimum Dutiable Value* ya nguo ghafi (*grey cloth*) yoyote iwe US$ 4.0 kwa kilo ya nguo ghafi kwa sasa, ambayo ndiyo bei ya chini kabisa. Na US$ 6.0 kwa kilo ya nguo iliyosafishwa (*finished cloth*). Kwa maana hiyo basi, kila kilo ya nguo ghafi inayoingizwa kutoka nje ya nchi ilipiwe kima cha chini cha ushuru wa US$ 1.0 (yaani 25% ya US$ 6.0). Hii itakuwa imevilinda vilivyo viwanda na ajira za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** hali ya uzalishaji wa viwanda nilivyovitaja pamoja na viwanda vingine hairidhishi. Aidha baadhi ya Viwanda hivi havijazalisha tangu

vibinafsishwe. Kambi ya upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania juu ya kiwanda cha General Tyre cha Arusha ambacho kilikuwa kinazalisha matairi yenye ubora. Kwa sasa hivi wataalam wale hawana kazi na teknolojia iliyopo kiwandani pale inachakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Upinzani**,** inataka maelezo ya kina kuhusu hatima ya kiwanda hicho, la sivyo natarajia kuleta hoja binafsi Tume iundwe ili kuchunguza matatizo ya kiwanda cha *General Tyre* kuangalia kama kuna mianya ya hujuma ikiwa ni pamoja na kurejesha shamba la mpira la Kihuhwi kwa *General Tyre*. Kiwanda hiki kimezungumziwa katika bajeti zote lakini Serikali imeziba masikio kwa nini?

Je, tutaendelea kuagiza mpira kutoka Malasia na Brazil na kuacha mashamba yetu ya mpira yavunwe kwa ajili ya BIG-G zinazotengenezwa Kenya mpaka lini? Kambi ya Upinzani inaishauri serikali ichukue kiwanda hiki chote na kuweka mkakati wa kukiendesha kwa ufanisi. Uamuzi huu uzingatie madeni ya kiwanda hiki kwa mashirika ya hifadhi ya jamii.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimanjaro *machine tools,* kiwanda hiki kilikuwa kinazalisha bidhaa mbalimbali ambazo zilitumiwa na wajasiriamali kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itueleze mchakato wa kufufua kiwanda hiki ili kianze kazi umefikia wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya ngozi viwanda vyote vya ngozi vilivyobinafsishwa vinafanya kazi chini ya matarajio. Kwa mfano kiwanda cha ngozi Moshi kinauza nje ngozi isiokamilika (*semi-process*) badala ya kuongeza thamani na kuuza ngozi iliyokamilika hapa hapa nchini. Kwa kufanya hivyo Taifa lingefaidika kwa kuongeza kipato na wananchi wangepata ajira. Lakini kwa kuwa wawekezaji katika kiwanda hiki hawana nia ya kuagiza technologia mpya ya kufanya hivyo na katika mikataba walihitajiwa kuviendeleza viwanda vile, Kambi ya Upinzani inaona huu ni uzoroteshaji wa maendeleo ya viwanda nchini. Pia Serikali inatuambia nini kuhusu utendaji huu mbovu wa kazi kwani huu ni uhujumu uchumi katika zoezi zima la kubinafsisha viwanda kama hivi. Hivyo Serikali ilikuwa na malengo ya kupata fedha walipoamua kubinafsisha hivi viwanda? Je mikataba ya ubinafsishaji haikuwa na vipengele vya kuendeleza uzalishaji uliokuwepo kabla?

Kambi ya Upinzani inataka maelezo ya kina kutoka serikalini kuhusu swala hili la viwanda vya ngozi ikiwa in pamoja na hatua zilizochukuliwa dhidi ya wahusika na tungependa kujua ni kwa kiasi gani *leather levy* inawasaidia hawa wajasiriamali wadogo wanaojifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hiki kimeacha kabisa shughuli zake za awali na mpaka hivi sasa wananchi Tanganyika *Parkers*, hawajaelewa mwelekeo wa kiwanda hicho. Kambi ya Upinzani inaungana na wananchi kudai maelezo ya kina kutoka serikalini kuhusu makubaliano ya mchakato mzima Wa ubinafsishaji wa kiwanda hicho.

Kwani kuna taarifa kwamba eneo la kiwanda limegeuzwa kuwa eneo la maduka au shule. Jambo ambalo tunaona ni kinyume na masharti ya mkataba wa ubinafsishaji wa kiwanda hicho aidha mkataba wa ubinafsishaji wa kiwanda hiki upelekwe kwenye kamati ya bunge ili kujua ukweli au ndio msemo wasemao chukua chako mapema?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda Vya MaguniaTanzania ina viwanda viwili vya kutengenezea magunia kile cha Moshi ambacho kina uwezo wa kutengeneza magunia milion 6 kwa mwaka lakini hakifanyi kazi. Hivi sasa jumla ya wananchi 500 wamekosa ajira kwa kutofanya kazi kwa kiwanda. Wakati kile cha Morogoro chenye uwezo wa kutengeneza magunia milion 10 kwa mwaka kinafanya kazi kwa kiwango cha asilimia 15 – 20 tu.

Soko la magunia limedorora kutokana na ukosefu mkubwa wa soko la magunia ya mkonge ndani na nje ya nchi kutokana na ushindani mkubwa kati ya magunia yanayozalishwa hapa nchini na magunia ya '*jute'* yanayoagizwa kutoka nchi za Banglasesh na India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za Bangladesh na India zinalinda viwanda vyao vya 'jute' kwa kutoa ruzuku au kwa kutumia sheria ya kulazimisha matumizi ya magunia ya jute ndani ya nchi zao. Nchi hizo hutoa ruzuku na ina sheria inayolazimisha kwamba asilimia 100 ya nafaka kwa ajili ya chakula na sukari ni lazima zihifadhiwe kwenye magunia ya jute.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inshauri ili kulinda ajira na viwanda vyetu itabidi Serikali yetu kuiga yale ambayo yanafanywa na Serikali za India na Bangladesh kwa kupitisha sheria inayoelekeza matumizi ya magunia ya mkonge katika kuhifadhi baadhi ya mazao (*focused mandatory use of sisal bags*) Mfano wa mazao kahawa, cacao, karafuu, korosho, kunde, mahindi n.k na kuongeza kodi kwa magunia ya '*jute'* ili kulisaidia soko la magunia yetu. (*Makofi*)

Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa Bunge lako Tukufu lipitishe Azimio la Bunge kulazimisha matumizi ya magunia ya mkonge katika Mazao ili kulinda ajira katika viwanda vyetu jambo litakalo inua kilimo cha mkonge hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda Cha Vibiriti Moshi (Kibo *Match*), Hiki ni kiwanda ambacho kinaajiri wafanyakazi karibia 600 lakini kiwanda hiki kipo hatarini kufungwa kwa sababu ya vibiriti ambavyo havikidhi viwango kuwemo katika soko. Biashara zote duniani sasa hivi zina ushindani mkubwa kutokana na uwezo mkubwa wa uzalishaji walio nao baadhi ya wajasiriamali ikilinganishwa na ukubwa wa soko na hali ya uchumi wa dunia kwa ujumla. Wafanya biashara wengine wanatumia njia mbalimbali ili waweze kuuza bidhaa zao na kujipatia fedha, ikiwa ni pamoja na zile zisizo halali (*Unfair Trade Practices*). Nitaeleza madhara ya bidhaa hafifu kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** mfanyabiashara huyo asie mwaminifu anaingiza ushindani usio halali (*unfair competition*) katika soko la bidhaa zitokanazo na viwanda vyetu nchini. Kwa kufanya hivyo anaweza kuuza bidhaa zake bei rahisi kuliko za

wenzake waaminifu au wazalishaji wenye viwanda vya ndani, na hivyo kuua kabisa viwanda vyetu vya ndani.

Matokeo ya hali hii ni kufunga viwanda vya ndani kama ambavyo tulishuhudia vingi vikifungwa miaka 90, na kupoteza ajira zaidi ya 15,000. Wakati makosa kama haya yaliporuhusiwa kufanyika, wenzetu wa nchi za mashariki ya kati na mbali walivilinda viwanda vyao na ajira za watu wao kwa mbinu mbalimbali, na hivyo kuweza kuendelea kuuza bidhaa zao kwao na huku kwetu kabla na baada ya viwanda vyetu kufungwa, na wanaendelea hadi leo. Tusipoangalia hata hivi vilivyofunguliwa upya navyo vitafungwa tena.

Mheshimiwa Spika, kambi ya upinzani inahoji Tanzania itaendelea kuwa jalala (*dumping*) la bidhaa zenye ubora usiokidhi viwango vya kimataifa mpaka lini? Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya upinzani inaitaka Serikali ieleze tatizo ni nini tunashindwa kuzuia uingizaji wa bidhaa hizi zisizokidhi viwango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokuthamini Wataalam Wetu na Taasisi Zilizopo Chini ya Wizara**,** Taarifa zilizopo zinazonyesha kuwa Serikali bado haijathamini mchango wa asasi hizo.Taasisi hizo ikiwa ni pamoja na *TIRDO*, *CARMATEC* na *TEMDO* katika mpangokazi wao wamepewa Tshs,899,784,000/= ,Tshs.827,901,000/= na Tshs.500,104,000/= kwa mfuatano.Jee ni kweli tumekusudia taasisi hizi kufanya kazi kwa ufanisi kwa fedha kiasi kidogo kama hicho? Hii ni kuonesha kiasi gani taasisi zetu na wataalamu wetu tusivyo wathamini kweli na kuwakatisha tamaa na matokeo yake wanakimbilia kwenye Siasa au sekta binafsi. Aidha hii inaonyesha ni kwa jinsi gani Serikali isivyothamini utafiti katika maendeleo ya viwanda kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mfano SIDO wana mpango mzuri wa kuwa na viwanja vidogo vya biashara vya kikanda. Kwani itawapunguzia wenye viwanda gharama za usafirishaji na kutoa fursa nyingi zaidi kwa wao kuweza kujitangaza. Pamoja na swala hili la kanda SIDO wameweka mchakato wa kuweka mazingira mazuri katika maeneo mbalimbali kikanda ili kuweza kuanzisha viwanda ambavyo vinauhusiano na mazao yapatikanayo kutokana na sehemu husika. Je kiasi cha Shs 3,413,543,000/=walizopewa wataweza kutimiza lengo hili zuri? Kambi ya Upinzani, inahimiza suala la viwanda vidogovidogo kupewa umuhimu kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANALEC* hiki ni kiwanda kilichojikita katika utengenezaji wa vifaa vya umeme zikiwamo Transfoma na *switchgear*. Kiwanda hiki kinatengeneza transfoma nzuri zenye ubora mpaka wanapata *order* kutoka nje ya nchi. Shirika letu la *TANESCO* wanazo hisa pale TANALEC lakini cha kusikitisha *TANESCO* hawanunui transfoma kutoka TANALEC wanaagiza kutoka nje na wakinunua ni chache sana. Sababu ambayo *TANESCO* wanatoa kwa kutonunua transforma za TANELEC ni kwamba sheria ya manunuzi inazuia (kwamba ni lazima watangaze zabuni kiushindani).(*Makofi*)

Kambi ya Upinzani inataka ufafanuzi ni sababu zipi zinapelekea *TANESCO* kuagiza transfoma kutoka nje wakati TANALEC wanatengeneza na ukizingatia tayari shirika lina hisa huko? Je hii sio moja ya sababu ya kuuwa viwanda vyetu? Kama sheria

na kanuni za manunuzi ni tatizo kwa kununua bidhaa za viwanda vyetu, Serikali iangalie jinsi ya kulegeza masharti ili kuimarisha viwanda vya ndani na kutengeneza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maeneo Maalum ya Kuzalisha Kwa Mauzo ya Nje (*Export Processing Zone Authority-Epz*), Pamoja na nia nzuri ya Serikali kutenga maeneo maalum ya uzalishaji kwa mauzo ya nje *(EXPORT PROCESSING ZONE – EPZ)* katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje. Kambi ya Upinzani ina wasiwasi na mafanikio ya mpango mzima kufikia malengo yake kwani hadi leo maeneo yaliyotengwa mengi hayana miundombinu ya kuridhisha kama kivutio kwa wawekezaji. Tukumbuke kuwa Duniani kote miundombinu ya kumvutia Mwekezaji ni kazi ya Serikali na siyo ya mwekezaji, vinginevyo ndiyo sababu kubwa ya sisi kupata mkia na wawekezaji kuchukua ngombe mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka kujua ni vivutio gani (*incetives*) wawekezaji katika EPZ wanapata na nchi imenufaika kwa vipi. Je hadi leo ni maeneo mangapi yaliyotengwa kwa EPZ na kwa shughuli gani? Tukijua matatizo ya uvamizi wa ardhi nchini, je maeneo yaliyotengwa ni mangapi yameshapata hati miliki? Je ni wamiliki wangapi wa maeneo yaliyochukuliwa na kuwa EPZ wameshalipwa fidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Agoa, Mpango wa Biashara ulionza mwaka 1999 ulitoa fursa kwa nchi za Afrika kufaidika na soko la Marekani kwa kuuza bidhaa zetu. Wenzetu wa nchi jirani Kenya na Uganda walichangamkia biashara hii na kuliingizia Taifa lao pesa za kigeni. Wakati nchi ya Kenya ilivyojiunga na AGOA Januari 2001 walichangamkia soko hilo na ilipata kiasi cha billion 60 wakati wenzetu wa Uganda walipata kiasi cha billion 40. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani, inataka majibu ya kina kutoka serikalini Je Tanzania imefaidika kwa kiasi gani katokana na fursa hii? Na jibu kama hatukufaidika ni sababu zipi zilipelekea Tanzania tusifaidike na fursa hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Wizara 2009-2010, Kambi ya Upinzani inaona bado Serikali haijachukulia Wizara hii kwa umuhimu unaostahili kwani fedha iliyotengewa ya shilling 55,704,669,000/= hazitoshi kabisa kulingana na majukumu yake. Nchi nyingi zilizoendelea waliweka mapinduzi ya viwanda na kuhakikisha viwanda vile vinafufua uchumi wake. Kwa mfano mzuri ni nchi za Malasya, Singapore, India na China.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** chuo cha CBE kipo chini ya wizara ya viwanda na biashara, cha kusikitisha chuo hiki kina matatizo mengi lakini fedha walizoomba wamepewa pungufu sana. Kwa mara nyingine Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wanachi imefikia wapi na ujenzi wa mabweni, *Library*, madarasa kwa vyuo vyote viwili kile cha Dar Es Salaam na Dodoma ukizingatia vyuo hivi vinategemewa na wanafunzi wengi sana? Serikali kupitia hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa wazee wa Dodoma imeweza kutengeneza mpango wa kuwanasua wafanyabiashara . Je Serikali inashindwaje kuwa na mpango wa kuvinasua viwanda na taasisi za elimu zetu?

Mheshimiwa Spika, *Programme* ya *ASDP* Katika Wizara ya Viwanda, kutokana na umuhimu mkubwa uliopo kwa sasa wa kuwa na viwanda vya kusindika mazao ya kilimo ili kwenda sambamba na kauli mbiu ya Kilimo Kwanza. Kambi ya Upinzani inaona fedha za ASDP shilingi 1,393,385,000/= ambazo zimetengwa kwa wizara hii.

Badala ya kufanya kazi ya kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za masoko ya mazao ingelikuwa ni vyema fedha hizo zikawa ndio msingi wa kujenga angalau kiwanda kitakachokuwa kinashughulikia mazao ya matunda kwa ujumla wake. Tunatoa ushauri huu kwani tunaamini kabisa fedha hizo ambazo ni mtaji uwezekano wa kurudisha mtaji huo kwa muda mfupi ni mkubwa sana na itakuwa imeondoa tatizo la matunda ya wakulima kuharibika kwa asilimia kubwa. Vingenevyo *PROGRAMME* itamalizika bila ya kuwa na hata kiwanda kimoja cha kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na hii ni aibu kubwa kwa wizara na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa ni karne ya sayansi na Teknolojia mitandao ya mawasiliano imeenea nchi nzima hivyo mtu kutengewa fedha eti ni kuwaunganisha wakulima na masoko ni sababu dhaifu na iliyopitwa na wakati na ni njia moja wapo ya kutumia vibaya fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maonyesho 33 ya Kitaifa ya Biashara ya Sabasaba, Kambi ya Upinzani inapenda kuwapongeza Bodi ya Biashara ya Nje (*BET*) kwa kuendelea kuboresha maonyeshao ya biashara kila mwaka. Mwaka huu maandalizi yalikuwa mazuri sana.

Pamoja na mambo mengine lakini katika maonyesho yale palikuwepo na tatizo kubwa sana la uegeshaji wa magari kwa wateja. Bodi ya Biashara imekuwa na mgogoro na wafanyabiashara wenye garage za magari ambazo zipo ndani ya viwanja vya maonyesho. Wafanyabiashara hao wamekataa kabisa kuhama katika sehemu ile licha ya sehemu hizo kuwa mali ya serikali. Kambi ya Upinzani inataka Serikali itueleze tatizo ni nini? Kwanini viwanja vile havirudishwi? Je hawa wafanyabiashara hao wana nguvu juu ya sheria na kama kuna kesi inachukua muda gani kumalizika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho, Kambi ya Upinzani inahitaji ufafanuzi na majibu ya kina kwa yafuatayo:-

1. Dira ya maendeleo ya 2025 imefikiwa wapi mbona katika utekelezaji wake miaka 13 baada ya kuanza? Je Serikali inatueleza nini kwa ujumla: Je ule ukuaji wa maendeleo ya viwanda wa 15% umefikiwa? Kama hapana, sababu ni nini na hatua gani zinachukuliwa kurekebisha?

2. Mwaka jana nilizungumzia suala la TBS kukagua magari (na sasa mizigo yote) yanayonunuliwa kutoka Japan na Dubai. Ukaguzi huu hufanywa na wakala aliyeteuliwa na TBS ukaguzi huu hufanyika kwa malipo ya USD

150 Kwa kila gari. Je Serikali imepata kiasi gani ya malipo hayo? Au inamfaidisha huyo wakala huko nje? Tunahitaji jibu la ufasaha.

3. Kwa kuwa Serikali imekuja na kauli mbiu ya "KILIMO KWANZA" Kambi ya Upinzani inataka kujua Wizara ya Biashara na Viwanda na Wizara ya Kilimo vinauhusiano gani katika kuipa kipaumbele kauli hiyo kwa vile viwanda haviwezi kukua bila ya kilimo na kilimo kinategemea sana viwanda ili kiweze kupata soko.

4. Ilani ya CCM inayoelekeza utafiti wa chuma cha Liganga uwe umekamilika 2010, Je mpaka sasa hivi utafiti huo umefikia wapi katika kutekeleza Ilani hiyo. Je ni lini kiwanda hicho cha chuma kitaanzishwa? (*Makofi*)

5. Wizara ya Viwanda na Biashara ni mwanachama wa *African Regional Centre for Engineering Design and Manaufacturing (ARCEDEM)* lakini kwa miaka sita haijalipia mchango wa uananchama na malimbikizo yamefikia jumla ya sh. 548,255,080. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani, inataka ufafanuzi je Wizara imefikia wapi? Inaendelea na uanachama au la? Je deni hilo litalipwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwahimiza watanzania wote kuwa tuthamini bidhaa zinazozalishwa hapa nchini kwani zina ubora unaokidhi viwango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani natoa salamu za rambi rambi kwa ndugu na familia waliofiwa na ndugu zao katka ajali ya basi la Mohamed Trans iliyotokea Korogwe juzi. Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kwa jambo la dharura, TBS waanze kukagua mabasi yenye kutumia chesesi za malori, pamoja na mambo mengine ikiwa ni njia mojawapo ya kupunguza ajali za barabarani ambazo zinaelekea kuwa janga la taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwa kuanzia tunaomba thamani zote za ofisi ya Bunge zianze kununuliwa kutokana na malighafi za viwanda zinazozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nawashukuru kwa kunisikilaza na Mungu awabariki, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kuweza kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa maoni yangu kwa Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko. Pia nikushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii. Kwa namna ya pekee nawashukuru wapiga kura wangu wa jimbo la Makunduchi, kwa kuwa naimani nami bado na kwa kunisaidia kwa kila njia ili kuniwezesha kufanya kazi zangu za Ubunge kama inavyotakiwa na kwa matarajio yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli mbiu kilimo kwanza inaweza ikachukua hatua kubwa pale ambapo viwanda havikuachwa nyuma. Na maendeleo ya nchi yoyote yanategemea sana viwanda. Na kwa bahati nzuri nchi yetu Tanzania tumebarikiwa na ardhi yenye rutuba kubwa sana na ardhi nyingi bado haijaendelezwa kilimo. Na ili kuendeleza kilimo lazima viwanda vishike hatamu vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina viwanda vya kusindika pamba 7628 vya ushirika mbalimbali ambavyo kati ya hivyo 12 havifanya kazi kabisa. Viwanda vya binafsi 48 ni viwili tu ambavyo havifanyi kazi. Ni dhahiri kwamba hivi viwanda vya binafsi ndivyo vinavyofanya kazi.

Ili tuweze kuendelea zaidi lazima hivi viwanda vingine vilevile vihuishwe, vifufuliwe na bado kazi kubwa ya kuwarekebisha hawa wawekezaji katika viwanda lazima iwepo. Na kuwepo kwao lazima waone wenzao kwanza waliopo hapo ambao wameshachukua hivi viwanda vya kuchambulia pamba vinafanya kazi kama ilivyotarajiwa na kupewa msukumo unaostahiki ili waweze kufanya kazi zao vizuri na kwa ufanisi

Tunavyo viwanda vya nguo, Kamati yangu ilitembelea baadhi yake na vingi vinajitahidi lakini utaona kwamba viwanda ambavyo vinafanya kazi bado ni vichache sana. Mahitaji yake bado ni makubwa na kama ilivyoelezewa na Kamati yangu, ripoti ya Kamati yangu utaona baadhi ya viwanda bado wanaagizia baadhi ya malighafi ya *grey cloth* ambayo utakuta mara nyingi wanakuja kuweka nakishi tu na kutengeneza Khanga na Vitenge.

Mbali kama utalinganisha na kiwanda cha mwananchi Mtanzania ambacho amebinafsishwa hapo mwaka 1998 cha 21 *century*, unahisi unapokwenda katika kiwanda kile unakuta kazi hapa inafanyika kwa sababu unakuta takriban robo tatu (asilimia 75) ya kiwanda imekuwa *modernized* amekwenda kwenye *state of the art* na kwa hivyo anaweza kufanya kazi yake vizuri sana. (*Makofi*)

Wawekezaji kama hawa wanafaa kulindwa, na kupewa kila aina ya msukumo kutoka Wizara ya viwanda vya biashara (Serikalini), kwa ujumla ili waweze kuendelea zaidi. Viwanda kama hivi ni muhimu vienee nchi nzima. Kama walivyokwishatangulia wasemaji kutoka Kamati yangu ya Viwanda na Biashara na Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani tuna tatizo kubwa la kutolinda viwanda vyetu.

Wakati tunatembelea viwanda, tulikwenda Moshi tukakuta kiwanda cha magunia cha Moshi hakifanyi kazi, tukajiuliza kwa nini kusema kweli tulimlaumu mwenye kiwanda kile kwa kusema kwamba amechukua na kiwanda kingine Morogoro kwanini kile hakifanyi kazi. Tulitoka tukaenda tukaangalia kwanini kule Morogoro kifanye kazi na huko Moshi kisifanye kazi. Kiwanda cha Moshi kina uwezo wa kutoa magunia ya

katani milioni 6 na kimelala, kiwanda cha Morogoro kina uwezo wa kutoa magunia milioni 10, kile milioni 6 hiki milioni 10. Na vyote hivi vinatumia grade ndogo kabisa ile ya katani, yaani kuhakikisha kwamba katani yote inatumika hapa hapa nchini bila ya kuagizia kutoka nje. (*Makofi*)

Tukarudi Morogoro, tuliporudi Morogoro tukakuta kwamba kiwanda kile kinafanya kazi na wafanyakazi ni wachache sana. Lakini tukauliza sababu ni nini? Sababu hakuna msukumo. India mwezi Septemba, mwaka 2001 Waziri wa Wizara ya *Textile* alitoa *order* kwamba hakuna vifunganisho au vifungashi vya kutumika au magunia ya aina yoyote zaidi ya jute kwa ajili ya sukari 100%, kwa ajili ya nafaka na vitu vingine vyote 100% na kuhakikisha kwamba amri hiyo inafuatwa.

Kwanini tusifikie hali hiyo na sisi Tanzania. Wenzetu wanajali, sisi tunawapelekea ajira, tunapeleka *raw materials;* Viwanda vyetu vingi hapa vya korosho na vingine, unapeleka ajira, unapeleka *raw materials* na *byproducts.* Sasa kwanini na sisi tusifikie hadi tukalinda viwanda vyetu. (*Makofi*)

Hivi karibuni India kulikuwa la tatizo na viwanda vidogo vidogo vya Usumba, na kwa sababu wanajali watu wao wanajali uchumi wao, na pia wanajua kwamba *Southern* India jimbo la Kerala, uchumi wao mkubwa ni katika viwanda vidogo vidogo vinategemea Usumba. Ninayo nakala ya gazeti hapa kwa ruksa yako nanukuu *heading* ya gazeti hii la the Hindu, la tarehe 6 Juni, 2009 linasema *developing market for a coir industry*, kuendeleza soko kwa ajili ya bidhaa za Usumba, na amesema Waziri wa Nchi ya Muungano ya India namnukuu, "nitafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba *industry* hii na bodi ya Usumba inapata kila msaada kuhakikisha matakwa ya wananchi na uchumi wa wananchi wadogo wadogo unaendelea kwa faida ya pato la nchi.

Hakusita hapo ametoa muongozo kuhakikisha kwamba makochi yote ya *train* na makochi yote ya magari wanayozalisha palepale nchini India wahakikishe kwamba wanatumia Usumba. Kwanini sisi Tanzania kama ni nchi ambayo tuna fursa zote hizo tusitoe juhudi makusudi tukasema tunatoa sheria na kwamba tunyanyue viwanda vyetu kuanzia sasa hivi hatununui magunia ya *jute* kwa kufunganisha vifaa vyetu mazao yetu yanayouzwa nchi za nje.

Inashangaza kwamba mwezi wa Mei, 2009 *TCA*, Tanzania *Coffee Association* inatoa mwelekezo kwa chama chake kwamba waagizie magunia ya jute kutoka India kuja kushona magunia hapa kwa ajili ya kufunganisha mazao yetu ya Kahawa kupeleka nje.

Gunia la katani lina kila aina ya sifa na mimi ningefikiri kwamba kutokana na ushauri uliotolewa na TISCO mwaka 2003, wa kusisitiza juu ya matumizi ya magunia yetu ya mkonge yatumiwe katika kila aina ya mazao tunayozalisha hapa nchini kwa ajili ya kusafirisha na kwa ajili ya matumizi yetu wenyewe hapa hapa nchini kwa sababu msululu wa ajira utakuwa ni mkubwa unaanza kwenye kiwanda ukitoka kwenye huko umeanzia shambani kukata mkonge, kwenye kiwanda cha mkonge wenyewe hata huku kwenye kiwanda cha kutengeneza magunia. Faida yake itakuwa ni kubwa sana kwa wananchi na watafaidika na ile ajira itakuwa imezidi.

Vivyohivyo kwa viwanda vya matunda. Leo ukienda UNAT pale Morogoro unahisi wameanza, wameanza vizuri ukienda kwa kiwanda cha Bakhresa kule Vingunguti unakuta ameanza kila aina ya matunda, tumekuta pale magari yanayotoka kwa wakulima wa Lindi wa maembe.

Tuone fahari na sisi kunywa maji au kunywa *juice* ya machungwa, ya mananasi na matunda mengine ambayo yametengenezwa hapa hapa nchini kwetu. Ifike mahali maziwa tunayokunywa hapa yawe ya Tanga *fresh* na mengine ya Mara yaliyozalishwa hapa kwetu kuliko kuwa na maziwa na maji na *juice* za matunda yanatoka nchi za jirani. Kuna haja ya kuwa na msukumo maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na hayo tu na mengine najua wenzangu watatoa mchango wao zaidi hili tulitilie mkazo kwamba chetu ni chetu chao kiwe chao basi baada ya hayo nakushukuru kwa fursa hii na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya ya kuja leo hapa kuzungumza katika hoja hii muhimu ambayo imetoka Wizara ya Viwanda na Masoko.

(i) Nimpongeze Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ukimya utilivu na uwezo wake mkubwa sana wa kusimamia ilani na nchi imetulia iko kimya ishallah tutamaliza miaka hii mitano vizuri na kuingia mingine mitano kwa amani na salama.

(ii) Nimpongeze Mheshimiwa Mary Nagu, na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, kwa kuongoza Wizara hii kwa makini na uwezo mkubwa sana.

Lakini kwa Mheshimiwa Mary Nagu, nikupongeze pia kwa vazi ulilovaa maana tangu nimewahi kukuona leo umevaa vizuri kuliko siku nyingine yoyote na hii ni kwa sababu ya vazi ambalo limetengenezwa na kuzalishwa katika nchi yetu ya Tanzania. Na hii ikupe moyo, nguvu uwezo wa kuvilinda viwanda vyetu vya ndani kama vya pamba, katani ili watu waweze kupata ajira tuendelee Watanzania. (*Makofi*)

(iii) Nitoe shukrani sana kwa wananchi wangu wa wilaya ya Mbinga, lakini jimbo la Mbinga Magharibi zaidi kwa kunichagua na kwa kuniwezesha kuwa Mbunge na nina hakika hawajutii kwa mimi kuwa Mbunge wao kwa kipindi hiki chote

ambacho niko hapa Bungeni. Mnakumbuka miaka miwili ya mwanzo nilikuwa napiga kelele humu ndani na kuna kipindi nilisema wale watu wa kwetu lazima apitie ndani ya maji ndiyo akazikwe.

Hali hiyo haiko tena kule, Serikali imeweza kusaidia barabara iko na mtu akifa mara moja anazikwa tu kwa sababu atafika leo hii na leo hii atazikwa, kwa hiyo pressure inayopanda na kushuka hakuna tena kule. (*Makofi*)

Tumeweza kujenga mashule ya primary na sekondari, tumejenga, zahanati, vituo vya afya barabara, mawasiliano ya simu, boti za ulinzi wa ziwa na kwa kweli tumefanikiwa kutekeleza ilani ya CCM kwa zaidi ya asilimia 80. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye tatizo dogo, lakini si dogo ni kubwa sana, dogo kwa Wizara lakini ni kubwa sana kwa wananchi wa Mbinga Magharibi hasa wanakokaa kando kando ya ziwa Nyasa.

Watu wale ni wavuvi, lakini baada ya kazi za uvuvi ni wafanyabiashara wajasilia mali biashara ndogo ndogo. Kazi yao kwa sababu wako mpakani, mara nyingi wanakwenda kufanya biashara Malawi ama Msumbiji, na wa Malawi walikuwa wanakuja kufanya biashara Tanzania na hivyo kubadilishana biashara na utamaduni wao.

Lakini hali ilivyo sasa ni mbaya sana. Hata hii inayozungumzwa Mtwara *corridor* kwamba tumefungua huu ukanda wa Mtwara ili biashara ziende kama kitabu chako ukurasa wa 18 kinavyosema kule ni kama tumefunga biashara hakuna kinachoendelea. Kwa sababu zamani tulikuwa tunaruhusu biashara ya sukari kutoka Malawi, kuja Tanzania na watu wa Tanzania wanapeleka mahindi kule, watu wanatembeleana.

Lakini leo tunaambiwa ni marufuku kuleta sukari kutoka Malawi, sukari ambayo inatakiwa kununuliwa ni sukari kutoka Tanzania tu. Ni kweli, tunalinda viwanda vyetu lakini uwezo wa kusheheneza kulisha nchi nzima ni mdogo, sukari ya Tanzania kule haipo na ikija kilo moja ni shilingi elfu mbili.

Lakini sukari inayotoka Malawi kuja Tanzania upande wa mpakani kilo moja ni shilingi elfu moja na iko nying. Sasa mfanyabiashara wa kule ziwani akileta sukari kutoka Malawi, wale watoza ushuru wakiiona ni kuichukua na kuimwaga ndani ya maji, wale watu hawana pesa au ni kuichukua na kuipeleka wanakokujua kwa hiyo wananchi

wanabaki maskini. Hivyo basi lawama yote inamwendea Mbunge wa Jimbo na ni mara nyingi kama mara mbili au tatu nimekuambia Mheshimiwa Waziri jambo hili.

Kwa hiyo, leo hii ninapoongea hapa wananchi wanasikia, wanaomba uwatolee kauli tu tamko tu kwamba kwa zao la sukari waruhusiwe kufanya biashara hiyo kwa sababu sasa vijana wale hawafanyi kazi wako vijiweni kazi yao ndiyo hiyo wakitoka kuvua Samaki wanakuwa hawana kazi nyingine, wakimuona Mbunge ni kumwambia Mbunge hawajaamka leo, uwasaidie hiki na kile lakini wakati walipokuwa wanafanya biashara ya sukari na Mahindi mambo yao yalikuwa yanakwenda vizur sana. Nakuomba Mheshimiwa Waziri jioni utakapokuwa una *wind up* unisaidie kutoa tamko kuhusu suala la sukari au biashara ya sukari ya Malawi na ya Tanzania.

Wenzetu wa mpakani wa Kyela kule wanaendelea kufanya biashara hiyo na kama nasema uongo labda Mbunge wa Kyela yupo anaweza kunisaidia. Wale wenzetu wanaendelea kufanya biashara lakini kule katika jimbo langu ni marufuku. Ni kwa nini wengine wafanye biashara hiyo na wengine wasifanye? Kwa ni ni mpaka wa Namanga wafanye biashara na mpaka wa Mbambabay wasifanye biashara?

Serikali imejenga Bandari ya Mbambabay vizuri kabisa na inapendeza, lakini meli haziwezi kuingi kwa sababu biashara hakuna. Kwa hiyo, naomba sana Bandari ya Mbambabay itumike kikamilifu ili vijana wetu waweze kufanya biashara.

Miaka miwili iliyopita Serikali iliahidi kujenga soko la kimataifa pale Mbambabay na mpakani mwa Msumbiji katika Jimbo la Peramiho na maghala ya kuhifadhia Samaki na Mahindi pale Mbambabay.

Lakini hii imekuwa ni ndoto, hakuna ghala na kama Samaki wanavuliwa basi wanawekwa kwenye mchanga, kama Mahindi yamevunwa yanawekwa kwenye mchanga lakini upande wa Malawi maghala yapo na masoko yapo, upande wa Tanzania hakuna kitu, ni aibu! Tunaomba Waziri jitahidi sana ahadi ile muitekeleze ili maghala na masoko yajengwe ili wananchi wale wafaidi hii keki ya taifa ambayo wengine nao wanaifadi.

Suala la tatu katika matatizo ni uwekezaji kandokando ya Ziwa Nyasa. Ziwa Nyasa liko kilimita 1200 kutoka Dar es Salaam, ni mbali sana na ukombozi wa wananchi wale ni uwanja wa ndege wa Mjini Songea. Uwanja wa Songea ni mkubwa, mzuri na hauna kasoro kwani unafanana kabisa na uwanja wa Mwanza, Iringa na kadhalika lakini hakuna ndege inayotua, hakuna biashara inayofanyika kule. Huwezi kumtoa mfanyabiashara au mwekezaji kutoka Dar es Salaam aende Mbambabay kwa gari kilomita 1200, hataweza!

Lakini ukimpeleka kwa ndege mpaka Songea akatembea kilomita 80 au 100 kwenda ziwani tutapata wawekezaji. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri utusaidie jambo hili. (*Makofi*)Mwenyezi Mungu amekubariki wewe, uwezo huo unao kwanza ni

mwanamke, sura nzuri, unauzika, ukiniambia nikutungie wimbo nikuimbie nitaweza kukutungia ili mradi tu tusaidie uwanja wa ndege utumike pale ili tupate wawekezaji. (*Kicheko/Makofi*)

Zamani Kusini tulikuwa na Mawaziri kama Mzee Rashid M. Kawawa, Ndugu Tandau, Mama Anna Abdallah na wengine wengi. Lakini hawa kazi yao ilikuwa ni kusaidia wenzao kwanza na huo ndiyo ubinadamu, saidia wenzako na wenzako wakusaidie wewe. Sasa wamesaidia Kaskazini wamemaliza, ninyi wa Kaskazini wenye madaraka mtusaidie wa Kusini sasa, wao kazi yao walishamaliza, Kaskazini kuko safi sasa kazi imebaki kwenu Wangoni wanasema 'Chama Kiwuyai' yaani wema ukienda halafu urudi pia upande wa pili. Kwa hiyo, naomba sana Mama Mary Nagu na Naibu wako karibuni sana Songea, Ruvuma, karibuni sana Kusini, Ziwa Nyasa ili mtusaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Capt John Komba ahsante sana kwa mchango wako, kama nilivyosema Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, atafuata na baada yake Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya ajiandae.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia.

Kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kusimamia hapa katika Bunge hili, pili nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Chambani ambao kwa kura zao na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu mbele yenu nipo hapa mimi na ninaahidi nitafanya kazo nao bega kwa bega katika matatizo yao mbalimbali.

Lakini mwisho niwapongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Idara zao za Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa kuwasilisha hotuba nzuri. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko ni kati ya Wizara ambazo zinaitwa Sekta ya Kilimo na mara hii wamepata shilingi bilioni 666.9 sawa na 7%. Zana hizi zinategemeana ufanisi wa Wizara moja huleta ufanisi wa Wizara nyingine na kama kuna matatizo ya Wizara moja basi nyingine vilevile huwa na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko ina matatizo na haijafanya vizuri sana katika Idara zote tatu yaani katika biashara, viwanda na katika masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika biashara sisi Watanzania badala ya kuuza nguo tunauza Pamba, badala ya kuuza viatu tunauza ngozi yaani tunauza malighafi kwa viwanda vya nchi nyingine, tunatoa ajira kule, tunakuza uchumi wa watu. (*Makofi*)

Lakini katika soko la ndani kwa mfano Dar es Salaam hatujaweza kufanya biashara nzuri na nchi jirani imefikia mpaka baadhi ya nchi ambazo zinachangia uchumi wetu wameanza kutukimbia kwa sababu hatuwezi kufanya biashara na wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika sekta ya viwanda, viwanda vingi vimekufa na vile ambavyo viko hai vinazalisha chini ya uwezo, viwanda vingi vimebinafsishwa na vile ambavyo vimebinafsishwa basi vinazalisha kinyume cha makubaliano. Kwa hiyo, sekta ya viwanda nasema inasuasua na kwa hiyo kilimo kinasuasua, mifugo inasuasua na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji basi viwanda vya kusindika mazao ya kilimo yaani *Agro processing industries* ambavyo Waziri katika randama yake hii ukurasa wa 25 nimesoma inasema kwamba ‘tunavutia uwekezaji wa viwanda kwa kuongeza thamani ya mazao mbalimbali ya kilimo na mifugo, ili kuvutia uwekezaji nchini TICN inaendelea kuvutia na kutoa motisha za uwekezaji yaani *investment incentives* kwa wawekezaji wa ndani na nje wakiwemo wasindikaji wa mazao mbalimbali.’

Mimi nashangaa hizi *incentives* kweli zipo? Na kama zipi basi hazifanyi kazi kwa sababu wawekezaji hao tunaowataka hatuwaoni, Tanzania kwa mujibu wa tafiti inazalisha tani milioni 2 za matunda kila mwaka yenye thamani ya shilingi *trillioni 1*, vilevile huzalisha tani milioni 1.2 za mbogamboga zenye thamani ya shilingi milioni 600. Lakini 40% hadi 60% ya mazao haya yanaoza kwa sababu ya kukosa soko, viwanda ama vya kusindika ama kuhifadhi. Sasa unaposema kuna *incentives*, *incentives* hizi ziko wapi mbona hatuwaoni hawa watu? Mbona bado mazao ya wakulima yanaoza mitaani?

Kwa hiyo, mimi nina wasiwasi kama *incentives* zipo basi *incentives* zenu hazijitoshelezi inabidi muangalie vizuri kuhusu hizo *incentives* ili wawekezaji wa nje na ndani waweze kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuwa na viwanda vya kusindika Samaki na viwanda vya kutengeneza zana za uvuvi endelevu kwa sababu zana nyingi sasa hivi hazifai. Tunahitaji viwanda vya kusindika Samaki na zana za uvuvi ziwepo. Lakini vilevile tunahitaji kutengeneza zana za kilimo, ni aibu Tanzania nchi ya kilimo ambayo tunasema kilimo kwanza hatuna viwanda vya zana za kilimo hata kidogo, vya UFI vimekufa, vya Mbeya vimekufa sasa tunaagiza mpaka jembe la mkono, ni aibu, kashfa na fedheha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivi basi hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kusukuma uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa mfano kidogo kwa sekta ya maziwa. Tulikuwa na viwanda 33 vya kusindika maziwa katika nchi hii, lakini viwanda 12 kati ya hivyo vimekufa na vilivyobakia vinasuasua. Nataka kutoa mfano wa viwanda ambavyo tunavyo na uwezo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Dar es Salaam peke yake tuna viwanda kama vitatu lakini nachukua mfano mfano wa kiwanda kimoja cha *Azam Dairy*. Uwezo wake wa kusindika ni lita 3,000 lakini kwa sasa kinasindika lita 2000 sawa na 67%. Tanga viko vingi lakini nachukua mfano wa kiwanda cha *Ami Brothers* ambacho kina uwezo wa kusindika lita 2000 lakini kwa sasa kinasindika lita 500 tu. Arusha viko vingi lakini nachukua mfano wa *Boksail Tanzania Ltd* ambacho uwezo wake wa kusindika ni lita 45,000 lakini sasa hivi kinasindika lita 2500. Kilimanjaro viko vingi lakini nachukua mfano wa Vonga Women ambacho kina uwezo wa kusindika lita 3500 lakini kinasindika lita 1250. Mwanza kuna kiwanda kinaitwa Mwanza *Mini Dairy* uwezo wake ni kusindika lita 3000 lakini kinasindika lita 500 na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo hali halisi tuliyonayo kwamba viwanda vyetu vingi ambavyo viko sasa hivi uwezo wake ni mdogo, na Wizara hii ipo. Sasa Tanzania ina maziwa mengi sana kwani inazalisha kiasi cha lita milioni 4.1 za maziwa kila siku, lakini maziwa yanayosindikwa ni lita 60,000 tu kwa hiyo soko la maziwa hapa limejaa.

Lakini cha kusikitisha ni kwamba pamoja na kuwa na soko kubwa la maziwa bado tunaendelea kupokea maziwa kutoka nje. Kenya kwa mfano wanaleta maziwa Tanzania kila mwezi lita 800,000 za maziwa, lakini kuna nchi nyingine vilevile zinaleta maziwa kwa wingi tu kwa mfano kuna maziwa ya unga ya Nido na vilevile kuna maziwa ya unga kutoka *South Africa* na nchi mbalimbali yanakuja hapa.

Ninataka nitoe mfano wa thamani ya fedha za kigeni ambazo Tanzania inapoteza kwa kuagiza au kupokea maziwa kutoka nje. Kwa mfano, mwaka 2003 Tanzania ilitumia shilingi bilioni 3.5 kwa maziwa kutoka nje. Mwaka 2004 ilitumia shilingi bilioni 3.3, mwaka 2005 ilitumia shilingi bilioni 3.4, 2006 ilitumia shilingi bilioni 4.4, 2007 ilitumia shilingi bilioni 5.6 na mwaka 2008 ilitumia shilingi bilioni 5, hizo ni fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungesindika maziwa ya kutosha na tukazuia uagizaji wa maziwa kutoka nje tunge-*serve* fedha za kigeni zisitumike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi vya maziwa vinaleta tija kubwa sana kwani tunatengeneza ajira, lakini pia vinasaidia MKUKUTA. Karibu kaya milioni 1.73 ambazo ni sawasawa na 24% za kaya Tanzania zinategemea maziwa kwa maisha yao ya kila siku, kwa hiyo naona umuhimu wa maziwa katika nchi hii.

Lakini viwanda vyote vyenye matatizo ni matatizo ya kodi, matatizo ya ushuru, matatizo ya marufuku ya vifungashio vya maziwa na kadhalika. Kwa hiyo, Serikali ina haja ya kuhakikisha kwamba viwanda vyetu vinafanya kazi vizuri kwa kuondoa yale mambo ambayo yanavizorotesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zinaonyesha kwamba lita 100 za maziwa yakisindikwa na kuuzwa basi yanaleta ajira ya kudumu ya watu wanne. Sasa nataka kusema tu kwamba hata ile ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ajira milioni moja basi inaweza kupatikana kutokana na maziwa tu, msiende mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Idara ya Ngozi, viwanda vya ngozi vimetetereka sana nchini. Kutokana na mtikisiko wa dunia wa kiuchumi uzalishaji wa ngozi umeshuka kutoka bilioni 21 mwaka 2008/9 hadi *billion* 12 mwaka 2009/10. Hivi sasa kuna ngozi yenye thamani ya shilingi *billion* 1.4 isiyosindikwa na ambayo haijauzwa iko ndani, sasa Serikali hapa inatakiwa itafute mambo mbadala, lazima tutengeneze viatu katika viwanda vyetu kwa ajila ya kuuza ili viwanda viweze kudumu. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi wa *secondary* na *primary* kwani ni basi hatuundi Sheria kwamba wanafunzi wote wa *primary* na *secondary* lazima wavae viatu made in Tanzania? Majeshi yetu vilevile Polisi kwa nini tusitengeneze viatu ambavyo watavaa wao? Hii itasaidia sana kwa sababu viwanda vyetu vitapata kuishi na nchi itapata fedha na itaokoa fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo nataka kuzungumza ni suala la masoko. Tanzania ni *damping place,* kila kitu kinachotoka nje kinakuwa *damping* hapa, kuna zana za elekroniki zinakuja na hapa zinakuwa *damping* hapa, *spears* ambazo ni mbovu zinaletwa hapa zimezagaa katika mitaa yetu, mipira ya gari na kadhalika.

Sasa kwa kweli inashangaza kuona nchi hii inapokea tu vitu ambavyo havifai kwa matumizi. Kwa hiyo, naishauri Serikali iwe makini katika hili kwa sababu wamegundua Tanzania ni mahali pekee ambapo unapeleka Waswahili wanasema ni jaa yaani unapeleka hapa na vinakubaliwa na wananchi wetu wanaendelea kupata hasara kwa sababu wananunua vitu kwa bei kubwa lakini baada ya muda mfupi vinaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru na ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAYAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kuhusu Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Awali ya yote ningependa kusema kwamba naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Pili, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mary Nagu, mimi namfahamu nilipokuwa Mkuu wa Mkoa alikuwa anafanya kazi kwenye viwanda pale na alipomaliza kusoma alianza kazi katika Wizara ya Viwanda alikuwa NDC. Kwa hiyo, yeye kwenda katika Wizara hii kwa kweli karudi kule alikoanzia nampongeza kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Naibu wake wanashirikiana vizuri sana katika kazi lakini pia wamepewa Katibu Mkuu ambaye ana uwezo mkubwa, huyu Mama katika akina Mama Tanzania wenye uwezo Tanzania ninaowafahamu ni pamoja na Joyce Mapunjo ambaye ni Katibu Mkuu. Ni mama hodari mwenye uwezo wa kusimamia mambo kwa hiyo Wizara kwa kweli imekamilika. Tunawatakia kila la kheri.

Baada ya hayo ninapenda kuungana na Mwenyekiti wa Kamati ya viwanda, mimi nimetembea katika maonyesho mbalimbali lakini nataka tujivune wenyewe kwamba

maonyesho ya 33 ya Kimataifa yaliyofanywa chini ya uongozi wa Wizara hii na EPZ yalikuwa ya kimataifa kweli, hongereni sana. (*Makofi*)

Baada hayo vilevile ninapenda kupongeza BET chombo kilichosimamia, nawapongeza pia washindi walioshinda Wizara ya Maliasi ambao walipata zawadi ya kwanza kwa upande wa Serikali, naomba niwakumbuke pia SIDO, mimi kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wabunge mimi ndiye Mwenyekiti mwanzilishi wa SIDO. Niliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa SIDO mwaka 1973 na nimekuwa Mwenyekiti wa SIDO kwa muda wa miaka 17.

Hili shirika la SIDO lilianzishwa chini ya Azimio la TANU wakati wa Halmashauri Kuu ya Taifa, iliamua kwamba nchi yetu inaweza kwenda mbele tukisimamia kuanzishwa kwa viwanda vidogo na mimi wakati wa Mwalimu Julius K. Nyerere nikateuliwa kusimamia uanzishwaji wa Azimio hilo. Nawapongeza kwamba wanaendelea vizuri. Naipongeza pia Serikali kwa kuendelea kuiunga mkono SIDO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya hayo naomba pia nitoe shukurani kupitia kwa Wizara hii ambayo ni ya Biashara, naomba nitoe shukurani kwa sababu tulipozungumza sisi wakati wa Wizara ya Kilimo nilieleza kuhusu ununuzi wa mazao hasa mazao ya chakula. nimepokea simu kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Kwera, Kalambo, Sumbawanga, Nkasi na kwa ujumla Mkoa mzima, wanaishukuru sana Serikali kwa uamuzi wake wa kwamba baada ya kununua Mahindi ya SGR Serikali itaendelea kununua Mahindi mengine yatakayosaidia kuziba pengo mahali ambapo itatokea njaa, hongera sana kwa Serikali ya CCM kwa uamuzi huo.

Nataka niseme busara ya hili jambo ni hivi Serikali kuwa na Mahindi badala ya kuyaacha kwa watu binafsi itasaidia kwa sababu mwaka kesho tuna uchaguzi, tuna uchaguzi mkuu wa Madiwani, Wabunge na Rais jambo ambalo ni muhimu sana ni kuwa na chakula kwa sababu chakula ni uhai kwa hiyo naipongeza sana Serikali kwa uamuzi huo.

Sasa baada hayo ninapenda niseme mambo machache kuhusiana na Wizara hii hasa ya kimaendeleo ya sekta yenyewe. Lakini kwa kuwa viwanda viko vya aina kadhaa na kila wakati raslimali tuliyonayo ndiyo muhimu, mimi kwa utafiti ambao nimefanya wa uhakika ni kuwa katika kanda yetu hii ya Maziwa Makuu, nchi tajiri zilizojaaliwa na Mwenyezi Mungu kupewa raslimali kubwa na nyingi ambayo Mungu alitaka binadamu awe nazo ziko mbili, DRC na Tanzania ndiyo matajiri katika kanda hii. Sasa uamuzi wa matumizi ni juu yetu wenyewe.

Sasa mimi nataka nitoe ushauri ninavyoona mimi, jana Rais wa nchi yetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ambaye tunamuombe afya njema Mwenyezi Mungu amjaalie ili apate nafasi ya kuongoza tena taifa kwa miaka mitano mingine ijayo. Yeye na Rais Yoweri K. Museven wamesema tuache kosa la kuendelea kuuza malighafi nje, badala yake tuuze mali zilizosindikwa, mimi ndiyo nitaanzia hapohapo. (*Makofi*)

Serikali imefanya vizuri tumesema kilimo kwanza, sasa mimi naomba kilimo kwanza iwe na usindikaji kwanza vyote viende kama (*package)* yaani viende pamoja kwa sababu ukivitenganisha kimoja kitaumia. Masoko hayatapatikana mtaendelea kuuza malighafi, na hii ninayosema ni kwamba kwa sababu tumeamua hivi mimi natoa ushauri kwamba Wizara ya Viwanda, Kilimo, Maliasili, na TAMISEMI na Wizara ya Fedha waunde timu ya pamoja namna ya kwenda pamoja katika kufikia malengo haya. Lakini kwa vyovyote vile itachaguliwa Wizara ambayo itaongoza nayo ni Wizara ya viwanda katika suala hili la usindikaji ili wote tujue tunazungumza na lengo letu liwe moja.

Mimi nitatoa kidogo maelezo, nitaeleza namna wenzetu walivyofanya na mimi nimewahi kujaribu kufanya hivyo kwa hiyo nitaeleza kitu ambacho nina hakika nacho. Kwa mfano, nitaanza na matunda. Kujenga kiwanda cha matunda ili kisindike *juice* ni uamuzi lakini jambo la pili ni namna gani yatapatikana matunda ya kusindika kwa hiyo lazima vyote viende kwa pamoja.

Kwa hiyo, ushauri wangu hapa ni kwamba la kwanza tutambue maeneo ambayo yanaweza kulima matunda, nani watawekeza, nani watalima matunda nayo. Kuna njia mbili nzuri, moja anayeanzisha kiwanda cha kusindika matunda anaweza akapewa eneo la kujenga kiwanda na akapewa pia eneo la kulima matunda lakini akipewa eneo azungukwe na wakulima wadogo. Kwa hiyo, yeye anakuwa ndiye msindikaji na yeye ndiye anakuwa soko, wale wakulima wadogo wanaweza kupewa mikopo ya kulima aina ya matunda ambayo mwenye kiwanda atasindika na hiyo italeta mafanikio tu.

Sasa tukisema kwamba matunda yatoke tu Lushoto yaende Morogoro haisaidii, lazima Mkulima anayejenga kiwanda akipewa hekta 20,000 au 30,000 kwa mfano yeye azungukwe na wakulima wadogowadogo ambao yeye atakuwa chimbuko ya kufundisha utaalamu wa namna ya kulima matunda, usindikaji wa kisasa na kadhalika. Kwa mfano, mimi nimeona tuje kwenye Michikichi, juzi kulikuwa na suala hapa la ushuru, mimi sitaki kuzungumza habari ya ushuru ule uliotolewa 10%.

Ninachotaka kusema hapa ni kwamba wale wote wenye viwanda nitatoa mfano wa *Mohamed Enterprise* wana kiwanda cha kusindika, mimi ninachotaka kusema ni kwamba hawa wachaguliwe maeneo yaani wapewe maeneo ya kulima, akipewa hekta 100,000 yeye anaweza kulima 20,000 na nyingine 80,000 zilimwe na wakulima wadogowadogo ili kujaza kiwanda chake na jambo hili lisiwe la hiari. Mkutano ufanyike kwa wakulima wa Mikoa hiyo inayohusika na Wabunge wakiwemo na wenye viwanda, mkutano huu hautakutana kuzungumza habari ya ushuru bali tukutane kuzungumza namna ya kujitosheleza kwa mafuta ya kula, kwa hiyo mkutano huu utapanga mipango kuchagua Mikoa na nani watakaolima kwa mfano, Singida. Tukizungumza Singida haitafanana Michikichi, Singida ni kuwatambua wakulima tunasema kila Wilaya ya Singida iwe na kiwanda kidogo cha kukamua mafuta ya Alizeti na Mkoani Singida kijengwe kiwanda kikubwa kitakachopokea crude oil ya Alizeti kupeleka kwenye kiwanda cha ku refine palepale Singida. (*Makofi*)

Maana yake ni kusema wakulima wa Singida wawe na uhusiano na ujenzi wa viwanda na bei iwekwe ili mkulima akilima anajua nikilima nitauza wapi na bei

inajulikana. Sasa hivi wakulima wanacheza kamari, analima Alizeti hajui atauza kwa nani na tarehe gani. Kwa hiyo, mimi nasema mpango wa kulima uende pamoja na usindikaji lakini kwa kuwa msindikaji utakuwa ni soko

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo mimi ninachoshauri ni kuwa katika mpango huu lazima tuseme kuhusu chakula kwa mfano, Tanzania tunajua ugali na nyama na maharage. Duniani chakula siyo nyama na maharage au wali na maharage na nyama tu ni pamoja na matunda. Kwa hiyo, mimi napendekeza kwamba katika mpango wetu tuzungumze afya ya watu wetu pia kwamba chakula ni pamoja na mafuta ya kupikia, ni pamoja na matunda pia.

Mimi nimewahi kwenda Uarabuni, Oman kutembelea ndugu zangu, kila nyumba niliyoingia nilikuta kapu la matunda limejaa mezani, sisi kwetu matunda siyo chakula, kumbe matunda ni chakula. Kwa hiyo, nashauri mpango huu uhusishe kwa maana ya kusema kwa miaka mitano na kumi ijayo Tanzania tutajitoshelezaje kwa chakula kinachoitwa mafuta ya kupikia na nani watashiriki, uwe ni mpango na malengo na utekelezaji. Huo ndiyo ushauri wangu.

Kwa mfano, Pamba. Wananchi wa Mikoa hasa ya lake zote wanalima kwa sababu iko ndani ya damu yao lakini hawalimu kwa sababu ya pato. Pato la kilimo cha Pamba itaongezeka tutakapoanza kusindika nyuzi na *greying sheet* hapahapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema hapa, swali ninaloweza kuuliza, simuulizi Waziri maana ni kazi yetu sote, nauliza nyumba yako Mheshimiwa Mwenyekiti. Nani aliyetuzuia kusindika nyuzi kutokana na pamba ili tugombane naye? Pili, nani ametuambia Dini yetu iwe ni kuendelea kuagiza *Gray Sheet* kutoka Pakistan tuje tuweke muhuri wa rangi ya kanga? Wanaoagiza ni sisi wenyewe na tunawasamehe kodi, tunatoa vibali wenyewe. Kumbe tungeweza kusema wanaendelea kuleta, lakini baada ya miaka mitano/kumi ijayo mradi uwe unafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sisemi tuzuie leo, lakini tuwe na mipango ya kuzuia kesho, kwa sababu mipango yetu itakuwa imetuwezesha namna ya kuwa na nyuzi zetu wenyewe, itakuwa imetuwezesha namna ya kutengeneza *Gray Sheet* yetu wenyewe. Kwa hiyo, tutasema mjomba ahsante, ulituuzia imetosha. Sasa kama hatufanyi hivyo, tutaendelea kuwa watumwa na soko la watu wengine kwa mambo ambayo tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kwenda wote kupanga, ndio maana mimi juzi nikasema nitaleta mawazo. Ninataka niseme rasmi, wala sileti hoja Bungeni, nitapeleka mawazo kwa Waziri wa Viwanda mwa mpango mzima ninaoufikiria mimi inavyowezekana, kwa sababu tunapata uzoefu kwa wenzetu. Nitapeleka mawazo yangu kwa maandishi, Wizara itaungana na wenzao, wakipenda watatuita, tukakae tutoe mawazo ya kujitegemea. Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ndio uamuzi wa duniani kote.

Mimi sina haki ya kuwa na mke kama siwezi kujitegemea. Sasa jambo la kwanza la uhuru ni kujitegemea na lazima uanze na vitu vinjavyokupa uwezo, kukuongezea uwezo. Kwa mfano, maliasili; nimekwenda hoteli zote zilizojengwa, nyingi zimetumia mbao za hapa hapa, lakini bado sisi ni tegemezi kwa kuagiza fanicha kutokana na mbao za bandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kubwa ni kuhusu katani. Mimi nilikuwa Wizara ya Viwanda, ndiye niliyesimamia Kiwanda cha Katani cha Morogoro kukamilika kwa maagizo ya Mwalimu Nyerere wakati ule. Sasa juzi kimetokea kichekesho hapa; mtu mmoja, sitaki kumtaja jina, ananiambia jamani kuna matatizo ya kiwanda cha …

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, naambiwa ni kengele ya pili!

**MHE. DKT. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Pia, niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu wa Wizara na Watendaji wote, kwa kazi nzuri. Bila kuwasahau wapiga kura wangu wa Mjini Tabora, kwa kuniwezesha kuwa hapa. Baada ya kusema hayo, napenda niwapongeze Wananchi wa Tabora, kwa kazi nzuri waliyofanya kwa kujenga shule za sekondari chini ya usimamizi mzuri wa DC Chang'a.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nirudi sasa kwenye kuchangia bajeti hii ya Wizara. Kama alivyosema Waziri katika kitabu chake cha hotuba, amekiri kwamba, viwanda ni sehemu nyeti na muhimu kwa uchumi wa nchi. Mimi nakubaliana naye na naendelea kukubaliana na wengine waliosisitiza umuhimu wa viwanda katika uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba, kusema kweli viwanda na kilimo ni watoto pacha. Nataka kutumia neno watoto pacha; kiwanda na kilimo ni watoto pacha huwezi kuwatenganisha. Kilimo kinategemea viwanda na viwanda vinategemea kilimo. Katika hili kama walivyosema wasemaji waliotangulia, inaonesha kabisa kwamba, Tanzania tuna matatizo ya kutenda yale tunayoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia dhana ya viwanda tena dhana ya kununua mali inayotengenezwa na viwanda vya Tanzania. Leo, Mheshimiwa Waziri, kwa heshima kubwa ya viwanda vya Tanzania, amevaa vazi linalotokana na viwanda vyetu. Kama walivyoeleza wasemaji waliotangulia, hivi tuna sababu gani ya kusema tutumie magunia ya *jute* na tusitumie magunia ya katani yanayotokana na katani, yanayotengenezwa na kiwanda cha Tanzania, yanayoajiri Watanzania ili kufanya hiyo kazi? Sasa hapa ndipo ninaposema hata Serikali yenyewe inasema ambayo haiyatendi. Jambo hili, Serikali liko machoni penu, linafanywa hadharani, mchana wala siyo usiku, inatoka *circular* inasema tumieni magunia ya *jute* acheni ya katani na Serikali ipo! Kwa maana hiyo, nakubaliana na pendekezo la Kamati, pamoja na Msemaji wa Upinzani, wanaposema kwamba Bunge litoe Azimio kwamba,

Serikali iagizwe itoe maelekezo kuwa kuanzia sasa kwa ajili ya kulinda viwanda vyetu na ajira zetu, tutatumia kwa kuanzia nguo za Tanzania, magunia yanayotokana na katani ya Tanzania na vitu vingine ambavyo nitavielezea baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndio wakati muafaka wa kuzungumzia nafasi ya Tanzania katika Soko la Afrika Mashariki. Katika Soko la Afrika Mashariki wakati ambapo litaanza kutumika kama Soko la Pamoja *(Common Market*), habari ya kwamba Tanzania wataweka ushuru kwa bidhaa zinazotoka Kenya halitakuwepo. Kwa maana hiyo, mimi kidogo nimeshtuka, baada ya kuangalia *statistics* ambazo Mheshimiwa Waziri amesema kwamba urari wetu wa malipo baina ya biashara ya Kenya na Tanzania, sisi tuna *export* zaidi Kenya kuliko Kenya wanavyonunua kutoka kwetu. Hapo kidogo napata wasi wasi, haiwezekani! Kwa hiyo, nini nafasi ya Tanzania katika Soko la Afrika Mashariki litakapoanza kuwa Soko la Pamoja katika hali halisi ya Soko la Pamoja *(Common Market)*? Tumejitayarishaje, ikiwa habari tunazozungumza humu ndani ndiyo hizo za kuua viwanda vyetu na kutukuza viwanda vya nje? Kweli sisi tutakuwa namna gani katika hili Soko la Afrika Mashariki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora kuna kiwanda cha kusokota nyuzi. Kinasokota nyuzi na hivi tunavyoongea, katika maghala ya kiwanda hicho kuna nyuzi zilizosokotwa ambazo hazina soko; ajabu kubwa sana!

Wakati huu tunavyoongea hivi sasa, huko upande wa Mwanza, Shinyanga na kadhalika, kuna maghala ya mabeli na mabeli ya pamba hayawezi kuuzwa kwa sababu eti hatuwezi kuuza nchi za nje. Wakati huo huo, nchi hii hii viwanda vyetu humu vinaagiza bafta kutoka nje inayotengenezwa na nyuzi za pamba, ajabu iliyoje hii! Tuna pamba haijauzwa, tuna nyuzi hazijauzwa, tunaagiza bafta kutoka nje, kwa sababu gani? Halafu tunasema nunua Tanzania, kuwa Mtanzania! Sasa ni aina gani ya viwanda tunavyovi-*promote* hapa nchini jamani? Kwa maana hiyo, inavyoelekea hata *Fiscal Regime* yetu kwenye upande wa *Taxation* haisaidii maendeleo ya viwanda vya nchi hii. Kwa hiyo, wenzangu mlioko kwenye Wizara ya Fedha, angalieni *the Taxation Policy,* kwa kiasi gani inasaidia maendeleo ya viwanda vya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja zinazungumzwa hapa, ooh kuna *World Trade Organization (WTO)* inasema kwamba, sasa biashara iwe huria tu, lakini hii hii *World Trade Organization* inatoa *exceptions* kwenye nchi ambazo zina sababu muhimu za kuendelea kuweka vikwazo ama vya *tariff* au vikwazo vya viwango. Kwa hiyo, sisi kama Tanzania, kusema kweli hata *World Trade Organization* haiwezi kutukatalia kulinda viwanda vyetu ambavyo vinatumia malighafi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niipongeze Wizara kwa usimamizi mzuri wa Maonesho ya Saba Saba Mwaka 2009. Chombo chetu cha *BET* kimefanya vizuri na ningependa kiendelee kufanya vizuri. Wakati huo huo, naiomba Serikali na hasa hapa Wizara ya Fedha, iangalie uwezekano wa kuiondolea mzigo wa madeni *Board of External Trade (BET)*, inayodaiwa na Serikali. Chombo hiki ni cha Serikali, madeni ya Serikali, hebu Serikali ikae iyaangalie haya namna ya kuayaondoa ili *balance sheet* yake iwe nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuendelea na habari ya viwanda bila kutengeneza utaratibu unaozingatia hoja muhimu kwamba ni lazima tuwe na Sera hasa inayoanza na Viwanda Mama. Viwanda Mama vyetu ni vipi? Viwanda Mama vyetu ni vile vinavyotumia malighafi ya nchi kutengeneza mali nyingine au bidhaa nyingine zinazohitajika na viwanda vingine. Kwa maana hiyo, tutakuwa na utaratibu wa kiwanda kimoja kutengeneza mahitaji ya kiwanda kingine ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina chuma, nchi yetu ina *soda ash* kule *Lake Natron*, nchi yetu ina mpira, nchi yetu ina mchanga mzuri kule baharini, unaweza kuwa ni malighafi ya kutengeneza kioo. Hivi vyote vingeanzishwa kwa utaratibu wa Viwanda Mama ili baadaye viwanda vingine vianze kukua kutokana na hivi viwanda Mama. Sera yetu inasema nini juu ya hilo? Tunahangaika siku zote namna ya kupata mwekezaji kule Liganga kwenye chuma chetu. Bila chuma hatuwezi kuwa na Kiwanda Mama ambacho ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi wetu. Hebu tuanze kutengeneza chuma pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muheza wanalima mpira. Jirani pale Arusha kuna kiwanda cha kutengneza matairi, hivi sasa tunavyoongea kimekaa, kimelala. Matairi yanahitajika nchini. Kama tija ni soko, soko la matairi lipo, kwa hiyo soko si tatizo, tatizo ni uzalishaji wa matairi nchini. Katika hali hii, eti sisi tumeona bora tuendelee kuagiza matairi kutoka nchi za nje kuliko kutumia matairi yanayotengenezwa Tanzania na Watanzania, tukatoa na ajira kwa Watanzania. Tunafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule *TABOTEX* nimesema kiwanda kipo kinatengeneza nyuzi, lakini nyuzi hazina soko.

Magunia tumeshaelezea. Sasa nataka nizungumzie suala zima la *package* ya kunusuru uchumi wa nchi kama ilivyotangazwa na Mheshimiwa Rais. Moja ya wale watakaonusuriwa ni viwanda, ambavyo vimeshindwa kuuza kutokana na matatizo ya masoko duniani. Sasa hivi tunataka huyu mwenye kiwanda cha magunia na huyu mwenye kiwanda cha nyuzi Tabora, nao waende kukinga bakuli katika utaratibu wa kunusuru uchumi? Wajenge hoja kwamba ameshindwa kuuza, kwa hiyo nao wanastahili kupewa msaada wa kupunguziwa hayo madeni kwa sababu ya kushindwa kuuza? Hivi kweli hii itakuwa ni hoja inayokubalika? Hivi kweli tunusuru viwanda hivi kwa kutoa *package* ya kunusuru uchumi? Viwanda ambavyo vina soko nchini lakini sisi wenyewe tumevinyima soko; Mheshimiwa Rais ana kazi hapa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuzungumzia suala la katani, wamesema wenzangu waliotangulia kwamba, wale wanaoleta *jute* Tanzania wanapewa ruzuku na nchi zao. Kwa hiyo, kama kisingizio ni kwamba tununue *jute* hapa nchini kwa sababu ni rahisi, ni rahisi kwa sababu huko inakotoka inapewa *subsidy*. Kwa vyovyote haiwezi kushindana na mtu ambaye amefungwa mikono nyuma halafu anaambiwa pigana. Utapiganaje na mwenzako wakati wewe umefungwa mikono nyuma? Unaambiwa pigana naye, huwezi kupigana naye!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa la gharama za kufanya biashara Tanzania. Mikopo haipatikani, ikipatikana ni ghali, umeme ni ghali, maamuzi hayatoki

kwa haraka, miundombinu yetu ndiyo hiyo, reli haifanyi kazi, barabara katika sehemu nyingine za nchi ni mbaya. Haya yote haya, huwezi kuyaondoa kama unataka kukuza Sekta ya Biashara. Lazima uyaweke vizuri ili uweze kufanya biashara vizuri. Huwezi kufanya biashara bila mikopo, huwezi kufanya biashara ya ufanisi kama mikopo ni ghali kuliko mapato yanayotokana na biashara unayofanya. Hiyo ndiyo Tanzania, kwa hiyo ni lazima tubadilishe haya yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kwa haraka haraka nisisitize suala la samani. Hatuna sababu Tanzania kununua samani zinazotokana na pumba pumba au vumbi la mbao. Kama sisi tunapenda sana samani zinazotokana na pumba na vumbi la mbao, basi hilo vumbi si tutengeneze sisi wenyewe tunazo mbao? Kama tunataka samani ya vumbi, basi tusage hizo mbao tupate vumbi; ni suala la kuchanganya vumbi na gundi. Ukishachanganya vumbi na gundi, juu ukapaka rangi, tayari umepata hiyo mbao ambayo ni *artificial*. Sasa sisi tunazo mbao, randa tunazo, mafundi tunao, kwenye Vyuo vya VETA tunawafundisha, lakini hatuwapi soko na mnunuaji mkubwa wa samani ni Serikali. Serikali ikitoa *order* kwa mafundi seremala wale kwamba tunataka madawati, tunataka meza za ofisini, tunataka viti vya ofisini, mbona tutatengeneza pesa! Tena uamuzi huo utakuwa ni chachu ya kuzungusha pesa ndani ya uchumi wetu wenyewe. Zile pesa tunazopeleka nje, zitakwenda kwa maseremala wa hapa nchini na hiyo kwa desturi ya uchumi ni kwamba, sekta moja itaamsha sekta nyingine na uchumi utakua kwa sababu uchumi kwa ujumla utakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. OMARI M. NIBUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika hoja hii muhimu ya viwanda, biashara na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukushukuru wewe, pia ningependa niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Morogoro Mjini, ambao wanaendelea kuniunga mkono siku hadi siku, tukishirikiana katika kutatua kero zetu kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza, ningependa pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, kwa uwezo wake jinsi anavyotekeleza majukumu haya katika Sekta hii ya Viwanda ambayo ni muhimu mno. Pia nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam, kwa namna moja au nyingine, ambao wamesaidia katika kuandaa hotuba hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, naomba niende moja kwa moja katika uchangiaji. Nchi zote duniani, ambazo zimeendelea ni zile ambazo zimeimarika sana katika Sekta ya Viwanda. Nchi hizi katika Sekta za Viwanda hazikuimarika tu, ni kwamba zimejitengenezea sera ambazo zinalinda viwanda vyao. Kwa mfano, wao wanazo sera maalum za kufanya kwamba kwanza viwanda hivyo vinaondolewa kodi au vinapunguziwa kodi; lakini pamoja na kuondolewa kodi, pia vinapewa ruzuku ya Serikali ili viweze kuwa na ufanisi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote ni kwamba, vinafanya kazi za kutoruhusu zile mali au mazao ambayo yanasindikwa na viwanda vyao, hawaruhusu mali kama hizo ziingizwe kutoka nje ya nchi, kwa sababu zitaleta upinzani katika soko la ndani. Kwa mfano, sisi Tanzania tunasema tunayo kaulimbiu inayosema Kilimo Kwanza. Tunaposema Kilimo Kwanza, lazima kiendane na uimarishaji wa viwanda vyetu katika nchi, kwa sababu mazao yote haya ambayo yanalimwa ni vizuri yasindikwe ili yaweze kuleta thamani ya mazao hayo, kwa sababu mazao haya yakiuzwa yakiwa ghafi, maana yake tunapata faida kidogo na nchi haiendi popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya kusindika mazao kwenye viwanda ni kwamba, kwanza inaongeza thamani ya mazao haya, lakini pia kunakuwa na hamasa ya uzalishaji wa mazao haya katika mashamba, hivyo basi yanaongeza ajira ya wananchi wetu au vijana wetu katika mashamba husika. Pia mazao haya yakishapelekwa kwenye viwanda, kule kwenye viwanda nako kuna ajira kwa wananchi wetu ambao wanatakiwa waajiriwe ili waweze kuboresha maisha yao.

Pia mazao haya yanaongezwa thamani, kwa mfano kama pamba ilikuwa iuzwe shilingi 5000, ikishasindikwa maana yake itauzwa shilingi 15,000, kwa hiyo itakuwa imeongezeka thamani. Kama hiyo haitoshi ni kwamba, pia Serikali inakusanya kodi kwenye viwanda hivi kupitia TRA, kwa hiyo kuna umuhimu mkubwa wa kusindika mazao kuliko kuyauza moja kwa moja nchi za nje yakiwa ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Zao la Mkonge lina *grade*; kuna *grade* ya kwanza, *grade* ya pili na mkonge mchafu. Unapotaka kuuza nchi za nje kama mkonge ghafi, lazima upeleke mkonge ule ambao ni safi wa *grade* ya juu sana, kwa maana hiyo *grade* zilizobaki hizi inabidi uzitupe; ambayo ni hasara kubwa. Kwa kupeleka kwenye viwanda na kwa bahati nzuri viwanda vya magunia vinatumia mkonge wa *grade* ya chini zaidi, kwa maana hiyo, mali yote ile ya mkonge inatumika. Mkonge wenyewe kama mkonge, unapokwenda kwenye jineri, ule uchafu unapotoka, unatoa gesi ya kutosha na unaweza ukafua umeme mdogo mdogo ambao unaweza kutumika katika majengo yetu. Kwa hiyo, usindikaji ni muhimu mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Morogoro pale, kuna viwanda vingi; kuna kiwanda kinachoitwa Morogoro Canvas Mills, kuna Kiwanda cha *Polyster*, kuna kiwanda kinaitwa TPM 1998 Ltd., Morogoro, Morogoro Turneries, Kiwanda cha Mafuta MOPROCO, Kiwanda cha Sabuni cha KOMOA, Leather Goods, Seramics, Moro Shoe, Kiwanda cha SIDO, Kiwanda cha Juisi na Kiwanda cha Tumbaku. Kati ya viwanda vyote hivi, viwanda vinavyofanya kazi ni vichache sana. Kiwanda kinachofanya kazi kwa asilimia kubwa ni Kiwanda cha Tumbaku. Pia Kiwanda cha Morogoro Canvas, kinafanya kazi kwa ufanisi mzuri.

Naomba nitumie nafasi hii, kuisifia sana Menejimenti ya Kiwanda cha Morogoro Canvas, kwa sababu hata ukifika kinaonekana ni kisafi kuliko labda viwanda vyote nilivyoviona Tanzania. Kwa hiyo, ningependa Menejimenti nyingine za viwanda ziende zikaige wanavyotunza mazingira pale kwao. Pamoja na kiwanda hicho, kuna Kiwanda cha *Polyster*, kiwanda cha nguo. Kiwanda hicho ni kikubwa, kinazalisha nguo nyingi za hapa nchini. Pia kuna kiwanda cha TPM 1998 Ltd, Morogoro, kiwanda hiki ni cha

magunia. Vile vile kuna Kiwanda cha *Turneries,* ambacho nacho kinafanya kazi kidogo sana, kiwanda hiki ni cha ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitoe mfano mmoja katika viwanda hivi. Jana tu nilikuwa na mkutano na Wafanyakazi wa Kiwanda cha Magunia, baada ya kuniomba niende nikawasikilize shida zao. Nilipokwenda pale, kusema kweli inasikitisha; Kiwanda hiki cha Magunia cha 1998 Morogoro, kina uwezo wa kuzalisha magunia milioni 10 kwa mwaka kama kikifanya kazi kwa uwezo wake wa asilimia 100. Kwa bahati mbaya, kutokana na mazingira ambayo si mazuri, kiwanda hiki kinazalisha magunia 1,500,000 tu badala ya magunia milioni 10 na ukiuliza sababu ni nini, ni kwamba soko hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokwenda pale nilitamani kulia, kwa sababu nimekuta stoo imejaa magunia yamerundikana, mahali pa kuweka hakuna, mengine yamewekwa nje. Nauliza kwa sababu gani, wanasema kwa sababu soko halipo. Soko halipo kwa nini? Wanasema kwa sababu yako magunia yanaitwa ya *jute* yanatoka India na Indonesia, magunia haya yanauzwa bei rahisi kulinganisha na magunia ya mkonge. Sasa nikajiuliza; kwa nini Serikali inafanya hivi wakati tuna viwanda vyetu wenyewe? Kwa nini tunalegeza masharti kiasi hiki kiasi kwamba viwanda vyetu haviwezi kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri, magunia ya mkonge ni magunia bora zaidi kuliko magunia ya *jute*. Kwanza, magunia ya *jute* hayaingizi hewa, kwa hiyo, yanaharibu mazao. Pia mazao yanayotoka mle, kwa mfano, ikiwa ni kahawa inatoa harufu. Magunia haya kwa sababu yanaingiza hewa, hakuna harufu hata kidogo. Magunia haya bahati nzuri yanaweza kutunza kahawa au mazao mengine kwa muda mrefu zaidi, kwa sababu hayana joto la kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hiki pale Morogoro sasa hivi kimeajiri wafanyakazi wasiopungua 500. Wafanyakazi hawa walikuwa wanalalamika wanasema Mheshimiwa Mbunge, hivi kiwanda hiki kikifungwa sisi tutaenda kufanya kazi gani? Chukulia kwa mfano wafanyakazi wale 500, kila mfanyakazi awe na familia ya watu 6; 500 mara 6 ni watu ni watu 3000. Watu 3000 hawa wakose chakula, wakose kulipa kodi za nyumba, wakose elimu, wakose mavazi na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiuliza sababu, Serikali yetu ndiyo iliyofanya kile kiwanda kisifanye kazi yake kwa kiwango cha juu, kwa sababu ya kuruhusu magunia mengine kutoka nchi za nje na kufanya kiwanda kile kisiweze kuuza magunia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri, miaka michache iliyopita, kabla ya mwaka 1999, kiwanda hiki kilikuwa kinauza magunia mengi tu, walikuwa wanauza magunia mpaka 900,000 kwa mwaka, kwa sababu kulikuwa na hii *International Coffee Organization.* Wao waliamua kwa makusudi kwamba mazao ya kahawa yawekwe kwenye magunia yanayotokana na mkonge na kwa bahati nzuri na Serikali yetu ilikuwa imeridhia. Kwa hiyo, tatizo la soko halikuwepo. Kwa bahati mbaya, hivi sasa hilo suala limeshaondolewa na Mamlaka ya Kahawa. Kwa hiyo, utakuta sasa magunia ya *jute*

yanaingia kwa sababu bei yake ni rahisi. Kama unavyojua, watendaji wetu hawaangalii faida ya nchi, wanaangalia faida zao binafsi. Kwa hiyo, akitokea mwekezaji ambaye atatoa chochote kuwaambia kwamba, jamani mkichukua magunia haya na ninyi mtapata chochote, basi hawajali kwamba Serikali itaumia au nini, matokeo yake wanaagiza yale magunia kwa wingi na matokeo yake kiwanda hiki cha magunia kinakosa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwombe dada yangu, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, kwa bahati nzuri ni mtendaji mzuri, msikivu, anajua mambo na mwenye uchungu na nchi yake. Naomba leo atupe tamko kwamba, katika suala hili la magunia, watapiga marufuku magunia ya *jute* kutoka Indonesia na India ili viwanda vyetu viweze kufanya kazi. Naomba sana na hilo jambo lipo hata katika mazao mengine, kwa mfano, mafuta, pamba na kadhalika. Naomba Serikali iamue kwa makusudi ili kuhakikisha kwamba, nchi yetu tunajitosheleza wenyewe kwa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema Kilimo Kwanza, kilimo lazima kiendane na viwanda na kama alivyosema shemeji yangu, Mheshimiwa Kaboyonga, huwezi kuviacha kwa sababu hawa ni watoto pacha. Kama huna viwanda, kilimo chako hakina maana, kwani utauza ghafi zote na ghafi bei yake ni chini kuliko mazao yaliyosindikwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nazungumza jambo hili kwa uchungu sana, kwa sababu wafanyakazi ambao ni wapiga kura wangu ndani ya Morogoro, walikuwa wananiambia kwa uchungu sana na wameniambia tunataka tukusikie ukizungumza hili vinginevyo kura zetu umezikosa. Ndio maana naongea kwa nguvu zangu zote, wajue kwamba ninawatetea. Naomba Waziri, awaonee huruma wafanyakazi hawa, Wananchi wa Morogoro ambao wanateseka. Kama nilivyosema, nimetaja viwanda chungu mzima vimekufa. Naomba tuvifufue kwa faida ya nchi yetu na hiyo si kwa faida ya Morogoro tu ni kwa faida ya nchi nzima. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mtu hakuelewi kabisa kwamba, unakwenda kulea mtoto wa mwenzako, unaacha mwanao afe, mimi sijaelewa kabisa! Unaweza ukasema nchi hii labda haina wataalam. Wakati mwingine tunawalaumu Mawaziri, lakini Mawaziri wanapewa ushauri na wataalam. Inawezekana wakati mwingine ushauri mwingine ni kutokana na Waziri kubanwa na kazi, linaweza likaja jambo anaambiwa asaini kwa haraka haraka, kwa sababu pengine anataka kusafiri akapiga mkono tu akiamini kwamba mtaalam wake kamuwekea mambo mazuri, kumbe kamchomekea. Wataalam wanasema amemchomekea.

Naomba sana, kama Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko yupo na watalaam mnatusikia, tunaomba sana, vinginevyo mwaka kesho mtakapokuja labda muwe mmehama kwenye Wizara, tutashika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Dkt. Mzeru Nibuka, naamini kabisa Mheshimiwa Waziri amekusikia. Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo moja kwa Wabunge wote kwamba, pale kwenye Viwanja vya Maonesho vya Bunge, wako ndugu

zetu wa Benki ya Wanawake, wanawaalika wote mkaone shughuli zao, mnakaribishwa. Kubwa zaidi, mnaombwa mwende mkanunue hisa katika Benki hiyo mpya. Hisa hizo zinanunuliwa na wanawake na wanaume. Kwa hiyo, haibagui katika kununua hisa. Tunakaribishwa sote. *(Makofi)*

Baada ya hapo, niseme kwamba, katika orodha niliyonayo hapa mezani ya walioomba kuchangia Wizara hii ni Waheshimiwa Wabunge 40. Kwa vyovyote vile, hatuwezi kumfikia kila mmoja wenu na kama mnavyoona waliochangia asubuhi wote sita ni wanaume; kwa Chama cha Mapinduzi watano, Upinzani mmoja. Kwa hiyo, kwa vyovyote jioni lazima itabidi meza iangalie, ichekeche kidogo ili kuweka ule uwiano ambao ndio utaratibu wetu.

Kwa hatua hiyo, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.56 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Katika uchangiaji wetu, naomba Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy aanze na atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Ally Salum.

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia leo hii nikaweza kusimama hapa kwenye Bunge lako na kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Napenda kumpongeza Waziri, Naibu, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote, kwa hotuba yao nzuri. Vile vile na Msemaji Mkuu wa Wizara hii kwa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa pole Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, kwa ajali kubwa iliyotokea na watu 28 kufariki. Mwenyezi Mungu, awajalie wale waliokuwa hai awape umri mrefu na wapone ili waendelee katika ujenzi wa Taifa na wale waliokufa, awalaze mahali pema. *(Amin*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa ku-*declare interest*, mimi ni mfanyabiashara, naanza kuchangia kuhusu viwanda. Serikali imetangaza Kilimo Kwanza na kilimo kama wenzangu waliotangulia walivyosema kwamba, kinakwenda sambamba na viwanda. Pamoja na jitihada za Serikali kuweza kuongeza viwanda, lakini bado viwanda havitoshi. Hasa ukilinganisha hiki Kilimo Kwanza kinachokuja basi viwanda ni vidogo sana. Ukiangalia na kwenda katika vijiji hasa Muheza, Chalinze, unakuta matunda mengi sana yanaoza na hii yote pamoja na kwamba kuna Kiwanda cha Bakhressa cha Azam, lakini bado kunahitajika viwanda vingi kwa ajili ya kutengeneza *juice* na vile vile matunda mengine mengi yanaoza katika mashamba. Kwa hiyo,

naiomba Serikali ifanye juhudi za makusudi ili ihakikishe kwamba, viwanda vinajengwa tena kwa kasi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, wenzetu tukienda nje tunaona sana matunda ambayo ukiangalia kama machungwa hata ladha hayana ukilinganisha na machungwa yetu hapa Tanzania. Vile vile utakuta mananasi madogo sana, yaani hata huwezi kuona kama lile ni nanasi utafikiri la plastiki, kumbe ni nanasi na bei zinazouzwa ni kubwa. Namwomba Waziri wa Wizara hii, awatafutie masoko ya uhakika katika nchi za Kiarabu na nchi nyingine nyingi, kwa sababu huku tunasubiri viwanda basi tuhakikishe kwamba, tunawapatia masoko ya uhakika ya kuweza kufanya *packing* vitu vyao na kuweza kusafirisha nje. Nchi yoyote duniani, haiwezi kuendelea kama haina viwanda. Vile vile na nchi yetu ina ardhi nzuri na kubwa, ambayo tunaweza kujenga viwanda vya kutosha na kuwapatia wananchi wetu ajira, lakini bado Serikali haijaweka mikakati ya uhakika kuhusu jambo hili. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijipange vizuri ili kuweza kuhakikisha viwanda vinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye TBS. Katika Gazeti la Mwanahalisi la tarehe 22 Julai, 2009 katika ukurasa wa 8, naomba kunukuu: "TBS yadoda na alama za ubora." Kwa kweli baada ya kuona hali hii, nilishtuka sana lakini nikaona nisifuate kwenye magazeti. Nikamfuata Mwenyekiti wa Kamati za Bunge ili kuuliza swali hili kwamba, TBS wameshindwa kukisaidia kiwanda kilichokuweko Moshi katika viwanja vya SIDO na kiwanda hicho kinaitwa *Nyera Farm Limited*, ambacho inasikitisha sana kuona kwamba kiwanda hiki kimepata viwango kutoka katika nchi ya Kenya. Hili ni jambo la aibu sana hasa ukizingatia kwamba, sisi tunapiga kelele sana kutaka kukuza uchumi wetu, lakini wenzetu wanaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujakataa kwamba, wafanye kazi zao kwa uhakika, lakini waangalie kwamba mambo kama haya ni muhimu sana ili kuwasaidia vijana wetu wapate ajira za uhakika. Viwango vinavyotolewa viwe vya uhakika na ndiyo maana utaona kutokana na uzembe wa kazi wanaofanya baadhi ya wafanyakazi wa Shirika hili la TBS, vitu vingi *fake* vinaingia hapa nchini. Kwa hiyo, naiomba Serikali ilichukulie kwa kina kabisa suala hili ili tuhakikishe kwamba, wananchi wanafaidika na mambo muhimu. Jambo lingine, mimi niko katika Kamati ya Miundombinu. Nimewahi kutembelea katika Chuo cha Dar es Salaam DIT na pale niliona zana nyingi za umeme, ambazo wananchi wangeweza kuungiza umeme kwa urahisi sana, lakini tulipouliza na kuona mambo mazuri kama yale, tukauliza kulikoni kwa nini hizi zana hazitumiki ili kuwapatia wananchi wa vijijini umeme kwa urahisi, tukaambiwa kwamba TBS bado haijathibitisha na kila siku wanapeleka barua lakini hawapati jawabu.

Kwa hiyo, namwomba Waziri mambo haya ya kufanya ukiritimba katika nchi yetu, tunasema kufanya zohari katika nchi yetu, hayatatupeleka mbele yataturudisha nyuma na hasa ukizingatia watafiti wengi wanatumia fedha nyingi na ni wa Watanzania ambao wanagundua watarudi nyuma kwa sababu hatuwezi kuwahakikishia kwamba, wataweza kupata soko kutokana na watu wa TBS kuweza kuzorotesha kazi hiyo. Naomba Wizara yako, ichukue juhudi za makusudi ili tuhakikishe kwamba, haya mambo ya kuzorotesha yaweze kuondoka na nchi yetu iweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwa wafanyabiashara. Nchi za wenzetu, wafanyabiashara wa kigeni hawawezi wakapewa leseni mpaka uhakikishe unafanya ubia na mwananchi wa nchi ile ambaye yuko yule mfanyabiashara. Kama jana mliangalia katika vyombo vya habari, tuliwaona wageni ambao wameingia katika nchi yetu kwa kutumia udanganyifu. Wamekuja kuwekeza, lakini wanafanya biashara za Watanzania, ambazo mwisho wa siku watawaharibia soko wafanyabiashara wa nchi hii. Wafanyabiashara ambao wanatumia ghiliba, tuhakikishe kwamba sheria inafuata mkondo wake, kwani itafika mahali tutakuwa na wafanyabiashara wadogo, hasa wanawake hawana nafasi. Kwa sababu mtu akija hapa kwa kuwekeza ni mgeni halafu akadanganya baadae akaingiza makontena pengine 20 au 40, lakini mfanyabiashara mdogo analeta kontena moja, kwa hiyo, bei yake inamfanya yeye arudi nyuma kwa sababu bei utakayonunulia kitu kimoja haiwezi kuwa sawa na bei aliyonunulia yeye mwenye makontena mengi. Kwa hiyo, naiomba Wizara yako pamoja na Wizara nyingine ambayo inayohusika, ifuatilie kwa kina ili kuwaokoa wafanyabiashara wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naiunga mkono hoja ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu azimio la kutumia magunia ya mkonge, badala ya kutumia magunia kutoka nchini India, kwani haya yatawasaidia kuwapatia kazi vijana wetu, ajira katika viwanda na vile vile kuboresha maslahi yao. Kwa hiyo, naungana na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, pamoja na Mwenyekiti wa Biashara na Viwanda kuhusu utumiaji wa magunia ya mkonge badala ya kutumia magunia ya nchini India na Indonesia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy. Kama nilivyosema, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum atafuata, Mheshimiwa Rosemary Kirigini ajiandae.

**MHE. AHMED ALLY SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, kwa hoja yake nzuri na timu yake nzima, walivyoiwasilisha hapa Bungeni.

Naomba nianze na viwanda katika Mkoa wetu wa Shinyanga. Tukija na ile dhana kwamba, Kilimo Kwanza, asilimia 60 ya pamba inatoka Mkoa wa Shinyanga, lakini ajabu ni kwamba, hatuna hata kiwanda kimoja kwenye Mkoa huu; ni aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama namna ambavyo msukosuko wa uchumi ulivyoikumba nchi yetu, moja katika mikoa ambayo iliathirika kwa kiasi kikubwa sana ni Mkoa wa Shinyanga. Wakulima wa pamba walipata tabu, yote kwa sababu tunategemea wanunuzi kuuza, tuna-*export* pamba kama *raw materials* siyo kama *finished product*. Hivi Mkoa wa Shinyanga kukosa kiwanda hasa tatizo lake liko wapi? Serikali ikisema siyo tatizo letu hapana, niiombe Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, waende

wakatutafutie wawekezaji waje kuwekeza Shinyanga. Tunahitaji viwanda kwa ajili ya kutengenezea nguo ili pamba yetu katika Mkoa wa Shinyanga iwe na *added value,* tutengeneze nyuzi, nguo na itakuwa ni suluhu kubwa au ni soko zuri kwa wakulima wa pamba katika Mkoa wetu wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kungelikuwa na viwanda viwili au vitatu katika Mkoa wa Shinyanga, Soko la Afrika Mashariki ni kubwa, Soko la SADC kubwa, Burundi/Rwanda karibu pale wangeweza kuja kununua tu. Soko letu la Tanzania vile vile ni zuri, lakini ukisema kwamba, Mkoa wa Shinyanga hauna Kiwanda cha Nguo kwa kweli ni aibu. Hivi kule nje mkiulizwa katika maeneo kama hayo kwa nini hakuna kiwanda Shinyanga, hivi Waziri kama Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko unaweza kweli ukajibu nini si aibu tu? Kwa bahati nzuri, Mheshimiwa Membe, Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa yuko hapa. Mheshimiwa Membe, nikuombe sana unapokuwa kwenye ziara zako nchi za nje, tutafutie wawekezaji wa viwanda vya nguo kwenye Mkoa wa Shinyanga. Mheshimiwa Membe, nimekufikishia salamu hizo, nakushukuru sana na nitakushukuru sana ukituletea wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna suala zima la magunia kama lilivyoongelewa na Wabunge wengi. Suala siyo tu magunia, kuna magunia yanaingia nchini kodi imeshushwa sana. Magunia ya Tanzania yanapandishwa kodi, sioni *vision;* hivi kule Wizarani kuna tatizo gain? Nashindwa kugundua kwamba, tunafanya hivi tunakwenda kuwaumiza wakulima wa mkonge. Tanzania katika historia, ilikuwa ndiyo ya kwanza kuzalisha mkonge duniani kote, leo inakuwa ya mwisho kabisa na tunakwenda kuiua. Fedha za Tanzania zinanunua magunia nje ya nchi, tunawafaidisha wakulima walioko nje, jamani tuna matatizo gani Wizarani kule? Naiomba Wizara ijaribu kwa namna moja au nyingine, ilitazame hili suala la magunia ya Tanzania ushuru wake futeni, pandisheni ushuru wa magunia ya nje ili magunia ya Tanzania yanunuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, hata saruji ni kweli kuna wakati saruji bei ilipanda sana, Serikali imefanya juhudi lakini sasa kwa namna moja au nyingine utaona viwanda vya saruji vina *stock* kubwa wanashindwa kuuza. Vile vile kuna ngano inatoka Uturuki inakuja kuuzwa kwa bei rahisi, kule wanapata ruzuku kwa *subsidy* kubwa tu hapa hamna. Sasa kama tunafanya namna hii, hata viwanda vya ngano, viwanda vya saruji vitakufa kama kilivyoanza kufa Kiwanda cha Magunia; ni hatari sana. Nimuunge mkono Mheshimiwa Dkt. Mzindakaya, alivyosema inapofika wakati wa kutengeneza bajeti, Wizara hizi muhimu sana Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na Wizara ya Fedha na Uchumi, mkae pamoja kuwe kuna *vision* moja kwamba tunafanya hivi, tunapanga bajeti kwa ajili hii na hii kwa ajili ya maslahi ya Watanzania na wakulima wake. Kila Wizara ikiwa inafanya namna hii, ndio unakuta kwamba mbele ya safari kunakuwepo na migongano na haiendi kuwalenga Watanzania kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia kuhusu wawekezaji ambao hawaisaidii nchi yetu. Sasa hivi tuna wawekezaji wanakuja kwa *gear* ya uwekezaji, lakini wanapofika katika kuwekeza wanakuwa Wamachinga, wanapata *documents* zote lakini wanapofika hapa wanakuwa Wamachinga. Mimi sipendi kusema kwamba, watu hawa hatuwataki; watu hawa tunawataka, wawekezaji wote tunawahitaji lakini waje

wawe *serious* na waje wawekeze kwenye maeneo ambayo Watanzania tunawahitaji. Dar es Salaam kuna Wamachinga wengi wa Kichina, nasikia wanauza mpaka karanga kule Buguruni, wengi wapo vichochoroni; hivi Wizara inalielewa hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *vision* ya China ni kukamata Afrika nzima na kuona kwamba, bidhaa zao walizokuwa wamezitengeneza wanauza Afrika, wanatumia mbinu mbalimbali. Mchina akija kuwekeza hapa, maana wale kwanza *population* yao ni 1.3, ukichukua *population* ya Tanzania kwa Wachina ni kama tone tu kwenye bahari. Viwanda vyao vinawatuma wawakilishi kuja huku Tanzania, kwa maana ya kuwekeza halafu wananunua mali zilizokuwa China wanaleta huku kwa bei nafuu na kuua viwanda vyetu. Uwekezaji wa aina hiyo unaisaidiaje Tanzania? Kuna makontena ya viatu na vitu ambavyo vinatoka China vinakuja kuua viwanda vyetu. Je, Serikali inalijua hili?

Naiomba Serikali iwe makini, hatusemi hatuwataki wawekezaji, hapana tunawataka wawekezaji Wachina, Wazungu, kila nchi, lakini waje kwenye maeneo ambayo sisi Watanzania tunawahitaji siyo wanakuja huku ku-*import* vitu ambavyo wanaleta kuharibu soko la Tanzania. Inafika mahali ambapo wanaanza kuweka vitu nchini, wanatembeza sijui *ice cream* njiani; hii ni hatari. Hii ajira Watanzania wa kiwango cha chini, wangeweza kuifanya kazi hiyo. Sasa wanakuja kukamata hata hizo ajira ambazo Watanzania wanazitamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie TIC. Wakati Waziri wa Fedha na Uchumi, alipotoa hoja yake ya bajeti hapa alisema, tunafuta *deemed capital goods,* kwa maana ya baadhi ya wawekezaji na Bunge likaridhia kuona kwamba, baadhi ya wawekezaji kweli tukiondoa misamaha hiyo itatusaidia, matokeo yake imekuwa tofauti sana. Naomba ninukuu kidogo ukurasa wa 52 wa Hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, aya ya 13 inasema: “Kufuta utaratibu wa sasa wa kutambua baadhi ya vifaa kama bidhaa za mitaji kwa baadhi ya wawekezaji.” Naomba kunukuu hapo; kwa nia ya kuvipa unafuu wa kodi, *deemed capital goods,* kwa mfano, wawekezaji katika Sekta ya Hoteli na Utalii, kutumia unafuu huu kuingiza vifaa kama mashuka, glasi, vijiko, visu, ambavyo hutambulika kama bidhaa za mitaji. Tulivyoelewa sisi ni kwamba, baadhi ya wawekezaji lakini utekelezaji wake sasa umekuwa kwa wawekezaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme madhara kama hii itaendelea hivi, maana kuondoa *deemed capital goods* inawaathiri Watanzania na siyo wageni. Kutoka mwaka 2005 mpaka 2008, waliohamasika kuwekeza nchini kwenye Sekta ya Utalii na Viwanda ni Watanzania. Ngoja niongee kwa takwimu. Mwaka 2005 katika Sekta ya Utalii, Watanzania walikuwa na miradi 86. Mwaka 2006, Watanzania walikuwa na miradi 124. Mwaka 2007, Watanzania walikuwa na miradi 135, mwaka 2008 walikuwa na miradi 167, Watanzania hao. Ukitazama wageni ni 33, sijui yaani walikuwa wachache kuliko Watanzania, ina maana Watanzania ndio walihamasika wenyewe kuwekeza Tanzania kukamata uchumi wao. Sasa kuondoa hii *deemed capital goods,* kutawaathiri kweli kweli hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika *manufacturing,* mwaka 2005 Watanzania walikuwa 60, mwaka 2006 walikuwa 66, mwaka 2007 walikuwa 76 na mwaka 2008 walikuwa 83. Wageni mwaka 2005 walikuwa 27 tu kwenye *manufacturing*

*sector*. Naomba Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko iliangalie hili. Mwaka 2006 walikuwa 62, 59 na 80. Kwa hiyo, ukitazama Watanzania ndio walihamasika zaidi kutoka mwaka 2005 mpaka 2008, kukamata uchumi wa nchi yao. Sasa wanapokuwa wako tayari na wanapokwenda kuwekeza, unakwenda kuwaondolea uwezesho huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtu aliweka bajeti ya shilingi 200,000,000, inabidi sasa asitishe huo mradi maana umemwongezea mzigo mkubwa wa kukamilisha huo mradi. Ile dhana ya kwamba sasa Watanzania tukamate uchumi wetu, tuweze kutekeleza uchumi wetu katika sekta zote za utalii na viwanda, sasa haiko tena. Tutakachoweza kumudu hapa, maana kuna watu wameanzisha miradi, wale watakaoweza kuikamilisha ni asilimia ndogo sana. Kuna wawekezaji ambao hawajaanza kutokana na kuondolewa *deemed capital goods*, wataacha kabisa na miradi. Madhara yake ni kwamba, TRA wameona hapa tutaongeza pato, lakini wamesahau kwamba wataweza kuongeza pato kwa muda huu tu kwa wale waliokuwa tayari kwenye uwekezaji, lakini huko mbele ya safari, uwekezaji kwa kiasi kikubwa utapungua sana na kuna hatari kama nchi inakamatwa na wageni asilimia kubwa ya viwanda vikiwa vya wageni ni sawa sawa na uchumi wenye nguvu ya mapovu tu. Kama ni Watanzania wote wanakamata angalau asilimia 70, kuwepo na *balance* baina ya Watanzania na *Foreign Investors* wanaokuja nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania sasa na TIC nimwombe Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko tangazeni kwamba, sasa hivi hakuna tena msamaha wa kodi TIC. Wawekezaji wanakwenda pale wanawasumbua Wakurugenzi wa TIC, hawajui wanachokifanya wala hawajui wawajibu nini wawekezaji. Semeni tu kwamba, tumefuta misamaha ya kodi kuanzia sasa mwenye kuweza aweze, ambaye hawezi aondoke. Nashauri kwamba, hii TIC sasa hivi nadhani iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa nini isihame Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko angalau mipango ya TIC na mipango ya EPZ ikaenda sambamba kwa maslahi ya Tanzania? Moja katika madhara makubwa sasa ambayo kama misamaha hii itaendelea ni kwamba, kutokana na misukosuko hii ya uchumi, nchi nyingi duniani waliweza kuwasaidia wananchi wao, waliweza kusaidia biashara zao au Mabenki yao ili yaweze ku-*survive* kutokana na matatizo haya. Sisi Tanzania badala ya kuwasaidia tumekwenda kuongeza mzigo; uliona wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii, nami niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Hoja hii ni muhimu sana ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote walioko kwenye Wizara hii, kwa kutuletea hotuba ambayo ni nzuri sana, nasi tumeipokea kwa furaha ingawa binafsi nilivyokuwa nikiisikiliza nilipata tabu sana na nimejiuliza maswali mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nilijaribu kurejea kwenye ile kaulimbiu iliyotolewa wiki chache zilizopita ya Kilimo Kwanza. Nilivyokuwa nikisikiliza bajeti hii nikagundua kwamba, hii kaulimbiu ya Kilimo Kwanza kwa upande wangu nimeona kama imewahi, yaani hakukuwa na mchakato wa kutosha kuhusiana na kaulimbiu hii.

Nilitegemea kauli ingekwenda sambamba kabisa na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. Kwenye hotuba yake ametueleza mikakati mbalimbali, lakini bado mimi binafsi sikuona kama kuna *connection* yoyote kati ya hotuba hii na kaulimbiu ile ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, mimi binafsi, nafikiri sote inabidi kwa dhati kabisa tufanye maamuzi ambayo ni magumu. Kwa kuangalia kaulimbiu ya Kilimo Kwanza, basi inabidi tuyatoe maamuzi haya na nilitegemea kwamba Wizara hii ingekuja na maamuzi magumu, lakini kwa faida ya nchi yetu na kwa faida ya Wananchi wetu wa Tanzania. Kwa hiyo, nilijaribu sana kuoanisha na nasikitika sana sijaona muunganiko huu. Wizara hii tunaitegemea sana kuinua kilimo chetu. Kilimo bila Wizara hii, hakiwezi kuwa Kilimo Kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mifano michache, kabla sijaja kuongea hapa, nilijaribu kufanya utafiti kwa siku chache na nikagundua kwamba, nchi yetu imekuwa kama dampo. Sasa huwa najiuliza; kuna bidhaa ambazo Wizara hii ingeweza kusimama kidete na kuzilinda kwa faida ya mkulima. Ukienda kwenye *supermarket*, kwa mfano, pale Shoprite na supermarket nyingine zilizoko nchini, utakuta mambo ya kusikitisha sana. Kuna kuku wako pale, lakini ukitafuta kuku kutoka Tanzania huwezi kuwapata. Kuku wale wanatoka South Africa, wanatoka Zimbabwe na kwingineko. Kuna mayai, kuna maziwa mengi tu yanayotoka nchi za wenzetu, hata bidhaa ndogo kama viberiti. Siku moja nilikuwa naangalia pale viberiti na nilitegemea vinatoka Kibo Match, hapana viberiti hivi vinatoka Singapore, Taiwan na Malaysia. Sasa inanipa tabu sana kufikiri. Najua Wizara hii ina wataalam wa kutosha, lakini ninachokiona hapa tunashindwa kufanya maamuzi ambayo ni magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Bangladesh na India, leo tunawazungumzia hapa ndani, wamefanya maamuzi magumu. Sasa hivi kwenye nchi yao, huwezi ku-*export* bidhaa za chakula na hata sukari, kwa kutumia magunia yoyote yale zaidi ya magunia ya *jute*. Sasa sisi hapa tuna viwanda vyetu vya magunia viwili; kuna kile cha Moshi ambacho kimefungwa kabisa na ajira za Watanzania wenzetu wapatao 500 imekufa kabisa. Kuna kiwanda cha magunia ambacho kiko Morogoro, nawapongeza sana Kambi ya Upinzani kwa kuliona hili, kwa kweli kwa sasa ufanyaji wake sasa ni asilimia 15 mpaka 20. Sasa kiwanda kile kinatakiwa kutengeneza magunia milioni 10, lakini utendaji wake umeshuka. Hii ni kwa sababu tuna-*export* bidhaa zetu za vyakula nje, lakini tunawafaidisha wenzetu waliokaa kwenye nchi zao wakapitisha sheria kwamba, sasa hakuna kutumia magunia mengine yoyote yale zaidi ya magunia yanayotoka kwenye chini yao na ni magunia ya *jute*. Sisi hapa bado tuna-*import* magunia hayo hayo ya *jute* kuja kutufungia bidhaa zetu nchini mwetu. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, afanye maamuzi ambayo ni magumu sana, lakini kwa ajili ya kulinda viwanda vyetu vya magunia vilivyoko nchini, kwa ajili ya kulinda ajira za Watanzania na kwa ajili ya kuongeza Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapouza magunia haya ndipo tunavyokuza kilimo cha mkonge. Tunaposema Kilimo Kwanza ni lazima tujali bidhaa zetu. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, afanye maamuzi magumu; aamue kuanzia leo kwenye *supermarket*

zote ni marufuku kuonekana kuku wanaotoka South Africa, kwa sababu tunao wafugaji wengi. Naambiwa hapa kuna kuku wa Singida; kwa nini wale wakulima tusiwape hii nafasi wakaenda kuuza kuku wetu kwenye zile supermarket? Sasa hivi hadi mchicha, pilipili hoho, matunda tunayosema yamerundikana kule Muheza na kwingine kama Morogoro, lakini matunda yaliyojaa kwenye *supermarkets* yanatoka nje ya nchi.

Kwa hiyo, mimi napata tabu kuelewa, tunapesema Kilimo Kwanza; je, tumeitayarisha Wizara hii ambayo ni muhimu kama *catalyst* ya hiki Kilimo Kwanza? Lazima tufikie haya maamuzi na ningependa kama itampendeza Mheshimiwa Waziri, wala usione choyo, wala usijisikie vibaya. Tunakuelewa wewe ni mama mahali na unaipenda nchi hii, tunaomba uchukue maamuzi. Tutakupenda zaidi, utakaposimama ukasema kuanzia leo hatutaki mchicha unaotoka South Africa, hatutaki juice zinazotoka South Africa na kwingine kokote. Tujaribu kuwa *selfish,* tuuze bidhaa zetu wenyewe na pale ndipo tutaweza kufikia kwenye dhana nzima ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitakuwa busara kukaa chini kabla sijaongelea masuala mazima ya *fake goods*. Sasa hivi nchi yetu ndiyo inaonekana ni sehemu ya ku-*dump* hizi *fake goods.* Tunawashukuru sana, waliojitahidi kuwakamata wale wanaoingiza *fake goods* kwenye nchi yetu. Kumekuwa na *fake goods* nyingi, mtu anaingiza TV zote ni *fake*, anaingiza vifaa vya umeme vyote *fake* na hii imepelekea matukio mengi sana ya moto, nyumba zinaungua kwa sababu ya hivi vifaa vya umeme ambavyo ni *fake*. Siku moja nilijaribu kukabiliana na yule jamaa wa TBS; yeye anasema nchi yetu ni kubwa sana, sasa sijui nchi hii tuikate kipande kingine tukihamishe tukipeleke sehemu nyingine? Mimi nadhani kunatakiwa kufanyike ufanisi. Mheshimiwa Waziri, leo anatuambia kwamba, ukaguzi utakuwa unafanyika nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tusilikubali hata kidogo, maana tumeona ukaguzi huu ukifanyika kwenye magari. Mtu ananunua gari Japan au Dubai ukaguzi unafanyika; na si ukaguzi wewe Mwenyekiti ni shahidi, unaulizwa tu gari linawaka? Halitoi moshi? AC inafanya kazi? Unabandikiwa *sticker.* Matokeo yake gari lile linakuwa *shipped* linaletwa hapa, lakini ni magari ambayo kwa kweli yapo chini ya kiwango. Sasa nataka niiulize Wizara; tumekuwa tukihamisha fedha zetu za ndani tukiwapelekea wenzetu kule Dubai na Japan, ambao wamekuwa wakitufanyia kazi hii ya ukaguzi. Napenda Waziri atakapofanya majumuisho, atuambie kama tumeingia ubia basi ni kiasi gani cha fedha tumepata kutokana na zoezi hilo na kama jibu halijulikani basi tusiingie kwenye huo mchakato unaotaka kufutwa wa kwamba bidhaa zote zikaguliwe nje ya nchi. Hii itakuwa haileti maana kwenye nchi yetu, kwa sababu ninaamini kabisa sisi pia tunao wataalam ambao wanaweza kufanya kazi hizi. Kwa hiyo, tusiruhusu wataalam wetu, wamesomeshwa na Serikali hii ni lazima waitumikie nchi hii katika kufanya kazi ambayo wameisomea. Hatuwezi kuendelea kuhamisha fedha za nchi kuwapelekea wenzetu, wakaendelea kuneemeka na sisi tukaendelea kuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaliomba Bunge hili tusikubaliane kabisa na hili suala la kwamba bidhaa zetu kabla hazijaingia nchini, zikaguliwe nje ya nchi. Tunaomba ukaguzi huo ufanyike pale bandarini, kwa kutumia kitengo chetu cha TBS na kama itagundulika bidhaa zile hazina ubora basi zitupwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja na nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Vilevile nawashukuru Wananchi wa Jimbo la Mpendae, kwa kunipa fursa leo hii kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Namshukuru Naibu Waziri, Katibu na Watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia biashara lazima tuzungumzie na fedha. Lazima sarafu yetu kuitukuza, jambo la kwanza. Kwa sababu nchi yoyote unayokwenda, huwezi ukatumia pesa ya kigeni, lazima utumie pesa ya nchi ile. Sasa kutengeneza biashara, lazima tuijali sarafu yetu tuipe thamani.

Mheshimiwa Mwanyekiti, tuna ndoa ya mkeka iliyofungwa na ndugu zetu wa TBS kule Japan, Dubai, Uingereza, Singapore na Hong Kong, kuhusu habari ya magari ambayo unapoyanunua TBS bila ya kuangalia magari yale ni kuwasha *indicator* ya kulia na kushoto tu gari hilo linapata kibali cha TBS. TBS hiyo inabidi uilipie kuanzia Dola 150 mpaka 200. Cha ajabu, kama hukulipia kule nchi za nje ukifika Tanzania faini ya laki nane kwa Dola uliyolipia 150. Kwa magari makubwa utalipishwa *fine* ya milioni mbili. Je, jamani hii ni haki? Tunamnyonya Mwananchi wa Tanzania, ambaye tunamtakia mema. Wakati huo huo gari tunaona ni *luxury*. Gari sio luxury sasa hivi, gari ni huduma ya lazima katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wenzetu hawa mikataba hii waliyoifunga na kule Japan wale waliofunga nao mkataba huu au hii ndoa ya mkeka, tegemeo lao nini na kiasi gani wanaziacha pesa zetu zinazoweza kusaidia nchi yetu? Kwa sababu tokea mwaka 2002 ndoa hii ifungwe, pesa zilizopelekwa kule jamani si tunapigwa bao la kisigino? Hii ni dhahiri kwamba, hela zetu zinakwenda nchi za nje haziwanufaishi Watanzania. Nitampendelea dada yangu Mheshimiwa Mary Nagu, sina matatizo na wewe wala Wizara yako. Nina matatizo na watu wako wa TBS, uje hapa na kauli thabiti na hatutaki fedha hizi zikusanywe nchi za nje. Tuna matatizo ya ujenzi wa barabara, mnatafuta bilioni 45 za Babati. Sasa TBS watupe hizi pesa ili tutengeneze Barabara ya Babati. Tangu mwaka 2002 fedha hizi ziko wapi? Nauliza na nipate jibu kamili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wafanyabishara ndogondogo. Utawala wa Dkt. Salmin, Zanzibar ilikuwa inafanya biashara kubwa sana na tegemeo lake ilikuwa Bandari. Wenzetu mkaona kwamba, sasa hivi ile biashara isifanyike na kumsaidia ndugu yako si kumpa mkate, kumsaidia mwenzako umsaidie kiuchumi ili asikuombe. Mkaanza sababu na wafanyabiashara wengi walikuwa wanateremsha mzigo Zanzibar. Soko lao liko Bara. Ikaja tena hapa baada ya kuteremsha Zanzibar ushuru anatozwa mwingi zaidi. Biashara hiyo mtu atafanya vipi? Wamehama wameelekea Bara na kule wamehama kwa sababu sasa hivi wamedhibitiwa. Mheshimiwa Salim alisema, suala la saruji kuna wafanyabiashara walikuwa wanateremsha saruji sasa hivi wamehamia Bara wana mipango yao wanapenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la wafanyabiashara ambao wanateremsha wanakwenda Zanzibar kufanya biashara wanatoka Tabora, Shinyanga, sehemu tofauti kwenda Zanzibar kufanya biashara. Matatizo wanayoyapata wanapotoka Zanzibar kuja zao bandarini ni kasheshe kubwa, iliyokuwa haina mfano maana wanaambiwa kwamba kule msiende. Manyanyaso wanaanza kuyapata kuanzia TRA na mpaka TPA, maana mzigo mtu amebeba mwenyewe anaambiwa alipe. Mfanyabiashara ndogondogo huyu, tegemeo lako afanye nini na hapa sisi tunasimama tuwasaidie wajasiriamali; tunawasaidia namna gani? Mpaka mfuko anakula mfanyabiashara yule. Tegemeo letu lipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri ninaoutoa ni wa bure, hautaki pesa. Naomba Wizara ya Biashara, Wizara ya Fedha na Wizara ya Miundombinu, mkae pamoja kwa sababu Miundombinu iko na Bandari. Ili mwondoshe matatizo yanayotukabili kwenye nchi yetu, kwa wafanyabiashara wadogo wadogo. La kama hamuwezi kukaa hivyo, tutarudi palepale kila siku kupiga kelele. Narudia tena, naomba Mheshimiwa Waziri wa Biashara, Katibu wako, tulimwita kwenye kikao cha PAC aeleze kuhusu utaratibu mzima, ulimshinda na mpaka leo hajaleta jibu kwenye Kamati ya PAC kuhusu habari ya magari ya Japan, Dubai, Uingereza, Hong Kong na Singapore. Kuna nini kwenye Wizara yako? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sitakuwa na mengi, naunga mkono hoja hii baada ya Mheshimiwa Nagu kutupa ufafanuzi kamili juu ya fedha zinazochangishwa nchi za nje kwa ajili ya kupatikana *sticker* tu za magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi*)

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii leo na namshukuru Mwenyezi Mungu, kuwepo hapa na Wapigakura wangu wa Mji Mkongwe. Kwanza, nataka nielezee nembo ya Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nembo ya Benki Kuu ya Tanzania inaonesha alama za majani ya mkonge yaani *sisal*. Historia yake tunaielewa ni nini? Kwa sababu Tanzania ilikuwa inapata zaidi ya bilioni 150/= kutokana na mauzo ya mkonge. Nini asili ya mkonge? Mkonge mbegu yake ilitoka Mexico katika mji mmoja unoitwa Yucatan, ndiyo maana ukawa umepata jina la katani na aliileta Mjerumani hapa. Ikawekwa Tanga, Same Kilimanjaro, Lindi, Mtwara na Morogoro. Wagiriki wakati ule Tanzania inatawaliwa na Muingereza na Cyprus ikitawaliwa na Muingereza, kukawa kuna ugomvi baina yao na kukawa kuna wakimbizi. Wakaondoka Ugiriki kutoka Cyprus, wakaingia Tanga kuendesha biashara ya *Sisal*. Wakavuna fedha nyingi sana mara baada ya Uhuru, Rais wa Cyprus, Askofu Makarios, alipoingia madarakani wakarejea makwao na fedha zao za kigeni. Mashamba yakabaki na Wahindi. Hawa Wagiriki walichotuachia zaidi pale hata kama watu wa Tanga mnakumbuka, kuna Galanos Secondary School, inatokana na jina la *Anautoglo* jina la Kigiriki, baadaye akaitoa kama *charity* kwa Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye Karimjee na Wahindi wenzake wakaendesha mashamba kwa muda ambao wameweza. Wakavuna walichokivuna, Wahindi

wakaondoka wakaelekea kwao India, Uingereza, Marekani wakayaacha mashamba yao Tanga. Mimi si Mhindi. Mimi ni Mwafrika tena Mmakunduchi safi hata kihindi sikijui. Nikizungumza kimakundushi, mtakwenda mbio sasa hivi hapa. (*Makofi*)

Baadaye wafanyakazi wa mashambani na viwandani wakakosa ajira. Baada kukosa ajira, Mwalimu Nyerere, akaunda chombo kinaitwa *Sisal Authority of Tanzania.* Akasema wagawiwe heka tano mpaka kumi ili waendeleze mashamba na viwanda, kwa sababu wamekosa ajira na anawatakia mema Watanzania. Zao la Mkonge linahitaji mvua kidogo tu milimita 10 -15 linastawi. Tanga, Morogoro, Lindi kule kwa jamaa yangu Mmachinga Mudhihir kwenye mashamba ya Mkoe, Kikwetu, Mtototo na Mtwara Tabisara, mashamba yote yamekufa hadi leo. Uzalishaji ulikuwa tani 200 kwa mwaka na ajira laki moja mashambani na 50 viwandani, wakati wa Mwalimu Nyerere na mkaona hata Tanzania tulivyochapisha pesa ya kwanza, shilingi mia nyuma ilikuwa na alama ya mkonge umeanikwa katika yale maeneo ambayo wanaanikia mkonge kwa heshima ya mkonge. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukawa tunatengeneza mazulia, tukatoa hata dawa inaitwa *hycogenin*, ambayo ilikuwa inatengenezwa *bath control pills* na tukawa tunapeleka Uingereza katika kiwanda kimoja kinaitwa *Wigos Worth*, ambao ndiyo walikuwa wana-*supply* hizi *material* na vitu vinavyotokana na mkonge kupeleka nchi nyingine za Ulaya. Ilifika wakati hata Rais wa Mexico wakati ule akiitwa Acheveria, aliwaleta watu kutoka Mexico kuja kujifunza Zao la Mkonge Tanzania. *This is just a history*, mambo bado. Baadae tumefanya nini? Viwanda vimekufa, uzalishaji hakuna, wakatokezea Watanzania wa ndani wakasema watavibeba kwa *capital* yao. Hicho ndicho kitu muhimu. Tuwajenge Watanzania wetu wenye *capital*, waweze kuendesha viwanda vya ndani na si kungoja watu kutoka nje waje na *capital* kutoka nje hapana. Sasa hivi tunazalisha tani 20,000, tumeajiri watu 10,000 mashambani na 500 viwandani. Ripoti ya TISCO inasema hivi; hali ya kisekta ya mkonge, *focus mandatory use of sisal bags* itaongezeka kutoka *bags*, yaani magunia milioni 1.5 mpaka milioni 5.5 na itakidhi haja katika mazao mbalimbali. *(Makofi)*

Mazao yetu ni kahawa, kakao, karafuu, korosho, mikunde, yaani maharage, mbaazi na kunde na dengu. Wakasema kahawa inaweza kutengeneza magunia 910,000, kakao magunia 25,000, karafuu 330,000, korosho milioni 1.25 na mikunde ikachukua 50,000 na mahindi ni 2.5. Yote kwa pamoja yanatoa magunia 5,515,000 kwa mwaka. Inaweza ikaongeza ajira viwandani kutoka watu 500 mpaka watu 1500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *International Coffee Association*, yaani Mamlaka ya Kimataifa ya Kahawa ikathibitisha kwamba, magunia yanayotengezwa kutokana na *sisal* ni bora kuliko *jute*. Kwa sababu kwanza, yanahifadhi ubora wa kahawa. Pili, yanapitisha hewa kwa wingi. Tatu, hayaweki harufu kwenye kahawa. Nne, hayanyonyi unyevu unyevu. *These bags* zinazotokana na *sisal* ni *ten times stronger* kuliko zinazotengenezwa za *jute* kutoka India na Bangladesh. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ghafla Wizara baada ya kutoa tamko kwamba, tutumie magunia ya ndani, ikafuta ikasema sasa ngoja tuwaagizie jute. Hatukatai, lakini kama

tunasema Kilimo Kwanza ina maana tulinde na viwanda vyetu vya ndani. Sasa kama hatukulinda tutafanya njia gani ya kuwasaidia wakulima kuweza kuinua haya mazao? Leo kama tutajitahidi zaidi kutengeneza hayo magunia yanayotokana na mkongo na faida zake nilizozitoa, tunaweza tuka-*extend market* yetu katika *East African Cooperation* tukawauzia Kenya, Uganda, Burundi na hata Rwanda na DRC. Sasa leo tunawaambia watu wa jute walete jute yao Tanzania, *sisal* tutamuuzia nani jamani?

Tunanyanyuaje kilimo cha *sisal*? Bangladesh kwa muda wa miaka 30 nyuma iliyopita, wametoa ruzuku ya dola bilioni 3 kwa wakulima wa *jute*. India na Bangladesh wameweza kuzuia soko la *jute* kwamba, watumie magunia yale kwa bidhaa zao zote kuanzia sukari na nafaka, wasitumie bidhaa nyingine yoyote kutoka nje ya nchi. Wanapata ruzuku na wameajiri kama watu 500 katika viwanda na mashamba ya *jute*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoa rai, tutoe azimio leo na si kwa jute peke yake, kwa mazao yote yanayotoka Tanzania, tuweze kuhifadhi mazao yetu na tuweze kuwapa nguvu wenzetu wanaofanya biashara ya viwanda ambavyo vinatengeneza bidhaa hapa. Tanzania ni wakati muafaka sasa kutoa hilo azimio ili tutakapotoa azimio hili, tujenge imani ya watu wetu wa Tanzania, ambao watataka kuwekeza katika viwanda. Iwapo tutaanza kuviua viwanda vilivyopo na wengine hawatakuwa na hamu ya kuweka viwanda katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema wenyewe kwamba, tukikiuka misingi ya maendeleo, basi misingi ya maendeleo itatukiuka sisi wenyewe. Tunafukuzia mambo ya madini, mambo ya ujenzi, haya ya muda tu gesi itakwisha, petroli itakwisha, dhahabu, almasi, Tanzinite tutabakiwa na mashimo, lakini kilimo cha *sisal* kitaendelea, kilimo cha mahindi kitaendelea kwa sababu ardhi bado tunayo, tukiiendeleza tukaitumia vizuri tunaweza kuvuna maisha, ni *sustainable* lakini hizi nyingine siyo *renewable*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusiwape nguvu hawa? Mimi nasema hizi amri za kusema kwamba magunia yaagiziwe kwanza, hawa wanaweza wakakiuka wakati mwingine tukaona bei ya jute ni ndogo, kwa sababu wengine siyo wafanyabiashara wazuri, wanakiuka taratibu za kulipa ushuru bandarini, wanapokiuka biashara zao zinakuwa za chini na *production* ya ndani inakuwa ya bei ya juu. Magunia ya ndani haya yanayotengenezwa kutokana na mkonge, tuliondoa VAT, kwa hivyo ni magunia rahisi na madhubuti. Kwa nini tuagizie magunia kutoka India? India hata siku moja hawataagizia magunia ya *sisal* kutoka Tanzania? Hawawezi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tupitishe azimio hapa, tuanze kujenga himaya ya kuvipenda viwanda vyetu. Tuna kiwanda cha nyama pale Sumbawanga, nyama safi kabisa na wamepata soko sasa hivi wanapeleka nyama DRC, wanapeleka Oman; kwa nini kiwanda hiki pamoja na kile cha Morogoro ambacho kinaitwa *Pride Best* tusivifanye vikauza nyama kwenye hoteli zetu na kwenye migodi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wamechukua mikopo katika mabenki yetu, wanahitajika kurejesha fedha, watarejesha lini tukiagizia nyama kutoka Brazil, kutoka Dubai, kutoka nchi za Ulaya? Ng'ombe wanaibwa Rorya wanapelekwa Kenya

wanachinjwa halafu tunakuja kuuziwa nyama sisi, tazameni maajabu hayo! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchinje ng'ombe wetu, nyama tule wenyewe kwanza, tuiuze ndani; kuna wanajeshi, kuna polisi, kuna hoteli za utalii, kuna wachimba migodi, tusafirishe nchi za nje ili tuinue kiwango cha viwanda katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri na Naibu wake nawapenda sana na wanajitahidi kwa sababu nawaona katika vyombo vya habari, kwenye televisheni, kwenye magazeti namna mnavyokaa na wawekezaji na wafanyabiashara, lakini nakwambieni leo hapa tukitoka Bungeni tutoke na tamko kwamba, kuanzia leo jute kutoka India na Bangladesh tarehe ya leo ndiyo mwisho wake. Kahawa yetu, muhogo wetu, sembe letu, nyama yetu, tunaitia katika gunia linalotokana na *sisal* tunasafirisha au tunahifadhi katika maghala yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Wizara hii na ni tabu sana kuongea baada ya Mheshimiwa Sanya, maana inabidi ufikie *standard* zake sasa ni kazi maana hata Uhindi ameukataa leo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo matatu na nusu; matatu ni ya kitaifa na moja ni la Jimbo. Mwaka 2007 nilikuwa na swali hapa Bungeni, kuhusiana na masoko maeneo ya mipakani na nilikuwa nina hoja kuhusu Soko la Kagunga, ambapo Wizara ikawa imeonesha utayari wa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Kagunga, mpakani na Burundi na kuweza kuchangamsha uchumi katika lile eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuifahamisha Wizara kwamba, tayari Halmashauri tumetekeleza wajibu wetu, tayari tumeshatenga fedha, tumejenga soko la shilingi milioni 300 pale Kagunga. Watu wa Mamlaka ya Bandari wametusaidia na ninapenda niwashukuru sana kwa mara nyingine, Waziri wa Miundombinu na Naibu wake na Viongozi wote wa Wizara ya Miundombinu kwamba, tunajenga sasa gati pale Kagunga kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, kunakuwa na biashara nzuri kati ya Kagunga na Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokiomba kwa sababu Burundi tayari imeingia kwenye *Customs Union* ya Afrika Mashariki, Wizara ishirikiane na sisi kuhakikisha kwamba, tunautangaza mpaka huu na moja ya njia ya kuutangaza ni ziara za viongozi. Viongozi wanapofika eneo linatangazwa, watu wanafahamu. Kwa hiyo, ama Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri, tungekwenda Kagunga, mkaweza kuona eneo lenyewe, likatangazwa watu wakajua kwamba hili ni eneo la kibiashara ili tuweze kuliendeleza eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nianzie pale ambapo Mheshimiwa Yahya Kassim Issa amezungumza, nadhani kama sijakosea, kuhusiana na TBS *Pre-shipment*. Watu wa TBS walikuja kwenye Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma, kuzungumzia hesabu zao na suala la gharama za *pre-shipment* za magari likazungumziwa sana na Kamati ikawa imeagiza kwamba, suala hili liangaliwe upya na ikibidi ukaguzi ufanyikie ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wakati wa Taarifa za Kamati za Bunge za Mahesabu, Kamati ya Bunge ya PAC ilileta hoja hapa Bungeni na Bunge zima likapitisha kwamba, suala la *Pre-shipment* ya magari na bidhaa nyingine zozote ambazo zitaingizwa kama jinsi TBS wanavyopendekeza, litaligharimu taifa pesa nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka 2002 mpaka mwaka 2007, kwa Japan peke yake jumla ya shilingi bilioni 48 (Dola za Marekani milioni 48), zimelipwa na waagizaji wa magari, maana yake ni kwamba, sisi kama nchi ambayo inahitaji *foreign exchange* kwa kiasi kikubwa sana, tunachukua pesa tunazipeleka kwa nchi ambazo tayari zina *foreign exchange* ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na hesabu ambazo tumezipiga zinaonesha kwamba, iwapo tutapanua zaidi bidhaa zote ambazo nchi inaagiza na kwa thamani ya mwaka 2008, taifa letu limeagiza bidhaa kutoka nje zenye thamani ya shilingi Trilioni Nne (TSh. 4,000,000,000,000), ndiyo *imports* zetu. Iwapo ukichukua asilimia moja ya hizi *imports* ndiyo ikawa gharama za *pre-shipments cost,* maana yake ni kwamba, Taifa lita-*export* Dola za Marekani milioni 48, ambayo ni takriban shilingi bilioni 62. Hali hii haikubaliki hata kidogo, kwa Taifa kama letu linalohitaji fedha za kigeni kuzitoa kuzipeleka nje. Kwa hiyo, ningependa kuungana mkono na Wabunge wote ambao wanapingana na hali hii. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili liko kwenye ukurasa wa 93 wa Hotuba ya Waziri, tunaomba alifute wala lisionekane kama lipo na kama kunahitajika *pre-shipment* zifanyikie hapa hapa Tanzania ili Makampuni ya Tanzania yapate fedha hizo na yawekeze ndani badala ya kupeleka fedha hizo nje. *(*Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili maana lile la Kagunga lilikuwa ni nusu. Suala la pili ni ubinafsishaji, katika ukurasa wa 15, kifungu cha 24 cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuendeleza ubinafsishaji wa mashirika ambayo yamebakia. Napenda kukutaarifu na kulikumbusha Bunge kwamba, tarehe 26 Aprili, kupitia Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, ambayo inashughulikia ubinafsishaji, Bunge lilipokea ushauri wa Kamati wa kusimamisha zoezi la ubinafsishaji mpaka tathmini ifanyike, kuangalia maeneo ambayo tulifanya vizuri na maeneo ambayo tulifanya vibaya ili tuweze kuona tunaendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sehemu hii ya hotuba nasikitika kusema kwamba, inapingana na maamuzi ya Bunge yaliyofanyika tarehe 29 Aprili, kuhusiana na suala la ubinafsishaji. Kwa hiyo, nilikuwa naomba suala hilo pia Mheshimiwa Waziri aliangalie na kulirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianzie alipoishia Mheshimiwa Sanya, sasa sijui kama nitafikia *standard* zake kama nilivyosema. Zao la Katani limepata matatizo makubwa sana katika Soko la Dunia. Mwaka 2007, katani ambayo Tanzania iliuza nje ni ya thamani ya Dola za Marekani 4.8 milioni tu. Mheshimiwa Sanya ametuambia hapa, miaka ya 1960 wakati sisi ndiyo nchi ya kwanza kwa uuzaji wa katani nje, tulikuwa tunapata Dola za Marekani zaidi ya milioni 100 kutokana na Katani, lakini imeshuka sana; mwaka 2007 tumeuza tani 9,700 tu za Katani nje na tukapata Dola za Marekani 8.8 milioni. Mwaka 2008 katani ambayo tumeuza nje ni ya thamani ya Dola 3.3 milioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeshuka kwa zaidi ya asilimia 62% na sababu kubwa ni moja wala si sababu ya bei, kwa sababu bei imepanda kutoka tani moja takriban wastani wa Dola za Marekani 900 mpaka zaidi ya dola 1000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la katani ni soko, katani yetu tulikuwa tunaiuza kwenye makampuni yenye tenda kwenye makampuni ya magari na ni makampuni mawili tu ambayo tulikuwa tunauza katani yetu nje. Baada ya msukosuko wa fedha duniani, makampuni ya magari yakapunguza uzalishaji, kwa hiyo, yalipopunguza uzalishaji maana yake ni kwamba, wale ambao wana-*supply* viti, *cushion* na kadhalika, vinavyotokana na katani, wakasimamisha kununua katani ya Tanzania, hawakununua kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhisho la katani ya Tanzania ni kuzalisha ndani, soko lipatikane ndani. Soko likipatikana ndani, siyo tu viwanda vyote vitafanya kazi, lakini pia wawekezaji wengine watafungua viwanda, kwa sababu wasiwasi wa baadhi ya watu ni kwamba, viwanda vya katani viko viwili tu, vina *capacity* na nililiongea suala hili na Mheshimiwa Gavana wa Benki Kuu, aliniuliza wakati wa mchakato wa ile *Task Force* kuhusu mgororo wa kiuchumi akasema viwanda hivi vina *capacity*? Nikamwambia hata kama havina *capacity*, wakati mwingine *demand* inakuwa *created*, baada ya kufanya maamuzi muhimu kama nchi na tayari Wabunge wengi sana, wameeleza maamuzi ambayo nchi ya India ilifanya kwa kuhakikisha *compulsory use* ya *jute bags* kwenye mazao yao yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wamezungumza, Msemaji wa Kambi ya Upinzani amezungumza, Mwenyekiti wa Kamati amezungumza jinsi ambavyo Bangladesh wanavyo-*subsidise* jute yao. Nadhani nilifahimishe Bunge lako Tukufu kwamba, katika kila jute ambayo tunanunua kutoka India au Bangladesh, tunatengeneza ajira 500,000 India na Bangladesh. Kwa hiyo, Mtanzania yeyote anapotumia magunia ya jute maana yake ni kwamba, badala ya kutengeneza ajira hapa Tanzania, anatengeneza ajira nje. Kwa hiyo, jambo la msingi la kuangalia ni kuhakikisha kwamba, tunakuwa na Sheria Maalum na kwa sasa kwa kuanzia ili uwe ni uamuzi wa Kibunge na Waziri apate nguvu ya kuweza kuamua ni kama Azimio la Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuamue kwamba, Serikali iweke utaratibu wa matumizi ya lazima ya magunia ya katani kwa bidhaa zetu. Sasa kwa vyovyote vile, panapokuwa na *monopoly* ni lazima kuweka taratibu za kuhakikisha kwamba, ile

*monopoly* haiathiri wananchi kwa sababu kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja alimuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu, kuhusiana na bei na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ndipo Serikali inapoingilia kati kwamba, *intervention* ya Serikali kuhakikisha kwamba, bei zinakuwa haziwaathiri wakulima zaidi ndiyo kazi ya Serikali! Huwezi kusema kwamba, hatuwezi kulazimisha matumizi ya katani kwa sababu bei zitakuwa kubwa, hapana! Kazi ya Serikali ambayo inaendeshwa kwa kodi za wananchi, inapaswa kuhakikisha kwamba, bei za mazao zinaendana na bei halisi za uzalishaji na mimi naamini kabisa kwamba, tukifikia uamuzi huo, tutaongeza uwekezaji mkubwa sana kwenye mashamba, lakini zaidi tutaongeza uwekezaji mkubwa sana kwenye viwanda ili kuongeza ukuaji wa uchumi kutokana na Sekta ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hapa kwamba, Kiwanda cha Moshi kimefungwa, kiwanda kile kina uwezo wa kuzalisha mpaka mazuria, lakini kimefungwa kwa sababu hakuna soko! Kuna Watanzania 500 wa Manispaa ya Moshi, hawana ajira kwa sababu kiwanda cha kuzalisha magunia ya katani kimefungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapoamua leo tunaamua hatima ya Watanzania ambao wanakosa ajira na kwenye uchumi kuna kitu kinachoitwa *backward and forward linkages* ni lazima Sekta za Uchumi za ndani zibebane zenyewe. Unapo-*externalise* matumizi kwa mfano ya jute, maana yake ni kwamba, unaua mahusiano kati ya Sekta kwa mfano, Sekta ya Kilimo na Sekta ya Viwanda na hicho ndicho kitu tunachokizunguza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba, ninaunga mkono hoja ambayo Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara ameitoa, Msemaji wa Upinzani ameitoa na Wabunge wengi humu ndani wamechangia kwamba, tutoke na Azimio la Bunge la Matumizi ya Lazima ya Magunia ya Katani kwa mazao ya Tanzania ili kuhakikisha kwamba, tunalinda katani, tunaongeza uzalishaji, tunapanua ajira na tunakuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DKT. GUIDO G. SIGONDA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara ina mpango wowote wa kufufua viwanda vilivyokuwepo miaka ya nyuma kama vile Kiwanda cha Magunia; Kiwanda cha General Tyre; Kiwanda cha Ngozi; Kiwanda cha Kuunganisha Magari na kadhalika ?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo baadhi ya watumishi waliokuwa wakifanya kazi kwenye Kiwanda cha General Tyre, waliachishwa kazi mwaka 2007, lakini hawakupewa mafao yao hadi sasa. Jitihada za baadhi ya watu hao kupitia Wizarani zimeshindikana. Mmoja wa wadai hao ni Mama Agness Ngahyoma wa Arusha, aliahidiwa na

Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami (Mb), kumsaidia apate mafao yake. Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, wanaendesha Operesheni ya Uvuvi Haramu unaotumia nyavu ndogo. Je, kwa nini Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko inaruhusu kuingizwa nyavu hizo haramu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilayani Chunya, wananchi wameendelea kulima Zao la Ufuta na Alizeti kwa wingi sana, tatizo ni ukosefu wa soko. Je, Wizara itawasaidiaje Wakulima wa Zao la Ufuta na Alizeti kwa kuwatafutia soko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma kulikuwa na biashara kubwa ya ngozi na mamba. Je, biashara hiyo kwa nini isiendelezwe rasmi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naipongeza Wizara hii kupitia Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa hotuba yao nzuri, yenye mwelekeo na yenye kujaa takwimu zenye malinganisho ya tulikotoka, tulipo na tunakoelekea; hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya saruji, (rejea Uk.40), TANCEM ya Shinyanga; Kampuni niliyoitaja hapo juu ina nia ya kuwekeza wapi Shinyanga? Naomba jibu tafadhali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Ngozi na Vioo: Moja ya Viwanda vya Ngozi vilivyojengwa hapa nchini ni pamoja na Kiwanda cha Ngozi kilichojengwa Mwanza, Wilaya ya Ilemela. Hivi sasa Kiwanda hicho hakifanyi kazi na vifaa vya ndani vinaibiwa tu. Je, Serikali inasema nini kuhusu Kiwanda hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mwanza ulibahatika kujengewa Kiwanda cha Kutengeneza Vioo (Nyanza Glass), Wilaya ya Nyamagana, Butimba. Kiwanda hicho kimetelekezwa hakifanyi kazi kabisa. Je, Serikali inasema nini juu ya hili? Tubadili matumizi ya viwanda hivi walau vitengeneze juice na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SIGFRID S. NG'ITU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kukumbushia tu jinsi Hanang inavyofanana na Ruangwa ila sisi hatuna ng'ombe; mbuzi wengi kama vile ninyi msivyokuwa na ardhi nyingi kama tuliyonayo sisi kule Mnacho, Mandawa na Ruangwa penyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atamke ni lini atawaleta wazee wa kule Hanang ili wakutane na wazee wenzao wa Rwangwa ili ku-*promote Internal Investment?* Sisi tunahitaji walichonacho ili nasi tuwape tulichonacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia, tunazo hekta 500 kule Naring'ombe kwa ajili ya kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali karibu, natoa tamko kwa kuwa wazee wanawasubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sisi ni wapole sana kama mlivyo ninyi.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imebahatika kuwa na ardhi nzuri na wananchi wenye bidii ya kufanya kazi katika sekta mbalimbali zikiwemo pamba, kahawa, katani na kadhalika. Aidha, Serikali iweke mfumo endelevu wa kueneza uchumi, kwa mfano, kaulimbiu ya Kilimo Kwanza inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wengi wameendelea kupata bei duni ya mazao yao, kwa vile hatuna mbinu mbadala ya kuongeza thamani ya mazao yetu ili kuboresha bei yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mkulima wa pamba, anauza pamba ghafi isiyoongezwa thamani ambapo anapata bei duni. Je, ni lini mkulima huyu tutamsaidia kuondoa umaskini na kuongeza kipato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa makusudi, Serikali imeendelea kuwabeba waagizaji wa bidhaa mbadala na pasipo kulinda viumbe vyetu vya ndani na wananchi wetu. Kuna ajira zaidi ya 20,000 kwa Wakulima wa Sekta ya Kilimo cha Mkonge, wakati viwanda pekee vinatoa ajira zaidi ya watu 5000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya hatuyaoni kuwa wananchi na uchumi wetu tunapaswa kuulinda sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, amevaa kitenge cha Tanzania. Hii ni fahari kwa bidhaa zetu. Iweje sasa tushindwe kulinda bidhaa zetu na viwanda vyetu kwa bidhaa ambazo zinachochea kukua kwa uchumi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nimeguswa sana na Sekta ya Mkonge, kwa maana ya kilimo chake na mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia uchungu kuona Mashamba ya Katani Morogoro na Tanga, yamezidi kudorora, huku viwanda vyake vikiwa hai. Kibaya zaidi familia za wananchi waliokuwa wafanyakazi mashambani na viwandani zinazidi kuwa maskini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako lipitishe azimio la kuweka matumizi ya lazima ya bidhaa zitokanazo na mazao yetu, kwa mfano, magunia na pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na ushauri wa Kamati ya Bunge na ule wa Kambi ya Upinzani, kuhusu kupitisha azimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Hii itakuwa hatua muafaka kwa maslahi ya Taifa letu.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isitegemee maajabu kutoka Wizara hii hususan NDC kama itaongeza mtaji wa kufanyia kazi. Kazi ya kuendelea na utafiti wa kijiolojia, kuwekeza kwa ubia katika Miradi ya Liganga na Mchuchuma, pamoja na miundombinu, zinahitaji fedha nyingi. NDC wapewe mtaji wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupatikana mwekezaji wa Mradi wa Kasi Mpya *(Sponge Iron).* Mazungumzo ya ubia kati ya NDC na mwekezaji yatakamilika lini na mwekezaji ataanza kazi lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi wa Miradi Funganishi utategemea miundombinu hasa kwa Mradi wa Kasi Mpya – Barabara ya Itoni – Mkiu – Mundindi na ile ya Mchuchuma. Katika bajeti ya mwaka huu, Wizara ya Miundombinu inasema itaanza kutafuta pesa. Serikali ione umuhimu wa barabara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha mazingira ya Miradi hii, Wizara iseme itachangia vipi katika kuandaa *Land Use Plan* ya Wilaya ya Ludewa ili kwenda sambamba na uwekezaji huu hasa baada ya Wizara ya Kilimo kuonesha utayari wa kushughulikia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iseme utaratibu utakaowaandaa Wana-Ludewa kuhusiana na uwekezaji huu hususan viwanda vidogo, kilimo, ufugaji na huduma za jamii.

Mhesimiwa Mwenyekiti, Soko la Kimataifa la Mlangali lilianza kujengwa 2006 na hadi leo halijakamilika. Wizara ichunguze kulikoni. Wananchi wanataka kuanza kutumia soko hilo msimu huu wa mauzo ya mazao. Waziri ahakikishe hilo linatokea.

**MHE AME PANDU AME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, pamoja na Naibu wake na Wataalamu wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Kilimo; nchi yetu imetoa *Slogan* isemayo Kilimo Kwanza. Dhana hii haitakuwa yenye maana kama mambo haya mawili hayatakwenda sambamba na kilimo na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu haitakuwa ya kimaendeleo kama haitakuwa na viwanda endelevu pamoja na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vyetu hapa nchini vimekufa na vilivyobinafsishwa haviendi vizuri, yaani vinasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inahitaji iwe na viwanda vingi tena viwe vyenye kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunazo malighafi nyingi sana, ambazo zitatosheleza kabisa kuendeshea viwanda vya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wa viwanda hapa nchini, wawe wawekezaji wa kweli na siyo wababaishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda viwili ni mfano mzuri hapa Tanzania navyo ni A to Z na TPC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, A to Z ni kiwanda kinachotoa ajira kwa vijana wetu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TPC ni kiwanda ambacho ni mfano mzuri, kwani kinatoa ajira, elimu ya shule, huduma ya afya, michezo ya kila namna kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kuona Kiwanda cha General Tyre kimekufa. Kufa kwa kiwanda kama kile hapa nchini ni aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko; je, kiwanda kile ndio kimekufa kabisa na hakitafufuliwa tena? Kama hakitafufuliwa, Serikali haioni kuwa hakikufa kiwanda tu bali pia teknolojia ya wale watu waliokuwa wakifanya kazi pale na kama kitafufuliwa ni lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tuamue tunaweza; tuimarishe kilimo sambamba na viwanda ndiyo tutaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Awali ya yote, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa kuwasilisha hotuba yake nzuri. Pamoja naye, nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa mchango wao mkubwa kwa maendeleo ya nchi yetu, kupitia shughuli wanazozifanya katika Wizara. Vile vile napenda kuipongeza Serikali, kwa uamuzi wake wa kuwakomboa Wakulima wa Pamba, kwa kuwawezesha kuuza pamba yao iliyokuwa imekwama kutokana na mtikisiko wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuzungumzia hali ya viwanda vyetu nchini. Kwa ujumla, baadhi ya viwanda hapa nchini hasa vya chakula, vinywaji aina ya juice na vya maziwa, vinakabiliwa na tatizo la uzalishaji ulio chini ya uwezo. Tatizo hili linatokana na mambo yafuatayo:-

(a) Gharama kubwa za uzalishaji kutokana na bei kubwa ya umeme.

(b) Miundombinu mibovu inavyoongeza gharama za kusafirisha malighafi kwenda viwandani na kusafirisha bidhaa kwenda kwenye masoko.

(c) Kodi kubwa inayotozwa kwenye vifungashio. Pamoja na mambo mengine yaliyotajwa hapo juu, yanachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza gharama za uzalishaji, ambazo pia hupelekea ongezeko la gharama/bei za bidhaa kwa mtumiaji wa mwisho. Tatizo hili hupelekea bidhaa za nje, ambazo huzalishwa nje na kuingizwa hapa nchini kwa gharama ndogo zaidi, kununuliwa kwa wingi zaidi na Watanzania kuliko bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni viwanda vyetu vya maziwa. Kipo kiwanda ambacho kimepewa udhamini na Serikali ili kiweze kuzalisha kiasi cha lita 120,000 za maziwa kwa siku, lakini kiwanda hicho kinazalisha lita 6,000 tu kwa siku. Kwa ujumla, viwanda vyetu vyote 13 vya maziwa vinazalisha lita 60,000 tu kwa siku, kutokana na soko la ndani kutawaliwa zaidi na bidhaa zitokazo nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza sana kuona kuwa, maziwa ya Tanzania yenye ubora wa uhakika, yanakosa soko la ndani na nje, maziwa kutoka Kenya lita zaidi ya 800,000 huingizwa nchini kila mwezi. Hata hivyo, bado yapo maziwa kutoka nchi nyingine mbalimbali yakiwemo maziwa ya unga kutoka Uholanzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mapendekezo yafuatayo:-

(a) Serikali iongeze ushuru kwa bidhaa zitokazo nje ambazo pia zinazalishwa nchini.

(b) Kuondoa au kupunguza kodi kwenye vifungashio vya maziwa na juice zinazotokana na matunda ya nchini.

(c) Kutotoza VAT kwenye bidhaa zetu za chakula, maziwa na juice zinazotokana na matunda ya nchini.

(d) TBS ifuatilie kwa umakini ubora wa bidhaa zinazotoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, tutaongeza uzalishaji katika viwanda vyetu ambavyo vitaongeza ajira na hatimaye kuongeza Pato la Taifa kutokana na kodi ya mapato kutokana na mauzo ya bidhaa na mishahara ya wafanyakazi viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na viwanda vidogo vidogo, SIDO ni kiungo kizuri kati ya wananchi wajasiriamali wadogo na viwanda hivi. SIDO ikitumiwa vizuri, inaweza kuwa chachu kubwa kwa zana yetu ya Kilimo Kwanza. SIDO ni chombo muhimu katika kupunguza umaskini katika nchi yetu, lakini kuna matatizo kwamba, haina fungu la kutosha kufanya kazi zake muhimu za kumkomboa Mtanzania kutokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali, iwapatie SIDO fungu la kutosha hasa kwa upande wa kutoa elimu ya ujasiriamali kwa Watanzania wasio na uwezo wa kulipa hasa wanawake. Pia SIDO wanapoagiza vifungashio kutoka nje kwa ajili ya wajasiriamali wadogo, wapewe msamaha wa kodi ya uagizaji bidhaa ili vifungashio hivyo viuzwe kwa bei nafuu, ambayo itawapunguzia wajasiriamali gharama za uzalishaji wa bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naishauri Serikali ichangamkie biashara ya chuma, nguo na vifaa vya umeme; vitu ambavyo vimeisaidia China kujikwamua kiuchumi kwa kiasi kikubwa. Chuma tunayo nchini, pamba tunayo nchini, hata wataalam waliosomea masuala ya umeme tunao. Tuwawezeshe wataalam wetu kupata vifaa na kuwapa mitaji ya kuanzisha viwanda vidogo vya kutengeneza vifaa vya umeme ili kuzuia uagizaji wa vifaa visivyo na ubora kutoka nje.

Wapo Watanzania wengi, wenye uwezo wa kuigiza bidhaa ni vyema Serikali ikawatambua hawa, itafiti mahitaji yao na baadaye iwawezeshe kutengeneza vifaa hivyo kwa kuwapatia mahitaji, kwani hivyo ndivyo nchi zilizoendelea zinavyofanya hadi kupata maendeleo waliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba niipongeze SIDO kwa kazi nzuri sana ambazo wanafanya katika jamii yetu ya Tanzania. Imekuwa mstari wa mbele kuwawezesha wajasiriamali wa Tanzania, pamoja na mafunzo mbalimbali na kuwapa mikopo midogo midogo kila wakati. Hii ni kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba wajasiriamali wote wapate mafunzo ya teknolojia ya kisasa ili wawe bora na shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze BET kwa kazi nzuri ya Saba Saba mwaka huu wa 2009, mambo yote yalikuwa mazuri sana, utaratibu mzuri sana. Naomba niwapongeze vile vile kwa kutoa fursa kwa wajasiriamali wengi.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba yake nzuri. Bila kusahau kuwapongeza wote waliomsaidia, akiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara. Kutokana na hali yangu ya afya, leo nilipenda sana

kuchangia kwa kuongea lakini nimeshindwa. Hivyo basi, naomba mpokee mchango wangu huu muhimu kwa maandishi. Tafadhali sana tena sana, naomba nipate majibu machache ambayo ningependa niyapate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba kukupa historia fupi ya Mafia na Gotland (Sweden), kulikuwa na urafiki wa visiwa viwili kwa wajasiriamali wadogo, walikuwepo mafundi seremala, mafundi wa kutengeneza boti, mafundi wa magari, viwanda vya samaki na uvuvi, mwisho hata akina mama wachokoa pweza na kuchoma samaki *(smoked fish).* Tulitegemea kupitia SIDO, mahusiano haya yaendelee kuwepo na kuendelezwa. Pia tulikuwa njiani kuanzisha hata kutengeneza vitu vya bati (sufuria, ndoo, vibatari, sinia na kadhalika). Sasa kupitia SIDO, nashukuru Ndugu Laizer ana ufahamu sana uhusiano huu wa Gotland, walikuja Mafia na wa Mafia walikwenda Gotland. Sasa ningeomba sana tena sana, hebu tuone ni kitu gani kilitokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na isiishie hapo, tuone jinsi gani tutaweza kufufua uhusiano huu kwa faida ya nchi yetu na hususan Vijana na Wanawake wa Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafurahi sana tena sana, kupata jibu la hili. Pili, sisi tuna kiwanda cha ku-*process* samaki, kamba, pweza na ngisi. Nilifuatilia suala la mabaki yanayotoka kwenye kiwanda, huwa yanafukiwa. Je, hivi kupitia SIDO hakuna njia inayoweza kuwasaidia wanawake au Vijana wa Mafia kupata njia ya kukausha mabaki haya na kuyasaga ili ikawa malighafi ya chakula cha kuku? Nina maana kiwanda kidogo chenye uwezo wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tulikuwa na mradi huko nyuma wa kutengeneza vifaa vya mnazi (kamba, nyuzi za makumbi kwa ajili ya mafagio na hata *door mats).* MAFIDECO imekufa, lakini bado vijana wapo na malighafi ipo. Vipi SIDO isije kutusaidia kuona viwanda vyetu vya vifaa vya mnazi vinakuwepo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua SIDO iko Mkoani, lakini Wilayani haipo. Pia hawa wataalamu, hebu waje Mafia wakutane na Wana-Mafia hasa akina mama na vijana kuhusu viwanda hivi. Mimi nitakuwa tayari kushirikiana nao kuona haya yanafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakukaribisha Mheshimiwa Waziri uje Mafia, uone tulivyo na mahitaji yetu ya kutaka kupata viwanda vidogo vidogo. Tuna malighafi nyingi. Tuna nazi ambazo leo wenzetu wanakausha na kuuza nazi iliyokunwa, tui la nazi kavu, maji ya madafu ambayo ni salama kuliko maji yote, pia mchanganyiko wa konyagi na maji haya ni mzuri sana kwa kunywa. Mazao ya Baharini ni mengi mno. Mkaa wa vifuu vya nazi na mapambo mbalimbali, hereni, bangili na vibanio vya nywele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vitu vingi, sisi tuko visiwani si rahisi kutuona, wenzenu tupo na tuna vitu vingi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawatakia kila la heri kwenye kutekeleza majukumu yenu.

**MHE. MGENI JADI KADIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijaalia kuwa na afya njema na kuniwezesha kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Timu yote ya Wizara na wale wote walioshiriki katika kuichambua Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda ni jambo muhimu sana katika kuleta maendeleo katika maisha ya binadamu na kukuza uchumi wa nchi yetu, kwa biashara na matumizi ya ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kuleta mapinduzi au mageuzi ya uhakika ya viwanda ni lazima mageuzi haya yaendane na Mapinduzi ya Kilimo Kwanza. Serikali kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji na kutoa kipaumbele kwa viwanda vya nguo, viwanda vya usindikaji wa vyakula, nyama, viwanda vya matunda, viwanda vya magunia na vile vile kufufua vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usindikaji wa vyakula na matunda, itakuwa ni chachu ya kuleta maendeleo kwa wananchi wengi kupata ajira na vile vile kuokoa matunda yetu kupotea bure na kupoteza pato la nchi yetu na baadaye kutumia bidhaa kutoka nje. Kwa mfano, Serikali inaona kuwa hapa nchini tunakula nyama za makopo kutoka nje ya nchi, wakati tuna mifugo mingi katika nchi hii; hilo ni jambo la aibu, na pia tunaagiza juice za makopo kutoka nje ya nchi. Je, Serikali haioni aibu wakati matunda yapo mengi yanaoza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Serikali haioni kuwa tunaagiza magunia kutoka nje ya nchi wakati sisi magunia yetu yanakosa soko? Naiomba Serikali kupitia Wizara hii, ivifufue viwanda vyetu na iviimarishe na kuagizia malighafi ya kutosha ili vizalishe kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na pia nawaombea Waziri na Naibu Waziri, Mungu awape afya njema na waweze kuwatumikia Watanzania.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu ina mazao mengi ya matunda kama vile machungwa, mananasi, maembe, mabungo na mapasheni; naomba Wizara hii iagize mitambo midogo midogo ya kukamulia matunda na iwakopeshe wananchi waweze kuzalisha *concentrates juice* nzito ili viwanda vikubwa vitengeneze juice na mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha General Tyre cha Arusha, lazima sasa kiokolewe na Serikali; hali ni mbaya na mkono wa Dola unahitajika haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika wa kuuza nje nyuzi za pamba, badala ya kuuza pamba ghafi ambapo wakulima wanakula hasara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. Ahsante sana.

**MHE. MARTHA M. MLATA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi. Naipongeza Wizara kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa hotuba nzuri na kazi wanazozifanya. Mimi naomba nitoe mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Utendaji wa Kitengo cha COSOTA bado nina mashaka nao, kwani sielewi hasa madhumuni yake ni nini? Naomba kuelimishwa. Nasema hivyo kutokana na kwamba, inaendeshwa ki-NGO, NGO hivi na pia ipo katika biashara zaidi ya kukusanya tu fedha tena zinazotokana na mirabaha kwenye Hoteli, Redio, TV na kadhalika kuliko kuendeleza na kulinda haki za wahusika. Jambo la kushangaza zaidi ni kwamba, hata Board haina! Sielewi jamani, naomba majibu inakuwaje tunapitisha fedha zao hapa na hali ya kuwa Board hakuna na hata kama ipo ni zaidi ya miaka miwili sasa haijakutana? Kwa mujibu wa Sheria ya Haki Miliki, kipengele cha 50(1)(b), bajeti yao imeletwa hapa Bungeni kwa *Authority* ipi nje ya Board? Kipengele cha 50(2) kinahusu *Audited Report* kuwa *Approved* na *Board.* Tafadhali, naomba hili mniweke sawa nilielewe. Vinginevyo, naomba Bajeti ya COSOTA itolewe mpaka hayo yote yatakapotekekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, COSOTA imekuwa ikikusanya fedha za mirabaha kuanzia Juni kutoka Maonesho ya Umma, yaani kutoka kwa wamiliki wa baa, hoteli, kambi za disko, maduka, Juke Boxes na kadhalika na pia kutoka mashirika ya utangazaji. Fedha hizo zimekuwa zikigawiwa kwa wasanii, lakini ni nani ana uhakika wa kuwa ndizo fedha sahihi zilizokusanywa na ni mgao halali bila Board kuidhinisha au kusimamia hayo? Tafadhali sana, tusije laumiana, kwani ni fedha za watu jamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, COSOTA imekuwa ikiajiri wafanyakazi wapya; je, hizo nazo nani ameidhinisha? Naomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Schedule 8(4), under Section 51* inasema wazi kuwa, Afisa Mtendaji Mkuu wa COSOTA anakuwa *Responsible* kwa Board. Je, kama Board haipo au haijakutana kwa muda wote huo tangu 2007 na chombo hakina usimamizi; mambo yakienda kombo ni nani wa kuwajibishwa? Nani wa kuulizwa? Nani wa kulaumiwa? Naomba jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi dhidi ya ukiukwaji wa hakimiliki:-

(a) Jumla ya kesi za uharamia 21 zilizofunguliwa dhidi ya wanaozalisha na kusambaza kazi za bandia, kati ya hizo zilizokwisha hukumu yake ilikuwa kama ifuatavyo: aliyekutwa na kanda 500 hadi 150, faini yake ilikuwa haizidi Sh.40,000. Aliyekamatwa na kanda zilizojaa magari matatu tani tatu alilipa faini ya Sh.200,000 na kuachiwa mzigo kuondoka nao. Jamani inatia uchungu. Naomba Wizara inipe maelezo kama hili inaliona na inasema nini juu ya sheria hii na dhuluma hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupatiwa maelezo inakuwaje Redio ya Taifa, Television ya Taifa kutokuwa na mfano kulipa mrabaha? Kuna redio ambazo ni ndogo

sana zinalipa, lakini vituo vikubwa vya utangazaji havina mpango kabisa; hivi kama ni uharamia ni nani anaongoza kama sio Serikali? Naomba Wizara itoe msimamo kwa kushirikiana na TCRA ili kuweza kutoa msimamo kwa vyombo vyote vya utangazji kuwa na *Log Sheet*, itakayosaidia kulipa mrabaha kutokana na matumizi ya kazi za sanaa wanazotumia, kwani kuna ugumu gani kulipa? Wanachotakiwa ni 5% tu! Hili kama Wizara mtalifanyia kazi, hakika mtakuwa na fedha kwani ulipaji wa kodi pia utaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulipatia Taifa pato toka kodi ya mauzo ya DVD, CD na kadhalika; Tanzania kuna wananchi si chini ya 35ml. lakini tukichukua wananchi 4ml. tu ambao ndio watakaonunua kanda na kila mtu anunue kanda tano tu kwa mwaka kwa bei ndogo tu ya Sh.1,000, hebu fanya hesabu hiyo tu uone ni kiasi gani zitapatikana? Je, kodi itakuwa kiasi gani na ni kanda tu bado CD, DVD na kadhalika? Kwa hali hii, inaonesha ni jinsi gani Wizara isivyokuwa makini na fani/kitendo hiki, hivyo kulikosesha Taifa pato kubwa sana. Labda niongee tu kwamba, naomba sasa Wizara igeuke na kuweka mazingira mazuri ya kulipatia Taifa pato, pia wasanii kwani ni ajira nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi ya vyombo vya muziki; tunaposema kuongeza ajira kwa vijana na Watanzania kwa ujumla ni lazima kuweka mazingira mazuri ya ajira hizo. Si mradi ajira tu, ni pamoja na pato unalopata toka katika ajira hiyo. Sasa vijana wengi wameamua kutumia vipaji vyao ili kuajiari wenyewe kwa njia ya sanaa. Tatizo kubwa lingine ni zana zao za muziki, zimekuwa na ushuru mkubwa sana, hivyo kusababisha bei ya vyombo vya muziki kuwa ya juu sana na kukwamisha juhudi zote za kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali naomba ushuru uondolewe kwenye vyombo vya muziki/sanaa ili kutoa fursa kwa wasanii wetu. Pamoja na ushuru wote huo kutolewa ni lazima Wizara ije na mkakati wa kudhibiti vifaa feki, kwani hata sasa vyombo vingi vinavyoingizwa hapa nchini vinakuwa feki. Utanunua kinanda au gitaa leo, baada ya siku chache linakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namwomba Waziri aje Singida atembelee viwanda vikubwa na vidogo vya Mkoa wetu ili aone na apate maelezo halisi toka kwa wawekezaji wenye changamoto zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie pia kwenye eneo la Zao la Alizeti hususan Mkoa wa Singida. Mkoa wamejitahidi kuhimiza wakulima walime Zao la Alizeti kama Zao la Biashara na wameitikia, pia wajasiriamali wamejitahidi kufungua viwanda vidogo na vikubwa vya kukamua mafuta. Tatizo moja ni kutokuwa na uwezo wa kuweka mitambo ya ku-*refine* mafuta ya alizeti.

Suala hili limeitia hofu Singida, baada ya TFPA kutishia kuwafungia viwanda vyao kwa kuwa mafuta yao siyo *refined.* Sasa je, Wizara inatambua hilo; na kama inalitambua imechukua tahadhari gani ya kuwasaidia Wananchi wa Mkoa wa Singida mara watakapofungiwa biashara yao? Je, imeweka mazingira yapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niombe jambo moja, Wizara ishirikiane na Mkoa wa Singida ili kuhakikisha wanapata mwekezaji ambaye atakuwa na mitambo ya ku-*refine* ili kuwasaidia wakamuaji wadogo ku-*refine* mafuta yao kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waziri atuombee TFPA wasitufungie viwanda vyetu. Vinginevyo, tutakuwa tumeua Soko la Zao la Alizeti na kuwarudisha nyuma kimaendeleo Wananchi wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kodi ya mafuta yanayotoka nje, irudishwe ili kulinda soko la mafuta ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika eneo la mpango wa Serikali kugundua bidhaa zote nchini kabla ya kuingia *(pre-shipment inspection).* Jambo hili lilielezwa katika Kamati ya Hesabu za Serikali, pato 75.10 mpaka 75.23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zilizotolewa kwenye PAC zinaonesha utaratibu wa kukagua magari umeigharimu nchi USD milion 12 kwa kituo kimoja tu cha Dubai, ambacho ni chanzo cha magari 80,000 kila mwaka na stika ni USD 150 kwa gari moja. Aidha, tangu 2002 hadi 2007, tumepeleka nchi za nje USD 48 milioni na zile zilizorudi kama mapato ya TBS ni USD.584,779.11 tu, ndiyo kusema nyingine zinabaki Dubai. Hii ni gharama kubwa sana kwa nchi isiyo na msingi imara wa kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kupoteza USD milioni 48 haitoshi, sasa Wizara inataka bidhaa zote zikaguliwe na hili litagharimu takriban USD milioni 48 kila mwaka. Jambo hili ni ufujaji mkubwa wa fedha za kigeni. Aidha, Wizara imekaidi maagizo ya PAC na Bunge, kwani uamuzi wa Bunge ulikuwa ukaguzi ufanyike nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili, siungi mkono hoja, natarajia kuomba CAG achunguze jambo hili.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua uwezo wa Waziri wa Viwanda na Biashara, uwezo wa Naibu wake na uwezo mkubwa wa Katibu Mkuu na Watendaji wake. Nawapongeza na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana kuona ya kuwa, T.B.L. inaua ushindani wa viwanda vya bia hapa Tanzania. Walikuja tukafikiri ni watu wema, lakini wamenunua na kufunga Kiwanda cha Bia cha Kibo Breweires cha Moshi na watu wengi sana wakakosa ajira. Wizara isimamie uendelezaji wa viwanda siyo kufunga viwanda. T.B.L. imenunuliwa na SAB Miller, ambao wana hisa 60%. Mkakati uliopo ni kutangaza *products* zao kama Castle na REDDS, wameacha kabisa *promotion* kubwa za safari na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamehakikisha CASTLE ndio ichukue nafasi ya safari kwa umaarufu. Hawauzi kabisa safari na kilimanjaro nje ya nchi kwa makusudi. Hawa Makaburu siyo watu wazuri; ni wa kusimamiwa barabara, wafuate sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kampuni ya Wazawa ya Bia, Serengeti Breweries, ambayo inakua vizuri na inatoa ushindani mzuri sana na pia ajira kubwa tu. Serengeti Breweries wanataka washirikiane na E.A.B.L. wajenge kiwanda kikubwa Moshi ili wazalishe bia kwa wingi, ikiwa ni pamoja na Tusker iliyokuwa inazalishwa na T.B.L.

Mheshimiwa Mwenyekiti, E.A.B.L. wanataka isitishe ushirikiano na T.B.L. lakini SAB Miller hawakufurahi na wako kwenye *arbitration* London. SAB Miller wamekwenda mbele zaidi, wanataka wainunue kabisa Kampuni ya Serengeti ili waue kabisa ushindani; Wizara inajua na Fair Competition Commission wanajua, naomba Wizara watoe tamko la kukemea tabia hii ya kuua ushindani.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu (Mb), Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa aliyowasilisha hoja vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Chami (Mb), Naibu Waziri, kwa jinsi anavyomsaidia kazi na utekelezaji bora wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni mojawapo kati ya zile zenye kushughulika na uwezeshaji wa Watanzania. Tunayo makundi ya wanawake na vijana, wanahitaji ukombozi wa kiuchumi. Wanawake na vijana, wanajitahidi kuanzisha shughuli zao za uzalishaji, kwa mfano, kuanzisha maduka, ushonaji na ufumaji; hata hivyo ni wabunifu wasio na ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Wizara hii, waliweke Jimbo la Mulemba Kaskazini katika programu ya kuwawezesha wananchi katika makundi hayo ili wapate elimu ya ujasiriamali. Elimu hii itawasaidia kuibua miradi yenye tija, kulingana na mazingira yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itainua hali ya kipato na kuongeza ajira kwa Watanzania. Naishauri Serikali, kwa kutumia kaulimbiu yetu ya Kilimo Kwanza, iwaangalie wale ambao wamezalisha mazao yanayoweza kusindikwa viwandani kama vile mananasi, mapasheni, nyanya, ndizi na maembe, wasaidiwe kupata mashine za kushindika mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii inaweza kufanywa vizuri na SIDO. Nashauri SIDO iwezeshwe ili iweze kufanya kazi hii vizuri. SIDO imethibitisha kushughulika na wajasiriamali wadogo wadogo na wamefanikiwa. Wakipewa nguvu zaidi kwa kupewa fedha, SIDO wanaweza kufanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niishauri Serikali, iongeze bidii kuwahamasisha Watanzania kutumia bidhaa zetu za ndani ya nchi hasa chakula. Vyakula kama mafuta ya kupikia, tunaletewa mafuta mabaya, yanayoganda na kusababisha matatizo makubwa ya afya kwa watumiaji. Mafuta haya yamejaa kwenye maduka na yanauzwa kwa bei nafuu, kulinganisha na mafuta mazuri kwa afya zetu yanayopatikana hapa nchini ni pamoja na alizeti iliyochujwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iliangalie hili, wakulima wa alizeti watiwe moyo ili mafuta ya alizeti yapatikane kwa wingi na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera una mafuta maarufu yaitwayo MKWANO, chimbuko lake ni Uganda. Wakati mafuta ya MKWANO yamekamata Soko la Mkoa wa Kagera, hakuna mafuta ya Tanzania. Soko la mafuta ya alizeti, karanga, lakini mafuta haya hayafikii. Naishauri Serikali, ivikuze viwanda vyetu nchini ili tunufaike sisi kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali sasa iangalie TBS kwenye vyakula vya muda mfupi kama vile mkate, nyama katika maduka makubwa, uyoga (mbichi na mkavu), maji ya kunywa na vyakula vyote viwekewe alama ya ubora na muda wa ubora huo. Tunanunua vyakula vilivyooza, wakati huo huo wenye maduka wamebandika vibao "mali ikishanunuliwa hairudishwi." Huu ni wizi maana kwa nini muuzaji auze kitu kibaya/kibovu, kisha aseme kisirudishwe pale mnunuaji anapokigundua. Serikali, iliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kwanza ya maendeleo, baada ya kuimarisha kilimo ni viwanda. Kasi ya viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo haionekani, kwa sababu mkazo katika viwanda vidogo vidogo haupo kabisa. Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO), kila mwaka linapunguziwa uwezo wake; kama dhamira ni kuleta maendeleo na ustawi wa wananchi na hususan vijijini ni kuimrarisha SIDO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, SIDO katika awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi hii ilipewa kipaumbele, lakini kadiri siku zinavyopita, haina thamani tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya Wizara ni kuwa na Maeneo Maalum ya Kibiashara kama EPZ na SEZ; jambo hili ni jema sana lakini ili kutoa fursa sawa nchini na hasa katika maeneo ya mipakani ni vyema tukatenga maeneo haya ya SEZ kama vile Tunduma, Mkoani Mbeya, Kasesya na Ikola, Mkoani Rukwa na maeneo ambayo zipo harakati za kibiashara na nchi jirani. Nategemea wazo hili, Wizara itajaribu kulipitia na kuona uwezekano wa kuwa na vituo hivi mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa katika nchi yetu la kupokea bidhaa hafifu toka nje. Hali hii haivumiliki, kwa sababu haiwasaidii Watanzania ambao

wanatumbukia katika kununua bidhaa zisizokuwa na ubora. Ningependa kufahamu hatua ambazo zimechukuliwa katika kurekebisha dosari hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha pale hatua inapokuja kuchukuliwa kwa mtu wa tatu (mfanya biashara wa kawaida), wakati bidhaa hizi zinapita katika vituo ambavyo ukaguzi ungepaswa kuimarishwa, kwa sababu hasara anaipata *retailer,* badala ya *wholeseller* au *importer.* Ili kuwanusuru hawa *retailers* ni vyema sasa tukaangalia vituo vya kupitisha bidhaa na kuimarisha ukaguzi katika vituo hivyo, kama hasara apate *importer* na si mwingine yeyote. Kufanya hivyo, utakuwa umemlinda mlaji, Mtanzania maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kupata ufafanuzi juu ya busara iliyotumika ya kufuta leseni ya biashara kwa wafanyabiashara ambao wanayo mitaji mikubwa na kumtoza ushuru wa Sh.2,000 kwa gunia muuza mkaa au ndiyo maandiko yanasema mwenye kingi anaongezewa? Nataka kupata maelezo ya kutosheleza, kwa kufuta leseni na kudai ushuru toka kwa watu maskini, wajasiriamali ambao wanapigana na hali ngumu ya maisha na kukosa mitaji ya kuanzisha biashara ndogo ndogo au za kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nimalizie tu kwa kusema machache juu ya Chuo cha CBE. Hali ya Chuo cha CBE – Dodoma ni mbaya sana. Wahenga walisema, usipoziba ufa utajenga ukuta. Kwa kuwa Serikali hii haina utamaduni wa kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya majengo yake, hali ya majengo CBE ni mbaya sana. Ukipita tu hapo nyuma, utaona jinsi paa lilivyo, hakuna anayejali au kuchukua hatua ya kurekebisha dosari hiyo. Wizara iangalie kila namna ya kuboresha majengo ya Chuo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kusema ahsante sana.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri sana. Aidha, nampongeza Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, atuleletee wataalamu wapime ubora wa *gypsum* iliyoko eneo la Nyumba ya Mungu, Wilaya ya Mwanga, kwa ajili ya kutengeneza sementi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sikubaliani na wazo la Wizara kuhusu *Pre-Shipment Verification of Conformity to Standards*, yaani mfumo wa ukaguzi wa ubora wa bidhaa huko huko nje kabla ya kuingizwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo hili linapingana na agizo la Bunge kupitia Kamati ya PAC. Katika *Report* ya Kamati, tulishauri kuwa, utaratibu huo wa kukagua bidhaa kabla ya kuingizwa nchini, ulishajaribiwa mara nyingi nchini Tanzania, kwa

kutumia Makampuni ya SGS na COTECNA na kwa sababu Tanzania imekuwa ikipoteza fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa magari tu, taarifa ya TBS ilionesha 2002 – 2007, TBS iliweza kukusanya Sh.672,341,550.28, sawa na USD 584,77911, ambapo hiyo ni ada inayotozwa kwa kila gari. Hiki ni kiasi kidogo ukilinganisha na gharama ya shilingi bilioni 48 inayolipwa na nchi, kupata mapato tajwa ya shilingi 672,341,550.28. Naamini pesa nyingi inapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi ni bora utaratibu ubadilike, magari na bidhaa nyingine zikaguliwe hapa hapa nchini. Tangu zoezi hilo la kukaguliwa bidhaa nje, kwa mfano, toka 2002 – 2007 kwa magari tu, tumepoteza takriban shilingi bilioni 62.9. Hivyo, magari yote yakaguliwe baada ya kufika bandarini. Utaratibu uwe aliyeleta gari alipe ushuru ila gari lisipatiwe namba ya usajili mpaka TBS wakague ili ile dola 150 inayolipiwa nje, ilipiwe hapa hapa nchini. Hili siyo agizo langu, bali ni la Bunge. Tuokoe pesa za kigeni, nchi yetu bado ni tegemezi kwa zaidi ya 30%. Kwa mwaka tunapoteza takriban USD 12,000,000, sawa na (Sh. 15,600,000,000) kwa magari 80,000 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Tanzania imeendelea kuwa soko la bidhaa feki kutoka nje hasa China. Hili lajulikana sana; Wizara inafanya juhudi gani kuzuia hali hii? Inasubiri viingie ili vichomwe moto. Nashauri *hyodryport* itengenezwe, uwepo upande wa magari na upande wa bidhaa nyingine zikaguliwe hapa hapa nchini baada ya kulipia ushuru ili ziingie sokoni *after* TBS kuwakagua ili wapate kibali cha kuuza nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Serikali kuna sera ya uhamasishaji wajasiriamali, uanzishaji viwanda vidogo vidogo mfano vya kusindika juice, matunda, asali na kadhalika. Lazima wapate kibali kutoka TFDA, baada ya Mkemia Mkuu kupima waki-*qualify* wanapewa leseni au kibali cha kuuza bidhaa zao. Kuna tangazo kuwa wananchi wasitumie bidhaa bila TBS; sasa Waziri anasemaje juu ya hili kwa wale wenye vibali vya TFDA pekee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, utaratibu ukoje; wanapewa muda gani kufikia viwango vya TBS baada ya kupata kibali cha TFDA? Je, tangazo kama hilo halipingani na sera ya ujasiriamali hivyo lirekebishwe ili wenye vibali vya TFDA nao wapate soko la bidhaa zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze mafanikio yaliyopatikana baada ya uazishwaji wa vituo vya biashara vilivyopo London na Dubai, ambavyo lengo lake lilikuwa kukuza uwekezaji ndani ya nchi yetu, pamoja na uuzaji wa bidhaa zetu nje ya nchi ili kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ieleze ina mpango gani na Vyuo vya CBE vya Dodoma na Dar es Salaam; hadhi yake imeshuka; miundombinu mibovu tena ile ile ya

zamani? Vyuo viendelezwe. Vile vile kuna umuhimu wa kuongeza Chuo kingine ili tuongeze wataalamu na masuala ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, SEZ na EPZ; Serikali itueleze maeneo mangapi yaliyolengwa na kwa shughuli zipi; na maeneo mangapi yameshapewa hati miliki hasa maeneo ambayo bado hayajaendelezwa ili pasitokee mgogoro hapo baadae? Je, wamiliki wangapi wa maeneo yaliyochukuliwa na kuwa maeneo ya EPZ wameshalipwa fidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma tuna Mpango wa SEZ; nampongeza *Regional Commissioner* wa Kigoma, ameshaandika mchanganuo mzuri na ameshaufikisha Serikalini, lakini sijaona chochote katika Hotuba ya Waziri. Je, halijafika ofisini kwako mbona hakuna lolote kwani Mkoa wa Kigoma umo katika mikoa sita iliyochaguliwa kwenye Mpango wa Kilimo Kwanza? Naitaka Serikali itangaze Mpango huu wa SEZ Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo Kwanza hakiwezi kuendelea bila viwanda. Viwanda vinasaidia kuongeza Pato la Taifa. Kurasa za 36 na 37 zinaonesha kuwa, Sekta ya Viwanda nchini haijalipatia Taifa pato linalohitajika au linalostahili. Vipindi vya miaka mitatu mfululizo, inaonesha Wizara inasuasua; 2008 ilikuwa asilimia 9.4 na 2007 asilimia 8.7. Hali ndio hii hii; mbaya zaidi hapaonekani kuwa na lengo angalau 2009/2010 tufike angalau 12% kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona Tanzania inaendelea kuwa soko la bidhaa tunazozalisha wenyewe, lakini zinatengenezwa nje kwenye viwanda vya wenzetu. Sisi tunauza bidhaa ghafi. Lazima tulinde soko la bidhaa zetu zinazotengenezwa nchini, kwa lengo la ulinzi wa viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza kuona Watanzania tunaingiza kwa wingi maziwa, juice na vimininika vingine, wakati tunaendelea kuwa na kiwanda chetu cha Tanga Fresh na kile cha Juice Morogoro. Tuweke ushuru mkubwa bidhaa hizo zisitoke nje, washindwe kuyaleta ili tutumie bidhaa za viwanda vyetu. *Automatically*, viwanda vitakua kwani *demand* itaongezeka; mwisho tutafikia *standard*s za kimataifa na tutauza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtaka Waziri atueleze ana mpango gani wa kufufua viwanda vyetu, mfano General Tyre. Kiwanda hiki ni muhimu; soko la matairi lipo, tatizo ni nini? Waziri aeleze kwa nini asikifufue Kiwanda cha UFI na ZZK Mbeya vitasaidia kupata pembejeo za kilimo hapa nchini kuliko hivi sasa Wizara ya Kilimo imepanga kuagiza matrekta madogo na makubwa kwa shilingi bilioni 12 kutoka nchini India na vingine kutoka China?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri aeleze nini hatima ya Kiwanda cha Ngozi cha Morogoro na kile cha Kilimanjaro kifanye kazi yake inavyostahili kwani kina-*under produce* ili tuepuke kusafirisha ngozi ghafi. Kiwanda cha Tanganyika Packers hatima yake nini? Mbona nchi hii hatuwi wakali, kama mwekezaji amechukua lazima kuwepo kipengele kitakachomlazimisha aendeleze uzalishaji ili tulinde ajira zetu na tuzalishe

kutokana na mali ghafi yetu. Vile vile Kiwanda cha Maguni lazima kihuishwe tuachane na magunia ya nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitaka Serikali ione umuhimu wa kutangaza utekelezaji na kufufua viwanda kwa awamu, kama inavyotangaza ujenzi wa barabara. Wizara hii nayo isaidie iwe na tija katika kufufua uchumi wa nchi unaosuasua; iige mfano wa Wizara ya Miumbombinu, tuhuishe viwanda vilivyopo na tujenge vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Mashariki ya Mbali, India, China na kadhalika waliweza na wamefikia 25 – 30%; kwa nini sisi tushindwe? Rejea ukurasa wa 98. Waziri kaeleza suala la mazingira, lakini hakutaja Kiwanda cha Chumvi cha Uvinza, ambacho kinatumia magogo/kuni katika uzalishaji wake. Anatoa mwongozo gani; kama Waziri haoni kuwa Kigoma itageuka Jangwa?

**MHE. HASNAIN G. DEWJI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hoja hii iliyo mbele yetu. Nampongeza sana Waziri, kwa hotuba nzuri. Nina machache ya kuchangia kuhusu viwanda vya juice.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kilwa, kuna matunda mengi hususan machungwa na maembe, lakini bado hatuna kiwanda cha kusindika matunda hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maembe na machungwa yanaharibika ovyo na kuliwa na nyani. Je, Waziri ana mpango gani kumuwezesha muwekezaji kuweka kiwanda cha matunda, ukizingatia Kilwa kuna gesi asilia na umeme wa kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkoa wetu wa Lindi una mashamba makubwa ya katani, lakini hatuna kiwanda cha kuzalisha vitu vinavyotokana na katani kama magunia ya katani, naomba tuongeze viwanda vya ndani kuliko kuagizia mali toka nje, tuokoe ajira. Naomba kuwe na mkakati maalumu, kuteketeza vifaa bandia kutoka nje ya nchi. Viwanda vyetu vinaathirika kwa kuletwa bidhaa bandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho, aniambie atafanya mpango gani kuvinusuru viwanda vyetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa hotuba nzuri. Tumefikia hatua gani katika mpango wa kujenga Masoko ya Kimataifa ya Makambako na Segera mbona kimya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaambie nini wananchi? Tafadhali, tuwe wazi.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote kwa ujumla, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ni kuhusu viwanda vidogo vidogo. Sekta hii ina mchango mkubwa wa kuboresha maisha ya wananchi kwa kutoa ajira. Hata hivyo, naipongeza Wizara kwa kuinua Pato la Taifa, limeongezeka kwa asilimia 9.4 na ajira imeongezeka kwa asilimia 92.015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu bidhaa feki ambazo zimeingia kwa wingi hapa nchini. Kwa kweli hii hali imeongezeka kwa kiwango kikubwa sana. Tunaiomba Wizara, ichukue hatua kwa wale wote wanaoingiza bidhaa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuwapongeza tena kwa kazi nzuri na naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa kazi yake nzuri sana anayoifanya katika Wizara hii. Pia nampongeza Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

(1) Serikali ijaribu kusaidia kukua kwa viwanda kwa haraka ili kuisaidia Sekta ya Kilimo na hatimaye kukuza uchumi. Serikali imejitoa kufanya biashara, lakini ifanye *facilitation* kama ifuatavyo: -

- Kuanzisha chombo mfano Tanzania Industrial Development Authority (TIDA) au kubadilisha NDC kufanya hayo majukumu.

- Serikali ibuni viwanda, kisha itafute utaalamu, technology, land, isaidie upatikanaji wa mikopo, itafute masoko ya kuuza bidhaa hizo nje na ndani, kisha iwakabidhi wawekezaji wa ndani wafanye hizo biashara. Hivyo ndivyo Malaysia walivyofanya, kutumia Malaysia Industrial Development Authority yao.
- Tuamue nchi yetu iingie katika Industrialization. Bila kufanya hivyo; ni vigumu kwa Watanzania kuanza wenyewe. Serikali lazima isaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. OSCAR R. MUKASA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa mchango wangu uongozwe na malengo *(objectives)* ya Wizara kama ifuatavyo:-

Zipo jitihada gani za kuweka mazingira ya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo yanayopatikana kwa wingi kama katani ili kuyarudisha mazao hayo kwenye thamani na hivyo kuchangamsha uzalishaji wake? Tunahitaji kuweka mazingira yatakayochangamsha ukulima wa mazao haya ili badala ya kuagiza mifuko kutoka nje, tuvijengee uwezo viwanda vya magunia vya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takriban 70% ya eneo la Wilaya ya Biharamulo ni misitu. 50% ya eneo hilo la misitu ni misitu ambayo shughuli za kiuchumi zinaruhusiwa, tofauti na maeneo ya hifadhi na mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukulima na uvunaji wa mazao ya nyuki na asali upo kwa wingi (kiasilia), hasa katika Kata za Rusahunga, Nyakahura, pamoja na Kalenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikwazo kikubwa cha uwezekano wa wakulima hawa wa Kata hizi kupata nta ya kutosha ni ukosefu wa namna ya kufanya uongezaji wa thamani kwenye mazao haya ya asali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikatazama uwezekano wa kuweka viwanda vidogo kwa ajili ya uongezaji wa thamani ili kuchangamsha kilimo hiki cha asali kifikie *full potential*. Pia faida za kuongezeka kwa kilimo cha nyuki na asali zitagusa sekta nyingine kama:-

(i) Mazingira; nyuki hawapendi moshi, hivyo wananchi wenyewe watafanya jitihada za kuzuia uchomaji wa misitu kwa kudhibitiana miongoni mwao wenyewe.

(ii) Tunahitaji kutengeneza mfumo wa soko la mazao ya kilimo kwa ajili ya kutuunganisha na mahitaji ya nchi jirani (Rwanda, Burundi na DRC kupitia nchi hizo mbili za awali).

- Kuna fursa kubwa ya kupeleka mazao ya chakula hasa muhogo, mahindi, dagaa kutoka Chato; lakini wafanyabiashara wa ndani ya nchi na wa kutoka nchi jirani, wanafika moja kwa moja kwa wakulima. Mara nyingine, wageni kutoka nje wanafika mpaka kwa wavuvi moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitengeneza mfumo wa soko utakaowezesha ujenzi wa maghala katika Wilaya za Biharamulo na Ngara na kupitia maghala hayo, wafanyabiashara wakafika kufanya ununuzi kwa kukutana na mfumo maalumu wa soko la pamoja, tutaweza kulinda maslahi ya wadau wote (wakulima/wafanyabiashara wa ndani na wa nje). *See general objective* ya Wizara. *"… While ensuring fair returns to all stakeholders …"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna gani tutashughulika katika mazingira hayo na uwekaji wa miundombinu ya masoko ya mazao yetu kwa Wilaya hizo (Biharamalo na Ngara), kwa kuwa ni Wilaya ambazo ni kiungo cha Wilaya nyingine nyingi, kwa maana ya kufikia mipaka ya Rwanda na Burundi kwa urahisi? *See specific objective; "Promote investment in agricultural marketing infrastructure."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tushirikishe sekta binafsi, majirani zetu Rwanda na Burundi ili kushughulikia mambo haya.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri anayofanya yeye binafsi na Naibu

wake, pamoja na Katibu Mkuu, mwenye uwezo mkubwa kielimu na kiutendaji, Madam Joyce Mapunjo na Wataalam wao wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina *issues* tatu ambazo naona ni muhimu sana. Kwanza, suala la General Tyre. Kwa sisi ambao tumekuwa jirani na Kiwanda hicho, tunaelewa umuhimu wa kuwepo Kiwanda hicho. Taarifa na matatizo ya Kiwanda hicho ni mengi, kikubwa ninachoomba, Kiwanda hicho kifunguliwe, kwani kwa akili ya kawaida, inaelekea kuwa wenye maslahi ya kuingiza matairi ya nje wanatumia mbinu mbalimbali kuhakikisha General Tyre haifanyi kazi. Ieleweke kuwa, wale wafanyakazi waliopo wakiondolewa basi tumeua na utaalamu, siyo rahisi kufundisha wengine tena. Pia kwa heshima, namwomba Mheshimiwa Waziri akitembelee Kiwanda kama bado hajakwenda ajue hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, suala la Soko la Segera nalo japo lipo chini ya ASDP, kutokana na maelezo ya Katibu Mkuu, bado sisi tunajadili kwenye Vikao vya RCC, hatuna taarifa kamili. Naomba Mheshimiwa Waziri, utusaidie soko hili lianze. Taarifa tuliyonayo, hata wale wafadhili waliokuwepo ni kama wanapunguza nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuhusu soko la magunia, Mheshimiwa Waziri nilimueleza jana. Ni muhimu tupitishe uamuzi kuwa ni lazima bidhaa zetu ziuzwe kwenye magunia ya katani. *My sister* tunamwamini kwa *seriousness* na maamuzi. *Don't let us down this time.* Fanya maamuzi sahihi na sisi tutakulinda. Ahsante.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri, yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naunga mkono hoja hii. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa zamani kulikuwa na Tume ya Bei na iliweza kudhibiti upandaji holela wa bidhaa mbalimbali kama vile sukari, vifaa vya ujenzi, mabati, saruji na kadhalika. Je ni chombo gani kinachodhibiti mfumko wa bei kwa kuwa hivi sasa wananchi wanashindwa kujenga nyumba kutokana na gharama/bei kubwa ya vifaa vya ujenzi mabati, saruji na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. HALIMA M. MAMUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwapongeza waheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, na Watendaji wa Wizara, kwa kazi wanazozifanya, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Arusha na hasa Manispaa ya Arusha, uchumi wake unategemea sana utalii, biashara, viwanda, kilimo na ufugaji. Mji wa Arusha umekuwa ukitegemea sana viwanda vilivyofanikiwa kutoa ajira kwa watu wengi kwa muda mrefu. Huu ni mwaka wa nne, Wizara imekuwa ikiliambia Bunge hili kuwa,

juhudi za kumpata mwekezaji wa kukifufua kiwanda cha General Tyre (EA) Ltd. Zinaendelea; kama inavyoonesha katika ukurasa wa 15 wa Hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, naomba niseme kuwa, usemi huu hauwezi kukubalika bila maelezo ya kina, yatakayoonesha hatima ya kiwanda hiki, wafanyakazi wake na miundombinu yake. Ni hivi karibuni, Serikali imelipa mishahara ya miezi sita ya wafanyakazi 317, wakiwa hawajawahi kufanya kazi kwa miezi yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani miaka mine, Serikali iendelee kulipa mishahara na kuwakatisha tamaa wafanyakazi ambao hata wao, hawaridhiki kulipwa mishahara bila kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo haya, naomba kupata maelezo yafuatayo ili niweze kuunga mkono hoja hii bila kinyongo:-

(a) Nini hatima ya Kiwanda hiki?

(b) Nini hatima ya wafanyakazi?

(c) Kiasi gani Serikali imekwishatumia kwa miaka minne kuwalipa mishahara wafanyakazi na gharama nyingine kama vile umeme, ulinzi na kadhalika?

(d) Malighafi zilizokuwepo wakati kiwanda kinasimamisha uzalishaji ziko wapi na katika hali gani?

(e) Inasemekana wapo wafanyakazi ambao walikwishastaafu lakini bado wanalipwa mishahara. Je, Wizara inalifahamu hili na kama inalifahamu hatua gani zimechukuliwa?

(f) Nyumba na maghala yameuzwa kwa sababu gani kabla mwekezaji hajapatikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha KILTEX Arusha kiliuzwa kwa nani na kwa nini hadi leo hakifanyi kazi na hakikutajwa mahali popote katika Hotuba ya Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya kutengeneza nishati mbadala kutokana na mabaki ya mazao na taka za asili *(organic waste)* na za majumbani, vinasaidiawaje na Wizara kwa maana ya kupata maeneo na fedha za kununua mitambo kutokana na ukubwa na thamani ya mitambo hiyo kuwa ni ya bei kubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kufahamu wenye viwanda na biashara ndogo na kubwa watapewa msaada gani ili waweze kumudu kuendeleza viwanda na biashara zao baada ya kuathiriwa na mtikisiko wa uchumi wa dunia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lini Mheshimiwa Waziri ataongozana nami kuwafahamisha wafanyakazi na Wananchi wa Arusha hatima ya Gneral Tyre na KILTEX?

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uzima ili nami niweze kuchangia hotuba iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Mheshimiwa Mary Nagu, Mheshimiwa Cryil Chami, Katibu Mkuu, pamoja na Wataalamu wote, kwa Hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu na suala la EPZ Centre. Naomba nichukue nafasi hii, kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa faraja kubwa sana, kwa Wananchi wa Manyara, kwa kuwa miongoni mwa maeneo yaliyotengwa ni pamoja na Mji Mdogo wa Mererani, kupandishwa hadhi na kuwa eneo maalum kwa ajili ya viwanda na masoko ya nje *(Export Processing Zone - EPZ).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa wamelipokea kwa shangwe na wameweza kutenga eneo la kutosha kujenga viwanda; karibu eka 2000 zipo tayari. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka ili kuweza kuanza kutengeneza miundombinu mizuri ya mji ule kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji ikiwa ni pamoja na kutengeneza ramani nzuri kwa viwanda kwa kuwa barabara ni muhimu sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuongea na kuwasiliana na Waziri wa Miundombinu ili Barabara ya KIA – Mererani iwekwe lami kuwarahisisishia wageni wanaokuja kuwekeza viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu eneo hilo kutangazwa kuwa eneo la EPZ ni sababu gani zinazozuia eneo hilo kupewa usajili? Je, Serikali kupitia Wizara hii iko tayari kufanya mazungumzo na Shirika la Akiba la NSSF waje kuwekeza majengo ya viwanda na makazi katika eneo hili la EPZ Mererani kwa kuwa sijasikia mahali popote Mkoa wa Manyara unatajwa hususan EPZ Mererani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008/2009 jumla ya wawekezaji 18 walipewa leseni za EPZ, ambapo miongoni mwao saba ni wajenzi wa miundombinu ya viwanda *(EPZ Developers).* Je, kuna mkakati gani wa makusudi wa kuwaelekeza wawekezaji hawa kwenda kuwekeza Mererani EPZ?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna viwanda vingi na vingine vinatengeneza bidhaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na viwanda vya mafuta ya kupikia. Tunahamasisha wananchi kulima ufuta na alizeti ili pia kuboresha viwanda vyetu vya hapa nchini. Kwa

nini Serikali inatoa mwanya kwa wafanyabiashara kuagiza mafuta kutoka nje na kuwatoza ushuru kidogo? Je, Serikali haioni kwa kufanya hivyo ni kudhoofisha maendeleo ya viwanda vyetu na wakulima kukata tamaa kwa sababu bidhaa zinazoagizwa nje ni rahisi kuliko zinazozalishwa hapa?

Serikali ina mkakati gani wa kupandisha ushuru wa bidhaa zote zinazoagizwa nje ili kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini ikiwa ni pamoja na kupandisha bei ya mazao yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa TANALEC ni kiwanda kinachotengeneza vifaa vya umeme na vyenye ubora sana kama transforma na *switch gear*; je, Serikali ina mkakati gani wa kukisaidia kiwanda hiki ili kiweze kuzalisha kwa wingi na kutangaza ubora huu kwa nchi nyingine ili ziweze kuagiza transforma Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Mashine Tools kilichoko Hai, kimeleta sifa kubwa kwa kutengeneza mashine nzuri na kiliajiri watu wengi sana kutoka Wilaya ya Hai, Mkoa wa Kilimanjaro, Arusha, Tanga na Singida. Mpaka sasa hivi kile Kiwanda majengo yake yanaharibika, bure. Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kukifufua kiwanda hicho? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Africa nzima hakuna kiwanda kinachozalisha bidhaa nzuri kama Kiwanda cha General Tyre. Tyres ni nzuri na zenye hadhi na viwango.

Je, Serikali imeshindwa kukiimarisha kiwanda hiki hadi kinashindwa kuzalisha tyres za kutosha hadi tunatoa mwanga kwa wafanyabiashara kuagiza tyres nje na kutuuzia kwa bei ya juu? Je, tatizo ni kampuni hii haina mtaji au ni ukosefu wa malighafi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kuhusu Kiwanda cha General Tyre kilichoko Arusha. Pia naomba ufafanuzi kuhusu Kiwanda cha Mashine Tools kilichoko Wilaya ya Hai, EPZ Centre Mererani na kuhusu Kiwanda cha TANALEC Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uzima wa afya na kunipa nguvu nami nichangie machache katika hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa uwasilishaji mzuri wa Hotuba yake. Pia nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa mashirikiano yao ya kuandaa Hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nilipata bahati kutembelea Moshi, kwa masikitiko makubwa nimeona viwanda vingi vimelala, yaani havifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi ni vya kizalendo na wananchi wengi walipata ajira kutokana na viwanda hivyo. Je, wafanyakazi wale wako wapi na hatima yao imefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya kosa kubwa kuvifunga viwanda hivyo na hivi sasa ninamwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na Wataalamu wake, kuangalia upya na kufanya mipango ya kuvifungua viwanda hivyo ili kukuza uchumi wetu na kuacha kukuza uchumi wa nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaiomba Serikali ianzishe viwanda vya matunda au kutafuta wawekezaji wa viwanda hivyo ili kununua mazao mengi ya matunda yanayozalishwa nchini mwetu, ambayo kwa sasa hayana soko yanaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna bidhaa nyingi nchini, lakini hakuna utaratibu mzuri wa kuzitumia kwa ukosefu wa viwanda. Hivi sasa ni aibu Tanzania kutumia juice zinazotoka nje, wakati matunda yanayotumika yanazalishwa kwa wingi sana hapa nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali suala hili waliangalie kwa makini na baadaye ifanye juhudi za makusudi kuanzisha viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. FELISTER A. BURA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote, kwa juhudi kubwa wanazozifanya katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha General Tyre kilikuwa kiwanda bora Afrika Mashariki na kilikuwa kinatengeneza magudumu mazuri kuliko viwanda vingine Afrika Mashariki; cha ajabu kiwanda hiki kimefungwa, Serikali inasubiri mwekezaji. Kwa kiwanda hiki kutokufanya kazi ni kutowatendea haki Watanzania wenye magari na Watanzania wanaopanda magari. Sioni sababu ya Tanzania kuagiza magurudumu wakati tuna kiwanda kikubwa kizuri. Kama Serikali haina uwezo, wapewe Mashirika ya Hifadhi ya Jamii wakiendeshe Kiwanda cha General Tyre.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chini ya Wizara hii kuna taasisi zinazofanya utafiti mfano TIRDO, SIDO, TEMDO na kadhalika. Kwa maoni yangu, taasisi hizi hazijatumika vizuri kwa lengo la kuinua/kuchangia Uchumi wa Taifa. Taasisi hizi pia hazijajitangaza ili wananchi waelewe shughuli zao na kushirikiana nao; wakati umefika taasisi hizi zijitangaze kwa wananchi. TIRDO ina wataalamu wazuri, wakitumiwa vizuri wataisaidia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa au kuuzwa kwa wawekezaji. Je ; ni vingapi vinavyofanya kazi vizuri na ni vingapi vilivyobadilisha matumizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa, baadhi ya wawekezaji baada ya kuuziwa viwanda, wamebadilisha matumizi ya viwanda hivyo na viwanda vingine vimekuwa godown.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya Serikali kuweka sera inayotoa upendeleo maalum, kwa bidhaa zinazozalishwa nchini, hasa katika suala la kodi. Bidhaa zetu ni ghali kwa sababu ya kodi inayotozwa ; hivyo soko la bidhaa zinazozalishwa nchini ni ghali ukilinganisha na bidhaa zinazoingizwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inazalisha matunda mengi, tuna ng'ombe wengi sana, lakini hatuna viwanda vya juice, hatuna viwanda vya kutengeneza viatu, tunasafirisha mbao nje ya nchi na wenzetu wanatengeneza fenicha kwa mbao zetu; viatu kwa ngozi za wanyama wetu; juice kwa matunda tuliyolima wenyewe, kisha wanatuuzia kwa bei ghali, nasi tunafurahia tukidhani malighafi zilizotengeneza bidhaa hizo ni zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika sasa tutumie malighafi zetu katika viwanda vyetu na tutafanikiwa tu iwapo kodi itapunguzwa kwenye bidhaa zetu na kuwepo na ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wataalamu wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri sana wanayofanya katika kuikuza Sekta hii ya Viwanda na Biashara. Aidha, pia ninawapongeza kwa Hotuba iliyoandaliwa vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu sasa utajikita katika maeneo yafuatyo:-

Nimekuwa miaka yote nikichangia kuhusu uwezekano wa kuokoa matunda mbalimbali yanayooza Korogwe hususan Mkoa mzima wa Tanga. Machungwa, maembe, passion, nyanya na kadhalika. Wananchi walizowea kuganga umaskini kwa kuuza matunda kwenye Kiwanda cha Matunda Korogwe (TANGOLD), lakini zimekuwepo ahadi za Serikali kwamba, watakifufua kwa aina mbili; aidha, kwa kutafuta mwekezaji ili apewe akiendeshe au kuingia ubia na watu wenye uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kufahamu jambo hili limefikia wapi? Serikali itatusaidiaje ili kiwanda hiki kiwepo wananchi wasiendelee kulalamikia Serikali na hasa Mbunge kuhusiana na kiwanda hiki? Ipo ahadi ya Serikali kujenga soko la matunda na mbogamboga Segera; je, jambo hili limefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Wizara ina mpango gani wa kuachana na magunia ya jute na kutumia magunia yanayotokana na malighafi yetu ya mkonge; hasa ikizingatiwa Zao la Mkonge nchini mwetu linazidi kuongezeka na matumizi ya magunia ya mkonge wafanyabiashara wengi wanayahitaji ila ni ghali sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri. Naomba wapange ni namna gani watalisaidia Soko la Kimataifa Matai linaloshughulikia uuzaji wa mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishauliza maswali mengi kuhusu Soko la mpakani Kasesya, sijapata maelezo ni vipi mtatusaidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Wizara haina takwimu na faida inayopatikana kutokana na biashara na Congo Kipili na Kirando?

**MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nawapongeza Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Cryil Chami, kwa Hotuba nzuri ya Bajeti ya Wizara, kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010. Bila kupoteza muda, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala kuhusu bajeti hii, suala la kuimarisha viwanda vya ndani, limesisitizwa sana na Wabunge wengi na hasa matumizi zaidi ya magunia ya katani kuliko ya jute. Hoja hii ni nzuri na ya msingi, ingawa inahitaji kufanyiwa kazi zaidi. Maana lazima sote tuelewe kuwa, mahitaji ya magunia nchini kwa mwaka ni milioni 60 na uwezo wa viwanda vyetu, haujawahi kuzidi magunia milion mbili katika miaka mitano iliyopita. Aidha, uingizaji wa magunia ya jute nchini, haujawahi kuvuka magunia milioni tatu kwa mwaka! Pengo la magunia zaidi ya milioni 55 linazibwa na viroba! Naongea haya kutokana na uzoefu wangu katika sekta hii, vile vile nikiwa mfanyabiashara wa magunia. Maslahi yangu nimeyaweka wazi. Hivyo basi, tukitaka matumizi zaidi ya magunia ya katani, tuongeze kilimo cha katani na vile vile uwezo wa viwanda vyetu.

Namalizia kwa kusema kuwa, baadhi ya mazao nchini, hayawezi kuhifadhiwa kwenye magunia ya katani; kwa mfano, viazi mviringo, pareto na mazao yote yenye punje ndogo ndogo; ni magunia ya jute tu yanayofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kurasa za 78 na 79 za Hotuba ya Wizara, zinaongelea masuala ya hati miliki. Swali langu kuu kwa Waziri; kwa kuwa mwaka 2006 Serikali ilitunga Kanuni chini ya Sheria ya Hatimiliki ya 1999; kwa nini Serikali imekuwa inashindwa kutenga bajeti inayotosheleza kila mwaka ili kanuni hizi zifanye kazi ?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni hizi zikianza kutumik, tutaanza matumizi ya HAKIGRAM ; nembo ya kulinda haki ya mwenye hati miliki na hivyo kuzuia *(piracy)* hizi na vile vile kuruhusu Serikali kujua idadi kamili ya kazi za sanaa na kupata kodi sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kutoa mchango wangu kwa hoja iliyopo mbele yetu katika maeneo yafuatayo::-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni zaidi ya mara nne sasa, nimekuwa nikiikumbusha Serikali, juu ya Ahadi ya Rais ya kuvifufua Viwanda vya Jiji la Mbeya; mara ya mwisho, Naibu Waziri akijibu swali langu la msingi kuwa, angefika Mbeya rasmi kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kukifufua Kiwanda cha ZZK – Mbeya. Kati ya viwanda vyote, Kiwanda hiki bado kina mashine ambazo zinaweza kuendelea kufanya kazi ya uzalishaji. Utafiti wangu unaonesha kuwa, teknolojia ya mashine za ZZK – Mbeya, bado ni *decent* na pia mtaalam wa Sweden, aliyefanya kazi ya ku-*instal* mashine hizo, bado yupo Tanzania na alikuwa tayari kusaidiana na Serikali katika kufufua Kiwanda cha ZZK – Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliniahidi kuwa, atafanya bidii kubwa kuhakikisha Kiwanda cha ZZK – Mbeya kinafufuliwa. Naomba kuieleza Serikali kuwa, hivi sasa Mhindi aliyepewa kutunza pale, anahamisha baadhi ya mashine; sijui anauza kama vyuma chakavu. Kiwanda kimegeuzwa kuwa bohari ya mambo yasiyohusiana na kiwanda. Serikali ifanye maamuzi ya kuyachukua majengo na Ndugu Gachuma arudishiwe fedha zake, hana mnunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri ZZK – Mbeya iwe ni mahali pa kuunganishia matrekta madogo *(power tillers)*. Kutoka nchi za nje ziagizwe *spare parts* tu, lakini uunganishaji ufanyike ZZK – Mbeya na vijana wetu wapewe jukumu la ku-*copy* teknolojia na kuifanyia mabadiliko ili iweze kufaa kwa matumizi ya mazingira ya Tanzania. Hii itakwenda sambamba na Sera ya Nchi ya Kilimo Kwanza. Tuthubutu sasa kuifufua ZZK – Mbeya. Lini Mheshimiwa Waziri atakuja kutembelea ZZK – Mbeya ?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiografia, Kiwanda cha Nyama cha Mbeya (Tanganyika Packers), bado ni muhimu sana katika uchumi wetu. Pia kuwepo kwa Uwanja wa Ndege wa Songwe – Mbeya, kunatoa fursa kwa Mbeya kusafirisha nyama sehemu mbalimbali za dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tujiulize ni kwa nini PSRC inakataa kukiachia Kiwanda hicho mikononi mwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi? Wizara ipo tayari kabisa kutafuta wabia wa kukifufua Kiwanda cha ZZK – Mbeya, baada ya kukaa muda mrefu chini ya PSRC bila kukifufua. Kwa nini PSRC inakatalia Kiwanda hiki? Naomba Wizara ipewe Kiwanda hiki ili ikiendeleze na hatimaye kupata ajira kwa vijana wetu. Naomba jambo hili lipewe uzito wa juu na Wizara hii, lengo ni kufufua viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuanze sasa kutekeleza Ahadi za Rais, kuwepo Kiwanda cha ZZK – Mbeya, Kiwanda cha Nyama – Mbeya, unakuwa umemaliza matatizo, lakini pia umeongeza ajira kwa Watanzania hasa vijana wa Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji. Naona tuna tatizo kubwa la mtazamo na mgando wa fikra, kwani mpaka leo Watanzania hatupendi bidhaa za nyumbani, bado tunapenda bidhaa za nje. Nashauri tufanye kampeni endelevu ya kushawishi Watanzania tupende bidhaa zetu ili kuendeleza viwanda na soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye kampeni kubwa ya kuwashangaa na kuwazomea, wanaokuwa malimbukeni wa bidhaa za nje. Serikali ianze yenyewe, vifaa vya ofisi na katika majumba ya Serikali, vyote viwe vya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri leo ameonesha mfano wa mavazi ya nyumbani, naomba iwe endelevu isiwe nguvu ya soda ya kupitishia bajeti. Taasisi ya BRELA, ina ofisi ambayo siyo nzuri, naomba wapewe fedha za ujenzi wa ofisi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi kama vile SIDO, CARMATEC na TIRDO, zinajitahidi kufanya kazi nzuri, bajeti zake pia ziongezwe ili shughuli zinazowafikia wananchi wengi ziwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma ni wazalishaji sana wa chakula, nashauri Serikali ishirikiane na Halmashauri zetu ili tuwe na wawekezaji wa viwanda vya unga, mchele na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, EPZ na SEZ, maendeleo yake pale Songea bado siyo mazuri. Fidia bado kwa wananchi na je, ni lini eneo hilo litaanza kuendelezwa na kuanza mauzo nje? Naomba Wizara ijitahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii, kuwapongeza Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa kazi nzuri ya kulijenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa SIDO inahusika na uwezeshaji wa wananchi kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali, pamoja na mikopo midogo midogo, napenda kujua mipango thabiti ya Serikali kuiboresha na kuiendeleza SIDO iweze kuboresha maisha ya wananchi?

Viwanda vya Samaki na Nguo (MUTEX), vilitoa ajira nyingi kwa watu wa Musoma na hii iliboresha maisha ya Wananchi wa Musoma. MUTEX sasa ni zaidi ya miaka miwili imefungwa, napenda kujua mpango wa Serikali kuhakikisha Kiwanda hicho na vile vya Samaki vilivyofungwa kama Fish Park vinafufuka ili kuendelea kutoa ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nianze kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa maandalizi mazuri ya Hotuba ambayo imefafanua vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda, Biashara na Masoko ni jambo ambalo ni la muhimu kwa kumnufaisha mkulima. Ili kufanikisha azma ya hili; ni lazima yafuatayo yatekelezwe:-

- Kulinda viwanda vya ndani kwa kutoruhusu bidhaa inayotoka nje kuingizwa nchini, kama itaingia basi itozwe kodi kubwa kwa nia tu ya kulinda viwanda vyetu.

- Tusindike mazao yetu na iwepo sababu ya lazima kuuza mazao yasiyosindikwa, lakini kubwa zaidi ni kusindika sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni Zao la Pamba, juhudi zifanywe za kuuza nyuzi na nguo; si kuuza pamba nyuzi (yaani pamba iliyochambuliwa). Tuuze nyuzi, nguo, mafuta na vitu vingine. Jambo hili litaongeza thamani ya zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zao la Mkonge limekuwa halifanyi vizuri, kwa sababu ya tatizo la magunia ya jute. Magunia haya hutoka nje ya nchi, yanaua viwanda vyetu hapa nchini. Sababu za makusudi zifanyike za kulinda viwanda vya hapa nchini. Viwanda vya magunia vitaongeza uzalishaji, ajira na uchumi wa jamii na Taifa kwa ujumla.

Mhshimiwa Mwenyekiti, nitapenda kujua juhudi za Serikali, juu ya mkakati wa uzuiaji wa uagizaji wa magunia nje ya nchi. Tuvilinde viwanda vyetu vyote viwe vya Korosho, Kahawa, Pamba, Pareto, Mkonge, Chai, Tumbaku na kadhalika. Ufafanuzi wa jambo hilo uzingatiwe ili uungaji mkono wa hotuba hii uwe na maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Dengu limekuwa matatizo sana; naiomba Serikali ione umuhimu wa kutafuta soko. Wananchi wa Wilaya ya Misungwi na Jimbo la Solwa, Mkoani Shinyanga, wana tatizo kubwa juu ya soko la dengu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa ujenzi wa masoko ya bidhaa ambayo yatasaidia sana wananchi katika maeneo yao, mfano Kijiji/Mji wa Masasi, unao mnada wa ng'ombe hapo Masasi, huwa wanachanganya na uuzaji wa mazao mchanganyiko; hivyo umuhimu wa tathmini ya kujengewa soko ni muhimu sana. Naiomba Wizara iufuatilie Mji huo ijionee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nisisitize juu ya yote niliyochangia yapate majibu. Naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko na Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami, Naibu Waziri, kwa kazi nzuri.

Naipongeza Wizara, kwa kuendelea kusaidia wafanyabiashara wadogo wadogo kupitia SIDO. Mkoa wangu wa Tanga, umenufaika kwa mikopo na mafunzo. Tatizo fedha haitoshi hasa kuweza kuwafikia katika Wilaya zilizo pembezoni kama vile Kilindi. Nampongeza Meneja wa Tanga, anajitahidi sana lakini fedha haitoshi.

Tunashauri SIDO itengewe fedha za kutosha na pia uwepo uwezekano wa hata Fedha za JK zipitie SIDO ili ziwafikie wateja kwa urahisi bila urasimu mkubwa.

Bado viwanda vinanyanyasa sana wale wafanyakazi wa kazi za muda. Tatizo hili linaonesha kukua hasa pale wafanyakazi wengi wanaponyimwa haki ya kupewa vitendea kazi vya kujikinga kiafya. Serikali (Wizara), hii ni changamoto kubwa, kwa vile Wizara ya Afya ilipitisha Sheria ya Afya ya Jamii, nashauri wawasisitizie wenye viwanda kulinda afya za wafanyakazi wawapo kazini. *Otherwise,* nawatakia kila la kheri katika kazi zenu.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie Wizara hii muhimu. Nitaanza na viwanda vyetu hapa nchini, ambavyo ni muhimu na ni ajira na vinakuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Viwanda vya Kahawa ambavyo ni Zao la Wana-Kagera, hebu okoa Wahaya kwa kuboresha viwanda vyetu. Umekuwa wimbo hapa Bungeni, tusage wenyewe tuuze nje tuondokanae na umaskini, pamoja na kuwa na soko kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepakana na Uganda wanalima ndizi, tunalima ndizi wanauza kwenye soko lao, pamoja na uwanja wa ndege na majani ya migomba, mboga, ndio maana unakuta uchumi wa Waganda unakua. Je, sisi tunashindwa nini kuwa na mikakati tuwaokoe wananchi wetu? Kama mnavyojua, Wakulima wa Kagera siyo wavuvi, viwanda vinawakatisha tamaa wakilima watauza wapi?

Wananchi wengi Kagera walichukua mikopo ya ng’ombe, wanadiwa kwa vile hakuna pa kuuzia maziwa. Pamoja na nyama; je, kwa nini Serikali haiboreshi ngozi zetu zinapelekwa nje? Tunasikitika sana. Niliona historia ya viwanda vya maziwa, vilikuwa 33 vikabaki kumi na viwili, vingine viko wapi na ni kwa nini tuwe na idadi na maeneo tu bila historia? Bukoba walilima sana majani ya chai, kukosa soko yamekuwa kama vichaka, kwani walikata tamaa kuyaendeleza. Naomba wananchi hao wafikiriwe.

Nchi jirani wanafanya mikakati gani na sisi tuige tusizidiwe na Rwanda; wana wasindikaji wakubwa wanne na wanaendelea kuwa na mikakati ya kuwa na viwanda UHT; je, sisi tuna mikakati gani? Uganda wana wasindikaji 33, ambapo siku hizi uchumi wao umeshuka sana. Kama sisi tunaua viwanda, wasindikaji waliopo Kenya kwa sasa ni

40; mimi naona wivu kuona tuko jirani tunashindwa kuiga hayo. Naomba Wizara iwe na mikakati mbadala, tuwaondolee umaskini watu wetu; ni kitu kinachowezekana.

Kituo cha kuzalisha maziwa, kusindika na suala mbadala ni muhimu kupunguza umaskini kwa wananchi wetu. Kuagiza maziwa kutoka nje, inatugharimu sana, tuige mifano ya jirani zetu wanavyofanya kwenye nchi yao. Naomba nikumbushe, maziwa ni muhimu kwenye mwili wa binadamu; tukiwa na viwanda vingi, maziwa ya wafugaji hayataharibika. Viwanda ni muhimu sana, sasa hivi hatuna viwanda, maziwa yanaharibika haraka, tunakuwa na samli ya kutosha, iliyo safi, matumizi ni mengi sana na manufaa ni mengi tu.

Sera ya Mifugo ya Taifa 2006, inataja vifungashio kuwa ni kikwazo kikuu kinachozuia ukuaji wa taasisi ya usindikaji. Nina uhakika Wizara pamoja na Serikali, yote niliyoyachangia yatafanyiwa kazi kulingana na matakwa ya Wana-Kagera, pamoja na Watanzania wote, bila kusahau kuviboresha Viwanda vya samaki Bukoba – Nyakazi, Kemondo, vilikuwa vinawasaidia sana vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba kuunga mkono hoja hii. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba nichangie kidogo katika eneo la biashara na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la wafanyabiashara ndogo ndogo (Wamanchinga), linakuwa ni kubwa katika maeneo mengi ya nchi yetu. Tatizo hili linatokana na kutokutengwa kwa maeneo maalum kwa ajili ya vijana hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika wa Serikali kutenga Maeneo Maalum (Ideal Sites) ili kuwawezesha vijana hawa kujiendeleza kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanjari na kutenga maeneo haya, lakini kuwepo na mpango wa makusudi, kwa kutoa elimu ihusuyo biashara. Elimu hii itawasaidia Watanzania wengi kuwa na uelewa wa biashara kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo naomba nilichangie ni kuhusu Kiwanda cha Nyama Tanganyika Packers Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hiki kilijengwa miaka zaidi ya 30 iliyopita. Tangu kimejengwa upya, hakijawahi kufanya kazi mpaka sasa. Naomba kupewa jibu, kwa niaba ya Wananchi wa Mbeya Vijijini, kitu gani kinakifanya kiwanda hiki kisifanye kazi hali Serikali iligharamia fedha nyingi kukijenga?

Mwisho, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maisha bora kwa Watanzania wote ni pamoja na kuwa na uwezo wa kujenga nyumba nzuri. Hata hivyo, Watanzania wengi wanashindwa kujenga nyumba bora za kuishi, kwa sababu ya bei kubwa ya vifaa vya ujenzi kama vile saruji, nondo, bati na kadhalika. Naomba kujua tatizo nini? Kinachoshangaza zaidi, hata katika maeneo ambayo bidhaa hizo zinazalishwa kama saruji kule Mbeya, Tanga na Dar es Salaam bado bei za bidhaa hizo siyo rahisi hata kidogo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tatizo ni mfumo wa kodi, kwa nini Serikali isirekebishe mfumo huo ili Watanzania wengi wapate unafuu na hivyo wamudu bei za bidhaa hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), limeanzishwa siku nyingi, kwa msingi wa kuibua miradi na kutafuta wawekezaji. Hata hivyo, kwa maoni yangu, Shirika hili halijafanya kazi zake sawa sawa; moja ya sababu, Shirika hili halijawezeshwa ili lifanye kazi zake vizuri. Hivyo, nashauri Serikali inapoanzisha Mashirika yake, ihakikishe kwamba, mashirika hayo yanawezeshwa ili yafanye kazi ambazo zilisababisha Mashirika hayo yaanzishwe. Vinginevyo, itakuwa ni kupoteza fedha za Serikali kwa kuendelea kulipa mishahara wafanyakazi, lakini *productivity* yake ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Zana za Kilimo Mbeya, maarufu kama ZZK, kilikufa miaka kadhaa iliyopita. Hivi ninavyoandika, majengo ya Kiwanda hicho yameendelea kuchakaa kwani hayana usimamizi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, jambo la faraja ni kwamba, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipoutembelea Mkoa wa Mbeya, mwezi Novemba, 2008, aliagiza Wizara ya Viwanda ihakikishe kwamba, Kiwanda hicho kinaanza kuzalisha zana za kilimo kama pale mwanzo ili kupunguza bei kubwa ya zana za kilimo.

Naomba kujua, tangu Mheshimiwa Rais atoe agizo hilo Wizara imechukua hatua gani hadi sasa?

Ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja.

Nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wataalam na Wadau wote wa Biashara na Viwanda.

Kwa muda mrefu sasa, Taifa limeshuhudia uharibifu wa miundombinu muhimu ya kitaifa na watu binafsi, unaofanywa na watu wanaofanya biashara ya chuma chakavu.

Kuta za madaraja na *culverts (headwalls)* zimevunjwa ili kuiba nondo, pampu za maji na miundombinu ya umwagiliaji imeibiwa na hata watoto wanashawishiwa kuiba majembe nyumbani ili wayauze kama chuma chakavu. Naamini upo uhusiano kati ya wanunuzi wa vyuma hivyo chakavu, wakusanyaji na pengine hata wasafirishaji wa vyuma hivyo.

Ipo haja ya kuwa na utaratibu wa Kiserikali wa kupambana na uharibifu huo, kwa sababu siyo tu kwamba, unaleta hasara ya fedha, lakini vile vile wizi na uharibifu wa miundombinu, unarudisha maendeleo nyuma, kwa sababu inabidi Serikali irudie tena kukarabati miundombinu iliyoharibiwa, badala ya kufanya maendeleo mengine.

Aidha, pamoja na mkakati utakaobuniwa ni vyema kuainisha matumizi ya sheria zilizopo, zinazoweza kulinda miundombinu, kwa mfano, Sheria za Maji Na. 11 na 12 za 2009, zitakazoanza kutumika Agosti 1, 2009. Sheria hizo mbili zinatoa adhabu kali (faini mpaka shilingi milioni tano na kifungo).

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Nawaomba waendelee na mwendo huo huo, kwa faida ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri; kwa kuwa kwenye Wizara yake kuna Kitengo cha Masoko, Wananchi wa Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Shinyanga ni wakulima wazuri sana wa alizeti, dengu, vitunguu maji/saumu, giligilani, katani na kadhalika. Mazao haya mpaka leo hayajapata soko la uhakika, ingawa wananchi wanasikia kwamba, mazao hayo yana bei nzuri sana kwenye Soko la Dunia. Tafadhali sana, watafutiwe masoko ya uhakika ya mazao haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa kitu kinachowaumiza sana wakulima wetu ni Serikali kutosimamia sawasawa ujazo wa mazao mbalimbali, yanayouzwa kwenye masoko yetu. Naiomba sana Serikali isimamie na kukomesha ujazo wa lumbesa, bali mazao yawe yanapimwa kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nchini tuna viwanda viwili vya kutengeneza magunia. Tunaomba Serikali yetu isimamie na kupitisha azimio la kupiga marufuku magunia toka nje, bali tutumie magunia yanayotengenezwa na katani tunayoilima sisi na wananchi wetu wengi wanapata ajira kwenye mashamba ya mkonge na viwanda vinavyotengeneza magunia na mazao mengine yatokanayo na mkonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Bangladesh na India, ambako magunia ya jute yanakotok, Serikali zao zinatoa ruzuku kubwa kwa viwanda vyao na kupitisha sheria ya kuwataka wananchi wao watumie magunia yao tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku Serikali inahimiza Wananchi wa Tanzania, tutumie bidhaa nzuri tunazotengeneza wenyewe. Serikali haiweki kodi kubwa kwenye magunia ili magunia yetu yatumike na wananchi wetu wapate ajira. Pia bado tunaitaka

Serikali iongeze bei kwenye mafuta ya kula toka nje ili mafuta yetu ya alizeti, mawese, nazi, karanga na kadhalika, mafuta mazuri kwa afya, yapate soko la uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii muhimu, kwa kuinua uchumi wa nchi yetu, pamoja na kutoa ajira kwa Watanzania, sambamba na kauli ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kutamka rasmi kuwa, ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia. Nawaombea Mwenyezi Mungu, awape nguvu, hekima, mshikamano, pamoja na maisha marefu ili waweze kutekeleza yote waliyoyaandaa kwa lengo la kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, kwa moyo wake wa uzalendo kwa Wananchi wa Singida, kwa kukubali kutuletea mwekezaji wa kujenga kiwanda cha kusafisha mafuta ya alizeti ili yaweze kuingia kwenye soko la ushindani duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sasa mtani wangu, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, aniletee mwekezaji, kwani Mkuu wa Mkoa anasubiri kwa hamu kubwa, pamoja na Wakulima wa Zao la Alizeti Singida.

Vile vile kijana mzawa ambaye tayari amefunga mashine ndogo ya kusafisha mafuta ya alizeti, pamoja na wengine Mkoani Singida, utawasaidia ni wapi wanaweza kupata mikopo ili waweze kujenga kiwanda kikubwa cha kusafisha mafuta ya alizeti ili kuwasaidia wakulima na wafanyabiashara wa Zao la Alizeti, mafuta yao yaingie kwenye Soko la Kimataifa na kuinua uchumi wa nchi. Ninategemea mtani wangu wakati wa majumuisho atatamka ni lini atakwenda Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitampongeza Meneja wa SIDO Mkoani Singida, kwa kazi nzuri anayofanya ya kutoa elimu mbalimbali kwa wajasiriamali, wakiwemo wanawake ili waweze kujua miradi ya kuwekeza na mambo mengine yanayolinda umoja wao na utunzaji wa fedha ili miradi yao isianguke. Vile vile namshukuru jinsi anavyotoa mikopo kwa wanawake wajasiriamali, yenye riba nafuu.

Ninaiomba Serikali itambue juhudi za Meneja huyu mwanamama na imwongezee fedha ili wateja wake ambao ni wengi sana, waweze kunufaika. Nasubiri jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli soko huria ndilo linatumika kwa mazao mbalimbali kuuza mazao yao. Pamoja na ukweli huo, sasa mafuta ya alizeti ni zao kubwa sana na mafuta ni mengi sana. Hivyo, kuna kila sababu Serikali kuwapatia soko la kudumu wakulima wa zao hili la alizeti kuliko soko huria, halina tija. Wafanyabiashara wa mafuta ya alizeti na wakulima, wawe na uhakika na soko la zao hili. Ninasubiri majibu ya Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na mtani wangu ama mwanagu Mheshimiwa Dkt. Chami, Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina matumaini kila mtu anaelewa kuwa Zao la Mkonge linalimwa katika mikoa mbalimbali hapa nchini; mfano, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro na kadhalika. Vile vile ni zao ambalo lilikuwa linaiingizia nchi yetu fedha nyingi za kigeni, kwa kukuza uchumi wa nchi. Pia ni zao ambalo lilikuwa linasaidia sana wakulima wa mazao mengine, kupata magunia ya katani kwa kufungia mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba ya Mkonge pia yalisaidia sana, tangu zamani hadi leo kutoa ajira kwa watanzania wengi katika kulima na kukata mkonge, jambo ambalo linaungana na hoja ya Mheshimiwa Rais kutoa ajira. Hivyo, kuna kila sababu zao hili kuendelea kulilima kwa maslahi ya nchi yetu, kuinua uchumi wa nchi, vipato vya Watanzania na ajira kwa Watanzania. Napenda kujua Serikali bado inalitambua zao hili mpaka leo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuielezea Serikali kuwa, kuna dalili kubwa sana za kuua Zao la Mkonge kwani sasa hivi magunia ya katani hayana soko kabisa, baada ya Serikali kupitia Bodi ya Kahawa kuruhusu soko la mifuko ya Jafafa (Jute Bags) kwa kufungia Zao la Kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifuko hii ya Jute Bags hutengenezwa nchi za India, Bangladesh na Vietnam. Wenzetu wa India, Serikali yao ilishatoa tamko kuwa ufungaji wa zao lolote, lazima itumike mifuko ya Jafafa (Jute Bags) na si vinginevyo. Hivi sisi tunaruhusu mifuko hii kutumika Tanzania kufungia mazao yetu kwa maslahi ya nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuinua uchumi wa wenzetu na kuna uchumi wetu wa Zao la Mkonge, ambalo pamoja na matumizi mengine, inatengeneza magunia ya katani. Zao la Mkonge ni kweli limesababisha ajira nyingi sana kwa Watanzania, kuanzia kwenye mashamba hadi kwenye viwanda; zaidi ya Watanzania laki tatu watakosa ajira endapo tutaendelea kuagiza Jute Bags. Vile vile kuna taarifa zinazosema kuwa, Jute Bags zinaharibu Zao la Kahawa, kwani mifuko haina nafasi ya kuingiza hewa, hivyo kahawa inavunda na soko lake kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba mtani wangu, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, kwa kutambua uwezo wake, umahiri wake, upendo wake kwa nchi yake na wanawake ambao wengi ndio walioajiriwa kwenye viwanda hivi vya TPM, ambapo sasa cha Moshi kimefungwa na cha Morogoro karibu kitafungwa, atatumia nafasi aliyopewa na Serikali kuwa ana mamlaka ya kutoa kauli mbili; kauli ya jumla; na kauli maalum.

Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, kwa kushirikiana na Waziri wa Kilimo na Chakula, watoe azimio au kauli maalum, kunusuru Zao la Mkonge na Viwanda vya TPM, ambavyo wananawake wengi wataathirika.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwomba mtoa hoja kuwa, nchi yetu inapaswa sasa kuondokana na adha potofu ya kukumbatia na kulinda bidhaa toka nje ya nchi, badala ya kulinda soko la ndani ya nchi, kwa ajili ya maslahi ya nchi na wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni wapi hapa duniani nchi inaenzi wageni badala ya kuwawezesha wananchi wake kiuchumi na kuwaendeleza? Leo hii mashamba yetu ya katani na viwanda vinakufa huku Serikali inaangalia tu.

Tunaruhusu kuingiza magunia ya jute kwa wingi na kupelekea mashamba ya katani na wananchi (wakulima), kuwa pamoja na viwanda kufa.

India na Bangladesh wajanja; marufuku matumizi ya magunia kutoka nje ya nchi zao. Licha ya kulinda viwanda vyao, pia zinatoa ruzuku kwa viwanda vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia Hotuba ya Viwanda na Biashara, Bunge lako lipitishe azimio la matumizi ya lazima ya magunia ya katani, kwa kufungia na kusafirishia mazao yetu yakiwemo kahawa, mahindi, cacao, kunde na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono tu pale azimio hili la Bunge litakapopitishwa kwa masilahi ya Taifa.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kutoa mawazo yangu kuhusu hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa umahiri wake mkubwa ambao anauonesha. Hivyo basi, nathubutu kusema akina mama tunaweza.

Pia napenda kumpongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Chami, kwa kufanya kazi bila kuchoka. Napenda kusema kwamba, Wizara ya Viwanda ni muhimu sana tena sana, hasa kwa ajira ya vijana wa Kitanzania walio wengi, pia biashara ni muhimu kwa wakulima wetu hapa nchini. Hivyo basi, kwa kuwa mwaka huu pamba imeshuka bei, lakini kama tungekuwa na viwanda vya kutosha katika nchi yetu ni ukweli usiopingika, tungeokoa pamba yetu kwa kuingiza viwandani kwetu na kuzalisha nyuzi na hata nguo; hivyo, biashara isingeathirika sana na tungewapatia wakulima wetu biashara na kuokoa pesa ambazo kwao imekuwa hasara. Pia katika Mkoa wa Mwanza, tunazalisha matunda mengi sana kama mananasi, maembe, machungwa na kadhalika.

Hivyo basi, kama wajasiriamali wadogo wangewezeshwa mashine za gharama nafuu za kusindika matunda, biashara ingekua na wananchi hawa wangejipatia kipato. Kama Serikali ingeweza kujenga kiwanda cha kusindika matunda katika Mkoa wa Mwanza, basi ni ukweli usiopingika kuwa ni vijana wengi ambao wangepata ajira na kingeleta tija kwa vijana ambao wangepata ajira hiyo na kukidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jiji la Mwanza, kulikuwa na Kiwanda cha Ngozi, ambacho kilikuwa sambamba na Chuo cha Ngozi. Kiwanda kiliuzwa na sasa Chuo kinafufuliwa, kwa kauli ya Serikali kupitia kwa Waziri husika. Sasa basi, Serikali haioni busara kama kiwanda hiki kingefanya kazi ya ngozi hata kama kiliuzwa kwa watu binafsi? Tunaiomba Serikali ikifikirie upya Kiwanda hiki cha Ngozi Mwanza, sambamba na kukiimarisha Chuo cha Ngozi. Nawatakia kheri kwa kazi zenu za kila siku, lakini ufufuaji wa viwanda ndiyo mkombozi wa ajira kwa vijana na ndiyo uinuaji wa Taifa la Tanzania.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *gypsum* ya Itigi, bao haina soko la uhakika. Ununuzi wa malighali hii ni kitendawili bado. Shughuli hii inaonekana kuendeshwa kiholela na wafanyabiashara wa nje na ndani huku wakiwanyonya wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa viwanda visiagize *gypsum* nje na badala yake wanunue *gypsum* nchini, ni uamuzi wa busara sana. Je, Wizara imehakikisha kuwa maagizo hayo ya Rais yanafuatwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Saruji, kwa muda mrefu nimeishauri Serikali isaidie kupata wawekezaji watakaoweza kufungua Kiwanda cha Saruji Itigi kutokana na kuwepo kwa malighafi ya *gypsum* na *lime*. Japokuwa chokaa *(lime)*, ni kidogo Itigi lakini kuna chokaa ya kutosha eneo la Ugwandi (Wembere) ambako si mbali sana na Itigi kunakopatikana *gypsum* kwa wingi. Serikali haijatusaidia kukamilisha utafiti na pia kuwashawishi wawekezaji kufika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara za Mawaziri wa Viwanda kuja Itigi zimeshindikana tokea nyakati za Mheshimiwa Chibulunje. Kila ziara zinapopangwa zinakuwa-*aborted* na hivyo Wizara kubakia na taarifa za makaratasi tu bila kujionea hali halisi. Itigi kuna kiwanda cha chaki na *POP*, kiwanda cha kusindika alizeti (tani 30 kila siku), (jumla ya viwanda vya kusindika alizeti ni vitano, Kiwanda cha mbao na machimbo ya jasi *(gypsum)* na kuna umeme wa grid ya Taifa.

Huduma mbalimbali za kijamii zinapatikana. Pia kuna kiwanja cha ndege na reli ya kati na barabara za kwenda Tabora, Mbeya, Singida na Dodoma. Kutofika kwa Mawaziri eneo muhimu kama hili, ni dhahiri kunafifisha juhudi za Mbunge na wananchi wa Jimbo hili kutafuta maendeleo kwa kutumia raslimali zilizopo. Hivyo, mpokee lawama hizi kama changamoto kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna tija katika kilimo kwa sababu hakuna nyenzo za kuchagiza kilimo. Kiwanda cha *UFI* kilishakufa na hivyo ongezeko la majembe ya mkono na ya kukokotwa na mifugo limedorora. Mchango wa Wizara hii kwenye sekta ya kilimo, hautatosheleza na hivyo kauli mbiu ya "Kilimo Kwanza" ya kutegemea *power tillers* na matrekta kutoka nje, ni kujidanganya kwa sababu wananchi wetu hawana uwezo wa kuyaendesha na kuyatunza na hivyo hufa mapema. Napendekeza upatikanaji

mkubwa wa majembe ya kukokotwa na ng'ombe kama vile Zimbabwe ili kuchagiza kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko kwa mazao mchanganyiko kama alizeti, dengu, hakuna, wakulima wanalanguliwa na hata mazao kununuliwa mashambani hata kabla ya kuvunwa. Nashauri chombo cha kusimamia bei za mazao haya kiundwe.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie katika hotuba hii ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. Napenda kumshukuru Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu kwa kuanzisha masoko maeneo ya mpakani hasa Wilaya ya Tarime ya Sirari, Borega, Nyamtura, Muriba na Kegonga. Kama tutakuwa na masoko, yatasaidia wananchi wa maeneo ya mpakani kuuza bidhaa na kuboresha biashara zote, hii itapunguza magendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna magendo ya ng'ombe kutoka Tanzania kwenda nje ya nchi lakini tutakapokuwa na soko la kiTaifa la ng'ombe litasaidia kupunguza biashara ya magendo ambayo hulikosesha mapato Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina wajibu mkubwa wa kuandaa semina kwa wajasiriamali ili waweze kufanya biashara kitaalamu. Wajasiriamali wanapaswa angalau wawe na elimu ya awali ya namna ya kutunza vitabu vya mahesabu na namna ya kutafuta masoko katika Mikoa na hata nje ya nchi. Wajasiriamali wawezeshwe kupata elimu ya kusindika matunda na kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya usindikaji. Naomba Wizara yako iendeshe semina kwa ajili ya wajasiriamali Jimboni kwangu, semina hii itasaidia wajasiriamali kupata faida kwa biashara zinazofanywa na kama unavyofahamu katika maeneo ya Jimbo, kumekuwa na mapigano ya mara kwa mara kuwepo kwa semina hii kutasaidia sana kupunguza na hata kumaliza ugomvi huo ambao husababishwa na umaskini uliopo kwa wananchi wetu, pamoja na wezi wa mifugo mpakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Awamu ya Kwanza, chini ya uongozi thabiti wa Mwl. J.K. Nyerere, Serikali ilianzisha viwanda vingi vya nguo ambavyo vilikuwa vinatumia pamba ambayo imekuwa ikilimwa hapa nchini hasa kwenye Mikoa ya Shinyanga, Mwanza na Mara. Serikali ilianzishwa viwanda, kama Mwatex, Mutex, Kiltex lakini mpaka sasa hakuna kiwanda kinachofanya kazi. Naishauri Serikali ifanye juhudi za makusudi kufufua viwanda hivyo ili wakulima wa pamba waweze kuuza pamba yao kwa bei nzuri katika viwanda hivyo na vyenyewe vizalishe na kuongeza pato la Taifa na kuongeza ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika Bungeni bila ya kushikwa mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, napenda kukupongeza wewe, Naibu Mwenyekiti, pamoja na wenyeviti wako kwa hisani yenu kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Wizara hii kwa hotuba yake nzuri ambayo imejaa matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inayoongozwa na Mheshimiwa Mary Nagu, ni Wizara mojawapo ambayo kama itawezeshwa vizuri, inaweza kuinua uchumi wa nchi yetu pia kumwezesha mwananchi kujiinua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walio wengi katika nchi yetu ni wakulima, eneo la uchumi wao ni hapa, kuwepo kwa viwanda na masoko nchini, kutainua hali zetu, kwani tutaweza kufanya biashara kupitia mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeipa kipaumbele Wizara ya Kilimo na kusema “Kilimo Kwanza” nini maana ya kilimo? Tukumbuke hivi sasa wakulima, mazao yao yanapotea kwa kutokuwa na viwanda na masoko. Sijui pale wakulima watakapoitikia wito wa Kilimo Kwanza, wakaweza kuzalisha mazao kwa wingi, yatapelekwa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda ni muhimu. Kufanikisha viwanda katika nchi yetu tunaweze kujikomboa katika umaskini. Tuangalie hasara inayowakumba wakulima wetu wakati wa mavuno ya mazao, kama vile machungwa, mananasi, maembe na kadhalika yanavyopotea. Hii ni kutokana na ukosefu wa viwanda na masoko. Tunamsaidia nini mkulima huyu ambaye tunataka apate maisha bora kwa kila Mtanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda katika Taifa hili ambalo kwa maumbile yake tulikuwa na viwanda vingi, ambavyo viliweza kukuza uchumi wa Taifa letu pia kutoa ajira kwa Watanzania, la kusikitisha mara tu baada ya viwanda vyetu kukabidhiwa wawekezaji, vimekufa. Tulikuwa na kiwanda cha Mwanza Textile, *Amboni Plastic*, *Bora Shoes,* Kamba Tanga Kange, Kamba Tanga Ngomeni na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni msiba kwa yule aliye na imani kwa nchi yake. Kuhubiri umaskini sio suluhisho, jema ni kujiuliza tunakotoka wapi na tunakwenda wapi. Viwanda vyetu hapa nchini viko wapi? Je, tunaweza kujikomboa kutokana na viwanda ama tumejizika hali tukiwa tuko hai? Nini hatima ya Taifa letu? Je, tumekuwa vipofu hadi tugonge ndio tujue tumefika? Sasa tumegonga, twaiomba Wizara itueleze ina mpango gani madhubuti wa kufufua viwanda vyetu? Kuua viwanda ni kuua ajira. Ni Watanzania wangapi ambao walikosa ajira kutokana na kufa kwa viwanda ndani ya nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona Serikali haijawa tayari kuikomboa nchi yetu kutoka katika dimbwi la umaskini. Fedha iliyotengwa ya shilingi 55,704,669,000/= haitoshi. Wizara ambayo imebeba makontena ya matatizo, unaipa fedha hii, si sawa na

kuchukua gunia la sukari ukasema nenda tia baharini ili maji yale ya chumvi yawe matamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mary Nagu, Naibu wake pamoja na timu yake iliyoandika bajeti hii. Naiombea Wizara ipate fedha hizi ili iweze kufanikisha azma yake ili kumkomboa Mtanzania.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda nchini ni muhimu sana. Pamoja na kazi nzuri ya Wizara hii, nina mchango ufuatao:-

Lipo eneo katika nchi yetu linaitwa Ludewa, kuna rasilimali ya chuma (Liganga) na makaa ya mawe Mchuchuma. Rasilimali hii ipo kwa muda mrefu sana lakini hatujaona maendeleo yoyote yakiendelea. Naomba kuuliza Mchuchuma na Liganga, uwekezaji wa viwanda vikubwa na vidogo utaanza lini? Mchuchuma na Liganga, wawekezaji wa ndani na nje wako wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo mengine katika Mkoa wa Iringa ambapo wananchi wanahitaji kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya uwashi. Je, Wizara itanisaidiaje kupitia Shirika lake la *SIDO* au mashirika yake kama *TIRDO*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 10, amesema hatua ya kupokea wawekezaji bora zinaendelea na ameleta mwekezaji wa kuzalisha chuma, *Sponge Iron* amepatikana na mchakato wa ubia kati ya mwekezaji na *NDC* unaendelea. Takriban miaka zaidi ya mitano sisi wananchi wa Ludewa tunaambiwa hatua zinaendelea. Niulize hatua hizo zitakamilika lini? Pia inatakiwa wapatikane wawekezaji wengi sio mmoja wa *Sponge Iron* na vilevile Wizara imejiandaa vipi na suala zima la miundombinu kama vile barabara/umeme eneo la uwekezaji?

**MHE. MUSSA AZAN ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi sana kwa *Fair Competition Commission* ambayo inafanya kazi kwa uadilifu na haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa magari nje ya nchi unatajirisha watu na Serikali haipati chochote na ukaguzi wenyewe haufanywi ipasavyo. Bora ukaguzi ukafanywa hapa na malipo yalipwe hapa, Serikali itapata mapato ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS* nayo inatakiwa kupima *lotion* na *cream* feki ambazo zipo kwenye maduka mijini na hasa Dodoma, mafuta mengi ya kupikia hayana viwango vya afya. Tunaomba *TBS* ifanye ukaguzi na kuthibitisha ubora wa *cooking oil* hapa nchini.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu biashara ya mpakani Kigoma na nchi jirani. Kwa kuwa moja ya dhima ya biashara, ni kuweka msukumo zaidi katika kutumia fursa za masoko, ni nini mikakati wa Wizara katika kujenga uwezo, mauzo kwa wafanyabiashara wa Kasulu na Kigoma? Wizara ingefanya utaratibu wa kuendesha mafunzo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ili wafanyabiashara wadogo wafahamu fursa zilizopo katika soko la *EAC* na

nchi kama *DRC*, Kongo. Nilishaomba kupatiwa mafunzo kwa wafanyabiashara wa Wilaya ya Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Wafanyabiashara *(NEDF).* Ninapenda Wizara inieleze tangu mfuko huu uanzishwe, ni wafanyabiashara wangapi wa Mkoa wa Kigoma na hasa Kasulu walionufaika na Mfuko huo? Je, Mikoa ya pembezoni kama Kigoma, ni kwa nini isipewe kipaumbele kwa kuzingatia *potential* iliyopo? Wafanyabiashara wa Kasulu, sasa wanafanya biashara kati ya Kasulu na Dubai na wengine wanasafiri hadi China. Ninashauri *strongly*, fursa ya mfuko huu basi uhudumie wafanyabiashara waliopo katika mji wa Kasulu ambao ni *very apprehensive.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kufikiria kuanzisha tawi la Chuo cha Biashara Kigoma. Kwa kuwa Mji wa Kigoma ni mithili ya Dubai katika nchi zetu za Maziwa Makuu na kwa kuwa Kigoma ni mji unaopakana na mipaka ya nchi nne, Zambia, (Ziwa Tanganyika) Burundi, Kongo DRC, Rwanda na kwa kuwa *potential* ya Mji/Mkoa wa Kigoma, ni kubwa isiyotia shaka, ni kwa nini Wizara hii isifikirie kuanzisha tawi la Chuo cha Biashara Kigoma? Kimkakati, nchi itanufaika na wafanyabiashara watapata chombo cha kujifunza, kuongeza ujuzi wao na hata ku- *control border* trade ambayo ni kubwa sana, *give it a thought.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa za *RCC*, bado EPZ ya Kigoma inasuasua. Wizara isimamie upatikanaji wa fedha toka Hazina kama bajeti inavyoonyesha ili *EPZ* ipate msukumo wa haraka kadri inavyowezekana. Bajeti ya *EPZ* Kigoma ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, pamoja na wafanyakazi wa Wizara hii muhimu katika nchi, kwa jitihada walizoonyesha. Napenda niwapongeze viongozi wakuu wote wa Mashirika yaliyo chini ya Wizara kama *SIDO, BET, TBS, TEMDO, TRIDO, CARMATEC, SEZ/EPZ, BRELA, WEIGHTS & MEASURES, FFC,* Wakala wa Maghala, Mashirika yanayofanya kazi katika hali ngumu ya ufinyu wa bajeti na vitendea kazi. Pongezi nyingi sana na nawatia moyo waendelee kusonga mbele ili kuinua nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu unalenga katika mambo machache yafuatayo:-

Kwanza, teknolojia ya kutengeneza mitambo, magari na vifaa vingine kama bunduki. Tuna watu, kwa karama walizonazo au kusomea au vyote vile, wanaweza kufanya mambo haya mradi tu wakitiwa moyo, kuongozwa na kuwezeshwa. Mfano, watengenezaji wa magobore, napendekeza watu hawa wapatikane, tuwe na utaratibu wa kuwapa majukumu ili waendeleze teknolojia hiyo.

Pili, utengenezaji wa matrekta – *Carmatec,* napendekeza Wizara ielekeze juhudi zake hapa ili *Carmatec* wapige hatua na tutapata kampuni au watu binafsi watakaotamani jambo hili ili mwaka ujao tuwe na matrekta bora zaidi na mengi ikiwezekana wafungiwe mahali ili watekeleze jukumu hili.

Tatu, Nyumbu, hawa pia wanatengeneza magari, napendekeza Wizara isaidie wazalishe magari mengi zaidi. Napendekeza pia Wizara, ikishirikiana na Nyumbu, watengeneze gari la wazi ambalo litatumiwa na Rais (siku ya kuapishwa kwake) mwaka 2010, inawezekana. Nunua mali ya Tanzania, dhana hii haiwezekani kuanzia chini, *fashion* huonyeshwa na *star* na *star* wetu hapa ni Rais wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Stakabadhi za Maghala. Kwanza Serikali isaidie bodi hii kwa kuwapa/kuteua watendaji na pili elimu kwa umma ni muhimu sana. Ni dhana nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TBS, hawa wanafanya kazi nzuri, hata hivyo ipo changamoto ya kufanya vizuri zaidi. Ninayo habari kwamba Kampuni nyingi za ukaguzi huko nje zinamilikiwa na Watanzania. Huu ni uzalendo mkubwa na nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO*, Shirika hili kwa kiwango kikubwa, ndilo lenye uwezo wa kumfanya Mtanzania kufanikiwa kwa kuwa na kiwanda. *SIDO* Arusha wanafanya vizuri, maonyesho ya Saba Saba yalithibitisha hayo. Pia Wizara inatakiwa kuisaidia sana *SIDO*. Wizara ifanye juhudi za makusudi na za lazima kuhakikisha kuwa kila Wilaya inakuwa na viwanda vidogo vidogo. Hii inawezekana. Kama Wizara, Ndugu Laizer watatembelea Halmashauri zote na kuzungumza nao na kuzielimisha maana fedha za *DADPS* zinaweza kutumika. Hili napendekeza na kwa kweli nina uhakika Mch. Laizer, katika *SIDO* aanze na Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitakia Wizara na mashirika yake, mafanikio makubwa zaidi katika mwaka wa fedha 2009/2010.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji, kwa kufika siku hii na kuweza kutusomea hotuba ya makadirio ya Wizara. Wizara ya Viwanda, ina majukumu mengi na ni sekta muhimu sana katika kuliletea pato Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na kilimo cha zao la mananasi katika Kata ya Kiwangwa, Jimboni kwangu, hivi sasa Serikali haioni kama inawakatisha tamaa wakulima wa mananasi, machungwa, maembe na ndizi, kwa sababu kila mwaka mazao hayo huoza na kupata hasara?

Tatizo kubwa ni kwamba hatukuwatafutia mashine ndogo ndogo za kukamua matunda! Leo tunakunywa *juice* za nje lakini mkulima wa Tanzania, matunda yanaozea shambani! Kama Serikali inaona mzigo kuwatafutia mashine za kukamua *juice* kwa nini

isiwatafutie soko la uhakika badala ya kazi hii kuachwa kwa Wahindi wachache ambao kazi yao ni kumnyonya Mtanzania halisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkonge (Katani), Jimboni kwangu lipo shamba la mkonge Ubena, lakini Serikali kwa kuua soko la magunia, imesababisha kilimo kukosa tija, ajira kupungua na kupunguza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magunia yasipotolewa mwongozo na taasisi za kimaTaifa kuwa magunia ya Katani ni mazuri, lakini kwa ukiritimba wa watu wachache hapa nchini hawataki na kuona raha pato la Taifa kupungua, vijana kukosa ajira na kuua mashamba/viwanda nchini.

Badala yake magunia yanaagizwa toka nje, wakati pamoja na kodi ya 50% hakuna jipya, yanaingizwa kiholela, kuna ukwepaji ushuru na yanatofauti gani kama yangezalishwa kupitia zao letu la Katani hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nchi zimeweka sera ya kutunza viwanda vyake. Je, kwa nini Serikali kwa mujibu wa sheria isiamue kuanzia sasa ni marufuku kuruhusu magunia ya nje badala yake matumizi yawe ni kwa magunia yetu yanayozalishwa hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi dhana ya kilimo kwanza ipo wapi? Ajira kwa Watanzania ipo wapi? Hapo nyumba viwanda/mashamba ilikuwa inatoa ajira ya watu zaidi 120,000 na mapato zaidi 200 bilioni kwa Taifa na sasa ajira zimebaki watu 10,000 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, hivi Watanzania hatuoni haya? Hivi sisi hatuyajui haya au ni makusudi au kuna maslahi ya watu binafsi badala ya Taifa? Je, tuwataje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa uzima alionipa na kuniwezesha kuchangia bajeti iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masikitiko makubwa sana kuhusu viwanda vinavyouliwa kwa makusudi katika Jiji la Tanga. Tanga vilikuwepo viwanda vya Chuma, Mbolea, Plastiki, Blanketi na *Silk Saw Mills* na vingine vingi. Viwanda hivi vilifanya kazi kiasi cha kutoa ajira nyingi sana jijini humo. Leo viwanda hivi vyote vimekufa na vingine kuhamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha mbolea *(Tanzania Fertilizer Company),* mitambo yote imeuzwa na kupelekwa Minjingu. Kiwnda cha Plastiki cha Amboni,

kimeuzwa Dar es Salaam. Kiwanda cha Chuma *(Steal Rolling Mills),* kilichokuwa maarufu, nacho kimeuziwa mwekezaji ambaye ana kiwanda cha chuma Arusha kinachojulikana kwa jina la *Hansa Steel Rolling Mills.* Huyu mwekezaji badala ya kufanya kazi ndani ya kiwanda cha chuma cha Jiji la Tanga yeye kazi anayofanya sasa anahamisha vyuma vyote chakavu *(scrappers)* na zilizobakia ni *billet* na huenda muda wowote nazo zitahamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii anayo taarifa kuwa mwekezaji huyu *Deepay Hans* aliyewekeza kiwanda cha chuma, ameanza kazi ya kuhamisha vifaa mbalimbali vilivyomo kiwandani humo kupeleka Arusha? Je, Serikali haioni kuwa lengo lake sio kuwekeza ila ni kupata malighafi atakazozipata ndani ya kiwanda hicho ambacho kilikuwa maarufu kwa utengenezaji vyuma na misumari? Nchi inaangamia na wawekezaji hawana nia ya kuinua pato la taifa lengo ni kuliua pato letu. kama mkazi wa Jiji la Tanga, naomba serikali imzuie mwekezaji huyu kuhamisha mali zilizomo katika Kiwanda cha Chuma – Tanga. tanga inakufa, viwanda vinahamishwa, je, Tanga kunani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandishi haya makubwa ni msisitizo, tuoneeni huruma wakazi wa Jiji la Tanga na Mkoa kwa ujumla kwa kuondolewa vitega uchumi vyetu na kutukosesha ajira.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba Serikali iweke azimio makusudi kwa ajili ya matumizi ya lazima kwa magunia yanayotokana na zao la mkonge kwa ajili ya mazao kama kahawa kwa sababu ya ubora na uhifadhi wa kahawa kwa ajili ya *export* na *domestic markets* kama ilivyokuwa miaka ya 1970.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mwaka 1970, zao la mkonge lilikuwa na ajira kwa watu 200,000 na hadi leo, ni watu takribani 15,000 tu wanaajiriwa kwa njia moja au nyingine kwa zao hili, napendekeza kufuata mfano wa Bunge la India kwa kufanya *jafafa bags* zitumike kwa kuhifadhia mazao yote, kwa nia ya kuhifadhi na kulinda ajira, *(jute bags)* zinahusika na kulinda idadi kubwa sana ya ajira nchini India. Dhana ya kilimo kwanza, haitakuwa na maana kama hatutafanya kila tuwezalo kulinda ajira na kuendeleza zao muhimu la mkonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sasa mwaka 2009 mkonge unakadiriwa kuwa 13% ya kiwango cha mwaka 1970, ni dhahiri kuwa asilimia 92 ya zao hili litasaidia wakulima na wenye viwanda ndani ya nchi na kuendeleza zao la mkonge.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. C. Chami,Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote kwa kutuletea hotuba nzuri licha ya ufinyu wa bajeti, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza kwa majibu waliyonipatia siku si nyingi kuhusu maswali yangu kuhusu maeneo ya uwekezaji kule Wilayani Hai yaani

eneo la Kia na pale *Kilimanjaro Medicine Tools.* Ninaomba tuongeze kasi ili shughuli zianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongezeni kwa maonyesho ya Sabasaba yaliyopita kwani maandalizi yalikuwa mazuri na maonyesho kufana, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kinachoendelea katika miradi ya Liganga na Mchuchuma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kuna hatua gani za makusudi zinazochukuliwa kuwadhibiti wageni wanaofanya biashara/kazi ambazo wazalendo wangezifanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri pia udhibiti upande wa mizani/vipimo. BRELA wanastahili kupata ofisi zenye hadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona tunazidi kuagiza matairi ya magari na mitambo kutoka nje ilihali kuna kiwanda pale Arusha? Tumefikia hatua gani katika kufufua viwanda vya mjini Moshi ambavyo vimefungwa siku nyingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri tuongeze udhibiti katika ubora wa bidhaa zetu ili tuweze kushindana na bidhaa kutoka nje pia ili tuweze kuvilinda viwanda vyetu. Hapa ninawapongeza *TBS* na waongeze kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeza *SIDO* na kushauri kuitumia zaidi *SIDO* kwani kwa njia moja ndio itakuwa mkombozi wetu. Je, ule mpango wa *SIDO* wa kila Wilaya kuwa na zao lao la kichumi mfano Hai ni maziwa bado upo? Kama upo, umefikia hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa mawazo yangu, napenda kumpongeza Waziri mwenye dhamana kwa hotuba yake nzuri. Napenda pia nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote kwa kuwa na ushirikiano mzuri wa kuweza kuwapatia ushirikiano mzuri Waziri katika kazi za kila siku. Kutokana na hali hiyo, pamoja na hotuba kuwa nzuri, napenda kusema kuwa ninaiunga mkono hoja iliyoko mbele yetu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno yangu hayo, sasa napenda kutoa mchango wangu wa mawazo katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa makusudi mazima, Maofisa Biashara katika Wilaya na hususani Wilaya yangu ya Kibondo, wanafanya kazi katika mazingira magumu ya kutokuwa na usafiri wa kuaminika na kusababisha kutokusimamia majukumu yake kwa Wilaya nzima. Wilaya hii iko mpakani na nchi jirani ya Burundi, kwa hiyo, Afisa Biashara anatakiwa kuwa kiungo muhimu na hasa katika kuhamasisha ujirani mwema katika nyanja ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Biashara kutokuwa na ofisi zenye hadhi. Idara nyingine zinaendesha zoezi la kujenga ofisi za kudumu katika Wilaya kwa kusaidiwa na Wizara zake. Ninashauri kwa makusudi mazima, Wizara ipandishe hadhi ya watumishi wake kwa kutenga fedha za kujenga ofisi zenye hadhi katika Wilaya kama vile Wizara za Kilimo wanavyojenga ofisi zao nzuri katika Wilaya na hususani katika Wilaya ya Kibondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza *SIDO* kuongezewa uwezo wa kifedha kwa kuwawezesha kuwakopesha wajasiriamali wadogo wadogo wanaojiunga kwenye vikundi vya uzalishaji. Kwa mfano, *SIDO* Kigoma wameonyesha uwezo mkubwa wa kubuni mbinu ya kutengeneza mashine za kuzalisha bidhaa mbalimbali kwa kutumia uwezo mkubwa alionao kiongozi wa *SIDO* Mkoa. Wananchi wamependa sana ufundi huo lakini kutokana na kutokuwa na mtaji wa kutosha, inawawia vigumu kwenda sambamba na utaalamu kutokana na kutokuwa na mtaji wa kutosha. Uwezeshaji kwa *SIDO*, ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma unazalisha mawese kwa wingi. Ukamuaji huo unafanyika kienyeji. Ninaomba Wizara ijipange kujenga kiwanda cha kukamulia mawese katika Mkoa wa Kigoma. Ni dhahiri ukamuaji mawese unaofanywa na *SIDO* hautoshelezi kutokana na wingi wa uvunaji wa zao hilo katika Mkoa. Naomba Serikali ilipe kipaumbele suala hili.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Waziri, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na Naibu Waziri Dr. Cyril Chami, Katibu Mkuu, Joyce Mapunjo na wasaidizi wao wote katika Wizara kwa kuandaa bajeti yao vema na kuwasilishwa vizuri na Mheshimwa Waziri katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana niliomba Serikali katika utaratibu wa uperembaji wa viwanda vilivyo binafsishwa na kuingia ubia na wawekezaji kwa nia ya kuviendeleza kimtaji na ufanisi kiuzalishaji lakini vimesimama kwa kutofikia lengo aliloombea ubia mwekezaji, Serikali ifike katika Kiwanda cha Tumbaku kilichopo Songea ambacho kilikuwa kinasindika tumbaku na kuajiri watu wasiopungua 3,000 na kulipa kodi lakini toka walipoingia mkataba wa kuwekeza na kuendesha kiwanda hicho mwekezaji hajawekeza kama alivyosema katika mkataba na kwa maana hiyo ana *shares* zilizo batili 40% lakini wanaushirika wanashindwa kuendeleza kiwanda kwa kupata mwekezaji mwingine au kukopa sababu ya huyu mwenye *domant shares*, ambaye anaogopesha wenye nia nzuri kusaidia kiwanda hicho. Naomba tena Wizara ipeleke wataalam wakafanye uperembaji ili wawarudishie wakulima wenye 60% ya *shares* waendelee na utaratibu wa kukiendesha kiwanda hicho na wenye uwezo wa kukiendesha na vile vile kwa kuzingatia kauli ya Serikali ya kuweka mikakati ya kusindika mazao zaidi ili kuyaongezea thamani na pia kuongeza muda wa kuyahifadhi *(shelf life)* kabla ya kuuzwa. Vile vile viwanda vyetu vikiongeza usindikaji wa mazao, ajira itaongezeka kwa wananchi, aya 78 ukurasa wa 51.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali ipeleke wataalam wake, washirikiane na Bodi ya Tumbaku Tanzania ambao wanajua vizuri matatizo yaliyopo lakini wanategemea mkono wa Serikali Kuu ki–sheria ndio unaoweza kuokoa kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Kamati katika kuokoa na kulinda viwanda vyetu vya ndani kwani katika *process* ya kuhifadhi mazao yetu, magunia ni muhimu sana kwa hifadhi hiyo kuanzia shambani. Sasa magunia ya Katani yanashindwa na soko la *jute bags* toka India na Asia lakini kama tunaweza kusaidia kwa kuweka kodi ya juu kwa *jute bags* na kufuta kabisa kodi kwa *katani bags,* tutasaidia kilimo cha Katani, tutasaidia viwanda vyake na kukuza uchumi wa *sisal industries* hivyo kuongeza pato la Taifa. Naomba Serikali isikilize maoni ya Wabunge kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote, kwa kazi nzuri na hotuba nzuri iliyojaa uzalendo. Naomba nichangie mambo kadhaa katika kuboresha hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata fursa ya kutembelea viwanda vya ngozi vilivyopo Dar es Salaam na Pwani, nilishuhudia jinsi ngozi zilizokuwa zikisindikwa na kuuzwa nchi za nje zikiwa zimerundikana kwa kukosa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kama nchi yenye mifugo mingi lazima pia ina uzalishaji mkubwa wa ngozi. Inasikitisha sana kuona hatuna viwanda vya bidhaa za ngozi kama viatu, mikanda, *bags* n.k. badala yake tunapata bidhaa hizi kutoka nje ambazo nyingine hazina ubora. Nashauri kwa makusudi, jitihada za Serikali kushawishi wawekezaji kwenye uzalishwaji wa viwanda hivi zifanyike ili viweze kuzalisha na kuchukua soko hili ambalo litatoa pia unafuu wa bei kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la viwanda vya mbolea. Naipongeza Wizara kwa jitihada zilizoonyeshwa ukurasa wa 37 na 38 juu ya kulitafutia ufumbuzi suala la uzalishaji wa mbolea kwa kutumia viwanda vya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tulipokuwa tunazalisha mbolea kwa kutumia kiwanda chetu cha Tanga, wakulima waliweza kunufaika kutokana na kuipata kwa wakati lakini kwa bei nafuu. Naiomba Serikali kuongeza kasi juu ya ufumbuzi wa jambo hili muhimu ili wakulima wetu waweze kupata nyenzo hii muhimu kwa kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katani ni zao linalozalishwa na wakulima wengi hapa nchini, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha soko la bidhaa hii linakuwepo. Kitendo cha kuachia magunia ya nje kuingizwa kwa wingi nchini kwa bei ya chini ukilinganisha na ile ya katani, ni kitendo cha kuliua zao hili la mkonge na wakulima wanaolitegemea kukosa shughuli ya kufanya na Tanzania kukosa fedha za ndani na nje kwa zao hili kukosa soko kwa kuruhusu soko hili kuchezewa na bidhaa kutoka nje.

Naiomba Serikali kwa nia ya kulinda bidhaa zetu na mazao yetu kama ulivyosema mwenyewe Mheshimiwa Waziri alipokuwa anawasilisha hoja yake, ‘Nunua bidhaa za Tanzania na Ipende Tanzania’, naiomba Serikali iige mfano unaofanywa na maTaifa mengine katika kulinda bidhaa zao kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuipatia fursa hii.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu, nampongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu (Mb), Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko pia ninampongeza Mheshimiwa Dr. Cyril Chami (Mb), Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuiendeleza kisera Wizara hii ambayo ni Wizara muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuchangia mchango wangu ili kuiboresha Wizara hii kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya viwanda, ni sekta nyeti sana. Nchi zilizoendelea, sababu kubwa ya maendeleo yao ni kutokana na viwanda, viwanda ndivyo vinavyojenga uwezo wa Taifa kiuchumi, sekta ya viwanda ndiyo inayojenga uwezo wa soko na hivyo kujenga uwezo wa kimapato kwa nchi na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uchumi wa viwanda ina nguvu kubwa ya kuziingiza sekta zingine za uchumi katika mkondo wa uchumi wa kisasa. Viwanda ndio sekta kiongozi ya uchumi. Makakati uko vipi katika kuimarisha viwanda vya ndani kwa uzalishaji wa bidhaa unaotokana na kilimo chetu mfano mzuri viwanda vya usindikaji mbegu za mafuta, viwanda vya usagaji wa nafaka, viwanda vya kusindika matunda, viwanda vya uzalishaji kama vile Katani na kadhalika. Wizara inao mkakati upi katika kusaidia kulinda bidhaa za ndani zinazotokana na kilimo chetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiimarisha viwanda vya usindikaji, utakuwa umekuza uwezo wa mkulima kwa kuongeza juhudi katika kilimo hatua itakayoongeza nguvu kazi (ajira) kupitia mashamba na baadaye kazi viwandani na hivyo kuongeza pato la Taifa. Vivyo hivyo, katika viwanda vya usagaji nafaka, viwanda vya nguo zinazotokana na pamba, viwanda vya usindikaji wa matunda na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kuhusu katani, katika mazao ambayo ni *naturality* na zao ambalo lilishatoa ajira kwa kiwango kikubwa kwa wananchi. Mkonge ni zao la ndani ambalo tuna kila sababu ya kujivunia kwa kuwa na zao hili ambalo lina uwezo wa kutoa ajira kwa kila hatua linalopitia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iweje zao la Mkonge liuawe na uzalishaji wa bidhaa mbadala toka nje ya nchi? Mfano mifuko *(jute bags)* zinazoagizwa na kuingizwa nchini bila ushuru! Kufanya hivyo, ni kuviua viwanda vya nchini hasa vinavyozalisha magunia ya mkonge kadhalika ni kuua kilimo cha mkonge na kufanya hivyo itatoa fursa ya

kushusha kiwango na kuondoa kabisa uwezo wa ajira na kulifuta kabisa zao la mkonge nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa sera za CCM katika miaka ya 2000 hadi 2010, zinaeleza bayana hasa pale zilipoeleza juu ya kushugulikia ufufuaji wa viwanda vilivyopo nchini hasa vya nguo, ngozi, kanvas/gunia, usindikaji wa mazao ya kilimo, mbao, madawa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na maelekezo ya sera za CCM za 2000 hadi 2010, ni dhahiri hatua ya kuruhusu *jute bags* kuingizwa nchini zinapigana kabisa na sera za CCM. Namwomba Waziri na Wizara kwa ujumla ifikie hatua ya kulinda viwanda vyetu vya mkonge na kutoa maagizo ya matumizi ya gunia za mkonge kuhifadhia bidhaa mbalimbali zikiwemo nafaka. Kama vile kahawa, korosho, mahindi, *cocoa*, mikunde, maragwe, alizeti, ufuta, ulezi na kadhalika. Itashangaza sana mazao yanayolimwa nchini magunia ya kuhifadhia yatoke nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ili kutoa uzito wa suala hili, ni vema likawepo Azimio la Bunge ambalo litatoa maelekezo ili kuwa na ulazima wa kutumia magunia ya mkonge wa Tanzania badala ya matumizi ya magunia toka nje ya nchi. Kufanya hivyo, tutaimarisha sekta ya viwanda vya ndani na hivyo kutoa fursa ya ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Masoko, namwomba Waziri kupitia Wizara yake, pamoja na Serikali kujiondoa moja kwa moja katika usimamizi wa soko kutokana na soko huria. Pamoja na hali hiyo, upo umuhimu mkubwa wa kusaidia wananchi hasa wakulima wa zao la alizeti waliopo Iramba Magharibi kuwa na soko la uhakika hatua itakayowaongezea tija katika uzalishaji wa mbegu hizi za mafuta ya alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo na katika kufanya hivyo, kutaleta imani na matumaini ya wakulima wetu.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu ya wasaidizi wao wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Nagu, ni Mchapakazi hodari, hakuna asiyetambua jinsi alivyoongoza Wizara mbalimbali kwa umahiri na kiwango cha juu. Ninaamini Wizara hii sasa imepata mtu. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi yetu iweze kupaa kiuchumi, michango ya viwanda vidogo na biashara ndogo, ni chachu muhimu, lazima vipewe vipaumbele vinavyostahili kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Serikali chini ya Wizara hii, iandae mpango mkakati wa kuimarisha *SIDO*. Hii ni pamoja na kuiwezesha kutoa huduma za mafunzo kwa wajasiriamali Wilayani na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, *SIDO* iwezeshwe kifedha kufungua ofisi zake Wilayani. Lengo ni kuwahudumia vikundi vya wajasiriamali wengi waishio vijijini. *SIDO* kwa sasa haina uwezo wa kuendesha kozi kwa vikundi vya wajasiriamali wengi kutokana na uwezo mdogo wa fedha. Kwa mwaka 2009, *SIDO* imeweza kuendesha kozi 49 tu katika Wilaya za Rorya na Tarime kwa wajasiriamali wachache kutokana na ukosefu wa fedha. Katika Wilaya ya Rorya, kuna vikundi 240 vya wajasiriamali vyenye wanachama wapatao 5,000, wengi wao hawapati mafunzo. Naomba Wizara iandae programu maalum ya kuimarisha *SIDO* kifedha ili wanachama 5,000 Wilayani Rorya waweze kufaidika na mafunzo hayo ya *SIDO*.

Tatu, fedha za JK zinazopelekwa Mkoani kwa ajili ya kukopeshwa wananchi, fedha hizo sasa zipewe *SIDO* kusimamia na kuratibu mikopo kwa walengwa kuliko ilivyo sasa. *SIDO* inayo taaluma na uzoefu wa kuendesha mafunzo kwa wajasiriamali na uanzishwaji wa viwanda vidogo vya wajasiriamali vijijini. Fedha hizi zitatumika kwa ajili ya mafunzo na kuanzisha viwanda vidogo na kusaidia wafanyabiashara. Naomba ushauri huu uzingatiwe na kufanyiwa uamuzi wa busara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, pamoja na Wizara kuratibu maandalizi ya ujenzi wa masoko ya kimaTaifa katika maeneo mbalimbali ndani ya nchi, nashauri Wizara sasa ichukue uongozi na hatua thabiti kusimamia, kufuatilia na kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu ujenzi wa masoko katika vituo vya uhamiaji vijijini ili kupiga vita na kukomesha magendo yanayofanywa na wafanyabiashara wasiowaaminifu kwa kuvusha bidhaa na mazao yetu nje ya nchi hususan katika Wilaya ya Rorya.

Wananchi wanaomba Wizara iwe inaratibu kwa kuwatafutia wahisani wa nje, kuwapatia msaada wa ujenzi wa masoko ya kisasa katika vijiji vya Kogaja, Kirongwe na Sota mpakani na Kenya. Naomba wataalam wa Wizara kusaidia katika kuandaa andiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa hotuba nzuri na naunga mkono hoja kwa 100%. Wilaya ya Lushoto, ina uzalishaji mkubwa wa mboga na matunda. Suala la viwanda vya kusindika, bado ni kitendawili. Wizara/Serikali ina mkakati gani wa kujenga kiwanda cha kusindika matunda na mboga zinazozalishwa Wilayani humo ili kuokoa mazao hayo ambayo huharibika haraka kama hayakusindikwa haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote wa Wizara, kwa kuongoza Wizara hii pia kuondaa hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania yetu nzuri yenye mazao ya msitu, kilimo, mifugo, madini na kadhalika, tumeshindwa kabisa kulinda viwanda vyetu na kuinua hali ya uchumi wa Taifa na hali ya wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina wingi wa mifugo, ni nchi ya tatu Afrika baada ya Ethiopia na Sudani. Mifugo hii ambayo ni mali, mazao yake kuanzia maziwa, nyama, ngozi, kwato, tumeshindwa kuvichakatua kwa kuwa na viwanda makini ili mazao haya yaweze kuleta faida kwa Taifa. Mifugo hii inatosha kabisa kutoa malighafi kwa viwanda vya nyama, vya maziwa na vya ngozi lakini ni ajabu kwamba viwanda vyetu vyote tumeviua na hata vichache tulivyonavyo tunashindwa kuviendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumekuwa na wauzaji wa bidaaa za viwanda vya nje kwa mfano nguo, viatu, nyuzi, mabegi, maziwa na kadhalika. Kiwanda cha ngozi cha Kibaha kinaelekea kufa, kiwanda cha ngozi cha Moshi kimefungwa muda sasa. Tunasafirisha ngozi ghafi kwenda nje badala ya kusindika hivyo kuongeza thamani. Kwa wiki moja, zaidi ya makontena 20 – 40 yanaingiza mabegi kutoka Dubai, China na Uarabuni. Wanafunzi wa *Primary* tu, wanatumia viatu, idadi kubwa sana, wale wa sekondari ndio kibao, bado vyuo! Kama viwanda hivi vingewezeshwa vingetengeneza viatu vya kutosha wanafunzi tu, ni pato kubwa sana kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa zinazotoka nje ni za *low quality*, havina ubora wowote, vingi ni feki lakini tunalipia gharama kubwa kuvinunua wakati fursa ya kutengeneza *quality products* tunayo lakini hatutumii fursa hiyo. Tunaona bora tusaidie kuinua viwanda vya nje na kutoa ajira kwa watu wao!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilibinafsisha Shirika la Uwindaji TAWICO ambayo ilikuwa ni sehemu ya Kiwanda cha Kufua Nyara za Taifa, kwa mfano TAXADEMY, kiwanda hiki kwa Tanzania tunacho kimoja tu kwa ajili ya kufua nyara na kutengeneza bidhaa mbalimbali kutokana na bidhaa za wanyamapori na hivyo kuongeza thamani kwenye nyara hizo. Mwekezaji wa kiwanda hiki amebadilisha matumizi ya kiwanda na kukifanya ni karakara ya kutengeneza mabodi ya magari. Kitendo cha mwekezaji huyu kwenda kinyume na makubaliano ya mkataba na kubadili matumizi ya kiwanda hiki, ni kukosesha Taifa mapato kwani Taifa sasa tunaendelea kuuza ngozi ghafi nje na hivyo kulinyima Taifa fedha za kigeni na kudhoofisha uchumi wa nchi. Naomba Waziri alieleze Bunge, ni kwa nini Serikali inafumba macho kwa mwekezaji huyu kwa miaka yote huku Taifa likiendelea kupata hasara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekereka vya kutosha na wafanyabiashara kutoka China ambao wamevamia nchi yetu na sasa wanaelekea kuingia hadi jikoni? Kwa nini Serikali imenyamaza kimya? Wachina wameingia kwa *speed* kubwa na ya ajabu, wanauza hata maua, midoli hadi biashara za wamachinga wanafanya wao, hivi tunakwenda wapi? Vijana wetu wafanye nini? Tunataka waende kuvuta bangi mitaani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maduka mengi ya Kariakoo, ni ya Wachina wamefanya Tanzania ni soko la bidhaa zao tena wanaleta zile za hali ya chini na feki kwa kuona sisi tuna uwezo mdogo wa kununua *(low purchasing power)*, hivi kweli Wachina watuonaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusikubali nchi yetu kuwa *dump* la bidhaa feki na zile za viwango vya chini tuwe na *standard* za bidhaa zinazoingia ndani ya nchi. Ukienda

Kariakoo, kuna viatu hadi Sh. 1000 – 500/= ukivaa leo basi kesho sio kiatu. Kanga zinaingia nyepesi sana kwa bei chee, wanauza sana na hivyo bidhaa zetu hazipati soko pamoja na ubora wake huo. Hivi kweli tunakwenda wapi? Tutafika lini? Tubadilike, Serikali iamke, saidieni Watanzania, *we need standards.*

**MHE. ELISA DAVID MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya viwanda iko taabani na hivyo utendaji wa sekta hii hauridhishi. Viwanda vingi vya umma vinakabiliwa na uchakavu mkubwa wa miundombinu, pamoja na matatizo ya umeme wa mara kwa mara. Viwanda vya *General Tyre* na *Kilimanjro Machine Tools* vilivyoko kwenye Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, ni mfano mzuri wa matatizo niliyotaja hapo juu licha ya kwamba madhumuni ya kuanzisha viwanda hivi bado ni muhimu leo kama ilivyokuwa wakati wa kuanzisha viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa nchi yetu inaagiza matairi kutoka nchi za nje zikiwepo Kenya, Uchina na Uingereza. Aidha, bidhaa/zana za viwanda vilivyokuwa vinazalishwa na *Kilimanjaro Machine Tools* zinaagizwa nchi za nje pia. Ajira iliyokuwa inatokana na viwanda hivi viwili, imepotea. Wafanyakazi waliobaki *General Tyre*, wanalipwa bila kufanya kazi kwa kuwa kiwanda hakizalishi. Serikali itazame, ni jinsi gani viwanda hivi vitafufuliwa ili vichangiie katika uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya kuzalisha magunia ya katani viko hoi. Kiwanda cha magunia Moshi kimefungwa, hakuna uzalishaji na ajira 500 zinapotea. Kiwanda cha magunia Morogoro kinazalisha chini ya asilimia 20% ya uwezo wake wa kuzalisha. Kwa kuwa uzalishaji wa magunia ya katani umeshuka sana, nchi yetu imebidi iagize magunia ya *jute* yanayozalishwa India na Bangladesh. Hizi ni fedha za kigeni zinapotea ikiwa ni pamoja na kupunguka kwa ajira kwa wananchi wetu. Serikali ishaurike, kuwa na Sera ya Matumizi ya Magunia ya Mkonge ili kulinda viwanda vya hapa nchini pamoja na kulinda na kukuza ajira za wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, viwanda vya kusindika maziwa hapa nchini vimeshuka kutoka viwanda 33 mpaka 12 vilivyopo sasa. Idadi ya viwanda hivi imeshuka kwa asilimia zaidi ya 66%, hii ina maana kuwa maziwa mengi yanayotumika hapa nchini, yanatoka nje. Ni vizuri Serikali iwawezeshe wenye viwanda vya maziwa hapa nchini ili tuwe na soko la maziwa hapa nchini na hivyo kuokoa fedha nyingi zinazotumika katika uagizaji wa maziwa kutoka nchi za nje. Aidha, hii itakuwa ni mojawapo ya chimbuko la kuongeza ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nizungumzie baadhi ya viwanda vilivyobinafsishwa ili viendeleze madhumuni na malengo ya viwanda hivyo. Napenda nitaje viwanda vya *Bora Shoes* na *Tanganyika Packers Ltd*. Walionunua viwanda hivi, wameachana na malengo yaliyokusudiiwa kwa viwanda hivi. Licha ya kuacha majukumu ya viwanda vyenyewe; hakuna lolote linaloendelea. Ni vizuri Serikali itazame hali hii isiendelee.

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Suala la ujenzi wa soko la matunda la Kitaifa Segera, *surely its long overdue*. Soko hili lililopo, Jimbo la Handeni, litasaidia sana Kanda ya Kaskazini katika

kupunguza *wastage* ya matunda mengi yanayozalishwa. Wakati tukiendelea kusisitiza suala la *value addition* na *processing* ya matunda, *opportunity cost* ya kutokuanzisha soko husika ni kubwa. Wilaya imeshatoa eneo, *study* imeshafanyika, *why the delay*? Ninashukuru kupata kauli ya Wizara kuhusu ujenzi wa soko la kimaTaifa Segera, Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda ni muhimu sana kwa kuongeza thamani ya bidhaa zetu na kutunufaisha. Kukua kwa uchumi wa kilimo, mifugo, uvuvi na sekta nyinginezo, kunategemea sana kuwepo kwa viwanda na kuzalisha vifaa vinavyotakiwa na sekta hizi kwa ajili ya uzalishaji. Pia viwanda vinatakiwa kutengeneza bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo, uvuvi na kadhalika na kuongeza thamani ya bidhaa hizi na kuwezesha *primary producers* kupata faida kutokana na wanachozalisha. Wizara iandae mpango mkakati na mpango huo ubainishe viwanda ili kuendeleza kilimo, mifugo na mazao yake, samaki, mbao na bidhaa nyingine ghafi zinazozalishwa Tanzania. *Market infrastructure and facilities*, zikazaniwe kujengwa ili kuhimiza masoko yetu na kuwezesha nchi kunufaika na rasilimali na mazao ya watu wetu.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe shukrani za wafanyakazi wote wa *General Tyre*, kwa Serikali kuhakikisha wanapata mishahara yao ya mpaka mwezi wa Juni mwaka huu. Lakini tunasikitisha kwamba mpaka sasa hawa wafanyakazi wanalipwa bila kufanya kazi na bado haijulikani hatma yao ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kusikitika kwamba kiwanda cha *General Tyre* bado kimefungwa. Kwa miaka minne iliyopita kwenye kila bajeti, tulikuwa tunahakikishiwa kwamba Serikali itahakikisha kuwa *General Tyre* haifi. Pamoja na ahadi hizo za kutia matumaini lakini haionekani kama kiwanda hiki kitafufuliwa karibuni. Hatuoni kwa nini mkakati wa kufufua kiwanda hiki usifanane au usishughulikiwe kama jinsi Serikali inavyoshughulikia matatizo ya zile asasi au kampuni zilizoathirika kutokana na msukosuko wa kiuchumi ulimwenguni? Kwa nini hatua kama hizo hazikuchukuliwa na hazichukuliwi ili kuinusuru/kuifufua *GTEA* ili kiendelee, ni kiungo muhimu na mashamba ya *rubber* kwenye Mikoa ya Tanga, Morogoro na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali ina nafasi ya kufanya hilo. Kwa vyovyote vile kwa sababu Waziri wa Fedha wa zamani, Mheshimiwa Zakia Meghji, alikwishawahi kuja kiwandani na kuonana na wafanyakazi, napendekeza Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko aje kuonana na hawa wafanyakazi kuwaeleza kinachoendelea lakini kubwa zaidi kukubaliana na mikakati ya siku za usoni ili kuwepo na amani pale kiwandani, wote wanahitaji kushirikishwa kikamilifu. Wote wanahitaji kuondolewa hofu tuliyonayo kwamba kwa Serikali kushindwa kufufua kiwanda, ni

utekelezaji wa azma ya wenye viwanda vya matairi Kenya kuiua *GTEA* na kutugeuza sisi tuwe soko la matairi yao na ya nje ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovyote vile hasa kwa sababu Mwenyekiti wa Bodi amemteua lakini Bodi haijapata kukutana kusimamia mambo pale kiwandani kuna umuhimu wa Wizara kukutana na wafanyakazi ili kuweka bayana kwamba ni nani anayesimamia kiwanda wakati huu wa mpito? Nini kifanyike na hatma ya wafanyakazi pamoja na kukubaliana nao juu ya nafasi ya wafanyakazi wakati huu wa mpito. Hii napendekeza ifanyike haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBL* na *EABL*, taarifa ya Serikali ya nini kinachoendelea, inatakiwa.

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuandaa hotuba nzuri inayoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *SIDO*, ni shirika lisilo na mtando mkubwa nchini kwa suala la viwanda vidogo vidogo, hivyo nashauri shirika hili lipatiwe fedha za kutosha ili liweze kutoa mafunzo na huduma kwa Watanzania wengi zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona kwamba bado Serikali haifanyi jitihada mahususi ya kuondoa urasimu pale bandarini Dar es Salaam, katika Kitengo cha Kontena. Hivi sasa kuna mgomo wa wafanyakazi unaendelea, mizigo ya bidhaa mbalimbali zinachelewa kupakuliwa hivyo kuongeza gharama kwa wenye bidhaa na wenye meli. Urasimu huu ungetoka endapo Serikali ingeruhusu makampuni zaidi ya moja ili pawe na ushindani wa kupakia na kupakua bidhaa hizo. Changamoto hii isipofanyiwa kazi, watoa huduma za usafirishaji wataendelea kususia kutumia bandari zetu hivyo kuongeza gharama za usafirishaji wa bidhaa/mazao toka nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na maoni ya Kamati kuhusu umuhimu wa kuendeleza viwanda vya kusindika mazao yetu kwa sababu wakulina watapata ari kuzalisha zaidi mazao mengi na mazuri, itawezesha kuongeza thamani kwa mazao yetu, hivyo kupata bei nzuri ndani na nje, kuvutia soko kwa walaji wa ndani na nje kwa sababu kuna usemi wa “chema chajiuza, kibaya chajitembeza” na kupunguza kama sio kuondoa kabisa umaskini kwa wakulima wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadiriki kufikiria kuwa bado Serikali haiwasaidii wanaviwanda wa nchini kuweza kufanikiwa katika sekta ya viwanda, uwezesho ni mdogo hivyo kuzuia uzalishaji wa ajira nchini. Wakati umefika sasa kutoa upendeleo maalum na wa makusudi wa kuwainua wanaviwanda hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo mfupi, napenda kuunga mkono hoja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. C. Chami (Mb), Katibu Mkuu, mama Mapunjo na wataalam wote, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii ifuatilie tatizo la *TABOTEX* ambalo limechukua muda mrefu tangu tarehe 13/6/2009 na kusababisha kiwanda kufungwa. Mnamo tarehe 1/7/2009, kiwanda hicho kimefunguliwa kwa kurudisha wafanyakazi wachache na wale walioachwa hakuna maelezo ya kina, kwani kufungwa kwa kiwanda hicho ni kusababisha hasara kwa mwekezaji na pia kuathiri maisha ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wanapoingia nchini, ni vema wakapewa mwongozo wa ajira na taratibu za marupurupu ya wafanyakazi ili wanapopewa ajira hiyo wajue maslahi yao. Pia washirikishe Vyama vya Wafanyakazi, kwa kupewa taratibu za viwanda hivyo na mikataba ili panapotokea migomo iwe rahisi kutatuliwa. Kwani migomo huchangia sana kurudisha nyuma wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji/soko, ninaomba Wizara isaidie kutafuta wawekezaji kwa ajili ya usindikaji wa zao la asali, kwani Mkoa wa Tabora unayo asali nyingi na tamu, hata asali ya nyuki wasiouma wapo Tabora kwa wingi (nyuki wadogo wadogo). Tutafutiwe soko la asali hiyo, ipo Sikonge, Urambo, Uyui, kwa wingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itenge fedha ya kutosha kwa ajili ya *SIDO*, kwani ina uzoefu sana kwa maendeleo ya wananchi ambao wengi wao wanapata elimu kutokana na *SIDO*. Kwanza wana uzoefu wa kuendesha ulipaji wa mikopo na urejeshaji namafunzo ya wajasiriamali wengi hapa nchini hasa wanawake wamepata toka *SIDO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara ishirikiane na Wizara ya Fedha, kuhakikisha mfuko wa JK unapitia *SIDO*, kuliko *PRIDE*, kwani kwa kufanya hivyo, elimu ya urejeshaji itakuwa kwa asilimia kubwa. *SIDO* iendelee kutoa elimu hiyo hasa kwa kupatiwa vifaa kama vile mashine za aina zote ambazo zitamsaidia mkulima mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. WILLIBROD PETER SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Kiwanda cha *General Tyre* kilikuwa fahari ya Tanzania, chanzo kikubwa cha kukuza uchumi wa Tanzania na *tyre* zetu zilikuwa na ubora kuliko *tyre* za nje. Baada ya kubinafsisha, tulidhani ubora wa *tyre* na uongozi wa kiwanda ungeliongezeka, hivi Serikali inaweza kueleza tatizo gani hasa lililotokea hadi kiwanda hiki kufilisika na kufika hatua hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vipindi mbalimbali, Serikali imewekeza/kopesha kiwanda hiki jumla ya shilingi ngapi na ni kwa nini hata pamoja na jitihada hizo, kiwanda kikazidi kudidimia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunatafuta mwekezaji mwingine. Je, hiyo ndiyo njia pekee ya kuokoa kiwanda hiki muhimu? Ni kwa nini Serikali isifanye tathmini ya kina kutafuta *options* nyingine mathalani kutafuta fedha za kufufua na *management contract,* tukaingia na watu wa nje kama tatizo letu ni *skills,* Serikali haifanyi biashara kwa nini isiunde chombo huru cha biashara kwa vyombo hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wanahangaika kwa kukosa malipo muda wote, Serikali ina mpango gani kuhakikisha Watanzania hawa wanaoteseka na familia zao wanalipwa mara moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inazungumzia kumtafuta mwekezaji, je, imeweka utaratibu gani wa uhakika kuhakikisha Watanzania hawa wanapata mafao yao kabla kiwanda haijakabidhiwa kwa mwekezaji mwingine, iwapo itakuwa lazima kufanya hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nchi yetu ni *"Signatory"* wa *Coton Agreement* na hivi karibuni tumekuwa kwenye majadiliano ya *EPA* na wezetu wa Jumuiya ya Ulaya, je, nafasi yetu iko ndani ya *EPA* ya kikanda na Serikali inaweza kueleza ni manufaa yapi tumeyapata hadi sasa japo ni muda mfupi na mwelekeo wa makubaliano hayo ukoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa jarida la *ACP/EU*, inaonekana Tanzania hatujaweza kutumia vema fursa zilizoko kwa maana ya fedha za uwekezaji ndani ya mpango wa *EIB* na hata *quota* zetu za *exports* kwa nchi za *EU.* Yote yanaonekana ni matatizo yatu ya ndani, je, Serikali inasema nini kuhusu hali hii? Serikali ina mkakati gani ili fursa hizo adimu, pamoja na uchumi wa dunia kuporomoka, ni sababu zipi zinatufanya tusitumie fursa hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa baadhi ya matatizo yetu katika kushindwa ku-*export* mazao yetu mathalani ndizi, vitunguu, ni kutokuwa na *quality control standard* zinazokubalika kwenye masoko ya KimaTaifa na hata *packaging material*, Serikali inatoa kauli gani na au inachukua hatua gani ya makusudi kuondoa matatizo haya kwa lengo la kuondoa matatizo ya masoko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kutoa hotuba za mara kwa mara na safari za gharama kubwa za uhamasishaji, Serikali inasema nini kuhusu kutengeneza mazingira sahihi ya biashara ambayo yana tija zaidi kuliko hotuba kavu/tupu ambazo haziko *backed up* na miundombinu muhimu kwa biashara na masoko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu Serikali itatoa majibu ya kina, naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, natoa pongezi kwa Wizara, hususan kwa Waziri wake, Mheshimiwa Mary Nagu pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, kwa kazi yao nzuri. Lakini pia naomba nichangie mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa ya kina juu ya mradi wa chuma cha Liganga, kwa kuwa wawekezaji wa *Ngaka Tancoal Energy Ltd*. ambao wana ubia na *NDC* wapo tayari, umeme huo kwa kuanzia unaweza kulisha Liganga na kisha Mchuchuma na wako tayari kulisha kwenye gridi ya Taifa? Nauliza hivyo kwa vile sijui kwa undani mipango ikoje lakini najua uwezo wa *TANCOAL LTD*. ni kuzalisha 400MW, naomba kuelezwa juhudi zilizofikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tanzania kuwa soko la bidhaa tu, hivi kuna *strategies* zipi? Mfano ubia wa *TBL* na wenzao wa Kenya, wengine wawe huru kuleta bidhaa Tanzania, lakini Tanzania tusiwe na uhuru huo, si sahihi! Pia nimesikia kuwa Serengeti ina mpango wa kuuza Kiwanda chao kwa wamiliki wengine lakini kinachosikitisha wote wanaotaka kununua ni watu wa nje mfano Kenya, basi kuna hatari ya kudhoofisha *TBL* na kujikuta Watanzania tumebakia kuwa soko. Lakini hata hivyo, bia ya Serengeti ni *special brand* ambayo ina jina linalotangaza hata utalii wa mbuga zetu. Ni vema *brand* hiyo imilikiwe na Watanzania. Kwa kuwa Watanzania tuna hisa *TBL*, kwa nini *TBL* isipewe nafasi ya kwanza ya kununua? Uzuri wauzaji ni Watanzania na kwa kweli ni mali yao, lakini hata hivyo, ipo haja ya kulinda Utaifa na maslahi ya Watanzania bila kuwaathiri wamiliki hao ama sivyo ajira zitahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Kiwanda cha Matunda cha Korogwe, kina matatizo gani? Inasemekana suala hili lilifika mpaka kwa Mheshimiwa Rais wetu, kama ndivyo, kwa nini agizo la Mheshimiwa Rais halikutekelezwa? Yawezekana lina utata, basi tufahamishwe kulikoni ili kama kuna tatizo ambalo Mheshimiwa Rais hakufahamishwa au *misleading information* basi zielezwe, hatutaki maagizo ya Rais wetu kuchukuliwa kama ya mtu wa kawaida, si sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iwasiliane na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), ili kuona jinsi gani wanaweza kusaidia katika uwezeshaji wa wajasiriamali hasa wanawake *(scholarship).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, mimi nilikuwa mjumbe wa Bodi ya *TIRDO*. Wakati nafuatilia suala la kiwanda cha *TIRDO*, mtu mmoja wa ardhi alinijibu akasema utafuatilia mpaka utamaliza muda wako lakini hili halitafanikiwa, ni kweli, kumbe sababu anaijua, nadhani kwa lugha ya sasa tungesema ni tatizo la kukusudia. Swali langu ni hili, je, kwa sasa *TIRDO* imeshamaliza tatizo hilo la kiwanja? Naomba nijibiwe, kwani nisipopata jibu lazima nitauliza tena kwenye kifungu au mwongozo. Naishukuru *TIRDO* kwa kutuwezesha mafunzo ya uyoga Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii, kuvipongeza viwanda vyote, kwa ufanisi hasa kwa wakati huu ambapo dunia yetu iko kwenye misukosuko ya biashara, lakini viwanda hivi vina changamoto ambazo ninaamini kama Serikali itazifungia njuga, yanaweza kuondoka na hatimaye viwanda vyetu vikaleta ufanisi wa ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa matatizo makubwa, ni bei za umeme na upatikanaji wake siyo wa uhakika. Viwanda vyetu vingi na hasa viwanda vya nguo, huzalisha nyuzi lakini nyuzi hizi hazitumiki kwenye viwanda vyetu vya nguo. Kuna viwanda vya nguo hapa nchini, tunaagiza mafuta ya kupikia kutoka nje wakati kuna malighafi nyingi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni bandari yetu, kwa kweli kuna urasimu mkubwa ambao unasababishwa na Kampuni ya *TICTS*. Wabunge wengi wameliona hilo na nashauri kwamba kampuni hiyo ipelekwe Mahakamani ili mkataba wake upitiwe upya. Mkataba mpya utengenezwe ili Makampuni mengine yaweze kushindana na tuweze kupata ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na misukosuko hiyo ya kiuchumi, ninashauri Wakuu wa Mikoa wote, wapate semina ili Mikoa yao iweze kuendelea kiuchumi. Miji yetu mingi baada ya saa tano usiku hakuna biashara yoyote ile kwa kuogopa usalama wa watu na mali zao, lakini badala ya kuongeza ulinzi wanaamua kufunga biashara zote baada ya saa tano usiku. Huu naona si uamuzi mzuri wakati maamuzi mbadala yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tatizo la ndugu zetu Wachina, kwa kweli kama yamepita kwenye utaratibu uliowekwa, mimi sina pingamizi nalo na kama wapo baadhi yao ambao wanakiuka sheria za kuishi kwenye nchi yetu, ni vema vikahusishwe vyombo vya sheria badala ya kutumia vyombo vya habari. Nimeona hivi karibuni wananyanyaswa kwenye vyombo hivyo na hii ikiachwa kuendelea inaweza kuleta maafa kama ilivyokuwa kwa wageni waishio kule Afrika Kusini. Kihistoria, hawa Wachina, ni ndugu zetu wa kweli kweli, wamefanya mambo mengi mazuri kwa nchi yetu na hasa ukiangalia reli yetu ya TAZARA na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo, ninaunga mkono kwa mara nyingine, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema katika kipindi cha asubuhi, kwa kweli orodha ya wachangiaji ni kubwa sana na kwa vyovyote vile si rahisi kuwafikieni. Kwa niaba ya Meza hapa, niwaombe muwe na uvumilivu, wale wote ambao hamkupata nafasi siyo kwa sababu nyingine yoyote ile ni kwa sababu ya hali halisi ilivyo kwamba, inatakiwa tumalize jambo hili leo leo. Katibu kwa hatua inayofuata.

Aah! Mheshimiwa Naibu kwanza, samahani.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii adimu, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa baraka alizonijalia na kunilinda mpaka siku hii ya leo. Pia napenda niwashukuru wanafamilia wangu, kwa ushauri katika mambo mbalimbali na daima kunitia moyo wa kuendelea na jukumu la kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kwa namna ya pekee, nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa mipangilio yake mizuri ya kutimiza majukumu yake ndani na nje ya nchi hii. Haiba yake kwa ujumla wake, inathibitisha uwezo alionao wa kuwatumikia wananchi bila kuchoka na lengo kubwa ni kuwaondolea Watanzania kero mbalimbali. Mungu aendelee kumpa nguvu na busara ili utumishi wake ulio mfano kwetu uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kuwa daima kiongozi wa mfano wa kuigwa katika kumsaidia Mheshimiwa Rais katika majukumu yake bila kuchoka. Hii inadhihirishwa na majukumu mbalimbali anayotekeleza kwa ufanisi na hasa eneo la kulinda Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze na kumshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, kwa uongozi wake mahiri ndani ya Bunge na katika kutekeleza majukumu yake ya kiserikali kwa ujumla. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni mfano wa kuigwa kwa umahiri wake, pamoja na mambo mengine, kujibu maswali ya papo kwa papo, ambayo kwa hakika yameongeza ufahamu wa Wananchi wa Tanzania juu ya utendaji kazi wa serikali na mambo muhimu yanayogusa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kumshukuru Waziri wangu, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, kwa kunishirikisha vyema katika kuiongoza Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Aidha, namshukuru sana Katibu Mkuu, Joyce Mapunjo na Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Shaban Mwinjaka. Ushirikiano wa Viongozi na Wafanyakazi wote wa Wizara, unanirahisishia kazi zangu za kila siku katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii, ambayo ni muhimu sana katika kuhakikisha Watanzania wanakuwa na maisha bora zaidi kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba niwashukuru Viongozi na Wanachama wote wa CCM na Wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini, kwa ushirikiano wanaonipa mpaka sasa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo tulizojipangia katika kipindi cha karibu miaka minne sasa. Naomba ushirikiano huu uendelee ili tuweze kufikia malengo ya maendeleo tuliyojiwekea katika kipindi hiki, tukiongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekti, naomba kabla sijaendelea kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wangu, nitamke wazi kuwa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ambayo imezungumzwa na wachangiaji wengi ni ufinyu wa bajeti kwa Taasisi zilizopo chini ya Wizara, ikiwa ni pamoja na bajeti ya kwenda kwa TIRDO, CAMARTEC na TEMDO na watu wengi wanadhani kwamba, bajeti hiyo inapokuwa ndogo, majukumu yale hayatekelezwi vizuri na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, alizungumzia hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ni kwamba, katika mwaka huu wa fedha, Serikali imeongeza bajeti ya fedha za maendeleo kwa taasisi hizo. Aidha, Serikali itaendelea kuongeza uwezo wa kifedha wa Taasisi zilizoko chini yake kadiri bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Owenya alizungumzia kwamba, fedha zilizotengwa shilingi bilioni 55.7 hazitoshi kabisa kulingana na majukumu ya Wizara. Jibu ni kwamba, hapa Bajeti ya Wizara itaendelea kuongezwa kwa kadiri mapato ya Serikali yatakavyoruhusu. Ameendelea vilevile kusema kwamba, kutokana na mafanikio na mipango mizuri ya kutenga maeneo mbalimbali ili kuweza kuwezesha viwanda vya kusindika mazao, Kambi ya Upinzani inahimiza SIDO kutengewa fedha za kutosha ili kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, tunakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Owenya na tutaendelea kuiongezea SIDO uwezo kadiri mapato ya Serikali yatakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wafuatao; Mheshimiwa Dkt. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi na Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, wote wamezungumzia umuhimu wa SIDO kuongezewa uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yake hasa kupeleka maendeleo katika maeneo yao na maeneo mengine nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda kukiri hapa kwamba, ni kweli majukumu ya ujasiriamali ni makubwa kuliko uwezo wa SIDO, kwa mfano chini ya Mfuko wa NEDF, maombi yaliyopokelewa yalikuwa 124,368, yanayohitaji jumla ya shilingi bilioni 58.3, ukilinganisha na uwezo wa Mfuko wa shilingi bilioni 3.75, sawa na asilimia 6.4.

Wizara inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, ambayo ndiyo inayosimamia Mfuko huu, kwa nia ya kuiwezesha SIDO kupata fedha kutoka Mfuko huo kwa ajili ya kuendeleza ujasiriamali.

Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mbunge wa Rorya, alishauri Serikali chini ya Wizara hii iandae Mpango Mkakati wa kuimarisha SIDO na hii ni pamoja na kuiwezesha kutoa huduma za mafunzo kwa wajasiriamali wilayani na vijijini. Ushauri huo tumeupokea na tutautekeleza kadiri bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili kubwa ilikuwa ni uendelezaji wa viwanda. Hoja hii imechangiwa na Wabunge wengi wa kwanza kabisa ni Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Dkt. Willibrod Slaa, Mheshimiwa Arch. Fuya Kimbita, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa na Wabunge wengine, kwa ujumla walizungumzia kwamba, Serikali ieleze hatima ya kiwanda cha magurudumu cha Arusha mpaka wakati huu ambapo hatima ya kiwanda hicho cha *General Tyre* hadi sasa hivi haijafahamika na Waheshimiwa Wabunge hawa wanahitaji ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi ufuatao; kwanza kabisa, Kiwanda cha *General Tyre* kinamilikiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 74 na Kampuni ya Continental AG kwa asilimia 26. Uzalishaji wa matairi umekuwa unatumia alama ya biashara, yaani *trade mark* ya *General* inayomilikiwa na mbia mwenza, ambayo ndiyo Kampuni ya Continental AG, chini ya Mkataba wa Menejimenti, Mkataba wa Alama ya Biashara na Huduma za Kiufundi, maana yake hapa ni kwamba, mwekezaji mwenza ndiye atashughulikia mambo yote matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu ulikwisha muda wake mwezi Juni, 2007, ili kuuongeza muda majadiliano yalianza wakati huo kwa mawasiliano ya maandishi na baadaye ana kwa ana mwezi Julai, 2008, katika majadiliano ya ana kwa ana ilikubalika kuwa, *Continental AG* watoe maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, endapo mpango wa biashara ulioandaliwa na Kampuni ya *General Tyre* ni mpango unaoweza kufanya kazi *(viable)* na kama siyo *viable* watoe ushauri wa nini kifanyike wakiwa kama ndio wanaohusika na menejementi. Pili, wapendekeze jinsi ya kulipa madeni ya *General Tyre*, ambayo yalikadiriwa kufikia Dola za Marekani milioni 20 kufikia Desemba, 2008. Tatu, washauri njia bora ya kutekeleza mpango wa biashara wa *General Tyre.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya Continental AG kujibu hoja zilizokubalika katika majadiliano walitoa masharti yafuatayo; Sharti la kwanza, walipwe deni la Dola za Marekani milioni 3.321, kabla ya kusaini Mkataba wa kuiwezesha *General Tyre* kuendelea kutumia alama ya biashara ya *General.* Hata hivyo, hawakueleza ni nani alipe deni hilo ukizingatia kwamba wao ndiyo walikuwa wanaendesha menejementi ya kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matairi ya *General Tyre* yatakayozalishwa yatauzwa nchi za Tanzania, Uganda na Burundi tu yaani tusiruhusiwe kuuza Kenya wala Rwanda wala maeneo mengine, hivyo masharti ya *Continental* AG yalionyesha wazi kuwa hawako tayari kufufua kiwanda bali wanataka walipwe deni lao tu. Ili kufufua kiwanda cha *General Tyre*, zitahitajika takriban Dola za Marekani milioni 28.984, kwa ajili ya kulipa madeni ambayo ni dola milioni 20.016, kufufua mitambo ambayo ni dola milioni 2.615 na fedha za uendeshaji ambazo ni dola milioni 6.353.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kiwanda kudaiwa jumla ya Dola za Marekani milioni 4.85 na mabenki ya nje ya HSBC na Sitbank, ambayo yalitishia kufilisi *General Tyre,* mwaka 2005 NSSF ilitoa mkopo wa Dola za Marekani milioni 10, ambao ulidhaminiwa na Serikali. Mkopo huu ulikuwa ulipe deni hilo na bakaa itumike kununulia malighafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukaguzi Maalum, yaani *Special Financial Audit* uliofanyika mwaka 2008, ulibainisha kwamba ufanisi wa kiwanda umeendelea kudidimia hata baada ya mkopo huo kutolewa. Ukaguzi huo ulionesha kuwa, mkopo huo

haukutumika kama ilivyokubalika kwa mfano; Dola za Marekani milioni moja zilitolewa kwa Kampuni ya *Debt Advisory International* kinyume na makubaliano.

Pili, Dola za Marekani milioni 3.048 zilinunulia malighafi bila kuwa na vithibitisho vya kutosha kuonesha manunuzi husika. Tatu, Dola za Marekani 368,569 zililipia deni la *Continental* kinyume na makubaliano. Nne Dola za Marekani 531,582 zilitumika bila maelezo. Tano, dola 121,663 ambazo ni bakaa hazina maelezo ya matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkopo huu ungetumiwa vizuri na menejementi ya kiwanda, kiwanda hiki kingekuwa kinafanya kazi. Kiwanda cha *General Tyre* kilisimamisha uzalishaji mwezi Septemba, 2007 kutokana na kutokuwa na fedha za uendeshaji. Niseme kwamba, Serikali imekuwa inalipa mishahara ya Wafanyakazi tangu Januari, 2008 hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufufua Kiwanda cha *General Tyre,* Serikali imekuwa ikiendelea na jitihada za kuhahakisha kuwa, kiwanda kinafufuliwa. Majadiliano na mbia, yaani Kampuni ya Continental AG kwa nia ya kuendesha Mkataba wa *General Tyre* ili kuendelea kutumia alama za biashara, kwa nia ya kukiwezesha kiwanda kupata mtaji na teknolojia ya kisasa yamefanyika na bado hatujafikia makubaliano hasa kutokana na masharti ya *Continental* ya kutaka walipwe deni hilo na yale mengine ambayo nimeyazungumza tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haiko tayari kulipa deni hili, kwani ni deni la kiwanda na sio deni la Serikali. Hata hivyo, kwa vile suala la Mkataba ni nyeti, inabidi tuhakikishe kuwa tunafikia muafaka wa aidha kuendelea na mbia huyu au kuzalisha matairi kwa kutumia alama ya biashara ya mbia mwingine. Serikali ina nia kubwa ya kufufua kiwanda hiki na ndiyo maana imeendelea kulipa mishahara ya wafanyakazi hadi sasa, pamoja na kurudisha mashamba ya mpira serikalini ili yatumike kuzalisha malighafi ya kiwanda husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa ni kuhusu Mradi wa Chuma cha Liganga na Makaa ya Mawe Mchumuma kwamba ni masuala tete. Mheshimiwa Arch. Fuya Kimbita, Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, walizungumzia suala hili. Majibu ni kwamba, miradi hii ni muhimu kitaifa hususan katika kujenga msingi wa maendeleo ya viwanda mama na upatikanaji wa nishati ya umeme wa kutosha na wa uhakika. Kwa kuzingatia umuhimu huu, Wizara haina budi kujiridhisha na kuhakikisha kuwa, inatekelezwa kwa ufanisi na kuleta manufaa kwa taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ilielekeza kuwa utekelezaji wake ufanywe kwa uwazi na ushindani. Zoezi la kufungamanisha miradi hii na kuitangaza kwa wawekezaji linaendelea, ambapo mpaka sasa makampuni 48 yamevutiwa na miradi hii na hivyo kuonesha nia ya kushindanishwa katika mchakato wa kupata wawekezaji. Zoezi hili linatarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha. Kuhusu miundombinu, umeme utawekwa na mwekezaji kutokana na mkaa wa Mchuchuma, ambapo barabara kutoka

Itonyi hadi kwenye maeneo ya mradi, imefungamanishwa katika Mradi wa Maendeleo wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna swali lingine hapa ambalo linauliza jitihada za kuyaongezea nguvu za fedha Taasisi za MDC na SIDO. Majibu ni kwamba, nimeshajibu wakati naelezea jitihada za Serikali na Wizara kuhakikisha kwamba, SIDO wanaongezewa fedha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Chirisant Mzindakaya na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, wametoa ushauri ufuatao: kwamba, Wizara ya Viwanda na Biashara na Serikali kwa ujumla, isisite kuingilia kati na kufanya maamuzi ya haraka haraka kwa madhumuni ya kunusuru viwanda muhimu kimoja au kisekta kwa uchumi wa nchi hususan vile vinavyoendana na utekelezaji wa Sera ya Kilimo Kwanza. Ushauri huu umepokelewa na utafanyiwa kazi. Vilevile kuna ushauri mwingine alioutoa Mheshimiwa Mzindakaya kwamba, Serikali iharakishe kutunga Sheria Mpya ya NDC, itakayokidhi mazingira ya uwekezaji kwa wakati huu na vilevile kutunisha mtaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Rasimu ya Sheria Mpya ya NDC imekamilika na ipo katika hatua mpya kupitishwa kulingana na taratibu za Serikali. Upo ushauri ambao umetolewa na Kamati kwamba, Serikali iweke miundombinu mapema ikiwemo umeme, maji, reli na barabara katika maeneo ya uwekezaji kabla ya kukaribisha wawekezaji. Majibu ni kwamba, Serikali itazingatia ushauri wa Kamati wa kuweka miundombinu na huduma muhimu katika maeneo ya EPZ na SAYS kabla ya kukaribisha wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine wa Kamati ni kwamba, Serikali itoe elimu juu ya umuhimu wa kuwekeza na kuwahamasisha wawekezaji wa ndani ili nao waweze kunufaika na faida itokanayo na mamlaka ya EPZ. Jibu hapa ni kwamba, mwitikio wa wawekezaji wa ndani katika Program ya EPZ bado ni mdogo. Serikali kupitia Mamlaka ya EPZ, imetenga fedha katika bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kuwekeza katika maeneo ya EPZ.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hoja ya Kamati kwamba, utekelezaji wa mpango wa Mini-Tiger 2020 umefikia wapi? Aidha, kwa nini ujenzi wa eneo la Mabibo umechukua muda mrefu? Je, itachukua muda gani wa maeneo 12 yaliyotengwa kwa ajli ya EPZ? Majibu ni kwamba, utekelezaji wa Mpango wa Mini-Tiger 2020 ulianza mwaka 2005 chini ya iliyokuwa Wizara ya Mipango Uchumi na Uwezeshaji na mwezi Februari, 2008 ulihamishiwa chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Mpango huu ulileta dhana ya maeneo maalumu ya wawekezaji, yaani *Special Economic Zones.* Mojawapo ya mikakati ya utekelezaji wa SAYS ni ujenzi wa eneo la Benjamin Mkapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi huu ulianza mwaka 2005 na ulichelewa kutokana na matatizo ya upatikaji wa fedha. Hata hivyo, ujenzi huo kwa sasa umekamilika. Aidha, Wizara inaendelea na mchakato wa kuunganisha mifumo ya EPZ na SAYS na kuanzisha mfumo unganishi wa *Economic Development Zones* (EDZ). Mamlaka ya EPZ kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, imeandaa mkakati wa kuyaendeleza maeneo 14 yaliyotengwa kwa ajili ya EPZ kwa awamu, maeneo haya

yataendelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi katika kipindi cha miaka 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja kwamba, Sekta ya Viwanda bado haitoi mchango stahiki katika Pato la Taifa. Aidha, ukuaji wa viwanda bado hauridhishi ukizingatia malighafi nyingi zilizopo nchini. Hii ni hoja ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Lucy Owenya. Ukuaji wa Sekta ya Viwanda umeongezeka kutoka 8.5 % mwaka 2006 hadi 9.9% mwaka 2008. Aidha, mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa, umeongezeka kutoka 9% mwaka 2006 hadi kufikia 9.4% mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili ni dogo kuliko ilivyotegemewa kutokana na uduni wa teknolojia zinazotumiwa, uhaba na uhafifu wa miundombinu, gharama kubwa na upatikanaji hafifu wa maji na umeme

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami. Sasa naomba nimkaribishe Mheshimiwa Waziri Dkt. Mary Nagu, kwa ajili ya kutupatia majibu kuhusiana na hoja zetu tulizochangia kwa kusema humu Bungeni na kwa maandishi. Mheshimiwa Waziri karibu sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge, bila kuonesha kuchoka wakati nilipokuwa nawasilisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara yangu. Napenda kuchukua fursa hii, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia kwa njia ya maandishi au kwa kuzungumza katika Bunge lako Tukufu, kwa madhumuni ya kuboresha utekelezaji wa malengo tuliyoyaweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kuwashukuru Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni, aliyemwakilisha Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara leo asubuhi.

Vilevile Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro na Mwenyekiti wa Kamati yenyewe. Napenda kurudia shukrani zangu za dhati kwa Msemaji Mkuu wa Upinzani wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Owenya, Mbunge wa Viti Maalumu na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja na michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kujadili Hotuba yangu, inaonesha nia thabiti ya ushirikiano wenu na Wizara yangu katika kuziendeleza Sekta za Viwanda, Biashara na Masoko na kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, hoja na michango mingi imelenga maeneo makuu yafuatayo: Maendeleo ya viwanda, viwanda vidogo na biashara; kuendeleza

biashara; kuendeleza masoko; usimamizi, udhibiti na ushindani; na mafunzo, utafiti na maendeleo ya teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Waheshimiwa Wabunge zaidi ya hamsini walichangia hoja wakati Mawaziri wakiwasilisha hotuba zao na wakati Waziri wa Fedha akiwasilisha Hotuba ya Bajeti na pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuwa anawasilisha na kujibu hoja yake. Aidha, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 14 leo walichangia hotuba yangu kwa kauli na Wabunge 66 walichangia kwa maandishi na wengine wengi wameleta michango yao hapa mwishoni, wataniwia radhi kama kuna mmoja ambaye nitakuwa nimemsahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ya Waheshimiwa Wabunge ni mingi na muhimu na inahitaji majibu ya kina, kwa muda mfupi nilionao nina hakika wataelewa. Kama sitapata nafasi ya kufikia hoja zote, napenda kuahidi kwamba, ninawahakikishia kwamba, Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia, nitawapa majibu ya kina kwa maandishi na vilevile nitapitisha kwenye ofisi yako kwa uhakika ili ijulikane kwamba nimekwisha wajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge waliochangia hoja yangu kwa kusema ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh, akimuwakilisha Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Lucy Owenya, Msemaji Mkuu wa Upinzani, Mheshimwa Abdisalaam Issa Khatib, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Dkt. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Dkt. Omari Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Hadija Al-Qassmy, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Ibrahim Muhammad Sanya, Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Issa Kassim Issa.

Walichangia kwa maandishi ni wengi, ninaomba niwataje kwa haraka: Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Dkt. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Mheshimiwa Mkiwa Kimwaga, Mheshimiwa Magreth Sitta, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatibu, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Damian Nsanzungwanko, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Nuru Bafadhil, Mheshimiwa Lazaro Nyarandu, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Mgeni Kadika, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Prof. Sarungi, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya na Mheshimiwa Elisa David Mollel.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Dkt. Willibrod Slaa, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Dkt. Guido Sigonda, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Halima Omar Kimbau, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa John Mamose Cheyo, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Dora Mushi, Mheshimiwa Felista Bura, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa John Bendera, Mheshimiwa Halima Mamuya, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Oscar Mukasa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, michango ni mingi na inaifanya Wizara yangu iwe imara zaidi. Michango ambayo vilevile haipo kwenye uwezo wa Wizara yangu peke yake, kuna Wizara nyingi zaidi lakini ninasimama hapa kwa niaba ya Serikali, kwa hiyo, nitajitahidi sana kuyajibu yale ambayo Wabunge wengi wameyaongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo ningependa kulichangia ni suala la kulinda viwanda vya ndani. Suala ambalo ni nyeti na muhimu kwa uchumi wa nchi yetu na kwa Waziri wa Viwanda. Haitakuwa vinginevyo, nakubaliana na Wabunge kwa moyo mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kulinda viwanda vya ndani, lazima mjue kwamba, tusiporuhusu ushindani ambao ni muafaka, viwanda vyetu havitakuwa imara. Kwa hiyo, tutavilinda na wakati huo lazima vikubali kushindana kusudi viwe tayari kwenda kushindana na masoko ya nje ya nchi, kwa sababu soko la ndani halitoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kulinda ni muhimu lakini suala la viwanda kuongeza tija na ufanisi na kupunguza gharama za uzalishaji ni muhimu, kwa sababu soko la ndani haliwezi kutosheleza uchumi wa Tanzania, inabidi twende kwenye masoko ya kikanda, inabidi twende kwenye masoko ya nje na kwa hiyo ni lazima ushindani uanze hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikirudi pamoja na kwamba, tutaruhusu ushindani, lakini kuna viwanda ambavyo ni nyeti. Viwanda ambavyo ni muhimu, hata WTO inaruhusu kwamba vilindwe na hasa kwa nchi ambazo zinahesabiwa kuwa zipo nyuma sana au *The Least Developed Countries*, ambazo Tanzania ni mojawapo; ni nchi ambazo ziko nyuma kiuchumi na kwa hiyo tusipolinda hivi viwanda, tutabakia nyuma bila kwenda kuungana na wenzetu walioendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuunganisha na hilo, naomba niongelee suala la magunia. Suala la kulinda viwanda ni muhimu kama nilivyosema na kwa hiyo suala la kulinda viwanda vya magunia na viwanda vingine, hasa hivi ambavyo vinatumia malighafi za ndani ni muhimu sana. Suala la kulinda viwanda vya saruji ni muhimu, suala la kulinda viwanda vya ngozi ni muhimu, suala la kulinda viwanda vya sukari ni muhimu na tutafanya hivyo kwa kutumia Sera ya Kodi au *Fiscal Policies*, ndio njia ambayo nchi nyingi zinatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile njia ya kulinda na kuimarisha viwanda vyetu hivi ni kwa Watanzania wenyewe kuamua kutumia bidhaa za viwanda vyetu. Watanzania wakiwa tayari kutumia bidhaa za viwanda vyetu, wala hatuhitaji kuvilinda na ndio kinachofanyika Kenya; Wakenya wakiona bia za Tanzania hawanunui kabla ya kununua bia za Kenya. Kwa hiyo, Watanzania tuige hivyo, kama nilivyokuwa nimewaasa leo kwamba, tutumie nguo na vyakula vya viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nililolisema, sisi tuna viwanda viwili vya Moshi ambavyo vina uwezo wa kuzalisha magunia milioni sita kwa mwaka ambavyo havifanyi kazi sasa hivi. Kiwanda cha Morogoro kinafanya kazi na kina uwezo wa kuzalisha magunia milioni 10 kwa mwaka. Hata hivyo, kiwanda hiki kinazalisha magunia milioni 1.5 kwa mwaka sasa hivi kwa sababu ya kutumia *capacity* ndogo. Kwa kuwa pengine soko halitoshelezi, kwa hiyo, rai ya Wabunge ina kila sababu ya kupokelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, magunia ya mkonge yanatumika zaidi katika kuhifadhi mazao mbalimbali. Sifa kubwa ya magunia ya mkonge ameisema vizuri sana Mheshimiwa Sanya na sina sababu ya kurudia, hasa nikizingatia kwamba, muda wangu ni mdogo sana. Matumizi ya magunia ya mkonge na hasa kwa sababu yanatokana na malighafi inayolimwa na wakulima wetu ni muhimu sana. Hapo awali magunia yalilazimishwa kufungiwa kahawa, korosho na karafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulazima huu ukaondolewa na Bodi ya Kahawa, sina uhakika kama na korosho wamefanya hivyo. Ndio maana nasema *mandate* yangu inaishia mahali, inaenda kwenye Wizara nyingine. Pamoja na kutambua umuhimu wa kulinda viwanda vya magunia, ninaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutakapotoka hapa, Serikali itakaa na kulitazama jambo hili kwa kina na ninataka niwaambie kwamba, kikao hiki tayari kimeanza. Sisemi hivi mnipitishie bajeti, isipokuwa nawaambia ukweli na wale wanaohusika wanajua kwamba, tuliwaita Wizarani tukakaa nao na wadau wengine wanaohusika na maongezi yetu yanaenda vizuri, tutafikia hatima nzuri ya kuweza kulinda viwanda vyetu na kuangalia yale mengine yote kwa mapana yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bidhaa za viwanda vyetu lazima liangalie gharama ya uzalishaji. *Management* iangalie viwanda ili kutumia rasilimali vizuri na wafanyakazi nao lazima watambue kwamba, lazima wafanye kazi kwa moyo, kwa bidii na bila migogoro isiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kuna pande mbili za shilingi katika kuongeza gharama za viwandani, suala la *Management* kutokuona mahitaji ya wafanyakazi halitakumbatiwa na Wizara yangu. Suala la wafanyakazi vilevile kuona kwamba, wana wajibu wa kuendeleza ajira na kuona umuhimu wa kutokimbilia migogoro, badala yake wajadiliane na *Management* na mimi nitahakikisha kila kiwanda kinakuwa na *Trade Union* ili masuala ya wafanyakazi yaweze kuongelewa kwa kina na *Management* inapaswa kusikiliza rai ya wafanyakazi, rai ambayo kwa kweli ni ya haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine viwanda vinataka vifanye *over time*, kwa sababu kuna *oder* kutoka nchi za nje, wafanyakazi wanapokataa maana yake wanahatarisha ajira yao. *Management* au Muwekezaji anapokuwa na faida, asipoona umuhimu wa kugawa faida ile kwa wafanyakazi, anafanya uwekezaji wake usiwe endelevu. Wizara yangu itasimamia hilo ipasavyo na itasimamia migogoro isiyokuwa na lazima. Nikiunganisha na suala la Kiwanda cha Magunia, ningependa kuongelea suala la TABOTEX.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TABOTEX inatengeneza nyuzi kwa kutumia pamba yetu. *Management* imewekeza fedha nyingi, wafanyakazi wana migogoro ambayo haiishi, wanashindwa kukaa kwenye meza moja. Napenda kuwaomba Wabunge ambao wameleta suala la TABOTEX kwamba, tutaanza kuliongea na *Management,* kuona mahitaji ya msingi ya wafanyakazi yatambuliwe na tutakaa na wafanyakazi kuona wanaacha migogoro ambayo siyo ya lazima, kusudi kiwanda kile kiendelee kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Nyuzi kina soko la kutosha ndani ya nchi na hata nje ya nchi. Kutokana na migogoro isiyokwisha, TABOTEX inazalisha chini ya kiwango ambacho kinaleta faida kwa kiwanda. Kwa hiyo, naomba nitoe rai kwamba, mazungumzo yaliyoanza yataendelea baina ya *Management* na Wafanyakazi. Wizara ya Kazi na Wizara yangu, zitashirikiana kuona kwamba, TABOTEX inaendelea kuzalisha kwa manufaa ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye suala la Bishara ya Kimataifa. Mheshimiwa Dkt. Willibrod Slaa, alijaribu kuniuliza kwamba, tuko wapi katika mazungumzo na Ulaya kuhusu Mkataba wa EPA? Mkataba wa awali ulitiwa saini ya awali na umetuwezesha kuwa na *duty free, quota free market* nchi za Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunauza bila kulipa *duty* na tuweza kuuza kiwango chochote tunachotaka. Katika Mkataba wa EPA, Ulaya inatafuta masoko kwetu na sisi tunatafuta masoko kwao, lakini uwezo wetu wa kutumia masoko ya Ulaya ni mdogo sana, kwa sababu miundombinu yetu bado ni duni na uwezo wetu wa kuzalisha bidhaa za kuuza Ulaya bado ni duni. Kwa hiyo, ndani ya Mkataba wa Ulaya, sisi Tanzania na Afrika ya Mashariki kwa ujumla, tunataka Ulaya ikubali kutuwezesha tuweze kutumia masoko ya Ulaya kama wao wanavyotumia masoko yetu.

Kwa hiyo, suala la ushirikiano wa kiuchumi na wa kimaendeleo, limetiliwa mkazo sana kwa upande wa Afrika ya Mashariki. Ulaya hawataki kuliweka hilo kwenye Mkataba na sisi tusipojadiliana vya kutosha na kuona hili limewekwa, maana yake sisi

tutakuwa soko la Ulaya na hatutakuwa na la kupeleka. Kwa hiyo, mpaka hapa tulipofikia, majadiliano yanaendelea kwa nia ya kuyamaliza, lakini suala muhimu kwa upande wetu ni kupata misaada ya kuweza kuondoa uduni wetu ili tuweze kutumia masoko ya Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la biashara ya sukari mipakani; viwanda vya sukari ni viwanda nyeti na muhimu kwa nchi yetu. Kwa hiyo ni moja ya viwanda ambavyo vinalindwa kutumia udhibiti na udhibiti huo unafanyika Wizara ya Viwanda na hasa Bodi ya Sukari. Kutokana na udhibiti huo, sukari inayoagizwa Tanzania ni ile tu ambayo haiwezi kupatikana ndani ya nchi ili kufidia ule urari kati ya ugavi na mahitaji ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wafanyabiashara wanapewa kibali cha kuagiza nje na mimi naona umuhimu wa wafanyabiashara wa mipakani na wao kupewa umuhimu wakati wa kuamua nani apewe vibali vya kuagiza nje, kwa sababu pengine inaweza ikarahisisha biashara kati ya nchi ambazo zinatuzunguka na sisi tunahamasisha biashara kati ya nchi jirani na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Capt. Komba alisema kwamba, majadiliano yanaendelea kati ya Wizara yangu na Wizara ya Kilimo, hususan Bodi ya Sukari, kuona kwamba wakati tunajaribu kutoa vibali na wale wa mipakani kwa utaratibu unaoeleweka, nao waweze kuzingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa vilevile kuongelea biasahara ya chuma chakavu. Chuma chakavu ni biashara ya ajabu sana, watu wamediriki hata kung'oa reli ili waweze kufanya biashara ya chuma chakavu. Kwa hiyo, umuhimu wa kuwa na utaratibu maalumu ni muhimu sana na kwa sasabu hiyo, Serikali ilikataza biashara ya chuma cha pua ambacho kinatumika katika miundombinu na mahitaji yake ndani ya nchi ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, biashara ya chuma inayokubaliwa ni kidogo sana. Pamoja na udhibiti huo, bado wafanyabiashara wasio waaminifu, wameendelea kung'oa miundombinu na kuendeleza biashara ya vyuma chakavu na kwa hiyo Wizara na Serikali, inakuja na Sheria kali ambayo itadhibiti biashara ya chuma kwa ujumla, kwa sababu biashara ya chuma cha pua inafanywa kupitia biashara ya vyuma vile ambavyo havina mahitaji makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inaonekana kwamba ni muhimu biashara ya vyuma vyote idhibitiwe na kwa hiyo muda si mrefu sheria hiyo itakuja. Suluhisho la kudumu ni lile la kuanza kutumia Chuma cha Liganga, hasa pale ambapo tumeshampata muwekezaji wa Mradi wa Kasi Mpya, tukianza kuvua chuma chetu basi tutakuwa na malighafi ya kutosha kwa ajili ya viwanda vya vyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, alisema kwamba, hakukuwa na uhusiano kati ya Hotuba yangu na Kilimo Kwanza. Nami naamini katika kila *para* niliyokuwa nimeizungumzia kwenye Hotuba yangu, nimeongelea umuhimu wa Wizara au Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Kilimo Kwanza. Kwanza,

kutokana na Viwanda, zana bora ndiyo zitapatikana, kutokana na viwanda pembejeo kama mbolea na dawa za kuua wadudu ndiyo zitapatikana. Mheshimiwa Spika, kutokana na Viwanda mazao ya kilimo ndiyo yatasindikwa na thamani kuongezwa. Kutokana na viwanda masoko ya mazao ya kilimo ndio yatapatikana. Kwa hiyo hili la viwanda kuwa na uhusiano wa karibu sana na kilimo, halina mjadala na ninyi nyote mmeweza kulielezea Bunge hili; nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lililobaki ni Wizara yangu kutumia fedha kidogo tulizopewa, kuona kwamba zinatumika kweli ili kufanya kilimo kiwe cha kwanza. Kadiri miaka inavyokuja na mapato ya Serikali yanavyoongezeka, nina hakika Serikali itaona umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Wizara ya Viwanda ili iweze kukifanya kweli kilimo kiwe cha kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuliongelea ni SIDO. Kama Wabunge walivyosema, SIDO ni mkombozi wa wanyonge. SIDO imewezesha Watanzania kuanzisha viwanda vidogo. SIDO imetoa elimu ya biashara kwa Watanzania. Kwa hiyo, Watanzania walio wengi sasa wameingia kwenye biashara ndogondogo. SIDO inatoa taaluma mbalimbali ya kufungasha bidhaa za viwanda vidogovidogo na katika kufanya hivyo, imewezesha bidhaa zinazotengenezwa na Wajasiriamali Wadogo kuweza kuuzwa hata katika masoko ya nje, hasa ya AGOA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la SIDO kupewa umuhimu na Serikali vilevile halina mjadala. Wizara yangu itaona kwamba, SIDO inapewa msukumo na inapewa msaada wa kila aina ili iweze kumuimarisha mjasiriamali wa Tanzania na kwa hiyo, suala la maeneo ya kufanyia biashara yamepewa kipaumbele na SIDO imeanza kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala ambalo limeletwa la kujenga viwanda kwa uwiano. Ili nchi yetu iweze kuendelea na kwa sababu nchi yetu ni tajiri kwa ardhi, kuna ardhi ya kulima na kwa ajili ya mifugo na vilevile tuna samaki, chini ya ardhi tuna madini mengi na hata na *gas* ipo, kwa hiyo, viwanda Tanzania vinaweza vikaanzishwa katika Mkoa wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la kuwa na uwiano katika kuanzisha viwanda kwenye Mikoa kama ya Shinyanga, Mwanza, Rukwa, Mtwara, Lindi nalo ni muhimu sana kwa sababu Wizara au Serikali imeshaondokana na jukumu la uzalishaji na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Serikali sasa ni kuhamasisha wawekezaji waende kwenye maeneo ya malighafi ya kutosha ili waweze kuwekeza huko; na kwa hiyo, itatoa kipaumbele katika kuhamasisha wawekezaji waende Shinyanga, Rukwa na Lindi ili malighafi zilizoko huko ziweze kuongezewa thamani na Tanzania iweze kupata manufaa ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ubinafishaji kusimamishwa na *POAC* ninalijua, lakini hii ni Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Pamoja na kuzingatia maagizo ya *POAC*, tunachojaribu kufanya sasa hivi ni uperembaji na kwa hiyo, tutakuwa tunaisaidia *POAC* kuona kwamba, ule upungufu uliojitokeza wakati wa ubinafishaji unazingatiwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Zitto Kabwe, anielewe kwa sababu nina jukumu la kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama changu na vile vile nina jukumu la kuzingatia maelekezo mbalimbali na vyote viwili vitazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna maeneo mengi sana ambayo nilitegemea Naibu Waziri angeweza kuyatolea maelezo, lakini kwa sababu ya muda mfinyu, basi kwa muda muafaka kama Wabunge watanikubalia, nitawapa majibu kwa maandishi, lakini kwa wale ambao wataona ni lazima sana kuwajibu, nitakuwa tayari kusimama wakati wa Kamati, lakini ninaomba msinifikishe kwenye *guilotine*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kurudia tena alichosema Mheshimiwa Naibu Waziri, kuhusu suala la *General Tyre* linaangaliwa kwa umakini sana. *General Tyre* ni moja ya viwanda ambavyo Serikali yenyewe inaona umuhimu wake, bahati mbaya mbia yule tuliyekuwa naye, wengi wanafikiri kwamba ana nia ya kuiendeleza *General Tyre*, lakini kwa kadiri tulivyofanya uchambuzi, tunaona kwamba, nia ya kuiendeleza ni ndogo sana hasa ukizingatia kwamba, alikuwa ametufungia ndani ya Tanzania tusiuze matairi Uganda na Kenya wakati katika Umoja wa Forodha tunapaswa kuuziana bidhaa zetu.

Vile vile matumizi mabaya ya fedha alizopewa, yanaonesha kabisa kwamba, hakuwa na nia ya kufufua kiwanda. Tulimpelekea *Business Plan,* tukitegemea kwamba, atarejesha majibu yake kutueleza yuko tayari sasa kufufua kiwanda kwa kutumia ile *Business Plan,* lakini mpaka leo hajatujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Serikali inaona umuhimu wa kuendelea kutengeneza matairi na hasa ukizingatia kwamba, tuna mashamba ya mpira, Serikali itafanya kila linalowezekana, kuona Kiwanda cha *General Tyre* kinafufuka kwa muda mfupi unaowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Machines Tools pia ni moja ya viwanda ambavyo sisi tunaviona ni muhimu sana. Kiwanda cha Kilimanjaro Machines Tools hakijabinafsishwa bali kimerudishwa chini ya *NDC*, nia ya kurudisha chini ya *NDC* ni kuona kiwanda hiki kinafufuka na tutajaribu kutafuta wawekezaji ambao ni mahiri, kwa sababu suala la kutaka *spare parts* ni muhimu sana ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache niliyoweza kusema kwa muda niliopewa, natoa tena rai kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa lile ambalo ni lazima sana kulitolea ufafanuzi, nitalijibu wakati wa Kamati, lakini majibu yote nitayatoa kwa kina kwa maandishi na kupitisha katika ofisi yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imetolewa na imeungwa mkono.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 44 - Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... Sh. 5.721,149,000

**MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina azma ya kuzuia mshahara wa Waziri, lakini kutokana na kauli aliyoitoa, kwa kumsaidia bado nasema kwamba, Kamati yangu ina azma ya kuleta Azimio la Bunge la kuitaka Serikali kuwa na Mikakati Mahususi ya kujenga bandari yetu ya ndani. Kwa hiyo, nataka kuliweka wazi hilo na hivyo naomba kutoa hoja kwamba hilo tutalitengeneza na kulileta Bungeni ili kuweza kumsaidia Waziri kujua ni mkakati gani aendelee nao. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Abdisalaam, tunaendelea.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa majibu mazuri. Mimi naomba maelezo kwamba, zamani tulikuwa na Tume ya Kudhibiti Bei na sasa tuna Soko Huria; je, hakuna chombo kingine ambacho kinaweza kudhibiti bei hasa bei ya saruji na mabati kwa sababu wananchi wanashindwa kujenga kwa sababu ya gharama kubwa ya vifaa vya ujenzi?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hoja ya Mheshimiwa George Lubeleje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wakati wa uchumi hodhi, tulikuwa na Tume ya Kudhibiti Bei, kwa sababu kwa kiasi kikubwa Serikali ndiyo iliyokuwa iko kwenye uzalishaji na iko kwenye biashara, bila ya kuwa na Tume hiyo ingeweza kuwaonea walaji. Baada ya sera ya nchi kubadilika na kuwa na uchumi wa soko, suala la udhibiti likawa halipo na inategemewa kwamba, soko ndilo ambalo litafanya bei zipangike zenyewe kutokana na ugavi na mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hivyo, Serikali iko pale kuona kwamba, inadhibiti na ndiyo maana nimesema kwamba, kazi ya Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Masoko ni kudhibiti na kuwezesha sekta binafsi ifanye kazi vizuri, lakini bila ya kuonea walaji. Kwa sababu kuna suala la kuhodhi uzalishaji wa bidhaa fulani na kwa hiyo Serikali ni lazima ione kwamba, kama kunakuwa na *monopoly*, basi inachukua

hatua ya kuagiza bidhaa kutoka nje ili kuvunja ile *monopoly* ya kiwanda ambacho kinazalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, nikichukua bidhaa kama saruji, mtakubaliana nami kwamba bei ya saruji ilikuwa juu sana na ilikuwa juu kwa sababu wakati ule uzalishaji wa bidhaa ya simenti ilikuwa chini, kuliko mahitaji yaliyopo. Mtakumbuka, Mheshimiwa Rais alizindua mtambo mpya pale Wazo na mwezi wa tisa ujao, Kiwanda cha Simenti Tanga nacho kinaongeza uzalishaji. Kwa hiyo, hivi karibuni tutakuwa tunazalisha simenti zaidi kuliko tunavyohitaji. Inawezekana tukauza simenti nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, unaweza ukakuta viwanda hivyo vikawa na uhusiano wa namna fulani wakaamua kupanga bei. Inapotokea vile, tuna chombo chetu kinaitwa *Fair Competition Commission* (*FCC)* na kama mambo yakizidi sana, wafanyabiashara au yeyote anayetaka anaweza kwenda kushtaki kwenye *FCC Tribunal*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuna vyombo vya udhibiti lakini inapokuja suala la bei basi tunaliachia soko. Hata hivyo, tunachokifanya ni kama vile nilivyosema, kutumia Sera za Kodi kuweza kuona kwamba, kama kuna uchache wa bidhaa ndani ya nchi, basi unatoa kodi ili bidhaa ile iwe nyingi kama tulivyofanya kwenye simenti. Sasa hivi saruji imeongezeka kwa vyovyote vile bei haitakuwa inapanda kama ilivyokuwa awali, lakini zaidi ya hivyo, tunahamasisha na viwanda vingine au wawekezaji wengine, ambao hawana uhusiano na hawa wa sasa ili waongeze uzalishaji wa bidhaa kama saruji. Hivyo hivyo kwa bidhaa nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchumi wa soko, hatuna chombo cha kudhibiti bei, bali tunaiachia soko na pale ambapo soko halifanyi kazi vizuri, basi Serikali inaingilia kupitia sera zake mbalimbali na sheria mbalimbali.

**MWENYEKITI**: Ahsante sana, sikutaja mwanzoni kwamba, nina orodha ya Waheshimiwa Wabunge 37 wanaotaka kuuliza. Kwa hiyo, nitaomba waulizaji na majibu yaende haraka ili angalau kila mmoja apate nafasi.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Nampongeza sana Waziri na Naibu wake, kwa namna wanavyojitahidi. Shida yangu ni tamko la Waziri au Serikali kuhusu *pre-shipment inspection* inayofanyika huko; ni lipi tamko la Serikali kuhusu hii hali tunayoilalamikia hapa ya *pre-shipment inspection*?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaombe radhi Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hili jambo la *pre-shipment inspection* hasa ya magari liliongelewa sana. Mimi sikupata muda wa kujibu hilo, naomba nitumie muda huu kulijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kufanya *pre-shipment inspection* ni kwamba, kwanza kuna umuhimu wa kufanya *pre-shipment inspection,* lakini kama

haifanywi ipasavyo ni jambo lingine. *Pre-shipment inspection* ni matakwa ya *WTO,* lakini hatufanyi kila kitu kwa ajili ya *WTO*.

Pili ni kwamba, usipofanya *pre-shipment inspection,* vitu vibovu vitaletwa Tanzania na sisi tutakuwa jalala na itakuwa *too late*; Mtanzania atakuwa ametumia pesa zake nyingi kununua na kuleta ndani ya nchi na gharama ya kusafirisha halafu uje uamue kwamba, bidhaa hiyo ni ya kuchoma moto. Mimi nafikiri athari hiyo ni kubwa kuliko kuacha *pre-shipment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama *pre-shipment inspection* haifanywi vizuri, nalichukua hilo na nimeshalichukua nitalifanyia kazi, tutaona itakuwaje ili tuweze kuwanusuru wafanyabiashara wetu wasipewe gharama ambazo siyo za lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sasa hivi watu wanatulalamikia sana, *FCC* inavyojaribu kuchoma bidhaa zao, wanasema kwamba wametumia hela nyingi. Fikiria tena mnavyolalamika kwamba, *pre-shipment inspection* haifai, inakuwa ni vigumu sana kuja kuona ni kitu gani Serikali ifanye. Nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba, kuna uwezekano kabisa *pre-shipment inspection* haifanywi ipasavyo, lakini umuhimu wa kuwepo ni kumpunguzia gharama Mtanzania, ambaye kwa bahati mbaya atanunua bidhaa mbovu halafu tuje tuzichome hapa Tanzania.

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, niliulizia kilichokuwa Kiwanda cha Ngozi cha Mwanza Tanneries.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kiwanda kile kuuzwa, kilibadilishwa matumizi na sasa hivi kinatumika kama *store*. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akanieleza nini kwa sababu Kiwanda hiki kiliweza kufanyiwa kazi na vijana wengi? Je, katika Sera ya Ubinafsishaji hili linaruhusiwa na kama haliruhusiwi Serikali inachukua hatua gani kuhusu Kiwanda hiki?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, kwa swali lake kuhusu Mwanza Tanneries. Kwa ufahamu wangu wa Sekta ya Ngozi, Kiwanda cha Mwanza Tanneries kilifanya kazi kidogo sana toka kianzishwe. Hata sasa kilibinafsishwa, lakini hakijaweza kufanya kazi vizuri. Kwa ujumla, viwanda vyote vya ngozi havijafanya kazi vizuri, kwa sababu ngozi yetu kwa kiasi kikubwa inatokana na ng'ombe ambao wanafugwa bila uangalifu na wafugaji hawajali bidhaa ya ngozi. Kwa hiyo, unakuta kwamba, ukisindika ngozi mia moja, pengine asilimia 25 ndiyo inayotoka vizuri na kwa hiyo gharama ya ngozi 100 inakwenda kwenye ngozi 25 na ukienda kuiuza nje, unakuta kwamba bei ya ngozi ya Tanzania ni kubwa kuliko bei ya ngozi ya nchi nyingine ambako ng'ombe wanafugwa wakati wafugaji wakijua kwamba ngozi nayo ni bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili hiyo, mwekezaji aliyenunua Kiwanda cha Mwanza ni sawa na yule aliyenunua Kiwanda cha Morogoro; alianza kufufua Kiwanda cha Morogoro na alifanya kazi nzuri, lakini mgogoro huu wa uchumi nao umefanya Mwekezaji yule naye atetereke sana. Kwa hiyo, sasa uwezekano wa kufufua Kiwanda

cha Mwanza Tanneries umekuwa na utata zaidi, lakini nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, tumeperemba viwanda vyote ambavyo vipo Mwanza na tumejaribu kuona upungufu na matatizo ambayo yanawakabili wawekezaji. Wale ambao wameacha kuvifufua kwa makusudi, tutawachukulia hatua na itabidi tukubaliane wote ndani ya Serikali kuhusu hatua hiyo, kwa sababu ukichukua hatua moja unaweza ukawakimbiza wawekezaji wote na kwa hiyo ni lazima tuifanye kwa uangalifu unaotakiwa.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nampongeza pia Waziri na Naibu Waziri wake, kwa maelezo yao ya kutia matumaini. Pamoja na maelezo hayo, nigusie suala la *General Tyre* Arusha.

Maelezo aliyoyatoa Waziri yanatia matumaini, lakini hayatofautiani sana na maelezo aliyoyatoa mwaka jana na pia hayatofautiani sana na maelezo ambayo tulikwishayapata kwa miaka mitatu mfululizo kutoka kwa Mawaziri waliomtangulia. Naibu Waziri alivyokuwa anatoa majibu yake, hayakutofautiana sana na maelezo yaliyotolewa siku za nyuma kama tumefika njia panda. Waziri haoni kwamba, kuna umuhimu sasa pengine wa kumshirikisha Mwenyekiti wa Bodi uliyemchagua kikamilifu na Menejimenti pamoja na Wafanyakazi wa *General Tyre* ili wote tuelewane vizuri, tuelimishane vizuri na tukubaliane na mchakato wa mpango wa kuendelea huko mbele ili tufike mahali ambako sisi sote tunataka tufike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba wakati umefika wa kuwashirikisha hawa wafanyakazi pamoja na wadau wengine ambao wanaweza kusaidia hiyo *process*?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Felix Mrema, kwanza, kwa kuelewa maelezo yetu. Namhakikishia kwamba, tutawashirikisha wadau wote akiwemo yeye, Wafanyakazi wa *General Tyre* na Mwenyekiti ambaye yupo katika kukitafutia ufumbuzi Kiwanda hiki kwa sababu ni nia ya Serikali kukifufua Kiwanda hicho.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia kuhusu Kauli ya Serikali ya Kilimo Kwanza. Kauli hii inakwenda sambamba sana na soko la bidhaa zinazotokana na kilimo, lakini mpaka sasa hivi sijapata jibu la uhakika kuhusu soko la mafuta ya alizeti kutoka Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama sana hapa. Mheshimiwa Waziri ana kila sifa; ni mchapakazi, ni mwadilifu, naomba afute mzizi wa fitina ili soko la mafuta ya alizeti Singida lipatikane leo.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Diana Chilolo, nilishamshukuru sana kwa kutambua jitihada zake za kutetea uchumi wa Mkoa wa Singida na amekuwa akijitahidi sana. Nilimwahidi kwamba, nitakwenda na Mwekezaji kuona uwezekano wa kuwekeza kiwanda cha ku-*refine* mafuta.

Namshukuru sana Waziri wa Fedha, baada ya Waheshimiwa Wabunge kuongea sana kuhusu suala la umuhimu wa usindikaji wa mazao ya kilimo hususan alizeti na mbegu nyingine za mafuta, baada ya kuondoa ile asilimia kumi kutokana na mafuta ghafi yanayoagizwa nje, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekubali kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* katika mafuta yanayozalishwa kwa kutumia mbegu za humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu hiyo ina manufaa zaidi kuliko hata kuondoa asilimia kumi. Kwa sababu tunapoongeza asilimia kumi wakati wa *duty* kwenye mafuta ghafi, wakati wenzetu Kenya hawaweki hiyo asilimia kumi na Uganda, basi yale mafuta ghafi yaliyopitia Kenya na Uganda yangepata njia ya kuja Tanzania, kwa hivyo hata hayo mafuta ambayo yanasafishwa hapa Tanzania yangekosa soko na ajira inayopatikana kutokana na viwanda hivyo ingekosekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tutaweka ratiba kwa wale ambao wanaagiza mafuta ghafi nje, tutakuwa tunakubaliana kila mwaka watakuwa wanasindika mbegu za mafuta kiasi gani ili wapunguze uagizwaji wa mafuta ghafi kutoka nje ikiwemo mbegu za mafuta kutoka Singida.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mwaka jana nchi ilipeleka chai nje kwa ajili ya kuuza kwa takriban shilingi bilioni 48. Ukiangalia gharama ya kufanya *pre-shipment inspection* ya magari kwa muda wa miaka mitano tumepeleka shilingi bilioni 48, leo Waziri anataka kuendeleza hilo itabidi tena tutafute shilingi bilioni 48 nyingine mara mbili ya chai ili kufanya *pre-shipment inspection*. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, hii iko ndani ya roho yako kwamba, sisi tuwalimie watu wa Dubai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonisikitisha zaidi, jambo hili limezungumzwa kwenye Bunge hili likapitishwa kwamba, kama kuna *inspection* zifanyike nchini. Kwa sababu wale wanaoleta bidhaa feki ni wahalifu, wewe unataka kutumia shilingi bilioni 98 kuzuia uhalifu wasiharibiwe mali yao hapa badala ya kuwapeleka jela unataka mimi niwalimie wahalifu chai!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaridhika kama Mheshimiwa Waziri ana njia ya kumtengenezea mtu hela aliambie Bunge hili ili tujue kwamba tunamlimia mtu na tunampelekea hela. Ahsante sana.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa John Momose Cheyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu ni kwamba, mimi nimekubali rai ya Wabunge kwamba, pengine *pre-inspection* inapofanywa siyo vile inavyotakiwa na nikasema kwamba kuna watu wengi ambao leo wanakuja Wizarani baada ya *FCC* kuamua kuharibu bidhaa zao kwa sababu ni feki. Rai wanayotoa ni kwamba, wametumia gharama kubwa matokeo yake nchi yetu inageuka kuwa jalala la vitu vibovu na feki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *pre-inspection* ya magari inapofanywa, tulichagua makampuni mbalimbali kule nje ambayo ni kweli Watanzania wanapoagiza magari ndiyo wanaolipia dola mia moja kwa kila gari moja. Nakubali ni gharama, lakini pengine gharama ya kusafirisha gari kutoka Japan mpaka huku inaweza ikawa ni kubwa zaidi kuliko gharama ya dola mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninaomba nisitoe uamuzi humu ndani. Naomba nikalifanyie kazi suala hili na nimepokea kwa dhati rai za Waheshimiwa Wabunge wote walizozitoa kuhusu suala la *pre-shipment inspection. (Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nami naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri kwamba, COSOTA imekuwa ikifanya kazi bila usimamizi wa Bodi yoyote takriban kwa miaka miwili sasa na imekuwa ikijikusanyia pesa nyingi kutoka kwenye makampuni mbalimbali, hoteli, mabaa na sehemu nyingine mbalimbali, kwa ajili ya kulipa mrabaha kwa wasanii na inalipa lakini bila uhakika kwamba wamekusanya hela kiasi gani na wamelipa kiasi gani. Pia uharamia ambao umekuwa ukifanywa unakuta kwamba, mtu anakamatwa na magari matatu yenye tani tatu anafikishwa mahakamani, lakini hukumu yake inakuwa ni faini ya shilingi laki mbili na zile kazi alizokamatwa nazo anaruhusiwa kuendelea na biashara ambayo ni uonevu. Nikadai kwamba, sheria iletwe hapa Bungeni ili irekebishwe na kutoa haki kwa wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anipe ufafanuzi kwamba *COSOTA* inafanya kazi kwa uangalizi wa nani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Martha Mlata, kwa swali lake alilouliza. Ni kweli Sheria ya *COSOTA* inatakiwa iletwe Bungeni, kwa sababu *COSOTA* inafanya majukumu mawili sasa hivi ya udhibiti na vile vile kama umoja wa wenye fani ya sanaa. Kwa hiyo, Sheria hiyo nitaileta mapema inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bodi, ninamuahidi Mheshimiwa Martha Mlata, Bodi hiyo itakuwepo muda si mrefu na mchakato wake tayari upo mezani kwang. Kwa hiyo, Bodi itatoka muda si mrefu. Kuhusu malalamiko mengine aliyoyatoa nitayafuatilia. Namshukuru sana kwa kunikumbusha tena, lakini naomba mjue kwamba, chombo hiki ni muhimu sana kwa wasanii wetu na wale wote wanaohusika.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuipongeza Wizara na hususan *NDC*, kwa juhudi walizofanya katika Mradi wa *Sponge Iron*, pamoja na mradi funganishi wa kuzalisha chuma, uzalishaji umeme wa mchuchuma na ujenzi wa miundombinu katika Wilaya ya Ludewa. Nataka kujua Miradi hiyo miwili inaanza lini kwa sababu huko nyuma tuliambiwa *Sponge Iron* ungeanza mwaka jana; na Mradi Funganishi alipokuja Mheshimiwa Rais Ludewa alisema kwamba mchakato huu utakamilika mwaka 2010 ili kazi ianze?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atuambie Miradi hii itakuwa tayari lini na itaanza lini?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, kwa kutaka kujua Mradi Funganishi wa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga pamoja *Sponge Iron* utaanza lini. Kwanza, napenda kumshukuru sana kwa kuufuatilia Mradi huu kwa karibu sana. Mwaka jana tulikuwa bado hatujachagua mwekezaji wa *Sponge Iron.* Hapa ninaposimama, mwekezaji ameshapatikana; *NBC* na mwekezaji wanajaribu kuweka mkataba ambao utainufaisha nchi na nafikiri inahitajika muda kidogo kusudi tuhakikishe kwamba, Mradi huu utakapoanza nchi itanufaika.

Kuhusu Mradi Mkubwa wa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Liganga, kazi kubwa imeshafanyika kwenye Mradi wa Makaa ya Mawe, lakini kwenye Mradi wa Chuma wa Liganga, bado tunapaswa kuchoronga kusudi tusimpe mwekezaji mali yetu bila kujua kule chini kuna nini. Sasa hivi kazi hiyo imepiga hatua, kwa sababu *NBC* wamejaribu kuona namna ambavyo watafanya uchorongaji ili kazi iende kwa haraka. Pengine nitakaporudi tena mwaka ujao, Mungu akipenda na kama tukiwa hai na nikiwa kwenye Wizara, nitakuja kueleza kwamba tumepiga hatua, kwa sababu na Ilani yetu ya Uchaguzi inatutaka Mradi huu uwe umemalizika utafiti wake ifikapo mwaka 2010.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, juu ya mafanikio yaliyopatikana baada ya kuanzishwa kwa Vituo vya Biashara, ambapo kimoja kipo Dubai kingine kiko London, kwa nia ya kuitangaza nchi yetu kwa utalii na kutangaza biashara zetu ili tuweze kukuza uchumi wa nchi yetu. Ahsante.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya kwa swali lake alilouliza. Naomba nitoe jibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida tuliyopata mpaka hivi leo ni kupata wawekezaji kwa wingi kuja huku na wao kutupatia masoko kwa ajili ya bidhaa zetu. Ningependa kumpa takwimu, lakini nisingetaka kumpa takwimu ambayo haina uhakika. Nitamletea takwimu hizo tutakaporudi Wizarani.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Itigi, Manyoni na Singida kwa ujumla, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa agizo alilolitoa takriban mwezi mmoja uliopita kwamba, viwanda vya saruji vitumie malighafi ya hapa nchini. Sasa hivi tani nyingi za *gypsum* jasi zinachukuliwa kutoka Itigi kwenda katika viwanda vya saruji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, ningependa nipate ufafanuzi kutoka Wizara hii kwamba, tuna ombi letu la muda mrefu la kufikiriwa kuwa na kiwanda cha saruji pale Itigi. Kwanza, *location* yake tu yenyewe ni *ideal* kwa ajili ya masoko ya Kanda ya Magharibi na Mikoa ya Ziwa, pamoja hata na nchi za nje.

Sasa ni muda mrefu toka mwaka 2007 na juhudi zimekuwa zikifanywa; wamekuja wawekezaji, wamejaribu kuchukua sampuli na kadhalika na wameahidi kurudi. Tunaona jitihada hizi zinafifia, kwa upande wa Wizara tuna *ingredients* tatu zinatakiwa kwa ajili ya kutengeneza saruji ya kwanza ni *lime*, halafu *gypsum* na *red soil*. Sasa *gypsum* na *red soil* tunayo kwa wingi. *Lime* haipo karibu na eneo hilo, lakini ipo *lime* nyingi maeneo ya Ugwandi. Sasa sielewi kwa nini Wizara inasuasua kuhusu ombi hili ambalo ni muhimu sana. Ahsante.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana kaka yangu John Lwanji na mimi ndiye niliyepokea rai yake mwaka jana, nakumbuka na naikumbuka sana na Itigi ni karibu na nyumbani kwetu na mimi najitahidi sana kuhamasisha.

Uchaguzi wa wapi mwekezaji anakwenda ni wa kwao na mimi nitajaribu sana kuona mwekezaji anapatikana Singida na hasa pale ambapo Barabara ya Mijingu kwenda Singida sasa inakuwa ya lami na hii ya Manyoni kuja Dodoma ni ya lami, nina hakika sasa wawekezaji wataona urahisi kuwekeza sehemu ya Itigi na Singida kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa Kanuni ya 104, nalazimika kuongeza nusu saa kutoka muda wetu wa kawaida wa saa 1.45 hadi hadi saa 2.15.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nimezungumzia suala la mgawanyo wa viwanda vya saruji katika nchi yetu. Katika Hotuba ya Waziri, ukurasa wa 40 kuna wawekezaji ambao wameonesha nia ya kutaka kuwekeza tena kwa kujenga viwanda hapa nchini. Mojawapo ni kiwanda kinachoitwa Tansem cha Shinyanga. Naomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri, inapotajwa Shinyanga nia ya mwekezaji huyu ni kuwekeza Shinyanga ili kukidhi hitaji la watu wa Kanda ya Ziwa. Naomba ufafanuzi tu.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Maria Hewa, kwa kuuliza swali na naomba nimjibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa mwekezaji niliyemtaja na aliyemtaja yeye, anayeitwa Tansem, alionesha nia ya kuwekeza Shinyanga. Ninafikiri ile *speed* imepungua, kwa sababu ya huu mdororo wa kiuchumi uliotokea duniani, lakini bado hajasema kama hatakuja. Kwa hiyo, tusubiri na mimi nitamfuatilia ili kuona kama kuna namna ambavyo tunaweza tukaongeza hiyo *speed* yake.

**MHE. DKT. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia mengi lakini moja lilikuwa *General Tyre,* nataka nipate maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotafuta wawezekezaji tunadhani kwamba, watatusaidia kutuletea utaalam wao, pamoja na fedha. Kinachoonekana hapa na ndiyo maana nilizungumzia, Serikali tumewekeza shilingi ngapi kule *General Tyre?* Nashukuru Serikali imetujibu kwamba, tumekopa Dola za Marekani milioni 10 toka

*NSSF,* sasa naishukuru Serikali imekuwa wazi kwamba huyu bwana hizi fedha tulizompatia, amezitumia vibaya na ndicho nilichokuwa nakitafuta.

Nilitegemea Serikali itakwenda mbele zaidi na kusema huyu ambaye ametumia vibaya hizi hela, tena tumezikopa kutoka kwenye Mfuko wa Wafanyakazi wa Tanzania, tumezidhamini sisi Serikali ya Tanzania; kama atashindwa tunalipa sisi walipa kodi wa Watanzania wakiwemo wafanyakazi wetu. Serikali inachukua hatua gani kwa mtu huyu hasa ikizingatiwa kwamba hivi karibuni hii hali ya wawekezaji kukopa kutoka kwenye Mifuko imejitokeza na hatimaye wanashindwa kulipa na hatujui hatima ya fedha hizi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru kaka yangu Dkt. Willibrod Slaa, kwa swali lake halafu kila wakati lazima niulizwe swali tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nimpe taarifa kwamba, Kiwanda cha *General Tyre* mpaka hii leo mwekezaji mkuu ni Serikali kwa asilimia 76 na mwekezaji kwa asilimia 24. Kwa kuona utaalam wa huyu mwekezaji, pamoja na kwamba alikuwa na teknolojia ya kuwekeza kwenye kile Kiwanda, tukafikiri tukimpa Menejimenti atakiendesha vizuri. Kwa hiyo, tulipokuwa tunatoa shilingi milioni 10, tuliitoa kwenye Menejimenti ya Kiwanda chetu ambacho kwa kiasi kikubwa *owner* ni Serikali. Kwa bahati mbaya, tulipompa tulimpa kwa nia njema kwamba, atakifufua kiwanda na ndiyo maana mimi nawaambia Wabunge kwamba, hatuoni kama kweli mwekezaji huyu alikuwa na nia ya kutusaidia hasa ukizingatia mambo ambayo yametokea, pamoja na matumizi ya hizi fedha.

Kwa hiyo, tumeipitisha *audit* na *Management Contract* imekwisha na ndiyo maana sisi tunajaribu kukataa kulipa zile fedha ambazo anazidai kwa ajili ya kutumia *trade mark* yao, kwa teknolojia ambayo inatumika na kwa ajili ya kulipia Menejimenti yao; kwa sababu tunaamini kwamba, hawakutumia utaalam na ujuzi katika ku-*manage* hiki kiwanda vizuri, hasa ukizingatia matumizi ya hizi fedha.

**MHE. HALIMA M. MAMUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, ningependa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mazuri na hasa baada ya kuwajibu watu wengi kuhusu *General Tyre,* ningeomba sasa atuambie atakapokuja kuwashirikisha wadau wote katika kulishughulikia suala la *General Tyre;* ni nini kinachoendelea katika Kiwanda cha Kilitex Arusha.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu dada yangu Halima Mamuya, kama ifuatavyo:-

Kwanza, namshukuru kwa kutambua majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Waziri amekuwa anatoa hapa Bungeni. Nataka niendelee kusisitiza kwamba, Serikali ina nia ya dhati ya kukifufua kiwanda hicho. Pili, nataka nimjibu kwamba, hilo alilolisema kuhusu *Kilitex,* ambalo bahati mbaya sana maandishi yake yamefika hapa wakati tunakwenda

kujibu hizi hoja; tutalifanyia kazi na tutamshikirisha katika utaratibu wote kuhakikisha kwamba na *Kilitex* nayo inafufuliwa kama uwezekano wa namna hiyo upo.

**MHE. DKT. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa maelezo mazuri aliyoyatoa. Naomba ufafanuzi kwamba, hapo nyuma kulikuwa na kilio kikubwa kuhusu ufungashaji wa mazao ya kilimo. Ikafika mahali Serikali chini ya Sheria ya 340, ambayo ilifanyiwa mapitio mwaka 2002, wakatunga jedwali jipya. Sasa katika lile jedwali likaweka kiwango cha kilo 250, kilo 500, kilo moja na baada ya hapo kilo moja mpaka kilo 10 na kilo 90. Hii ina maana kwamba, mtu akiweka gunia la kilo 80 atakamatwa na ukamataji umekuja sasa kama wimbi, nchi nzima watu wanakamatwa kabla mazao hayajafikishwa sokoni.

Sasa nauliza kwa huyu ambaye ananunua mazao kwa mfano Kigoma anapeleka Dar es Salaam ili akafungashe kulingana na mahitaji ya yule mtu anayeagiza kutoka nje; atayafikishaje mazao hayo Dar es Salaam? Mimi nilidhani lumbesa na mambo mengine yaliyotajwa, yalikuwa yanamaanisha kuzuia watu kupeleka magunia ambayo yanazidi kilo 90 na siyo kupungua kilo 90. Sasa naomba ufafanuzi hili jedwali lilipotengenezwa mlifanya uhakiki unaohitajika au kuna makosa yalifanyika; na je, mtayarekebisha lini? Jedwali lenyewe ninalo.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, hatuna vyombo kama vile vya kupanga bei kwa sababu sasa tuko kwenye uchumi wa soko, lakini soko lisipokuwa na utaratibu itakuwa ni fujo. Kwa hiyo, ndiyo maana tumeweka vipimo hivi ambavyo viko kwenye jedwali kwamba, kila mfanyabiashara anayefanya biashara, ajue vipimo vinavyotumika ni hivi.

Mimi nategemea kwamba, watu wangu hawa wa Vipimo, hawatakuwa na mashine; ni binadamu kama mtu anaeleza kwa mfano hiki ni chakula cha kwenda kula nyumbani kwangu, natoa mfano tu, hana lazima ya kuweka mahindi yake kwenye gunia la kilo 90. Kwa hiyo, kama mtu anakwenda mahali kuchukua kwa *convenience*, nina hakika hawa watu watakuwa wanatumia busara na kuamua lipi ambalo linakwenda kisheria na lipi ambalo haliendi kisheria.

Nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, wafanyabiashara ambao si waaminifu, wamekuwa wakitumia vipimo batili kuwaibia wakulima. Bunge lililopita, nakumbuka rai ya Waheshimiwa Wabunge wote ilikuwa hivi vipimo ambavyo ni batili kama lumbesa. Kwa hiyo, ni kazi ngumu tuwaachie watalaam wetu wafanye kazi na watumie busara katika kusimamia sheria hizi ambazo tumeziweka ili biashara ifanyike kwa haki.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia asubuhi, nilikuwa nimetoa ombi kuwa Mheshimiwa Waziri, awaruhusu wafanyabiashara ndogo ndogo wa kule Ziwa Nyasa, wafanye biashara ya sukari. Sasa jibu ambalo nimelipata hapa ni kwamba, vibali vitatolewa lakini vitatolewa Dar es Salaam.

Je, haoni kwamba ingekuwa bora zaidi kama vibali hivyo vingepelekwa Wilayani kwa sababu kutoka Wilayani kwetu mpaka Dar es Salaam na hawa ni wafanyabiashara wadogo wadogo ni mbali sana na itawapa tabu kwenda huko na kurudi wakiwa na mitaji midogo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa swali la Mheshimiwa Capt. John Komba kama ifuatavyo:-

Kama nilivyomweleza Mheshimiwa Capt. John Komba kwamba, udhibiti huu wa bidhaa nyeti ya sukari na kulinda viwanda vyetu vya sukari uko Bodi ya Sukari hapa nchini kwetu, ambayo iko chini ya Wizara ya Kilimo. Hata hivi leo tulikuwa na afisa mmoja kutoka Bodi ya Sukari, ambaye tulikaa naye na tukakubaliana kwamba, hili suala alilolileta Mheshimiwa Komba ni muhimu katika kuwazingatia wafanyabiashara wadogo nao wapewe fursa kama wanazopewa wafanyabiashara wakubwa, hasa pale bidhaa inapopatikana nchi jirani.

Kwa hiyo, tukasema kwa sababu nchi yetu inafuata utaratibu, acha tukae chini tuangalie utaratibu mzuri wa kuweza kuwanufaisha hawa wafanyabiashara wadogo na ili kuendelea kulinda viwanda vyetu ambavyo ni nyeti na ni muhimu ndani ya uchumi wetu.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi Fulani, Mheshimiwa Waziri amejaribu kujibu yale ambayo nilitaka ufafanuzi. Nasema kwa sababu amekubali kwamba sasa atazipa kipaumbele bidhaa zinazozalishwa hapa nchini, labda tu nimuulize; maana nikimuuliza mikakati nitakuwa ninamwonea kwa sababu muda ni mfupi. Labda ni baada ya muda gani Mheshimiwa Waziri unaweza ukatuambia kwamba angalau tutaanza kuona hatua zimechukuliwa katika bidhaa za ndani? *(Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza kwamba, Serikali itatumia taratibu mbalimbali kulinda viwanda vya ndani kama kutumia Sera za Kodi, kudhibiti uletaji wa bidhaa nyingine kutoka nje. Nimesema vile vile, Watanzania waone umuhimu wa kununua bidhaa zinazotokana na kazi ya Watanzania wenzao ili kujenga ajira na ili kujenga uchumi wa nchi yetu. Kwa kuanzia, pengine ningesema na kwa vile Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa, atakubaliana na mimi pengine nitapeleka Waraka wa Baraza la Mawaziri ili Serikali tuanze kununua samani zinazotengenezwa na Watanzania humu nchini na mahitaji mengine yote ambayo yanapatikana hapa nchini kwa matumizi ya Serikali.

Kwa Watanzania wengine, nitaendelea kuwahamasisha kwa sababu huwezi kuwashurutisha. Kwa hiyo, tutafanya hivyo mapema iwezekanavyo, kwa sababu Serikali ndiyo mnunuzi mkubwa mpaka sasa wa bidhaa nyingi hapa nchini, basi tukiamua kununua samani tu peke yake za maofisi yetu, nina hakika tutakuwa tumewajenga wajasiriamali wetu na tutakuwa tumejenga uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi swali langu ni dogo tu. Nilitaka kuelewa ukurasa wa 17 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia juu ya Mfuko wa Maendeleo ya Wafanyabiashara Wananchi *(National Entrepreneurship Development Fund).* Nnilitaka kujua, nilidhani Mfuko huu ungejielekeza pamoja na mambo mengine, ku-*support* na ku-*promote* biashara za mipakani. Maeneo ya mipakani kama vile kule Kasulu, Manyovu, Kigoma, Kagunga, kwa maana ya *promotion* ya *boarder trade*. Sasa nilitaka kujua huu Mfuko ambao mpaka sasa kwa mujibu wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, umenufaisha wajasiriamali 5,670 na kutoa ajira 13,000. Je, ni lini Mfuko huu utafika katika Mkoa wa Kigoma ambao una wajasiriamali wengi na wengine wanafanya biashara mpaka kule China na Kasulu sasa hivi ni mithili ya Dubai katika nchi za Maziwa Makubwa? Nilikuwa naomba ufafanuzi ili nipate *exactly* ni lini Mfuko huu kwa Sera iliyopo utafika Kasulu na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Wafanyabiashara Wananchi *(National Entrepreneurship Development Fund),* ambao uko chini ya *SIDO* kama ifuatavyo:-

Ninaamini Mfuko huo umetumika *SIDO* pengine ni kiasi tu na mimi nakubaliana na rai yake kwamba, tupeleke zaidi Mikoa ya pembezoni ili biashara ya mipakani iweze kushamiri. Nitajaribu kuwasukuma *SIDO* wafanye hivyo na Mkuu wa *SIDO* yuko hapa, atakuwa amesikia na atachukua hatua zinazostahili. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Kilimanjaro, umekuwa na matatizo ya viwanda vingi kutokufanya kazi na jambo hili tumelijadili katika vikao vyetu vya *RCC* na tumekuwa tukipata majibu kama aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri. Kutokana na viwanda hivyo kutokufanya kazi, uchumi wa Mkoa wetu umepungua na ajira zimekosekana kwa Wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro. Nini *commitment* ya Waziri juu ya Kiwanda cha Machine Tools?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiwelu, jana Mheshimiwa Spika, alitoa *ruling* hapa kwamba, masuala ya *commitment* yasikubalike. Sijui kama unaweza ukali-*frame* vizuri swali lako?

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Nini hatima ya Machine Tools?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kufufua viwanda ni muhimu sana, ikiwemo Machine Tools na bila shaka kama Mheshimiwa Kiwelu amenisikiliza, nimesema kwamba, Machine Tools imepata mwekezaji ambaye ame-*team up* na *NDC* katika kukifufua Kiwanda hicho na mimi nitafuatilia ili harakati hizi za kukifufua Kiwanda hicho ziende kwa kasi zaidi kuliko ilivyo sasa. *(Makofi)*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania Breweries kwa kushirikiana na South African Breweries Miller, walikinunua Kiwanda cha Kibo

Breweries kilichopo Moshi na badala ya kukiendelea wakakifunga. Kwa mujibu wa Sheria ya Fair Competition, mpango huu ulikiuka Sheria za Nchi. Leo hii watu hao hao wanaihujumu Kampuni ya Bia pekee iliyobaki ya Serengeti, ambayo inamilikiwa kwa asilimia 100 na Watanzania. Naomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri, nataka kujua hatua wanazochukua Wizara kuzuia huu uvunjaji wa Sheria wa Tanzania Breweries kwa kushirikiana na South African Breweries Miller?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kuhusu hoja ya TBL na Sub Miller ya South Africa kununua Kibo Breweries na hatimaye kuiua; jambo ambalo halikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wataalam wa biashara, kwenye uchumi wa soko; *acquisition* na *mergers* ni jambo la kawaida katika soko la namna hiyo isipokuwa *monopoly* au *cartel* haikubaliki ndani ya soko hilo. Kwa vile kuna bia nyingine ambazo zinatoka nje na zinaruhusiwa kuingia Tanzania, inabidi sasa hilo jambo tuliangalie kwa makini na tulione na kama kulikuwa na namna yoyote ya kutokuwa na ushindani wa haki kwa hatua iliyochukua TBL, pamoja na Sub Miller, basi ilibidi twende *Fair Competition Commission* ili watufafanulie. Kuhusu kuihujumu Serengeti Breweries, inabidi nifuatilie; ninalolijua TBL na Serengeti Breweries wote walishakuja Wizarani kueleza matatizo, kila mmoja kwa upande wake. Tanzania Breweries ilikuja kusema kwamba, walikuwa na maelewano ya kibiashara *under licence* kuzalisha bia za East African Breweries na East African Breweries kuzalisha bia. Nachelea kusema TBL angalau Castle walikubaliana kufanya hivyo, East African Breweries izalishe bia za Castle na kuziuza. Kwa maelezo niliyopata, ilikuwa ni pamoja na bia nyingine za TBL ambazo hazijawahi kuzalishwa kule Kenya.

Sasa baada ya Kenya kwa kudai kwamba Wakenya hawataki bia hizo, hawakutekeleza makubaliano waliyokuwa nayo. TBL mpaka leo inazalisha bia za Tusker na kuzisambaza na ninyi mnajua, lakini naambiwa kwamba idadi ya mauzo ya bia ya Tusker nayo yameshuka. Hivi karibuni Eastern African Breweries wamevunja makubaliano hayo ya bia zao kuwa *produced under licence* na kuuzwa *under licence,* badala yake wamepeleka makubaliano hayo kwa Serengeti Breweries na nafikiri kwamba kulikuwa na makubaliano ambayo pengine yalivunjwa, TBL imekwenda kushtaki mahakamani kule Uingereza. Sasa hilo ndilo linalochukuliwa kama ni uhujumu. Kwa vile suala lenyewe liko mahakamani na kwa vile wote wawili wamekuja Wizarani, sisi tutalifuatilia kwa karibu sana na Mtendaji Mkuu wa FCC yuko hapa na yeye atakuwa anafuatilia kwa karibu ili aweze kuishauri Wizara kama kuna sheria zinazokiukwa za biashara ama kuna utaratibu unaokiukwa basi tutachukua hatua sahihi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Wakati Mheshimiwa Waziri anazungumzia habari ya *mergers* na *acquisitions,* mmenikumbusha wiki iliyopita kuna kampuni moja ya magari, Ulaya nadhani ni Bosch ambayo imekuwa *acquired* na kampuni nyingine, sasa yule *CEO* wa kampuni ile amelipwa dola milioni 50 kama *golden handshake*.

**MHE. DKT. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka Waziri anisaidie; ni imani yangu Rais akitoa ahadi, Wizara husika inajaribu kusaidia utekelezaji wake. Rais akiwa katika kampeni, aliahidi ili Wilaya ya Kibaha Mjini isiwe maficho ya Mkoa wa Dar es Salaam, atahakikisha anafanya kila njia viwanda vingi vinaletwa Kibaha Mjini, akijua kulikuwa na vingine pale; na kwa kutekeleza ahadi hiyo, Halmashauri yangu ya Kibaha Mjini imetenga eneo Zegeleni. Tangu Rais ameahidi mwaka 2005, utekelezaji sijauona na kwa bahati mbaya juzi nimetazama katika kile Kitabu cha Ahadi za Rais hamkuandika, watu wangu wanalalamika. Je, Waziri atanisaidiaje; ni hujuma ilifanywa kwa makusudi au anaamua atatekeleza ahadi?

**MWENYEKITI:** Au amesahau? Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa hoja aliyoitoa Mheshimiwa Dkt. Zainab Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahadi ya Rais ikitolewa ni kweli ni jukumu la Wizara husika kuitekeleza. Kwanza kabisa, napenda kumjulisha au kumpa taarifa Mheshimiwa Dkt. Zainab Gama, hivi karibuni kuna mwekezaji ambaye atakuja kuwekeza kiwanda kikubwa cha nguo pale Kibaha. Alikuwa anahitaji eneo pale Kibaha, aliomba sehemu ya eneo ambalo lilikuwa la TAMCO, siyo ndani ya kile kiwanda nje na NDC ikampa hilo eneo. Wamemwandikia juzi kwamba anaweza na yeye alikuwa analifuatilia kwa karibu sana, kwa sababu alikuwa na hamu sana ya kuwekeza kule Kibaha. Kwa hiyo, namshukuru sana kwa sababu ameniwezesha kutekeleza Ahadi ya Mheshimiwa Rais na vile vile kama kutakuwa na wengine, tutawaelekeza Kibaha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Owenya na kama muda utaruhusu Mheshimiwa Bafadhili.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mheshimiwa Waziri, ametueleza kwamba, katika Kiwanda cha *General Tyre* Serikali inamiliki hisa 76; je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka za kununua zile *share* zilizobaki 24 ili Serikali imiliki asilimia 100 kama walivyofanya katika Mgodi wa Kiwira? Muwekezaji aliyeko pale, huyu mbia aliyeko na *General Tyre,* anaonesha kabisa hana nia ya kukifufua kiwanda kile, ana nia ya kukilinda kiwanda cha *Fire Stone*, nafikiri inabidi achukue hatua hiyo kama jambo la dharura. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, Serikali inajitoa katika uzalishaji na kufanya biashara, lakini wakati linapokuja jambo ambalo ni muhimu na ni nyeti kwa Taifa kama *General Tyre,* tunachukua pendekezo lake na tunalifanyia kazi.

**MHE. NURU A. BAFADHIL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka ufafanuzi kuhusu Kiwanda cha Chuma Jijini Tanga, ambacho kimepewa mwekezaji Toxi Hans kutoka Arusha. Mwenye Kiwanda cha Arusha

Hans Rolling Mining Steal ambaye sasa hivi kazi anayoifanya ni kuchukua *scrappers* zote kuhamishia Arusha na nadhani hatimaye Kiwanda cha Tanga kitakuwa ni magofu. Waziri anipe ufafanuzi kwamba tunaandaa kuweka majambazi na vibaka katika kiwanda hicho kitakachohamishwa?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Bafadhil, kwa hoja yake na ninaomba kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Pamoja na aliyoyaeleza, lakini muda si mwingi huko nyuma mwekezaji huyo alikuja Wizarani kueleza nia yake ya kukifufua Kiwanda cha Chuma Tanga na anataka kuweka mitambo ya kisasa; na aliyatoa mambo ambayo angetaka Wizara ijaribu kumsaidia. Sasa nitaangalia kama alikuwa anafanya hivyo kwa dhati ama sio kwa dhati na kwa hiyo tutafuatilia.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia kuhusu leseni za biashara. Leseni za biashara Serikali imeziondoa na kile ni chanzo kikubwa cha mapato kwa Serikali na Halmashauri zetu, matokeo yake wenye biashara kuanzia milioni moja mpaka mabilioni hawalipii leseni, lakini muuza mkaa wa shilingi elfu nane kwa gunia anatozwa ushuru wa shilingi elfu mbili! Hawa watu masikini mbona wanaendelea kukandamizwa? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kuhusu hoja ya Mheshimiwa Arfi kama ifuatavyo:-

Kwa sababu tumetoka uchumi hodhi kwenda kwenye uchumi wa soko, Serikali inajaribu kuhamasisha wajasiriamali wadogo waweze ku-*formalise* watoke kwenye *Informal Sector* kwenda kwenye *Formal Sector*, kwa kuwapa leseni bila ya kutozwa na ina kikomo chake sio kila mtu alipie leseni. Kuhusu ushuru wa mkaa, hizo ni *by-laws* za Halmashauri ambazo Serikali Kuu ilishatoa kibali chake na kwa hiyo siwezi nikalisemea.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, pamoja na juhudi za Meza kujaribu kumuwezesha kila Mheshimiwa Mbunge apate fursa, kwa kweli sasa muda haupo upande wetu na Wabunge 11 wamebaki bila kupata nafasi. Tusameheane kwa hilo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Kwa mujibu wa Kanuni ya 104(2), sasa tutapitisha makadirio yetu haya kwa ujumla wake kwa utaratibu wa *guilotine.*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*…………………….. Sh.276,283,000
Kif. 1003 - *Policy and Planning*……………………….. Sh.3,891,026,000
Kif. 1004 - *Information, Educat,*
*Communication Unit*… ................................................Sh.112,159,000
Kif.1005 - *Internal Audit Unit*………………………...… Sh.129,862,000

Kif. 1006 - *Legal Services Unit*………………………… Sh.10,174,253,000
Kif. 2001 - *Industry*…………………………………… Sh.3, 116,821,000
Kif. 2002 - *Small and Medium Enterprises Division*…Sh.6, 804,532,000
Kif. 3001 - *Commerce*…………………………………Sh.1,691,227,000
**Kif. 4002 - *Commodity Market Development*……… Sh.7,828,500,000**

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

**Fungu 44 - Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko**

Kif. 1001 - *Administration and General*……….............………… Sh.0
Kif. 1003 - *Policy and Planning*………………...…… Sh.19,509,677,000
Kif. 2001 - *Industry*………………………......……………Sh.410,500,000
Kif. 2002 - *Small and Medium Enterprises Division*… Sh.4,418,923,000
Kif. 3001 - *Commerce*……………………...………..Sh.1,381,882,000
**Kif. 4002 - *Commodity Market Development***……….Sh.3,485,235,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja na nawashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, kwa utaratibu sasa natakiwa niwahoji ili tuiamue.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka 2009/2010 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Kwa hatua hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tunawatakia kila la heri Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara ya

Viwanda, Biashara na Masoko, kwa mwaka mzima unaokuja kuitekeleza bajeti yetu vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo, ninalo tangazo moja tu nalo ni kutoka kwa Mheshimiwa Ngeleja, ambaye ana mgeni wake, Ndugu Edmond Bernard Mndolwa, Mtaalamu wa Ushauri wa Masuala ya Fedha, lakini pia ni Mjumbe wa Baraza la Wazazi Mkoa wa Tanga. Natumaini yupo kwenye *gallery*. Ahsante sana na karibu sana ndugu yetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo, shughuli zilizopangwa kwenye *Order Paper* kwa siku ya leo zimekamilika zote, kwa maana hiyo naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.08 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 29 Julai 2009 Saa Tatu Asubuhi)*